JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI,2020

MIRADI YA MAENDELEO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' Simu: 255(026) 2161200, Nukushi: 255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz.Tovuti: www.nao.go.tz

Kwa majibu, tafadhali nukuu

Kumb.Na. CAG.319/421/01-A/11 **28 Machi 2021**

Mheshimiwa. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere, Chamwino,
40400 DODOMA.

YAH: KUWASILISHA TAARIFA YA MWAKA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO YA MWAKA WA FEDHA 2019/20

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008. Ninawasilisha kwako Ripoti yangu ya kumi ya Mwaka juu ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2020.

Nawasilisha.

Charles E. Kichere
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Uanzishwaji

Madaraka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 pamoja na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009.

Dira

Kuwa Taasisi ya Kuaminika na ya Kutukuka katika Ukaguzi wa Sekta ya Umma.

Dhamira

Kutoa Huduma Bora za Ukaguzi wa Hesabu ili Kuimarisha Utendaji, Uwajibikaji, Uwazi, na Thamani ya Fedha katika Kukusanya na Kutumia Rasilimali za Umma.

Misingi ya Maadili

Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

- **Uadilifu:** Sisi ni Taasisi adilifu inayotoa huduma kiuhakikifu na bila upendeleo.
- **Ubora:** Sisi ni Taasisi yenye weledi inayotoa huduma bora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi.
- **Uaminifu:** Tunazingatia na kudumisha kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.
- **Kuwalenga watu:** Tunalenga zaidi matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia wateja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.
- **Ubunifu:** Sisi ni Taasisi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.
- **Matumizi bora ya rasilimali:** Sisi ni asasi inayothamini na kutumia kwa umakini mkubwa rasilimali za umma ilizokabidhiwa.

Tunatimiza haya kwa kufanya yafuatayo:

- Kuchangia matumizi bora ya fedha za umma kwa kuhakikisha kwamba wakaguliwa wetu wanawajibika kutunza rasilimali walizokabidhiwa;
- Kusaidia kuimarisha ubora wa utoaji huduma kwa kuchangia usanifu kwa matumizi bora ya rasilimali za umma;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wadau wetu kuhusu mapungufu katika uendeshaji wa shughuli zao;
- Kuwahusisha wadau wetu katika mfumo wa ukaguzi; na

- Kuwapa wakaguzi nyenzo za kufanyia kazi ambazo zitaimarisha uhuru wa Ofisi ya Ukaguzi.

© Kwa mujibu wa Kifungu cha 39 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa), Taarifa hii ya Ukaguzi imekusudiwa itumiwe na mamlaka za Serikali. Hata hivyo, mara baada ya kupokelewa na Spika na kuwasilishwa Bungeni, taarifa hii huwa kumbukumbu ya umma na usambazaji wake hauzuiliwi.

Yaliyomo

Dibaji.. xiv
Shukrani xvi
MUHTASARI xviii

SEHEMU YA KWANZA 1
SURA YA KWANZA 2
UTANGULIZI NA USULI WA MIRADI 2
1.1 Utangulizi 2
1.2 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 2
1.3 Aina za Kaguzi 3
1.4 Miradi Iliyokaguliwa 4
1.5 Wajibu wa Maafisa Masuuli 9
1.6 Wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 10
1.7 Mawanda na Viwango vya Ukaguzi Vilivyotumika 10
1.8 Mbinu za Ukaguzi 11
1.9 Muundo wa Taarifa 12
SURA YA PILI 13
HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA TAARIFA ZA KAGUZI 13
2.1 Utangulizi 13
2.2 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita 13

SEHEMU YA PILI 15
SURA YA TATU 16
UTENDAJI WA KIFEDHA 16
3.1 Utangulizi 16
3.2 Ufadhili wa Miradi 16
3.3 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa 36
3.4 Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Fedha 40
SURA YA NNE 58
USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA 58
4.1 Utangulizi 58
4.2 Usimamizi wa Manunuzi 58
4.3 Usimamizi wa Mikataba 63

SEHEMU YA TATU 77
SURA YA TANO 78
UJENZI WA RELI YA KISASA (SGR) KUTOKA DAR ES SALAAM HADI MAKUTUPORA 78
5.1 Utangulizi 78
5.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi 78
5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi 79
SURA YA SITA 96

UJENZI WA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE 96
6.1 Utangulizi 96
6.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi 96
6.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi 97
SURA YA SABA 129
MRADI WA MIUNDOMBINU YA MABASI YAENDAYO HARAKA JIJINI DAR ES SALAAM 129
7.1 Utangulizi 129
7.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi 129
7.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi 130
SURA YA NANE 154
UPANUZI WA BARABARA YA MOROGORO KIPANDE CHA (KIMARA-KIBAHA) 154
8.1 Utangulizi 154
8.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi 154
8.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi 154
SURA YA TISA 165
MRADI WA USAMBAZAJI MAJI SAME, MWANGA NA KOROGWE 165
9.1 Utangulizi 165
9.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi 168
9.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi 168
SURA YA KUMI 239
UTEKELEZAJI WA MRADI WA UZALISHAJI WA SUKARI MBIGIRI 239
10.1 Utangulizi 239
10.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi 239
10.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi 240
SURA YA KUMI NA MOJA 254
UPIMAJI WA UTENDAJI HALISI KATIKA MIRADI SABA 254
11.1 Utangulizi 254
11.2 Tathmini ya Mwaka ya Utendaji wa Miradi Saba Inayotekelezwa 254
SURA YA KUMI NA MBILI 270
MASUALA MENGINE YA UTENDAJI WA MIRADI YALIYOBAINIKA WAKATI WA UKAGUZI WA FEDHA 270
12.1 Utangulizi 270
12.2 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi 270

SEHEMU YA NNE 277
SURA YA KUMI NA TATU 278
HITIMISHO 278
SURA YA KUMI NA NNE 287
MAPENDEKEZO 287
VIAMBATISHO 289

Orodha ya Majedwali

Jedwali 1- 1: Miradi iliyokaguliwa kwa sekta katika mwaka wa fedha 2019/20 ... 11
Jedwali 2- 1: Utekelezaji wa mapendekezo katika taarifa za kaguzi za miaka ya nyuma ... 13
Jedwali 3- 1: Muhtasari wa mapato na matumizi – Sekta ya Kilimo ... 17
Jedwali 3- 2: Muhtasari wa mapato na matumizi – Sekta ya Elimu ... 19
Jedwali 3- 3: Muhtasari wa Mapato na Matumizi – Sekta ya Nishati na Madini ... 21
Jedwali 3- 4: Muhtasari wa mapato na matumizi – Sekta ya Afya ... 23
Jedwali 3- 5: Muhtasari wa mapato na matumizi - Sekta ya Uchukuzi ... 26
Jedwali 3- 6: Muhtasari wa mapato na matumizi - Sekta ya Maji ... 28
Jedwali 3- 7: Muhtasari wa mapato na matumizi - UNDP ... 30
Jedwali 3- 8: Muhtasari wa mapato na matumizi – UNICEF ... 32
Jedwali 3- 9: Muhtasari wa mapato na matumizi - Miradi Mingine ... 34
Jedwali 3- 10: Muhtasari wa Hati ya Ukaguzi zilizotolewa ... 37
Jedwali 3- 11: Mwenendo wa Hati ya Ukaguzi zilizotolewa ... 38
Jedwali 3- 12: Kutolewa kwa fedha pungufu kwenye miradi ya maendeleo ... 41
Jedwali 3- 13: Mapungufu katika usimamizi wa masurufu ... 51
Jedwali 4- 1: Manunuzi ya yalifanyika bila kushindanisha wazabuni ... 59
Jedwali 4- 2: Manunuzi yaliyopangwa ambayo hayajafanyika ... 61
Jedwali 4- 3: Manunuzi ambayo hayakujumuishwa katika mpango wa manunuzi . 62
Jedwali 4- 4: Mikataba iliyotekelezwa bila ya kuwapo kwa dhamana halali za utendaji ... 65
Jedwali 4- 5: Madai ya wakandarasi ambayo hayajalipwa ... 68
Jedwali 4- 6: Orodha ya wakandarasi ambao dhamana zao za utendaji ziliisha ... 74
Table 5- 1: Kutotambuliwa kwa gharama zilizotumika ... 86
Jedwali 6- 1: Muhtasari wa wafanyakazi wa kigeni wa mkandarasi waliokosa vibali vya kisheria/halali vya kufanya kazi nchini ... 118
Jedwali 6- 2: Bajeti ya mradi kutoka mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2020/21 ... 121
Jedwali 7- 1: Riba Kutokana na Malipo yaliyocheleweshwa kwa M/s Interconsult 142
Jedwali 9- 1: Uchambuzi wa gharama juu ya athari za kuzidisha idadi ya watu . 172
Jedwali 9- 2: Uchambuzi wa gharama za uendeshaji kutokana na kuwa na moundombinu mikubwa zaidi ... 173
Jedwali 9- 3: Vipengele ambavyo havikupaswa Kujazwa katika Nukuu ya Gharama za Vifaa na Huduma ... 181
Jedwali 9- 4: Vipengele vilivyoonekana mara mbili katika nukuu ya gharama ya vifaa na huduma ... 183
Jedwali 9- 5: Vipengele vilivyojazwa bei na mkandarasi bila kufafanua kazi katika kipengele cha Kazi na huduma za awali ... 186
Jedwali 9- 6: Orodha ya barua za zabuni zenye utata katika Mkataba wa III ... 189
Jedwali 9- 7: Hoja za mzabuni na majibu ya mwajiri ... 196
Jedwali 9- 8: Gharama ya nyongeza kutokana na mabadiliko ya bei mabomba . 197
Jedwali 9- 9: Ukamilifu wa miradi yote mitatu kama ilivyochukuliwa ... 205

Jedwali 9- 10: Ongezeko la muda wa kukamilisha mradi na sababu zake 205
Jedwali 9- 11: Vipengele ambavyo havikuathiriwa na muda lakini gharama zake ziliongezeka 207
Jedwali 9- 12: Hali ya malipo ya vipengele vya awali 210
Jedwali 9- 13: Kasoro zilizoonekana wakati wa ukaguzi wa ujenzi 210
Jedwali 9- 14: Matokeo ya miundo ya zege na udongo kwa mkataba Na. 1 212
Jedwali 9- 15: Matokeo ya vipimo visivyoharibifu katika miundombinu ya mradi 214
Jedwali 9- 16: Matokeo ya Vipimo vya ushindiliaji katika maeneo ya mradi 215
Jedwali 9- 17: Matokeo ya vipimo vya nguvu ya zege kwa mkataba Namba III ... 215
Jedwali 9- 18: Matokeo ya Vipimo vya udongo na zege kwa Mkataba Namba 1 .. 217
Jedwali 9- 19: Kuchelewa kuidhinisha Mabadiliko ya Mkataba kwa ajili ya kuongeza muda wa mkataba 218
Jedwali 9- 20: Idadi ya wataalam wa kiufundi kwenye vitengo vya maji vilivyohitajika Wizara ya Maji 221
Jedwali 9- 21: Idadi ya wataalamu wa kitengo cha manunuzi katika Wizara ya Maji 222
Jedwali 9- 22: Ucheleweshwaji wa malipo ya kujikimu kwa msimamizi wa mradi 225
Jedwali 9- 23: Orodha ya watendaji muhimu waliojitokeza katika mkataba 226
Jedwali 9- 24: Kiasi cha mkopo kilichobajetiwa na kiasi kilichotolewa na kila mfadhili 228
Jedwali 9- 25: Kiasi kilichobajetiwa na kiasi kilichotolewa.......................... 229
Jedwali 9- 26: Mchanganuo wa malipo yaliyofanyika kwa wakandarasi........... 230
Jedwali 9- 27: Makato ya fedha za matazamio zilizokatwa lakini hazitunzwi na mwajiri 231
Jedwali 9- 28: Kiasi cha mkataba kilichorekebishwa Juu ya 15% 232
Jedwali 9- 29: Dhamana ya utendaji na malipo ya awali yaliyogharamiwa na mwajiri 236
Jedwali 9- 30: Malipo ya bima yaliyolipwa bila ushahidi wa kukatwa kwa bima . 238
Jedwali 10- 1: Bei tajwa/iliyosomeka kwenye zabuni Na. PA/150/2019-2 246
Jedwali 10- 2: Kujumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani katika bidhaa zilizona msamaha wa kodi 249
Jedwali 10- 3: Kiasi kilicholipwa na kampuni moja kwa moja kwa vibarua 250
Jedwali 11- 1: Miradi Inayoshughulikiwa na Ukaguzi wa Kiufundi 254
Jedwali 11- 2: Maelezo ya kucheleweshwa kwa malipo ya awali 259
Jedwali 11- 3: Gharama za riba kutokana na malipo yaliyocheleweshwa 268
Jedwali 12- 1: Kazi ambazo hazijakamilika kutokana na miradi iliyotekelezwa .. 270

Orodha ya Viambatisho

Kiambatisho 3- 1: Watekelezaji wa Miradi Wenye Hati Zisizoridhisha 289
Kiambatisho 9- 1: Nukuu ya Gharama za Vifaa na Huduma 296
Kiambatisho 10- 1: Vipengele Vilivyolipwa kwa Mkandarasi Bila Uthibitisho...... 297
Kiambatisho 11- 1: Maendeleo ya Utekelezaji wa Kazi za Ujenzi 298

Vifupisho

AFD	Shirika la Maendeleo la Ufaransa
AfDB	Benki ya Maendeleo Afrika
AFROSAI-E	Umoja wa Taasisi za Ukaguzi katika Nchi za Afrika Zinazozungumza Kiingereza
AG	Mwanasheria Mkuu wa Serikali
AQRB	Bodi ya Usajili wa Wasanifu na Wapimaji
AUWASA	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha
AWP	Mpango Kazi wa Mwaka
BADEA	Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Uchumi Afrika
BMGF	Mfuko wa Bill na Melinda Gates
BOQ	Makadirio ya Gharama za Ujenzi
BOT	Benki Kuu ya Tanzania
BRN	Matokeo Makubwa Sasa
BTIP	Mradi wa Uwekezaji wa Miundombinu ya Msingi ya Kusafirisha Umeme
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
CCHP	Mpango Kabambe wa Afya wa Halmashauri
CDC	Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa cha Marekani
CHMT	Timu ya Usimamizi wa Afya ya Halmashauri
CHSB	Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri
CIDA	Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Kanada
CML	Maabara Kuu ya Ujenzi ya Serikali
DANIDA	Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Denimaki
DDCA	Wakala wa Kuchimba Visima na Ujenzi wa Mabwawa
DFATD	Shirika la Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo
DFID	Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza
DMGP	Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam
DUTP	Programu ya Uboreshaji wa Miundombinu ya Usafirishaji Jijini Dar es Salaam
EFD	Mashine ya Stakabadhi ya Kielektroniki
EIA	Tathmini ya Athari za Mazingira
EIA	Upimaji wa Athari za Mazingira
EIB	Benki ya Uwekezaji ya Ulaya
EOT	Kuongezewa Muda
ERB	Bodi ya Usajili ya Wahandisi
ESCBP	Mradi wa Kujenga Uwezo wa Sekta ya Nishati
ESMP	Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Kijamii
ESPJ	Elimu na Ujuzi, Kazi za Uzalishaji
EU	Umoja wa Ulaya
FYDP II	Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili
GAFSP	Programu ya Kimataifa wa Kilimo, Usalama wa Chakula
GCC	Masharti ya Jumla ya Mkataba
HBF	Mfuko wa Uchangiaji wa Afya

HFGC	Kamati ya Usimamizi wa Vituo vya Afya
HSE	Afya, Usalama na Mazingira
HSPS	Programu ya Sekta ya Afya ya Msaada
ICT	Zabuni ya Ushindani wa Kimataifa
IFAC	Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu na Wakaguzi
IFAD	Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo
INTOSAI	Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi
IPC	Madai ya Wakandarasi
IPSAS	Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji Hesabu katika Sekta za Umma
ISSAIs	Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vya Ofisi za Ukaguzi wa Umma
JICA	Shirika la Maendeleo la Japani
KCCMP	Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi Vyanzo vya Maji Kihansi
KfW	Benki ya Maendeleo ya Ujerumani
KOICA	Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea
LAAC	Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa
LAAM	Muongozo wa kifedha wa Serikali za Mitaa
LANES	Mpango wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu
LGAs	Mamlaka za Serikali za Mitaa
LGFM	Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa
LIC	Mradi wa Programu ya Maboresho ya Mazingira ya Wawekezaji wa Ndani
MDAs	Wizara, Idara na Wakala wa Serikali
MGR	Reli ya Zamani
MHCL	Kampuni Hodhi ya Mkulazi
MIVARF	Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji wa Thamani, na Msaada wa Fedha Vijijini
MoCLA	Wizara ya Katiba na Sheria
MoEST	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
MoIT	Wizara ya Viwanda na Biashara
MoU	Hati ya Makubaliano
MoW	Wizara ya Maji
MSD	Bohari Kuu ya Dawa ya Serikali
MWAUWASA	Mamlaka ya Maji safi na maji taka Mwanza
NACTE	Baraza la Kitaifa la Elimu ya Ufundi
NCMC	Kituo cha Kudhibiti Hewa ya ukaa Nchini
NCT	Zabuni ya Ushindani wa Kitaifa
NEMC	Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira
NFAST	Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia
NORAD	Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Norwei
NSSF	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii
OFID	Mfuko wa Maendeleo ya Kimataifa wa Jumuiya ya Nchi Zinazozalisha Mafuta Duniani
OPEC	Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta

OR-TAMISEMI	Ofisi ya Raisi-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PAC	Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali
PCC	Masharti Maalumu ya Mkataba
PFMRP	Programu ya Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma
PMO	Ofisi ya Waziri Mkuu
PPRA	Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma
PSSN	Mpango wa Kunusuru kaya Maskini
RBF	Mfumo wa Ufadhili kwa Matokeo
REA	Wakala wa Nishati Vijijini
REGROW	Mradi wa Maliasili Endelevu kwa Ukuaji
RUWASA	Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini
RWSSP	Programu ya Usambazaji wa Huduma ya Maji Safi Vijijini
SATTFP	Mradi wa Uwezeshaji Biashara na Uchukuzi wa Kusini mwa Afrika
SCC	Masharti Maalumu ya Mkataba
SE4ALL	Mradi Endelevu wa Nishati kwa Wote
SGR	Reli ya Kisasa
Sh.	Shilingi ya Kitanzania
SIDA	Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi
SMMRP	Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Raslimali za Madini
STVET-TE	Programu ya Kusaidia Elimu ya Ufundi, Mafunzo na Elimu kwa Walimu
SUA	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine
SWIOFish	Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi na Ukuaji wa Pamoja Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi
TANESCO	Shirika la Umeme Tanzania
TANIPAC	Mradi wa Mpango wa Tanzania wa Kuzuia Mfumuko wa Bei
TANROADS	Wakala wa Barabara Tanzania
TASAC	Shirika la Mawakala wa Usafirishaji Tanzania
TASAF	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii
TCU	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania
TECU	Kitengo Cha Ushauri wa Kihandisi cha Wakala wa Barabara
TEDAP	Mradi wa Maendeleo ya Upatikanaji na Ukuzaji wa Nishati Tanzania
TEITI	Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta, na Gesi Asilia Tanzania
TEMESA	Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania
TIRDP	Mradi wa Maendeleo ya Reli Tanzania
TPRS	Mpango wa Kupunguza Umaskini Tanzania
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
TRC	Shirika la Reli Tanzania
TSCP	Mradi wa kuboresha Miji Tanzania
TSSP	Programu ya Msaada wa Sekta ya Usafiri
UDSM	Chuo Kikuu cha Dar es salaam
UN	Umoja wa Mataifa

UNDP	Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa
UNEP	Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa
UNICEF	Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto
USAID	Shirika la Misaada la Watu wa Marekani
UTC	Mradi wa Kuboresha Chuo cha Ualimu
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani
VPO	Ofisi ya Makamu wa Rais
WASH	Usafi wa Maji na Mazingira Shuleni
WB	Benki ya Dunia
WSDP	Programu ya Maendeleo Katika Sekta ya Maji

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT

Dibaji

Ninayo furaha kuwasilisha Taarifa ya 10 ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020. Taarifa hii inakusudia kutoa ujumbe kwa wadau wetu (Wabunge, Watendaji wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Vyombo vya Habari, Washirika wa Maendeleo, Asasi Zisizo za Kiserikali, na Taasisi za Kijamii) kuhusu uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi yaliyotokana na kaguzi husika za miradi ya maendeleo zilizofanywa na Ofisi yangu kwa kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020. Muhtasari wa mambo muhimu yaliyooneshwa katika taarifa hii ya jumla yanaweza kusomwa kwa undani katika taarifa kamili za ukaguzi zilizopelekwa kwa kila Afisa Masuuli anayesimamia utekelezaji wa miradi husika ya maendeleo.

Taarifa hii inajumuisha taarifa za miradi mikubwa 104 ya maendeleo iliyokaguliwa na Ofisi yangu kwa mwaka wa fedha 2019/20. Miradi hii inafadhiliwa na Serikali ya Tanzania na wahisani kupitia Mfuko wa Pamoja. Wahisani hao ni Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (DFID), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW), Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la Maendeleo la Japani (JICA), na Umoja wa Ulaya (EU).

Aidha, taarifa hii inajumuisha wafadhili wengine ambao ni Umoja wa Mataifa (UN) kupitia taasisi zake kama vile Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto (UNICEF), Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP), Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa cha Marekani (CDC), Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, UKIMWI, na Kifua Kikuu (Global Fund), na Wadau Wengine wa Maendeleo.

Aidha, taarifa hii inajumuisha Washirika wa Maendeleo wengine kama vile, Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Mfuko wa Bill na Melinda Gates (BMGF), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Kanada (CIDA), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Denmaki (DANIDA), Shirika la Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo (DFATD), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Norwei (NORAD), Mfuko wa Maendeleo ya Kimataifa wa Jumuiya ya Nchi Zinazozalisha Mafuta Duniani (OFID), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID).

Kwa mujibu wa Ibara za 143(2)(c) na 143(4) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa), Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa, angalau mara moja kwa mwaka, kufanya ukaguzi na kutoa taarifa ya ukaguzi wa hesabu hizo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ataiwasilisha Bungeni.

Ni matarajio yangu kuwa taarifa hii itasaidia wadau wa miradi ya maendeleo kutathmini iwapo fedha zilizopelekwa kwenye miradi ya maendeleo zimetumika kwa usahihi na kwa malengo yaliyokusudiwa, zimechangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na zimetoa thamani ya fedha.

Ninatumaini kuwa Serikali, Bunge, Washirika wa Maendeleo, na Umma kwa ujumla, wataichukulia taarifa hii kwa umuhimu mkubwa katika kuelewa jinsi Maafisa Masuuli wanavyosimamia miradi ya maendeleo na namna mafanikio yake yanavyosaidia kutatua matatizo yanayowakabili Watanzania. Hivyo, ili kuboresha taarifa hii siku zijazo, nitashukuru kupata maoni kutoka kwa umma na watumiaji wengine wa taarifa hii kwa muda muafaka.

Charles E. Kichere
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI
Machi 2021.

Shukrani

Ni heshima kubwa kufanikisha suala hili la kikatiba la kuwasilisha taarifa kuu ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wakati kwa mujibu wa sheria.

Nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na naahidi kushirikiana naye kikamilifu kuisadia Serikali yake katika kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi na tija katika kuboresha ustawi wa nchi hii.

Napenda pia kutambua msaada wa Hayati Rais, Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli kwa Ofisi yangu. Dk Magufuli alikuwa mzalendo, Mwanamajumui wa Afrika na kiongozi mkuu wa wakati wake. Ni kupitia msaada wake Ofisi yangu iliweza kutekeleza takwa la kikatiba na kufanikisha dhamira yake ya kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa hali ya juu ili kuboresha utendaji wa sekta ya umma, uwajibikaji, na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma. Roho yake ipumzike kwa amani.

Napenda pia kulishukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haswa wajumbe wa Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali kwa kujitolea kupitia taarifa zangu za ukaguzi, na kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa mapendekezo yangu ambayo yanalenga kuhakikisha usimamizi mzuri wa fedha za miradi ya maendeleo ndani ya Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma.

Ningependa kutoa shukrani za kipekee kwa Washirika wote wa Maendeleo na watu wengine wenye nia njema ambao walichangia fedha zao kwa ajili ya kujenga uwezo na rasilimali za kufanyia kazi kuelekea kuzifanya kazi za ukaguzi kisasa.

Nashukuru pia kwa ushirikiano nilioupata toka kwa Maafisa Masuuli wote wa taasisi zilizokaguliwa pamoja na watumishi wao kipindi chote wa ukaguzi.

Kwa kuzingatia changamoto zilizokuwepo katika mwaka wa fedha 2019/20, kufanikisha ukaguzi wa miradi ya maendeleo ni sifa na juhudi za kujitoa kwa dhati kwa watumushi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Napenda kipekee kutambua uchapakazi uliotukuka wa timu yangu ya uongozi na wafanyakazi wote kwa kufanya kazi kwa bidii na kujitolea kwao hasa katika mwaka huu uliokuwa na changamoto kubwa.

Wengine wa kuwashukuru ni pamoja na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, vyombo vya kusimamia sheria ikiwa ni pamoja na TAKUKURU, Taasisi za kitaaluma na sekta pana ya umma inayohusika katika kazi yetu, kwa msaada na ushirikiano wao katika kukamilika kwa ukaguzi wa mwaka huu, na wataalam mbalimbali ambao walishirikiana nasi katika kuongeza ujuzi wa kazi zetu.

Mimi na ofisi yangu tunatarajia ushirikiano utaongezeka kati ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na wadau wetu wote katika kaguzi zijazo.

MUHTASARI

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na Kifungu cha 34 (1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa), ninawasilisha kwako taarifa ya kumi inayohusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020.

Taarifa hii imelenga kuwapatia wadau wetu uchambuzi wa hoja mbalimbali zitokanazo na jumla ya kaguzi 303 za miradi ya maendeleo, ikijumuisha kaguzi za hesabu 290 na kaguzi za kiufundi 13. Kwa ujumla wake, kaguzi hizo zilifanyika kwa watekeleza miradi 104 kutoka kwenye jumla ya taasisi 248 kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2020. Miradi hii kiujumla inafadhiliwa kwa fedha za Serikali ya Tanzania pamoja na Wadau wa Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2019/20, miradi hii ilikuwa na jumla ya kiasi cha Sh. trilioni 3.744, ambapo Sh. trilioni 2.587 zilitumika na kubakiwa na kiasi cha Sh. trilioni 1.157 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020.

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa, kulikuwa na jumla ya mapendekezo 3,126 yaliyotakiwa kutekelezwa kutoka katika taarifa 290 za ukaguzi wa hesabu wa mwaka wa fedha ulioshia tarehe 30 Juni 2020. Kati ya mapendekezo hayo, mapendekezo 1,071, sawa na asilimia 34, yalitekelezwa. Mapendekezo 623, sawa na asilimia 20, yanaendelea kutekelezwa. Mapendekezo 1,024, sawa na asilimia 33, hayakutekelezwa. Mapendekezo 245, sawa na asilimia 8, yamejirudia na mapendekezo 163, sawa na asilimia 5, yamepitwa na wakati. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/20 nimetoa jumla ya hati 290 zilizotokana na taarifa za fedha. Kati ya hizo, 275 ni hati zinazoridhisha na 15 ni hati zenye shaka. Hati nyingine 21 ni zile zinazohusu mifumo ya udhibiti wa ndani, na uzingatiaji wa sheria na kanuni.

Uchambuzi wa hoja zangu umetokana na taarifa za ukaguzi wa hesabu na kaguzi za kiufundi kwenye mwaka wa fedha

2019/20 zikilenga maeneo ya udhibiti na usimamizi wa kifedha, manunuzi, usimamizi wa mikataba, utendaji wa miradi na hoja kuu kutoka kwenye kaguzi za kiufundi zilizofanyika katika miradi ya kimkakati. Baadhi ya hoja kuu zilizoibuliwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Usimamizi wa Bajeti Usioridhisha Sh. Bilioni 82.65

Uchambuzi wangu wa masuala ya fedha umebaini kwamba, usimamizi wa bajeti usioridhisha huchangia sana kuathiri utekelezaji na utendaji wa miradi. Nimebaini kwamba baadhi ya watelekeza miradi walishindwa kumalizia kazi zao mpaka mwisho wa mwaka kutokana na miradi husika kupokea kiasi kidogo cha fedha, kinyume na bajeti iliyopitishwa.

Kwa mfano, nimebaini upungufu Sh. bilioni 55.85 ambazo hazikutolewa kati ya bajeti ya Sh. bilioni 253.87 (ambayo ni sawa na 22%) kwa miradi 11 kwenda kwa watekeleza miradi 144 ambao wapo katika sekta ya Kilimo, Elimu, Nishati na Madini, Afya, Sekta mchanganyiko (Multi sector), Sekta ya kijamii (Social sector) na Sekta ya Maji.

Sababu kubwa zilizopelekea usimamizi wa bajeti usioridhisha ni kuchelewa kutumwa fedha za miradi kutoka Hazina na Washirika wa Maendeleo, kinyume na ilivyoainishwa katika bajeti na mpango kazi wa mwaka wa watekeleza miradi. Washirika wa Maendeleo hushindwa kutuma fedha kwa wakati kutokana na watekeleza miradi kushindwa kutuma taarifa zinazohitajika na Wadau wa Maendeleo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi kwa wakati. Sababu nyingine ni pamoja na changamoto zilizotokana na utekelezaji wa Waraka wa Hazina Na. 2 wa Septemba 2019 unaohusu utaratibu wa kuomba na kuhamisha fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwenda kwenye miradi ya maendeleo.

Aidha, nimebaini watekeleza miradi 13 wamefanya matumizi ya kiasi cha Sh. bilioni 26.54 nje ya bajeti na mpango wa kazi wa mwaka 2019/20. Sekta ya Elimu ndiyo

ilikuwa na kiwango kikubwa cha matumizi yaliyo nje ya bajeti, (Sh. bilioni 25.62). Hali hii ilisababishwa na upungufu wa rasilimali fedha kuendeshea shughuli za kawaida za miradi ambazo hazikuwa zimejumuishwa katika bajeti kutokana na upangaji usioridhisha wa shughuli za miradi.

Ninapendekeza: (a) Watekelezaji wa miradi kuwasiliana na Washirika wa Maendeleo, ikiwamo Serikali ya Tanzania kupitia Hazina, juu ya kutolewa kwa fedha za kutosha kwa ajili ya miradi zinazolingana na bajeti zilizopangwa ili kuhakikisha miradi hii inakamilika. Hii ni kwa kuzingatia kuwa miradi hii mingi ina muda maalumu wa kukamilishwa; (b) Watekelezaji wa miradi kuhakikisha mipango ya shughuli za miradi inaandaliwa kwa usahihi na kuhakikisha shughuli zote zilizopangwa zinatekelezwa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa.

(ii) Kutokulipwa kwa Madeni ya Wakandarasi Sh. Bilioni 81.52

Ukaguzi wangu kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2020, umebaini kutokulipwa kwa madeni ya wakandarasi yapatayo kiasi cha Sh. 81,520,228,140.06 kutoka kwenye miradi inayotekelezwa katika sekta ya elimu na usafirishaji.

Nilibaini kuwa kutokulipwa kwa madeni ya wakandarasi hawa kulisababishwa na Wizara ya Fedha na Mipango kuwapatia fedha pungufu watekelezaji wa miradi. Kutowalipa wakandarasi kwa wakati kunaweza kusababisha ongezeko la deni la wakandarasi kwa Serikali kutokana na tozo ya ucheleweshaji malipo ambayo inaweza kufanya miradi hii kusimama au kutokamilika, hivyo kuwanyima wananchi kufaidika na miradi hii kama ilivyokusudiwa. Madeni ya wakandarasi yapo kwenye miradi inayotekelezwa na TAMISEMI, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Wizara ya Madini.

(iii)Tozo Ucheleweshaji wa Malipo – Sh. Bilioni 14.84

Wakati wa ukaguzi nilibaini miradi tisa ilikuwa ikidaiwa tozo ya kiasi cha Sh. bilioni 14.84, ikiwamo miradi saba iliyopo katika sekta ya usafirishaji iliyokuwa ikidaiwa tozo ya Sh.

bilioni 11.61 kutokana na adhabu ya kuchelewesha malipo ya madai ya wakandarasi. Hii ni kinyume na kifungu 51.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kinachosema kuwa "Mkandarasi anapaswa kulipwa madai yake ya kazi ndani ya siku 28 baada ya hati zake za madai kuthibitishwa na Meneja wa Mradi".

Uchambuzi wangu unaonesha sehemu kubwa ya deni la tozo hii imetokana na miradi ifuatayo: mradi wa Reli ya Kisasa kwa sehemu ya 1 na 2 kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora unaotekelezwa na Shirika la Reli Tanzania Sh. bilioni 2.98, Programu ya Kusaidia Maendeleo ya Usafirishaji Sh. bilioni 3.47, Mradi wa Maendeleo ya Reli Tanzania Sh. bilioni 2.2, Mradi wa Kimataifa wa Barabara Arusha – Holili/Taveta – Voi Sh. bilioni 1.85, na Mradi wa Uboreshaji wa Usafiri Mijini Sh. bilioni 0.67. Miradi mingine ni pamoja na Mradi wa Barabara wa Mabasi Yaendayo Haraka Sh. bilioni 0.14 na Mradi wa Upanuzi wa Barabara ya Morogoro Sh. bilioni 0.30.

Pia, ukaguzi wangu umebaini tozo kiasi cha Sh. bilioni 3.1 za Mradi wa Kusambaza Maji wa Same-Mwanga-Korogwe, na kiasi cha Sh. bilioni 0.13 kwenye Mradi wa Kimataifa wa Kuunganisha Nishati wa Kenya na Tanzania (KTPIP).

Uchelewaji wa Wizara ya Fedha na Mipango kutuma fedha kwa wakati kwa Wakala wa Barabara na Shirika la Reli Tanzania kwa wakati ndio unachangia Wakala wa Taifa wa Barabara (TANROADS) na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kushindwa kuwalipa wakandarasi. Ni mtazamo wangu kuwa, ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi sio tu unapelekea miradi isikamilike kwa wakati, bali huchangia pia kuongezeka kwa gharama za mradi, kinyume na makadirio ya awali.

Ninapendekeza watekelezaji wa miradi kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kutoa fedha za kutosha za miradi kulingana na bajeti ambazo zitawawezesha watekelezaji wa miradi kulipa madai ya wakandarasi kwa wakati.

(iv) Kuchelewa kwa Malipo ya Motisha na Gharama za Kiutawala Sh. Bilioni 91.65

Nimepitia taarifa za utekelezaji na nyaraka nyingine za Programu ya Kuimarisha Afya ya Msingi kwa Matokeo inayotekelezwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na kubaini kuwa, malipo ya motisha na gharama za kiutawala, kiasi cha Sh. Bilioni 91.65 hazijalipwa kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Taasisi za Afya. Deni la malipo hayo lilitegemewa kulipwa kabla ya tarehe 30 Juni 2020. Hata hivyo, mpaka wakati wa ukaguzi wangu mwezi Novemba 2020, deni hilo lilikuwa bado halijalipwa. Hii ni kinyume na kifungu 1.2 na 3.18 cha Mwongozo wa Utendaji wa Ufadhili Kutokana na Matokeo.

Tatizo hili la malipo limesababishwa na kutokufuata taratibu na kanuni kama zinavyoainishwa na Mwongozo wa Utendaji wa Ufadhili Kutokana na Matokeo. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ofisi ya Rais TAMISEMI wamekuwa hawasimamii kwa umakini taratibu kama zinavyoininshwa katika Aya 1.2 ya Mwongozo wa Ufadhili kwa Matokeo (*Result Based Financing*). Hali hii inaweza kupelekea kupungua kwa morali ya wafanyakazi kwenye kutekeleza majukumu yao na kuathiri kufikiwa kwa malengo ya programu yaliyokusudiwa.

Nashauri menejimenti ya Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa pamoja kuhakikisha malipo ya motisha na gharama za kiutawala yanafanyika kwa wakati kwa watekelezaji wa Programu ya Mfumo wa Ufadhili kwa Matokeo.

(v) Mkandarasi Kulipwa Sh. Milioni 704.16 kwa Kazi Ambayo Hakuifanya

Wizara ya Madini iliingia mkataba Na. ME/008/SMMRP/W/12 na SUMA JKT (mkandarasi) kwa ajili ya uboreshaji wa ofisi

za madini kwenye miji ya Bariadi, Musoma na Bukoba kupitia mkataba wa thamani ya Sh. 3,601,151,671.

Nilipitia makabrasha ya mikataba na hati za malipo na kubaini kuwa, mhandisi mshauri (M/S Sky Architects Consultants) alilipwa jumla ya Sh. 735,314,131.69 kupitia cheti cha malipo namba 3 cha tarehe 14 Desemba 2018 kwa huduma yake kwenye ujenzi wa uboreshaji wa ofisi tajwa hapo juu. Aidha, nilibaini kuwa malipo mengine ya kiasi cha Sh. 704,155,443.20 yalifanyika kwa kutumia cheti cha malipo namba 3 ambacho kilitumika kufanya malipo ya awali kwa huduma ambayo ilikuwa bado haijafanywa na mhandisi mshauri. Malipo haya kwa kazi ambayo haikufanyika ni kinyume na Kanuni Na. 243 (2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (iliyorekebishwa mwaka 2016) ambayo inaelekeza kwamba, malipo yafanyike baada ya kuthibitishwa na kujiridhisha kiwango cha kazi iliyofanyika kama itakavyooneshwa na mkataba husika.

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Madini kuhakikisha mhandisi mshauri arejeshe kiasi cha fedha kilicholipwa kwa kazi ambayo haijatekelezwa.

(vi) Kukosekana kwa Mpango Mkuu wa Kina wa Jiji *(Detailed City Master Plan)* Kumepelekea Ongezeko la Gharama Kiasi cha Sh. Bilioni 28.05 (Bila VAT) kwenye Mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT)

Kifungu kidogo cha 7 cha kifungu 5.1 cha Mapitio ya Muundo na Huduma za Awali za mkataba kwenye mradi wa BRT, awamu ya pili, kinamtaka mhandisi mshauri kupitia kiundani taarifa za usanifu wa kiuhandisi, ikijumuisha taarifa za muundo, ramani na michoro. Pia, kinamtaka kuhakiki usahihi wa taarifa za data za utafiti eneo la mradi, zikiwamo taarifa zilizopita (kama zipo). Vilevile, kinamtaka kuboresha taarifa za kina za usanifu wa kina.

Ukaguzi wangu wa taarifa mbalimbali za mradi umebaini kutofanyika kwa mapitio ya upembuzi yakinifu ya mradi wa BRT tangu kufanyika kwa upembuzi wa awali mwaka 2015

kutokana na kutokuwapo kwa taarifa zinazohusu miundombinu (kama barabara na reli) kwenye mipango ya serikali. Hali hii ilisababisha mabadiliko ya makadirio na muundo kwenye awamu ya pili, ilihali mradi ukiwa kwenye hatua ya juu ya utekelezaji. Mabadiliko hayo yalisababisha kutengeneza daraja la reli la juu kwenye barabara ya bandari ili kuruhusu reli ya SGR kupita kwa urahisi katika eneo hilo na hivyo kupelekea kuongezeka gharama ya mradi kwa kiasi cha Sh. 28,047,114,893.02. Mabadiliko haya yalipitishwa kupitia mabadiliko ya kwanza ya mkataba.

Mabadiliko haya yalitokana na kutokuwepo kwa Mpango Mkuu wa Kina wa Jiji *(Detailed City Master Plan)* kwa miaka zaidi ya 10 tangu usanifu wa ujenzi wa mradi ulipoandaliwa. Mpango Mkuu wa Kina wa Jiji ulitakiwa kuandaliwa na Wizara ya Ardhi.

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa kushirikiana na menejimenti ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kuimarisha ushirikiano kati ya sekta mbalimbali na taasisi husika wakati wa kuandaa Mpango Mkuu wa Kina wa Jiji ili kuhakikisha kuna ujumuishaji wa kutosha ili kupunguza mabadiliko ya usanifu na ongezeko la kazi za ziada.

(vii) Uwezekano wa Kuwa na Msongamano wa Magari kwenye Makutano ya Barabara Kituo Kikuu cha Mabasi ya Mikoani cha Mbezi Mwisho Kutokana na Kituo Hicho Kujengwa Nje ya Mpango wa Ujenzi wa Barabara

Nilibaini ujenzi wa kituo cha mabasi unakinzana na lengo la mradi huo la kupunguza msongamano katika eneo hilo. Ujenzi wa kituo cha mabasi ya mikoani cha Mbezi Mwisho ulianzishwa ilihali utanuzi wa barabara ya Morogoro unaendelea, hivyo kutokuwepo wakati wa usanifu wa mradi. Hii imeathiri lengo la kupunguza utumiaji muda mrefu katika eneo husika. Pia, shughuli za kituo cha mabasi zinaweza kusababisha msongamano wa magari na kuwa na muingiliano katika makutano barabara ya Morogoro kutokea kituo cha mabasi. Kituo kinakadiriwa kuhudumia mabasi 700 kwa siku. Wakati Wakala wa Barabara

inapanga upanuzi wa barabara ya Morogoro, OR-TAMISEMI kupitia Manispaa ya Dar es salam ilikua inapanga ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Mbezi Mwisho. Mipango hii miwili haikuratibiwa kwa pamoja. Ukosefu wa mpango jumuishi wa sekta na taasisi husika ndiyo chanzo kikuu cha kasoro hizi.

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara kuwasiliana na Mamlaka za Manispaa za Mji husika ili kutafuta njia bora ya kutatua changamoto hii ili kupunguza msongamano wa magari ambao unaweza kujitokeza katika kuendesha kituo kipya cha mabasi cha Mbezi Mwisho.

(viii) Matatizo ya Ubora Kwenye Tabaka la Zege Lililojengwa Kwenye Njia ya Mabasi Yaendayo Haraka

Kwa mujibu wa michoro na miongozo ya viwango vya ubora, tabaka la zege kwa ajili ya njia ya mabasi yaendayo haraka lilitakiwa kuwa na unene wa milimita 220, upana wa mita 3.5 kwa tabaka la saruji la C1 na tabaka lililoboreshwa la udongo kiwango cha G15. Nilibaini barabara kuwa na nyufa kati ya kilomita 6.40 hadi 8.91.

TANROADS iliamua kuchunguza sababu ya kushindwa kufikia ubora. Kwa mujibu wa taarifa ya uchunguzi, sababu kuu za kasoro hizo kwenye barabara ya zege zilihusishwa na usafirishaji duni wa zege kutoka kwenye sehemu inayohusika na uzalishaji hadi mahali pa kazi. Kutoka sehemu ya uzalishaji, zege lilisafirishwa kwa gari kubwa. Kisha katika sehemu ya kazi, zege lilibebwa kwa mtambo wa kuchimbia miundombinu na kuweka kwenye mtambo wa kusambaza zege. Hivyo, taratibu za ubebaji huu wa zege zilisababisha kutengana kwa zege. Sababu nyingine zilizohusishwa na zege hilo kutoa nyufa zilijumuisha: mkandarasi kutotoa kwa kiwango cha kutosha udongo wa mfinyanzi na uchafu uliotokana na masalia ya mimea katika mchanga. Hii ilisababisha idadi kubwa ya mashimo kwa juu na ndani ya barabara ya zege. Sababu nyingine ni kwamba, mkandarasi kutobeba kwa kiwango cha kutosha vifaa vya ujenzi (mchanga, kokoto, saruji na zege) kutoka sehemu vifaa vilipokusanywa ili kuhifadhiwa (mchanga, kokoto) hadi sehemu ya kumwaga zege. Hii ilisababisha mchanganyiko

usiofanana wa zege ambao baadaye ukatengeneza nyufa. Uchunguzi ulibaini kwamba, mkusanyiko wa vifaa vya ujenzi (mchanga, kokoto), utengenezaji wa kokoto za saizi kubwa na ubebaji wa mara kwa mara wa zege safi kabla ya kulimwaga ni sababu kuu zinazohitaji zitatuliwe.

Aidha, nilibaini aina za nyufa zilizoenea upana wote wa barabara pasipo kuthibitika ni za aina moja. Vilevile, zilibainika nyufa zilizozama ndani kati ya maungio ya kuruhusu kutanuka. Ukaguzi ulibaini hali hii ilitokana na kuchelewa kukatwa kwa maungio. Hata hivyo, nilibaini kwamba, Wakala wa Barabara hakuchukua hatua kali na stahiki kwa mkandarasi licha ya matatizo ya ubora yaliyojitokeza.

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara: (a) Kuhakikisha mkandarasi anarekebisha sehemu zote zilizobainika kuwa na ubora duni kabla hajaweka tabaka la kudumu la zege; (b) Kuchukua hatua kali kwa mkandarasi kwa kazi zote zilizofanyika chini ya kiwango.

(ix) Mapungufu Kwenye Mpango wa Ununuzi wa Mradi wa Upanuzi wa Barabara ya Morogoro

Usanifu na makabrasha ya zabuni kutotayarishwa kiusahihi kutokana na makadirio ya vifaa na gharama kutojumuisha masuala yafuatayo: fidia ya ardhi; ujenzi wa ofisi ya mhandisi; udhibiti wa usambaaji wa UKIMWI na magonjwa ya zinaa pamoja na gharama za kuhamisha miundombinu ya huduma iliyo kwenye barabara. Kwa mfano, kutengwa kwa kiasi cha Sh. Milioni 10 kwa kampeini ya UKIMWI wakati kiasi sahihi kilikua Sh. Milioni 100 na Sh. Milioni 200 kwa ajili ya kuhamisha miundombinu kilitarajiwa kutumika ilihali kiasi cha zaidi ya Sh. Bilioni 6 kilitumika.

Bajeti ya zabuni ya mradi huu ilikuwa Sh. bilioni 170. Kiasi hiki kinahitaji utaratibu wa manunuzi wa Zabuni wa Ushindani wa Kimataifa (ICT). Hata hivyo, utaratibu wa ununuzi uliotumika ni wa Zabuni ya Ushindani wa Kitaifa (NCT) ambao ukomo wake ni wa zabuni zenye thamani ya hadi Sh. bilioni 15. Hii ni kinyume na Ibara ya Saba ya Kanuni ya 151 (c) ya Tangazo la Serikali Na. 446 ya mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016).

Kushindwa kutumia zabuni ya ushindani wa kimataifa kunainyima serikali faida ya kupata ushiriki mpana wa zabuni, ikiwa ni pamoja na kupata bei ya ushindani na fursa ya kupata teknolojia mpya kutoka kwa wazabuni wa nje.

Nimepitia makabrasha ya uchambuzi wa zabuni na kubaini kuwa, vigezo vya uchambuzi wa zabuni havikujumuisha taarifa za uzoefu wa mkandarasi, vifaa, ujuzi na uzoefu wa wafanyakazi, makadirio ya chini ya kipato kwa mwaka, na uwezo wa kifedha. Hii ilisababishwa na makosa ya TANROADS kutopitia kwa kina makabrasha ya zabuni wakati wa uandaaji na kupelekea ugumu kwa timu ya uchambuzi wa zabuni kufanya upembuzi sahihi wa uwezo wa mkandarasi.

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara kuboresha mfumo wake wa kudhibiti ubora katika usimamizi wa ununuzi ili kuhakikisha kuwa kila hati inakaguliwa kwa uangalifu kabla ya kupelekwa kwa hatua zingine za uamuzi.

(x) Mapungufu kwenye Menejimenti ya Muda wa Kutekeleza Mradi wa SGR

Tathmini ya maendeleo ya mradi wa SGR umebaini hadi kufikia Desemba 2020 utekelezaji wa kazi 'Lot 1' upo 88.39% ikiliganishwa na makisio ya 95.96%, ambapo 'Lot 2' ni 52.2% ikilinganishwa na makisio ya 98.7%. Maendeleo ya ujenzi wa SGR yasiyoridhisha yamesababishwa na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchelewaji wa ukusanyaji wa vifaa kwa 'Lot 1 na 2'; uchelewaji wa ujenzi wa maeneo muhimu makuu; na uchelewaji wa kuanza shughuli za usanifu na ujenzi wa kilomita 3 'Port Link'.

Ninapendekeza Shirika la Reli kuongeza juhudi kwenye usimamizi wa mikataba ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kwa kutatua changamoto zote za kimkataba ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyopangwa kwa wakati kulingana na matakwa ya mikataba.

(xi) Usimamizi Hafifu wa Rasilimali Watu kwenye Mradi wa SGR Awamu ya Kwanza na ya Pili

Mapitio yangu ya taarifa ya utekelezaji wa mradi wa SGR ya mwezi Novemba 2020 yamebaini kuwa, kiasi cha wafanyakazi wa kigeni 586 kati ya 924 na wafanyakazi 952 kati ya 1,484 kutoka kwenye awamu ya kwanza na ya pili ya mradi hawakuwa na vibali vya kufanya kazi nchini Tanzania. Aidha, hali hii pia imepelekea kutokulipwa serikalini kiasi cha Dola za Marekani 1,538,000, sawa na Sh. 3,537,400,000, kama gharama za vibali vya kazi. Pia, nimebaini jumla ya wafanyakazi wa kigeni 1,026 wanaofanya kazi kwenye mradi huu bado hawajasajili vyeti vyao vya kitaaluma. Kati yao, 83%, wamewekwa pembeni kutokana na kukosa vyeti halisi. Wafanyakazi hao bado wanavisubiri vyeti vyao ambavyo bado vipo kwenye mchakato wa kusajiliwa nchini Uturuki.

Aidha, nimebaini wafanyakazi watano (mhandisi wa udhibiti ubora, mhandisi wa miamba, mhandisi wa michoro sanifu, mhandisi msanifu wa njia, na daktari wa binandamu) kwenye awamu ya kwanza ya mradi bado hawasajiliwa na bodi za taaluma husika. Hii ni kwa sababu maombi yao bado yapo kwenye mchakato wa kupitiwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Baraza la Tiba Tanganyika. Pia, kwenye awamu ya pili ya mradi nimebaini jumla ya wafanyakazi 272 bado hawajasajiliwa na bodi husika za taaluma zao. Wafanyakazi hao wanajumuisha: madaktari watatu wa binadamu, wahandisi 72 na wataalamu 197 kutoka kada mbalimbali.

Ninapendekeza menejimenti ya Shirika la Reli: (a) Kuweka mfumo wa udhibiti ambao utazuia ajira kwa watu wasio raia wa Tanzania ambao hawana kibali halali cha ajira na matakwa mengine ambayo ni muhimu; na (b) Kuimarisha mfumo wa utekelezaji wa mafunzo na programu za ujengeanaji uwezo kwa ufanisi na kwa wakati.

(xii) Hasara ya Sh. Milioni 379.34 Kutokana na Kuharibika kwa Miwa Kwenye Shamba la Miwa Mbigiri na Uwezekano wa Kupoteza Thamani ya Fedha Sh. Milioni 499.93 kwenye Shamba la Miwa Mtibwa

Ukaguzi wangu ambao umehusisha kutembelea eneo la mradi tarehe 20 na 24 Novemba 2020 umebaini kuwa, miwa

ambayo ilipitiliza muda wake wa kuvunwa kwenye mradi wa shamba la miwa Mbigiri iliharibiwa na kusababisha hasara inayokadiriwa kufikia kiasi cha Sh. 379,338,245. Mahojiano yangu na menejimenti yameonesha kuwa miwa hiyo iliharibiwa kutokana na kutokuwepo kwa mashine za kuichakata ambazo zilitakiwa kuwa zimeshasimikwa kufikia Desemba 2020. Hii ni kutokana na mpango mkakati wa Kampuni Hodhi ya Mkulazi (MHCL) wa mwaka 2019/20 mpaka 2023/24.

Aidha, mapitio yangu ya taarifa mbalimbali yamebaini kuwa Kampuni Hodhi ya Mkulazi (MHCL) na Kampuni ya Sukari Mtibwa ziliingia makubaliano mnamo tarehe 17 Septemba 2020 kwa ajili ya uvunaji wa miwa iliyopitiliza muda wa kuvunwa. Ilipangwa kuwa miwa hekta 740.43 ivunwe kwa mwaka kwenye msimu wa Septemba 2020 mpaka Februari 2021, lakini MHCL ilifanikiwa kuvuna hekta 318 ambazo ni sawa na 43% ya makadirio ya uvunaji yaliyopangwa awali. Nilibaini kuwa, ifikapo Februari 2021 miwa hii itakuwa na umri wa miezi 30, hivyo itakuwa haifai kuvunwa hivyo inakadiriwa kuweza kuleta hasara ya kiasi cha Sh. 499,934,750.

Napendekeza Kampuni Hodhi ya Mkulazi iharakishe ununuzi na usimikaji wa kiwanda cha uzalishaji sukari katika shamba la Mbigiri.

(xiii) Mapungufu kwenye Uandaaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Mradi wa Maji Same-Mwanga na Korogwe

Ukaguzi wangu wa Mradi wa Maji Same-Mwanga umebaini kuwa mpango wa utekelezaji wa mradi haukuandaliwa vizuri. Hii ilipelekea mapungufu kwenye utabiri wa mahitaji ya kiwango cha maji, miundombinu ya maji, uandaaji wa makabrasha ya zabuni na taratibu za ununuzi kwa ujumla. Mathalani, mapitio ya Taarifa ya Usanifu na Ufuatiliaji yamebaini kuzidishwa kwa makadirio ya ukuaji wa wakazi kwa 37%, ambapo pia iliongeza mahitaji ya maji kwa kiasi cha mililita za ujazo 40,891 (*40,891*m^3). Hii ilitokana na makadirio ya mradi kutokuwa sahihi kwenye idadi ya

wakaazi wa wilaya za Same, Mwanga na Korogwe ambapo walikadiriwa kufikia watu 456,930 kufikia mwaka 2038. Hii ni kinyume na makadirio ya wakaazi 287,989 kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Makosa haya kwenye makisio yameongeza gharama za usimikaji wa mabomba na pampu kwa kiasi cha Dola za Marekani 5,388,514. Aidha, nimebaini tofauti ya mwendo na muda wa kutibu maji, ambapo inaongeza hatari ya maji yanayotibiwa kutokuwa salama. Makadirio yanaonesha kuwa, maji yanatakiwa kutibiwa kwa dakika 20 kwa mwendo wa mita 0.5 kwa sekunde, ilihali hali halisi imeonesha kuwa maji yanatibiwa kwa dakika 13.23 kwa mwendo wa mita 0.052 kwa sekunde.

Naishauri menejimenti ya Wizara ya Maji: (a) Ipitie upya makisio yake ya mahitaji ya maji kuendana na idadi ya makadirio ya watu ili kuepuka uwezekano wa kuongeza au kupunguza makadirio ya mahitaji ya pampu na mabomba kwa ajili ya kuondoa uwezekano wa kuongezeka kwa gharama za mradi; na (b) Ifanye upembuzi wa haraka ili kuunda mtambo wa uhakika wa kutibu maji kwa ajili ya kuzuia uwezekano wa mafuriko kwenye kituo cha awali cha kusukuma maji na kuchakata uzalishaji wa maji safi. Nashauri hii ifanyike kabla ya kutafuta mkandarasi mpya ili kuepusha uwezekano wa migogoro kwa wakati ujao.

(xiv) Mapungufu kwenye Kufuata Taratibu za Ununuzi kwenye Kutekeleza Mradi wa Maji Same-Mwanga na Korogwe

Mapitio yangu ya makabrasha ya ununuzi yamebaini mapungufu yafuatayo: makabrasha ya zabuni hajaandaliwa vizuri kutokana na wazabuni kutakiwa kutengeneza bei ya dhamana, baadhi ya vipengele vimerudiwa mara mbili kwenye makadirio ya gharama za vitu, na kukosekana kwa uwazi kwenye makadirio ya vifaa vya awali. Mapungufu haya yote yamepelekea ongezeko la gharama za mkataba kwa kiasi cha Sh. 4,081,939.

Aidha, nimebaini mapungufu kwenye kufuata taratibu za ununuzi. Mathalani, ukosefu wa kumbukumbu za ununuzi zinazohusiana na wakandarasi na wahandisi washauri, kutokufuata taratibu za mikataba, kufanyika marekebisho kwenye nyaraka za zabuni na michoro pasipo kufuata taratibu, pamoja na kutofuata taratibu za kiununuzi na kimkataba kati ya mradi, wakandarasi na wahandisi washauri.

Mapungufu haya yameathiri ubora wa kazi, kusababisha migogoro ya kimkataba, mabadiliko ya kazi za kimkataba, na kuchelewa kumalizika kwa utekelezaji wa mkataba. Mathalani, bei za mabomba (DI pipes) zimepanda kwa kiasi cha Dola za Marekani 504,435.92 kutokana na kutokadiriwa vizuri kwenye hatua za awali za kutengeneza makadirio ya zabuni. Pia, nilibaini makosa yaliyofanyika wakati wa uchambuzi wa zabuni pasipo kuwa na sababu zilizothibitishwa. Makosa hayo yalikuwa na thamani ya kiasi cha Dola za Marekani 2,020,367, sawa na Sh. 445,000,000.

Naishauri Wizara ya Maji: (a) Ihakikishe kwamba makadirio ya kiasi na gharama za vifaa yanapitiwa kwa umakini ili kuepuka uwezekano wa kuzidishwa kwa bei za vifaa; na (b) Iwasilishe nyaraka za manunuzi kwa ajili uhakiki.

(xv) Kuchelewa Kumalizika kwa Muda Mikataba ya Mradi wa Maji wa Same-Mwanga na Korogwe

Ukaguzi wangu uliopitia makabrasha ya mikataba umebaini kuwa mikataba miwili inayohusiana na mradi huu (mikataba Na. I na IV) haijakamilishwa ndani ya muda uliokubaliwa kwenye mikataba hiyo; ambapo, mkataba Na. I ulichelewa kumalizika kwa muda wa siku 1,253 na mkataba Na. IV ulichelewa kumalizika kwa muda wa siku 509 mpaka kufikia Desemba 2020. Ucheleweshaji huu umesababisha gharama za ziada kwenye mkataba katika maeneo ya: gharama za awali na usimamizi - Dola za Marekani 2,584,257.17 (sawa na 43.45% ya gharama jumla ya mkataba), usimamizi - Dola za Marekani 906,947.44 (sawa na 210% ya gharama jumla ya

mkataba), na gharama za awali Sh. 1,175,019,439.70 (sawa na 931%). Aidha, nimebaini kulikuwa na makadirio ya chini ya muda wa usimamizi wa mkataba yaliyosababisha kuongezeka kwa gharama hizo kwa kiasi cha Sh. 1,770,750,000.

Naishauri menejimenti ya Wizara ya Maji iongeze usimamizi wakati wa kutekeleza mikataba ili kuhakikisha kazi zinazotekelezwa kwenye mkataba zinamalizika ndani ya wakati uliokubalika.

(xvi) Mapungufu Kwenye Menejimenti na Idadi ya Watumishi Katika Utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Same-Mwanga na Korogwe

Mapitio yangu ya Idara za Wizara ya Maji zinazotekeleza Mradi huu yamebaini upungufu wa wafanyakazi 52 (sawa na 76%) ikilinganishwa na idadi iliyokadiriwa ya wafanyakazi 68. Aidha, katika Idara ya Ununuzi (PMU) kulikuwa na upungufu wa wafanyakazi watatu, na upungufu wa wafanyakazi wanne katika Idara ya Ukaguzi wa Ndani.

Aidha, nimebaini kuwa Wizara ya Maji haikuwapeleka kwenye mafunzo wafanyakazi wake tangu mwaka 2018. Pia, bado haijandaa mpango wa kuwaendeleza wafanyakazi wake, hasa kwenye maeneo yenye wafanyakazi wa kigeni au yanayohitaji utaalamu wa kigeni. Kuwapo kwa mpango wa kuwaendeleza wafanyakazi kungesaidia Serikali kupunguza gharama za fedha na muda za kuleta wataalamu kutoka nje ya nchi.

Hivyo, naishauri Wizara ya Maji izingatie yafuatayo: (a) Kutatua tatizo la upungufu wa wafanyakazi kwenye maeneo ya wataalamu, kitengo cha ukaguzi wa ndani, na kitengo cha menejimenti ya manunuzi; (b) Kuboresha programu za mafunzo na kuendeleza wafanyakazi; (c) Kuandaa mpango endelevu wa wafanyakazi wataalamu watakaoziba pengo pindi wale waliopo wakiondoka; (d) Kuteua meneja na meneja msaidizi wa mradi; (e) Kuhakikisha kwamba madai ya watumishi yanalipwa kwa

wakati; (f) Kuhakikisha wataalamu kutoka nje wanakabidhi vibali vyao vya kazi bila ya kuchelewa zaidi; (g) Kuhakikisha kwamba mtendaji mkuu mwingine anaajiriwa kwa ajili ya mikataba namba III na IV; na (h) Kuhakikisha wakandarasi wanawasajili wafanyakazi wao katika bodi husika za kitaaluma.

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI NA HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MWAKA ULIOPITA

Sehemu hii ya kwanza inajumuisha Sura ya Kwanza na ya Pili, ambazo ni Utangulizi na Usuli wa Miradi Iliyokaguliwa na Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya kaguzi za miaka ya nyuma, mtawalia.

Sura ya Kwanza inawasilisha historia, lengo la bajeti ya miradi ya yaendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/20, aina za ukaguzi uliofanywa, na maelezo ya msingi ya miradi ya maendeleo iliyokaguliwa na kupangwa kwa kisekta. Inazungumzia pia majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Maafisa Masuuli, mawanda ya ripoti ya jumla na mbinu zinazotumika katika kufanya kaguzi hizi.

Sura ya Pili inawasilisha utangulizi na utekelezaji wa hali ya mapendekezo ya mwaka uliopita pamoja na uchambuzi wa mwenendo wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka mitano.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI NA USULI WA MIRADI

1.1 Utangulizi

Mpango wa miaka mitano wa Maendeleo ya Taifa awamu ya pili (FYDP1I) 2016/17-2020/21 unaelezea hatua mpya za kuwezesha Tanzania ya viwanda kwa njia ambayo itabadili uchumi na jamii. Kuna maeneo manne yaliyopitishwa katika mpango huu, ambayo ni ukuaji na uanzishaji wa viwanda; kukuza maendeleo ya watu na mabadiliko ya kijamii; kuboresha mazingira kwa ajili ya maendeleo ya biashara; na kuwa na utekelezaji sahihi. Kwa kuzingatia hatua hizi, Serikali imekuwa ikianzisha na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Sura hii inaonesha mwelekeo wa bajeti ya mwaka 2019/20 kwenye miradi ya maendeleo, aina za miradi inayotekelezwa, historia ya undani wa miradi ya maendeleo (kwa mpangilio wa kisekta) wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za serikali, wajibu wa Maafisa Masuuli, madhumuni na mawanda ya taarifa kuu, mbinu zilizotumiwa kufanya kaguzi, na muundo wa taarifa hii.

1.2 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/20

Katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, ilitengeneza makisio ambayo yanasaidia utelelezaji wa miradi ya maendeleo kulingana na maeneo manne yaliyopitishwa katika Mpango wa Maendeleo awamu ya pili. Serikali pia imejikita katika utekelezaji wa miradi ya vielelezo *(flagship projects)* katika sekta ya Nishati, Uchukuzi na Maji. Mifano ya miradi hii ni Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, Reli ya Kisasa (SGR), Mradi wa Maji wa Same-Mwanga na Korogwe, pamoja na miradi mingine ambayo haijatajwa hapa.

Kutokana na bajeti hii, Serikali ilipanga kukopa shilingi trilioni 4.96 kutoka soko la ndani. Kati ya hizo, shilingi trilioni 3.46 zilipangwa kulipia hati fungani na dhamana zilizoiva na shilingi trilioni 1.50, sawa na asilimia 1.0 ya Pato la Taifa (GDP), zilijumuisha mikopo mipya ya kufadhili miradi ya maendeleo. Ili

kuharakisha utekelezaji wa miradi ya miundombinu, Serikali ilipanga kukopa Shilingi trilioni 2.32 kutoka katika vyanzo vya mikopo ya kibiashara iliyo na masharti nafuu.

Katika kuhakikisha kuwa fedha zinazopatikana zinatumika kama ilivyokusudiwa, Serikali imejitolea kuendelea kusimamia utararibu unaotakiwa katika matumizi ya fedha za umma na kufanya ufuatiliaji na tathmini, hasa kwenye miradi ya maendeleo. Lengo kuu ni kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana.

Sambamba na bajeti hii, ofisi yangu ilifanya ukaguzi wa kifedha na kiufundi juu ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Taasisi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/20. Lengo ni kuijulisha serikali, washirika wa maendeleo, raia na wadau wengine juu ya utendaji wa miradi hii na kushauri ipasavyo juu ya njia bora ya kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

1.3 Aina za Kaguzi

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilifanya kaguzi wa aina mbili kwenye miradi ya maendeleo ambayo ni ukaguzi wa fedha na ufundi. Nimetoa maelezo kuhusu kaguzi hizi ili wasomaji wa ripoti hii waweze kuelewa sura zinazofuata za taarifa hii.

1.3.1 Ukaguzi wa Fedha

Ukaguzi wa fedha unazingatia zaidi tathmini ya mfumo wa uhasibu, udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa fedha na kufuata sheria na kanuni, ikiwa ni pamoja na ununuzi na mahitaji mengine ambayo yanasimamia shughuli za miradi maalum. Hivyo, chini ya ukaguzi huu, maoni ya ukaguzi hutolewa juu ya taarifa za kifedha. Matokeo ya sasa yanahusiana na udhaifu wa udhibiti wa ndani na kutofuata sheria, kanuni na mahitaji mengine yanayohusiana nayo kama ilivyoainishwa katika makubaliano ya fedha na Mikataba ya makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kifungu 48 (3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 inanitaka kueleza katika taarifa yangu ya ukaguzi ya mwaka ikiwa taasisi iliyokaguliwa imefuata taratibu zilizowekwa katika Sheria ya Ununuzi na Kanuni zake.

1.3.2 Ukaguzi wa Kiufundi

Katika miaka ya hivi karibuni Serikali ya Tanzania imekuwa ikijitahidi kukuza shughuli za kijamii na kiuchumi na viwanda nchini ili kuboresha utendaji wa uchumi na Pato la Taifa (GDP), ikilenga kufikia nchi ya kipato cha kati. Katika juhudi hizi, Serikali iliongeza juhudi kwenye uwekezaji wa miradi mikakati mikubwa katika maeneo ya sekta ya nishati (umeme wa maji), sekta ya usafirishaji (barabara, reli, maji na anga), sekta ya maji, na sekta ya afya.

Kama sehemu ya majukumu yangu, ofisi yangu kama mwangalizi wa rasilimali za umma nina wajibu wa kukagua juhudi za Serikali juu ya uwekezaji huu wa kimkakati ili kutoa hakikisho juu ya ugawaji mzuri na matumizi ya rasilimali na uendelevu wa uwekezaji uliofanywa.

Katika mwaka huu wa fedha, nilifanya kaguzi za kiufundi 13[1] kwenye miradi ya ujenzi chini ya sekta za uchukuzi, nishati, maji na kilimo. Niliwasilisha matokeo yaliyopatikana katika kaguzi hizi katika nyanja nne ambazo ni Mipango, Usanifu na Uandaaji wa Zabuni; mchakato wa manunuzi; Afya, Usalama na Mazingira pamoja na Usimamizi wa Utekelezaji wa Mkataba.

1.4 Miradi Iliyokaguliwa

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilikagua miradi 104 iliyotekelezwa na taasisi 248 na ripoti za ukaguzi 303. Kati ya kaguzi 303 ziliofanywa, 290 zilihusisha ukaguzi wa kifedha na 13 zilihusu kaguzi za kiufundi. Muhtasari wa matokeo yaliyotokana na taarifa za ukaguzi yanahusu sekta tofauti ambazo ni: Kilimo, Elimu, Nishati na Madini, Afya, Uchukuzi, Maji, Sekta ya Jamii na zile zinazohusu sekta zaidi ya moja.

---

[1]. Baraza la Kitaifa la Ujenzi (NCC) linafafanua ukaguzi wa kiufundi wa mradi wa ujenzi kama "uchunguzi huru na/au uchunguzi juu ya upangaji, usanifu, ununuzi na utekelezaji wa mradi wa ujenzi, kwa nia ya kuwapa watendaji wakuu na wafadhili uhuru wa kutathmini maswala yote yanayoathiri utendaji wa mradi." NCC ilianzishwa na Sheria ya Bunge Namba 20 ya mwaka 1979 (toleo lililorekebishwa mwaka 2007) ili kuishauri Serikali juu ya mambo yote yanayohusiana na maendeleo ya tasnia ya ujenzi nchini Tanzania.

Sekta ya Kilimo
Serikali imeendelea kuboresha sekta ya kilimo ili kuleta ufanisi mkubwa wa uzalishaji, ukuzaji biashara, uongezaji faida, na uzalishaji wa ziada ili kukidhi soko la ndani na la kimataifa. Katika suala hili, utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kilimo unazingatia sana uanzishaji na uboreshaji wa mifumo ya miundombinu ya masoko, kusaidia kuongezeka kwa tija na uzalishaji wa mazao mbalimbali kupitia ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Pia miradi katika sekta ya kilimo imelenga kutoa zana na vifaa vya kilimo, utoaji wa huduma za ushauri na huduma zisizo za ushauri, uimarishaji wa uwezo kwa taasisi na jamii kwa kutoa mafunzo, pamoja na kusaidia utafiti na programu mbalimbali za kuwatembelea walengwa ili kuhakikisha usalama wa chakula nchini. Katika mwaka huu wa fedha, miradi tisa inayohusiana na Sekta ya Kilimo, ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa kiufundi wa Mradi wa Uzalishaji Sukari ya Mbigiri ilikaguliwa kama inavyooneshwa katika **Jedwali na 3-1.**

Sekta ya Elimu
Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu wa 2016/17 - 2020/21 unakusudia kuongoza mipango ya mageuzi iliyoundwa ili kuleta mabadiliko katika Sekta ya Elimu. Kwa kifupi, inakusudia kuhakikisha maendeleo ya elimu ya msingi na vyuo vikuu, kuweka mkazo katika upanuzi wa elimu ya ufundi na mafunzo, na kuandaa wafanyakazi wenye ujuzi kama sehemu muhimu ya mkakati wa maendeleo ya rasilimali watu nchini. Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilikagua miradi 9 inayohusiana na sekta ya elimu kama inavyooneshwa katika **Jedwali na. 3-2.**

Sekta ya Nishati na Madini
Katika sekta hii ya nishati, serikali ilijitolea kuboresha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo ya vijijini na mijini kupitia uhandisi na kuboresha taasisi ya uzalishaji wa umeme, usafirishaji na usambazaji na kuboresha utendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Kulingana na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili, Serikali ililenga kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme kutoka Megawati (MW) 1,501 iliyokuwepo 2015 hadi MW 4,915 ifikapo 2020. Kwa juhudi hizi ongezeko la

umeme limeboreshwa hadi kufikia asilimia 60 ikilinganishwa na asilimia 36 katika mwaka 2014/15.

Chini ya Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo Awamu ya Pili (FYDP II), sekta ya madini inataka kukuza utengenezaji wa rasilimali ili kuongeza thamani katika madini ya viwandani, madini ya thamani na vito. Ili kufanikisha hili, miradi kadhaa ilitekelezwa katika sekta ya madini inayohusiana na ujenzi wa ofisi za madini za mikoa na kujenga uwezo, chini ya Usimamizi Endelevu wa Mradi wa Rasilimali za Madini na kuingilia kati katika uwazi na uwajibikaji chini ya Taasisi ya Uwazi wa Uwajibikaji Katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania (TEITI).

Katika mwaka wa ukaguzi (2019/20), miradi 19 ilikaguliwa, ambapo 16 inatoka katika sekta ya nishati na mitatu inatoka sekta ya Madini. Katika sekta ya Nishati, nilifanya kaguzi za kiufundi kwenye miradi mitano kati ya miradi 16 iliyotekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania ambayo ni; Mradi wa Kuunganisha Umeme wa Kenya na Tanzania (KTPIP), Mradi wa Upembuzi Yakinifu wa Bwawa la Kikonge, Mradi wa Umeme wa Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo, Mradi wa Uwekezaji wa Miundombinu ya Msingi ya Kusafirisha Umeme (BTIP) na Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Mwalimu Julius Nyerere kama inavyooneshwa katika **Jedwali na. 3-3.**

Sekta ya Afya

Mikakati katika sekta ya afya inazingatia zaidi kuboresha afya na ustawi wa jamii ya Kitanzania kwa kuimarisha mifumo ya kitaifa ili kuongeza utoaji na upatikanaji sawa wa huduma bora za afya kwa wote. Miradi iliyoanzishwa na Serikali katika sekta ya afya inazingatia sana kuboresha ubora wa huduma za msingi za afya kitaifa kwa kuzingatia huduma za mama, mtoto mchanga na afya ya watoto kwa ujumla. Pia, huzingatia kujengea uwezo Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa juu ya masuala muhimu yanayotokea katika sekta ya afya. Zaidi, husaidia ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya afya, ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vifaa vinavyotumika katika vituo vya afya pamoja na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) katika kuimarisha huduma za afya. Katika mwaka huu wa ukaguzi,

miradi minane ilikaguliwa katika sekta hii kama inavyooneshwa katika **Jedwali na. 3.4.**

Sekta ya Uchukuzi

Chini ya sekta ya uchukuzi, Serikali imejitolea kuboresha miundombinu ya usafirishaji kulingana na Sera ya Kitaifa ya Uchukuzi ya 2011-2025. Kwa kuzingatia hilo, Serikali inaendelea kuboresha viwanja vya ndege, barabara, reli na bandari nchini ili kurahisisha shughuli za kiuchumi na kijamii, ndani na nje. Hivi karibuni, Serikali ilichukua hatua ya kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) ili kudhibiti usafiri wa ardhini, hususani usafirishaji wa mizigo na abiria. Vivyo hivyo, serikali iliendelea na ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) na miradi mingine ya ujenzi wa barabara katika mikoa mbalimbali nchini.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, mbali na kufanya kaguzi za kifedha 12, pia nimefanya kaguzi za kiufundi katika miradi mitano iliyo chini ya sekta ya uchukuzi; ambapo, miradi minne inahusiana na ujenzi wa barabara na mmoja kwenye mradi wa reli. Miradi minne ya ujenzi wa barabara ni pamoja na; Mradi wa Kimataifa ambao unajumuisha uboreshaji wa barabara kutoka Rumonge-Gitaza-Kibondo-Kasulu-Manyovu; Programu ya Usaidizi wa Sekta ya Uchukuzi (TSSP) ambayo ilijumuisha uboreshaji wa Barabara ya Tabora-Koga-Mpanda (km 347) na Mbinga-Mbamba Bay (67 km); Mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo kwa Haraka wa Dar es Salaam; Mradi wa Kupanua Barabara ya Morogoro (Kimara-Kibaha). Kwa upande wa ujenzi wa reli, mradi uliokaguliwa ni Mradi wa Reli Kisasa (SGR). Mchanganuo halisi umeoneshwa kwenye **Jedwali na. 3-5**

Sekta ya Maji

Wizara ya Maji ilikuwa ikitekeleza mabadiliko ya kisekta yenye lengo la kuboresha usimamizi jumuishi wa rasilimali za maji na kuboresha huduma ya maji na huduma za usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini na mijini. Ili kuoanisha malengo ya Dira ya Maendeleo ya Kitaifa ifikapo mwaka 2025, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) ilianzishwa kupitia mwongozo wa Sera ya Kitaifa ya Maji wa mwaka 2002. Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) imekuwa mradi mkubwa katika Sekta ya Maji na miradi mingine inayochangia lengo kuu la

kuboresha usambazaji wa maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini na mijini.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali ilianzisha Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) iliyoanzishwa na Sheria ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Namba 5 ya 2019 kuanzia 1 Julai, 2019. RUWASA inawajibika kwa maendeleo na usimamizi endelevu wa maji, usambazaji na miradi ya usafi wa mazingira na utoaji wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijini.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilikagua miradi minane inayohusiana na Sekta ya Maji. Miradi miwili kati ya hiyo ilihusiana na kaguzi za kiufundi zilizofanyika katika mradi wa Usambazaji Maji wa Same, Mwanga na Korogwe na Mradi wa Uimarishaji Endelevu wa Mifumo ya Maji na Usafi wa Mazingira – Arusha Mjini kama inavyooneshwa katika **Jedwali na. 3-6.**

Sekta ya Jamii

Miradi mikuu inayozungumziwa katika sekta hii ni pamoja na: Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania Awamu ya Tatu (TASAF III) / Mfuko wa Usalama wa Jamii (PSSN) na miradi inayofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia watoto (UNICEF). Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania Awamu ya Tatu (TASAF III) ni sehemu ya Mkakati wa Kitaifa wa Kutokomeza Umaskini ulioanzishwa ili kuziwezesha jamii kupata fursa ambazo zinachangia kuboresha maisha, ikihusishwa na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDG) kama ilivyoelezwa katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini Tanzania (TPRS). Madhumuni yake ni kuunda mtandao kamili wa usalama wa jamii wenye tija, ubora, na unaolengwa kwa watu maskini na walio katika mazingira magumu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi unatekelezwa katika Halmashauri ambazo walengwa ndiko wanapatikana.

Miradi mingine inayofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto (UNICEF) inatekelezwa na Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) ikilenga kuunga mkono Programu ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu,

jinsia, mazingira endelevu, msaada wa afya, maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kujenga uwezo na usimamizi wa program zinazozingatia matokeo.

Katika ukaguzi huu, nilikagua miradi 22 chini ya Sekta ya Jamii, ikiwa ni pamoja na mpango wa Mfuko wa Maendeleo ya jamii awamu ya tatu (TASAF III), miradi nane ya Shirika la Maendelo la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto (UNICEF) na miradi 13 ya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kama inavyoonekana katika **Jedwali na. 3-7 & 3-8.**

Miradi ya Sekta Mbalimbali

Serikali pia inatekeleza miradi yenye shughuli mtambuka katika nyanja mbalimbali kama vile mazingira, utalii, uvuvi, sheria, kujenga uwezo, ulinzi wa watoto na hatua za kuishi na kutokomeza umaskini. Ufadhili wa miradi hii hutoka kwa wafadhili mbalimbali chini ya mipango ya nchi mbili na kimataifa.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilikagua miradi 16 katika sekta mbalimbali kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali na. 3.9.**

1.5 Wajibu wa Maafisa Masuuli

Kifungu Na. 25(2) cha Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2004) kinaelekeza Maafisa Masuuli[2] kuandaa taarifa sahihi za fedha kwa kila mwaka wa fedha zinazoonesha mapato na matumizi ya miradi hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha husika.

Aidha, Maagizo Na. 11, 14 na 31(1) ya Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009, na Mkataba wa Makubaliano baina ya watekelezaji wa miradi na Washirika wa Maendeleo vinawataka wahusika kuhakikisha kwamba, kumbukumbu sahihi za kihasibu za miradi zinatunzwa vizuri. Pia, kuhakikisha mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani katika taasisi unakuwepo.

[2] Maafisa Masuhuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara, Mashirika ya Umma Idara, Wakala wa Serikali na Taasisi nyingine za Serikali

1.6 Wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kifungu Na. 10 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008 kinanitaka nijiridhishe iwapo taarifa za fedha zimeandaliwa kwa misingi ya viwango vya kihasibu, na kwamba tahadhari za kutosha zimechukuliwa kulinda ukusanyaji wa mapato. Aidha, kifungu kinanitaka nijiridhishe iwapo matumizi yote yameidhinishwa na kutumika kwa kusudi lililopangwa kwa mujibu wa sheria na kwamba miongozo na maelekezo husika yamezingatiwa, na iwapo kuna ufanisi katika matumizi ya fedha za umma.

Pia, Kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma cha Mwaka 2011 kinanitaka katika taarifa yangu nitoe tathmini iwapo taarifa nilizokagua zinakidhi matakwa ya sheria na kanuni zake.

Ripoti hii inatoa muhtasari juu ya masuala yaliyotajwa kutoka kwa ukaguzi uliofanywa kwenye miradi ya maendeleo. Inalenga kusaidia Wadau wakiwemo Wabunge, Serikali, Vyombo vya Habari, Umma na wengine katika kuchukua maamuzi sahihi ili kuboresha utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini.

1.7 Mawanda na Viwango vya Ukaguzi Vilivyotumika

1.7.1 Mawanda ya Taarifa

Taarifa hii inatoa mchanganuo wa hoja za ukaguzi zinazopatikana katika taarifa za kaguzi 303 zinazotokana na taarifa ya kaguzi za kifedha 290 pamoja na kaguzi za kiufundi 13, zilizofanyika katika miradi ya maendeleo 104 iliyotekelezwa na Taasisi za Serikali 248[3] katika mwaka wa fedha 2019/20 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 1.1** ambayo inachambua miradi kisekta. Pia kaguzi sita[4] kati ya kaguzi 13 za kiufundi zililenga mawanda ya ukaguzi yanayojumuisha zaidi ya mwaka wa fedha 2019/20, wakati ukaguzi wa miradi mingine saba ulikuwa na mawanda yanayolenga mwaka wa fedha 2019/20.

[3] Taasisi moja inaweza tekeleza mradi zaidi ya mmoja

[4] Uboreshaji wa Mradi wa Maanguko ya Maji Same Mwanga na Korogwe, Upanuzi wa barabara ya Morogoro(Kimara Kibaha) Reli ya kiwango cha Kisasa (SGR), Mradi wa Bwawa Lakuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere na Mradi wa Uzalishaji Sukar - Mbirigiri

Jedwali 1- 1: Idadi ya miradi iliyokaguliwa kwa sekta katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20

Na.	Sekta	Idadi ya Miradi Iliyokaguliwa	Idadi ya Taasisi Zilizokaguliwa	Idadi ya Taarifa za Ukaguzi
1	Kilimo	9	6	9
2	Elimu	8	2	11
3	Nishati na Madini	19	3	23
4	Afya	8	188	193
5	Usafirishaji	14	6	17
6	Maji	8	6	22
7	Jamii na Miradi Mingine	22	21	44
8	Miradi Mingine	16	16	17
Jumla		**104**	**248**	**303**

Chanzo: *Taarifa za kaguzi za fedha na kiufundi kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2020*

1.7.2 Viwango vya Ukaguzi Vilivyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama wa Jumuiya ya Kimataifa ya Asasi Kuu za Ukaguzi wa Hesabu (INTOSAI) na Jumuiya ya Asasi Kuu za Ukaguzi kwa Nchi za Afrika Zinazozungumza Kiingereza (AFROSAI-E). Hivyo, taratibu zilizotumika zimezingatia viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi kama vile ISSAI vinavyotolewa na INTOSAI na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu na Wakaguzi (IFAC) mtawalia.

Viwango hivi vinanitaka kuzingatia maadili katika kuandaa na kutekeleza ukaguzi wangu ili kupata uhakika kwamba taarifa za fedha ni sahihi na hazina makosa makubwa na zimeandaliwa kwa mujibu wa makubaliano yaliyosainiwa baina ya wabia.

1.8 Mbinu za Ukaguzi

Mbinu zangu za ukaguzi ni pamoja na kutathmini kumbukumbu za kiuhasibu na taratibu nyingine ili kukidhi malengo ya ukaguzi. Taratibu za ukaguzi wangu zinajumuisha hatua zifuatazo:

- Kupanga ukaguzi ili kutambua na kutathmini hatari za kuwa na taarifa zisizo sahihi, ama kutokana na udanganyifu au dosari; na kwa kuzingatia uelewa wa taasisi na mazingira yake, ikiwa ni pamoja na mifumo ya udhibiti wa ndani ya kila taasisi.

- Kupata uthibitisho sahihi na toshelevu iwapo kuna taarifa zisizo sahihi kwa kusanifu na kutekeleza hatua stahiki dhidi ya viashiria vyote vya hatari vilivyoainishwa.
- Kutembelea shughuli za miradi na kutathmini utendaji na utekelezaji wake.
- Kutathmini ili kuona iwapo sheria, kanuni, na matakwa ya miradi yamezingatiwa kikamilifu.
- Kutoa maoni juu ya taarifa za kifedha zilizokaguliwa kulingana na hitimisho linalotokana na ushahidi wa ukaguzi uliopatikana.
- Kufuatilia utekelezaji wa matokeo ya ukaguzi wa mwaka uliopita na kuhakikisha kwamba hatua sahihi zimechukuliwa kuhusiana na masuala yote yaliyoainishwa.

1.9 Muundo wa Taarifa

Taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne ambazo zina sura 14. Sehemu hizo nne ni: Utangulizi na Hali ya Utekelezaji wa Ukaguzi wa Mwaka Uliopita, Utendaji wa Fedha, Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba, Tathmini ya Utendaji Halisi pamoja na Hitimisho na Mapendekezo. Kila sehemu inatoa sura zinazohusika na sehemu hiyo ili kurahisisha usomaji na ufuatiliaji wa taarifa hii.

SURA YA PILI

HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA TAARIFA ZA KAGUZI

2.1 Utangulizi

Mapendekezo 3,126 yalitoka kwenye taarifa za kaguzi 290 za miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2019. Sura hii inawasilisha hali ya utekelezaji wa mapendekezo. Mapendekezo yangu yanakusudia kusaidia Watekelezaji wa Mradi kurekebisha mapungufu ambayo yamebainika wakati wa ukaguzi na kupendekeza suluhisho husika kwa uboreshaji wa siku zijazo.

2.2 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita

Kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 2.1, mchanganuo huu unaonesha kuwa kati ya mapendekezo 1,071 sawa na 34% yalitekelezwa; mapendekezo 623 sawa na asilimia 20 yanaendelea kutekelezwa; mapendekezo 1,024 sawa na asilimia 33 hayakutekelezwa, mapendekezo 245 sawa na asilimia nane yamejirudia, na 163 sawa na asilimia tano yamepitwa na wakati. Hali ya utekelezaji hutolewa katika taarifa ya ukaguzi kwa kila mkaguliwa (Watekelezaji wa Miradi).

Jedwali 2- 1: Utekelezaji wa Mapendekezo Katika Taarifa za Kaguzi za Miaka ya Nyuma

Sekta	Jumla mapendekezo ya Miaka ya Nyuma	Mapendekezo yaliyotekelezwa	Mapendekezo yanayoendelea kutekelezwa	Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa	Mapendekezo yaliyojirudia	Mapendekezo yaliyopitwa na wakati
Kilimo	44	10	23	4	1	6
Elimu	151	80	36	5	8	22
Nishati na Madini	76	21	33	7	8	7
Afya	2,277	671	403	894	206	103
Jamii	285	169	47	60	2	7
Uchukuzi	122	41	43	28	2	8
Maji	68	23	9	20	7	9
Miradi Mingine	103	56	29	6	11	1
Jumla	**3,126**	**1,071**	**623**	**1,024**	**245**	**163**

Asilimia	100	34	20	33	8	5

Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi za mwaka 2019/20*

Jedwali 2-1, linaonesha kuwa hali ya utekelezaji hairidhishi, kwani ni 34% tu ya mapendekezo yaliyotekelezwa kikamilifu.

Kwa kuongeza, uchambuzi wa utekelezaji wa mapendekezo kuhusu miradi ya maendeleo kwa miaka minne mfululizo inaonesha kiwango cha utekelezaji hakiridhishi (chini ya asilimia 50) kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo 2.1**. Nawasihi Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa kiwango cha utekelezaji kinaboreshwa ili kuwe na ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Kielelezo 2-1: Mwenendo wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi



	Mapendekezo yaliyotekelezwa	Mapendekezo yanayoendelea kutekelezwa	Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa	Mapendekezo yaliyopitwa na wakati
2019/20	34	20	41	5
2018/19	30	20	42	8
2017/18	35	18	34	13
2016/17	29	17	35	19

Kielelezo 2.1: Mwenendo wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi

SEHEMU YA PILI

UTENDAJI WA KIFEDHA, USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA

Sehemu ya pili inajumuisha Sura ya Tatu na ya Nne zinazohusu tathmini ya utendaji wa kifedha na usimamizi wa manunuzi na mikataba mtawalia.

Sura ya tatu inawasilisha maelezo ya ufadhili wa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2019/20. Sura hii inawasilisha muhtasari wa kiasi cha fedha zilizopokelewa na zilizotumika na watekelezaji wa miradi. Pia, inatoa maelezo ya hati za ukaguzi zilizotolewa kwa watekelezaji wa miradi, pamoja na uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa fedha.

Sura ya nne inawasilisha masuala ya usimamizi wa manunuzi na mikataba, kwani haya ni mambo muhimu katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi. Kwa hiyo, sura hii inatoa uchambuzi wa matokeo yanayohusiana na usimamizi wa manunuzi na usimamizi wa mikataba uliochambuliwa kutoka kwenye taarifa za kaguzi za kila mradi husika zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2019/20.

SURA YA TATU

UTENDAJI WA KIFEDHA

3.1 Utangulizi

Usimamizi wa Matumizi ya Umma ni njia ya kutekeleza bajeti katika sekta ya umma inayolenga kufikia matokeo matatu ya kijamii ambayo ni nidhamu ya pamoja ya kifedha, ufanisi wa matumizi, na ufanisi wa kiutendaji. Hii inajumuisha kudhibiti usimamizi wa kifedha kwa Watekelezaji wa Miradi ili kuwezesha matumizi mazuri ya rasilimali za umma, kuimarisha uwajibikaji na kutoa mamlaka ya kisheria na udhibiti wa masilahi endelevu ya umma.

3.2 Ufadhili wa Miradi

Ufadhili wa miradi uko katika mfumo wa mikopo na misaada kutoka kwa Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Programu ya Kimataifa wa Kilimo na Usalama wa Chakula (GAFSP), Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo (DFATD) Kanada na Washirika wengine wa Maendeleo. Serikali ya Tanzania ina jukumu la kuchangia fedha kwenye utekelezaji wa miradi kulingana na makubaliano yaliyowekwa na kusainiwa kati ya Serikali na Waadau wa Maendeleo. Serikali pia hubuni vyanzo mbalimbali vinavyosaidia uendeshaji wa miradi ikiwemo mapato ya ndani, mapato yatokanayo na kodi na mapato yasiyotokana na kodi. Sura hii inatoa maelezo ya fedha zilizotolewa na kutumiwa na watekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta nane ambazo ni; Kilimo, Elimu, Nishati na Madini, Afya, Uchukuzi, Maji, Miradi ya kijamii na miradi mingine.

3.2.1 Sekta ya Kilimo

Sekta hii imehusisha ukaguzi wa fedha katika miradi nane na ukaguzi mmoja wa kiufundi iliyotekelezwa katika sekta ya Kilimo. Miradi hii ilifadhiliwa na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Programu ya kimataifa wa Kilimo, usalama wa

chakula (GAFSP[5]), Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na Serikali ya Tanzania na imetekelezwa na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), Ofisi ya Waziri Mkuu (PMO), Wizara ya Kilimo (MoA), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Baraza la Kitaifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na Kampuni Hodhi ya Mkulazi (MHCL). Matokeo ya ukaguzi wa kiufundi wa Mradi wa Uzalishaji Sukari wa Mbigiri umewasilishwa kwa kina katika sura ya 11.

Uchambuzi wa kifedha wa miradi nane unaonesha kuwa, miradi hii ilikuwa na jumla ya Sh. 68,382,117,891.54 kwa ajili ya matumizi ambapo Sh. 53,829,478,354.08 zilitumika na kiasi cha Sh. 14,552,639,537.46 kilibaki kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizosalia kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 3-1.**

Jedwali 3- 1: Muhtasari wa Mapato na Matumizi (Kiasi Katika Shilingi/Milioni)- Sekta ya Kilimo

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika(Sh)	Bakaa (Sh)
1	Mradi wa Kituo Mahiri cha Teknolojia Bunifu za Udhibiti wa Panya na Uendelezaji wa Teknolojia za Unusaji	Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine	1.59	0.69	0.89
2	Kituo cha Utafiti wa Ufundishaji Mahiri wa Maendeleo Endelevu ya Kilimo (CREATES)	Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST)	2,578.84	1,414.37	1,164.47
3	Usimamizi wa Kiikolojia na Kilimo Endelevu cha Panya na Usalama wa Chakula barani Afrika (EcoRodMan)	Chuo kikuu cha Kilimo cha Sokoine	550.16	145.29	404.87

[5] Mpango wa Kilimo Duniani na Usalama wa Chakula

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika(Sh)	Bakaa (Sh)
4	Mradi wa Upanuzi wa Uzalishaji wa Mpunga (ERPP)	Wizara ya Kilimo	16,877.88	13,385.87	3,492.01
5	Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji wa Thamani, na Msaada wa Fedha Vijijini (MIVARF)	Ofisi ya Waziri Mkuu	41,155.01	33,391.87	7,763.14
6	Kuimarisha Ujuzi na Uwezo wa Mafunzo katika Mradi wa Sekta ya Kilimo cha Bustani	Baraza la Kitaifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)	0.12	0.12	0.00
7	Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu	Wizara ya Kilimo	2,156.19	1,618.52	537.67
8	Kituo cha Ubora cha Afrika kwa Magonjwa ya Kuambukiza ya Wanadamu na Wanyama Kusini na Mashariki	Chuo kikuu cha Kilimo cha Sokoine	5,062.33	3,872.75	1,189.58
	Jumla		**68,382.12**	**53,829.48**	**14,552.64**

Chanzo: ***Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2020***

3.2.2 Sekta ya Elimu

Katika sekta ya elimu, nilifanya kaguzi za taarifa za fedha kwa miradi 11 inayotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) kupitia fedha zilizopokelewa kutoka Benki ya Dunia, Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo (DFATD) Kanada na Serikali ya Tanzania. Katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi, kulikuwa na kiasi cha Sh. 477,830,427,898.88 kwa ajili ya matumizi ambapo kiasi cha Sh. 268,190,107,422.85 zilitumika na kubakiwa na Sh. 209,640,320,476.03 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizosalia **(Jedwali Na. 3.2).**

Jedwali 3- 2: Muhtasari wa Mapato na Matumizi (Kiasi Katika Shilingi/Milioni) – Sekta ya Elimu

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika (Sh)	Bakaa (Sh)
1	Matokeo Makubwa Sasa katika Mradi wa Elimu ya Malipo kwa Matokeo (BRN EPforR)	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	252,339.71	174,365.74	77,973.97
2	Mradi wa kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki - Chuo cha DIT Dar-es-Salaam	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	11,160.79	407.04	10,753.75
3	Mradi wa kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki - Chuo cha DIT Mwanza	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	11,105.35	143.47	10,961.88
4	Mradi wa kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki - Chuo cha -Taifa cha Usafirishaji	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	14,545.31	1,281.56	13,263.75
5	Mradi wa kuleta Mabadiliko katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki - Chuo cha Ufundi Arusha	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	11,145.46	89.44	11,056.02
6	Programu ya Elimu na Ujuzi kwa Ajili ya Kazi za Uzalishaji (ESPJ)	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	116,610.34	63,066.19	53,544.14
7	Mpango wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (LANES) II	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	12,472.57	837.21	11,635.36
8	Mradi wa Chuo Kikuu cha Sayansi	Wizara ya Elimu	1,976.57	1,571.63	404.94

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika (Sh)	Bakaa (Sh)
	na Teknolojia cha Afrika - Nelson Mandela	Sayansi na Teknolojia			
9	Programu ya Kusaidia Elimu ya Ufundi, Mafunzo na Elimu kwa Walimu (STVET-TE)	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	2,122.14	2,119.09	3.05
10	Mradi wa Kusaidia Elimu kwa Walimu (TESP)	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	32,983.18	21,088.04	11,895.14
11	Mradi wa Kuboresha Vyuo vya Ualimu	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	11,369.01	3,220.70	8,148.31
Jumla			**477,830.43**	**268,190.11**	**209,640.31**

Chanzo: *Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2020*

3.2.3 Sekta ya Nishati na Madini

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilifanya kaguzi za taarifa za fedha za miradi 18 na kaguzi za kiufundi tano iliyotekelezwa na Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania na Wizara ya Madini kupitia fedha zilizopokelewa kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Idara ya Mambo ya Nje, Biashara na Maendeleo (DFATD), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Uchumi Afrika (BADEA), Mfuko wa Maendeleo ya Kimataifa wa Jumuiya ya Nchi Zinazozalisha Mafuta Duniani (OFID), Jumuiya ya Ulaya (EU) na Serikali ya Tanzania.

Matokeo ya ukaguzi wa kiufundi wa miradi mitano iliyo chini ya sekta ya nishati na Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Mwalimu Nyerere yamewasilishwa kwa kina katika sura ya saba.

Uchambuzi wa taarifa 18 za kifedha kwa mwaka 2019/20 unaonesha kuwa, miradi hii ilikuwa na fedha zilizopatikana kiasi cha Sh. 203,941,912,223.38 ambapo Sh. 148,658,430,090.72 zilitumika kubakiwa na Sh. 55,283,482,132.74 sawa na 27%

ambazo zitatumika kwa utekelezaji wa shughuli zilizosalia **(Jedwali Na. 3.3).**

Jedwali 3- 3: Muhtasari wa Mapato na Matumizi (Kiasi Katika Shilingi/Milioni)- Sekta ya Nishati na Madini

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika (Sh)	Bakaa (Sh)
1	Uwekezaji wa Miundombinu ya Msingi ya Kusafirisha Umeme (BTIP) II	Shirika la Umeme Tanzania	47,407.37	47,407.37	0
2	Bulyanhulu-Geita 220kv Mradi wa kusafirisha umeme na Uwekaji umeme Vijijini katika Wilaya ya Geita	Shirika la Umeme Tanzania	11,633.58	10,360.25	1,273.33
3	Mradi wa Kujenga Uwezo wa Sekta ya Nishati (ESCBP)	Wizara ya Nishati	1,948.35	1,948.35	0
4	Mradi wa Maendeleo wa Kukuza Nguvukazi	Wizara ya Nishati	10.73	0.43	10.30
5	Mradi wa Kusafirisha Umeme Mkubwa na Uwekaji Umeme Vijijini - Geita- Nyakanazi 220kv	Shirika la Umeme Tanzania	22,017.04	21,925.96	91.08
6	Mradi wa Kuunganisha Umeme Kenya na Tanzania	Shirika la Umeme Tanzania	55,800.13	47,723.25	8,076.88
7	Upembuzi Yakinifu wa Mradi wa Bwawa la Kikonge	Shirika la Umeme Tanzania	0.97	0.97	0
8	Mradi wa Kusafirisha Umeme Mkubwa na Uwekaji Umeme Vijijini - Makambako-Songea 220kv	Shirika la Umeme Tanzania	16,144.56	15,480.73	663.83

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika (Sh)	Bakaa (Sh)
9	Mradi wa Kusafirisha Umeme Mkubwa (400kV) Nyakanazi - Kigoma)	Shirika la Umeme Tanzania	563.56	563.56	0
10	Mradi wa Umeme wa Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo	Shirika la Umeme Tanzania	3.80	2.22	1.58
11	Mradi wa Ukarabati wa Kituo cha Umeme wa Nguvu ya Maji - Hale	Shirika la Umeme Tanzania	19,283.19	174.36	19,108.83
12	Wakala wa Nishati Vijijini - Mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia	Wizara ya Nishati	161.08	3.36	157.72
13	Mradi Endelevu wa Nishati kwa Wote (SE4ALL)	Wizara ya Nishati	24.78	23.04	1.74
14	Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini - II (SMMRP) II	Wizara ya Madini	2,403.99	1,832.61	571.38
15	Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia - Umoja wa Ulaya	Wizara ya Madini	71.32	0.18	71.14
16	Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (Serikali ya Tanzania na CIDA)	Wizara ya Madini	674.93	624.91	50.02
17	Mradi wa Kuunganisha	Shirika la Umeme Tanzania	25,769.75	564.12	25,205.63

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika (Sh)	Bakaa (Sh)
	Umeme Zambia na Tanzania				
18	Mradi wa Kuboresha na Kukarabati Gridi ya Umeme (TTGRUP)	Shirika la Umeme Tanzania	22.77	22.77	0
Total			**203,941.90**	**148,658.44**	**55,283.46**

Chanzo: *Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2020*

3.2.4 Sekta ya Afya

Katika sekta ya afya, nilifanya kaguzi za taarifa za fedha za miradi 193 zilizotekelezwa na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ofisi ya Waziri Mkuu, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na Halmashauri 184 zinazotekeleza mradi wa Mfuko wa Afya wa Pamoja (HBF). Fedha hizi za miradi zilipokelewa kutoka Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Denmaki (DANIDA), Benki ya Dunia, Kanada, Ireland, Shirika la Uhusiano wa Kimataifa la Korea Kusini (KOICA), Uswisi na Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Norwei (NORAD), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa cha Marekani (CDC), Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Mradi wa Kupambana na Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI unaofadhiliwa na Mfuko wa Afya wa Kimataifa. (Global Fund) na Serikali ya Tanzania.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, kulikuwa na Sh. 209,451,499,088.35 kwa ajili ya matumizi, Sh. 173,326,995,613.71 zilitumika ambapo Sh. 36,124,503,474.45 zilibaki kwa utekelezaji wa shughuli zilizosalia kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 3.4.**

Jedwali 3- 4: Muhtasari wa Mapato na Matumizi (Kiasi Katika Shilingi/Milioni)- Sekta ya Afya

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika(Sh)	Bakaa (Sh)
1	Mradi wa Mtandao wa	Wizara ya Afya	10,669.38	9,728.24	941.14

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika(Sh)	Bakaa (Sh)
	Maabara kwa Umma - Afrika Mashariki				
2	Mfuko wa Afya	Wizara ya Afya	3,612.88	3,612.88	0
3	Mradi wa Kusaidia Sekta ya Afya (HSPS)	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	46,073.64	28,394.49	17,679.15
4	Mradi wa Kituo Mahiri cha Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kwa Ajili ya Sayansi ya Matibabu ya Mishipa ya Moyo	Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	2,989.74	2,504.38	485.36
5	Mradi wa Ushirikiano katika Tafiti za Afya, Mafunzo na Uvumbuzi kwa ajili ya Programu ya Maendeleo Endelevu.	Chuo Kikuu Muhimbili	3,324.46	2,053.18	1,271.28
6	Mradi wa Utafiti katika Kujenga Uwezo wa Kupambana na Maradhi ya Selimundu.	Chuo Kikuu Muhimbili	1,685.11	1,227.28	457.83
7	Programu ya Kuimarisha Afya ya Msingi kwa Matokeo (SPHC4R)	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	200.21	200.07	0.14
8	Programu ya Kuimarisha Afya ya Msingi kwa Matokeo	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	25,264.27	18,075.52	7,188.75
9	Utaratibu wa Kitaifa wa Mfuko wa Kimataifa -	Ofisi ya Waziri Mkuu	290.63	248.36	42.27

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika(Sh)	Bakaa (Sh)
	UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria				
10	Mfuko wa Afya - Mamlaka za Serikali za Mitaa	Halmashauri mbalimbali	82,712.05	76,238.91	6,473.14
Jumla			**209,451.50**	**173,327**	**36,124.50**

Chanzo: *Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2020*

3.2.5 Sekta ya Uchukuzi

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilifanya kaguzi za taarifa za fedha za miradi 12 na kaguzi za kiufundi tano iliyotekelezwa na Wakala wa Serikali wa Barabara (TANROADS), Shirika la Reli (TRC), Mfuko wa Bodi ya Barabara, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Shirika la Mawakala wa Usafirishaji Tanzania (TASAC) na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia fedha zilizopokelewa kutoka AfDB, Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa Japani (JICA), Tume ya Umoja wa Afrika, Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (DFID) na Serikali ya Tanzania. Matokeo ya ukaguzi wa kiufundi wa miradi miwili iliyotekelezwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) imewasilishwa kwa kina katika sura ya tano, na mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) na Mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) na Mradi Upanuaji wa Barabara ya Morogoro (Kimara Kibaha) zimewasilishwa kwa kina katika Sura ya tano, saba na nane wakati matokeo ya kaguzi mbili[6] za kiufundi kwa miradi iliyotekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania imewasilishwa katika sura ya 11.

Mchanganuo wa taarifa za kifedha za miradi 12 iliyotekelzwa kwa mwaka wa fedha 2019/20, unaonesha kuwa Sh. 1,319,627,746,063 zilipatikana kwa ajili ya matumizi, kati ya hizo Sh. 933,658,000,565 zilitumika na Sh. 385,969,745,495 zilibakia kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizosalia **(Jedwali Na. 3.5).**

[6] Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kimataifa :Rumonge - Gitaza (45km) and Kabingo - Kasulu - Manyovu (260km) na Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji (TSSP)

Jedwali 3- 5: Muhtasari wa Mapato na Matumizi (Kiasi Katika Shilingi/Milioni)- Sekta ya Uchukuzi

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Shs)	Kiasi kilichotumika(Shs)	Bakaa (Shs)
1	Mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka(BRT) Awamu ya pili	Wakala wa Barabara	15,998.61	9,721.38	6,277.23
2	Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam (DMGP)	Mamlaka ya Bandari Tanzania	138,760.06	69,026.21	69,733.85
3	Mradi wa Maendeleo ya Jiji Kuu la Dar es Salaam (DMDP)	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	122,090.15	98,778.74	23,311.41
4	Programu ya Uboreshaji wa Miundombinu ya Usafirishaji Jijini Dar es Salaam (DUTP)	Wakala wa Barabara	157,626.48	80,453.85	77,172.63
5	Mradi wa Kimataifa wa Usafiri na Mawasiliano wa Ziwa Victoria	Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)	186.68	57.56	129.12
6	Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kimataifa :Rumonge - Gitaza (45km) and Kabingo - Kasulu - Manyovu (260km)	Wakala wa Barabara	16,160.00	8,593.80	7,566.20
7	Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kimataifa Arusha-Taveta/Holilii-Voi	Wakala wa Barabara	18,610.85	13,872.44	4,738.41
8	Mradi wa Uwezeshaji	Wakala wa Barabara	132,324.94	37,317.79	95,007.15

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Shs)	Kiasi kilichotumika(Shs)	Bakaa (Shs)
	Biashara na Usafirishaji Kusini mwa Afrika (SATTFP)				
9	Mradi wa Maendeleo ya Reli Tanzania (TIRDP)	Shirika la Reli	372,189.10	339,515.36	32,673.74
10	Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji (TSSP)	Wakala wa Barabara	130,761.52	129,789.79	971.73
11	Mradi wa Kuboresha Miji Tanzania - Fedha za ziada 2 (TSCP-AF 2)	Wakala wa Barabara	193,093.91	124,705.65	68,388.26
12	Mradi wa Kuboresha Barabara za Vijini kwa Ajili ya Programu ya Kuboresha Tanzania.	Mfuko wa Bodi ya Barabara	21,825.44	21,825.44	0
Jumla			**1,319,627.74**	**933,658.01**	**385,969.73**

Chanzo: *Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2020*

3.2.6 Sekta ya Maji

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilifanya kaguzi za taarifa za fedha za miradi 9 na kaguzi mbili za kiufundi kwa Mradi wa Uimarishaji Endelevu wa Mifumo ya Maji na Usafi wa Mazingira – Arusha Mjini na Miradi ya Maji wa Same-Mwanga na Korogwe. Miradi hii inatekelezwa na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha (AUWASA), Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza (MWAUWASA), Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), Wizara ya Afya, Wizara ya Maji, Wizara ya Elimu Sayansi na Tekinolojia na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) kupitia ufadhili kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Misaada la Ujerumani na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD).

Miradi yote iliyokuwa inatekelezwa na Halmashauri chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) sasa inatekelezwa na RUWASA na nimeijumuisha katika taarifa yangu ya ujumla ya Serikali Kuu ya mwaka 2019/20.

Nimewasilisha matokeo ya ukaguzi wa kiufundi wa Mradi wa Maji wa Same-Mwanga na Korogwe katika Sura ya tisa na Mradi wa Endelevu wa Uimarishaji wa Mifumo ya Maji na Usafi wa Mazingira – Arusha Mjini umewasilishwa katika Sura ya 11.

Mchanganuo wa taarifa za kifedha za miradi tisa iliyotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 unaonesha kuwa miradi hii ilikuwa na fedha Sh. 1,198,378,211,333 zilizopatikana kwa ajili ya matumizi, kati ya hizo Sh. 836,775,528,319.57 zilitumika na Sh. 361,602,683,012.80 zilibaki kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizosalia, **Jedwali Na. 3.6.**

Jedwali 3- 6: Muhtasari wa Mapato na Matumizi (Kiasi Katika Shilingi/Milioni)- Sekta ya Maji

Na.	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika (Sh)	Baka (Sh)
1	Mradi Endelevu wa Uimarishaji wa Mifumo ya Maji - Arusha Mjini	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha	91,672.69	64,301.58	27,371.11
2	Kituo cha Miundombinu ya Maji na Nishati Endelevu kwa Matumizi ya Baadaye (WISE-FUTURES)	Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST)	3,904.57	1,893.07	2,011.50
3	Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira - Ziwa Viktoria (LV WATSAN)	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza	56,657.78	26,061.88	30,595.90
4	Usafi wa Maji Shuleni (SWASH)	Wizara ya Elimu Sayansi na Tekinolojia	17,085.82	16,526.05	559.77
5	Mradi wa Kusaidia Sekta ya Maji II - 2018/2019 (WSSP II)	Wizara ya Maji na Mamlaka ya Maji Safi na	129,214.70	36,474.67	92,740.03

		Maji Taka Dar es Salaam			
6	Programu ya Usambazaji wa Huduma ya Maji Safi Vijijini (Programu ya matokeo makubwa)	Wizara ya Maji	178,822.46	75,760.89	103,061.57
7	Programu ya Usambazaji wa Huduma ya Maji Safi Vijijini	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	25,628.73	24,726.48	902.25
8	Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Fungu 52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	416.74	384.91	31.83
9	Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II)	Wizara ya Maji	694,974.74	590,646.00	104,328.74
Jumla			**1,198,378.23**	**836,775.53**	**361,602.70**

Chanzo: *Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2020*

3.2.7 Sekta ya Jamii

Katika mwaka wa fedha 2019/20, kaguzi katika sekta ya kijamii ulihusisha miradi mitatu ambayo ni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya Tatu (TASAF III), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto (UNICEF).

Mawanda ya Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya Tatu (TASAF III) yalihusisha kipindi cha miezi tisa kutoka 1 Julai 2019 hadi 31 Machi 2020 wakati kwa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto (UNICEF) Ukaguzi ulihusisha kipindi cha miezi 12 kwa kufuata mwaka wa kalenda yaani Januari hadi Desemba 2019.

TASAF III PSSN

Shughuli za TASAF III PSSN I zinafadhiliwa na Serikali ya Tanzania, Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (IDA), Mfuko wa Maendeleo wa Kimataifa wa Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (OFID), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UN Agencies), Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA), Mfuko wa Bill na Melinda Gates (BMGF) na Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania (FSDT).

Katika mwaka wa fedha 2019/20, TASAF III PSSN I ilikuwa na jumla ya Sh. 77,849,626,232.68 zilizopatikana kwa ajili ya matumizi zikijumuisha salio anzio la Sh. 9,389,093,102.54. Hadi tarehe 31 Machi 2020 jumla ya Sh. 74,487,722,738.07 sawa na 96% zilitumika na Sh. 3,361,903,494.61 zilibaki kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizosalia.

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP)

Programu ya Serikali ya UNDP kwa miaka mitano (2016-2021) kati ya maswala mengine, inazingatia kushughulikia umaskini na uharibifu wa mazingira kupitia uwekezaji na utawala bora ili kuwawezesha wanawake, walemavu, vijana na kuongeza ushiriki wao katika maswala ya uchumi, mazingira na utawala.

Katika mwaka wa fedha uliomalizika tarehe 31 Desemba 2019, miradi 13 ya UNDP iliyokaguliwa ilikuwa na Sh. 11,790,961,488 zilizopatikana kwa ajili ya matumizi; Sh. 11,519,304,938 zilitumika na Sh. 271,656,512 zilibaki kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za UNDP zilizosalia (Jedwali Na. 3.7).

Jedwali 3- 7: Muhtasari wa Mapato na Matumizi (Kiasi Katika Shilingi/Milioni)- UNDP

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika (Sh)	Bakaa (Sh)
1	Kujenga Uwezo kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Uratibu na	Tume ya Mipango Zanziba	1,006.66	1,006.32	0.34

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika (Sh)	Bakaa (Sh)
	kuripoti MKUZA III Zanziba				
2	Kuongeza Uwezo wa Matokeo ya Maendeleo ya Miradi	Ofisi ya Taifa ya Takwimu	223.24	211.28	11.96
3	Kuongeza Uwezo wa Matokeo ya Maendeleo ya Miradi	Wizara ya Fedha na Mipango - Tanzania Bara	595.22	584.37	10.85
4	Kuongeza Uwezo wa Matokeo ya Maendeleo ya Miradi	Wizara ya Fedha na Mipango - Zanzibar	285.85	234.56	51.29
5	Mradi wa Kushughulikia Madhara ya tetemeko la ardhi Kagera na Ukarabati thabiti wa Majengo.	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kagera	1,161.20	1,161.20	0
6	Programu ya Uwezeshaji na Upatikanaji wa haki za kisheria	Wizara ya Katiba na Sheria - Zanzibar	357.46	357.46	0
7	Mradi wa Kusaidia Kuwajengea Wabunge Uwezo - Awamu II	Ofisi ya Bunge	2,644.17	2,643.98	0.19
8	Mradi wa kujumuisha malengo katika kupambana na athari za Mazingira, Umaskini na Jinsia katika Kuleta Maendeleo Endelevu na Kuondoa Umaskini	Chuo Cha Mipango Dodoma- Kanda ya Ziwa - Mwanza	949.55	815.65	133.90
9	Kuzuia na Kutuliza Vurugu nchini Tanzania	Jeshi la Polisi Tanzania	57.87	57.87	0
10	Kuzuia na Kutuliza Vurugu nchini Tanzania	Jeshi la Magereza	376.00	375.99	0.01
11	Mradi wa Kunusuru Vyanzo	Bonde la Mto Pangani	2,834.26	2,834.26	0

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika (Sh)	Bakaa (Sh)
	vya Maji (SLM) - Bonde la Mto Pangani				
12	Kuimarisha Upataji na Ulinzi wa Haki za Binadamu nchini Tanzania	Wizara ya Katiba na Sheria - Tanzania Bara	697.42	697.07	0.35
13	Kuimarisha Upataji na Ulinzi wa Haki za Binadamu nchini Tanzania	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	602.06	539.30	62.76
Jumla			**11,790.96**	**11,519.31**	**271.65**

Chanzo: *Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2020*

UNICEF

Programu ya Serikali ya UNICEF kwa miaka mitano (2016-2021) unazingatia njia za vitendo za kutambua haki za watoto nchini Tanzania. Mpango huo unashughulikia maeneo saba yakiwemo ya afya, Ukimwi, lishe, maji, usafi wa mazingira na usafi (WASH), elimu, ulinzi wa watoto na sera ya kijamii. Programu hii pia inalenga kusaidia watoto na familia za kitanzania kuhakikisha zinapata na kufaidika na huduma bora za kijamii, maarifa na fursa.

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2019, Sh. 11,095,839,450 zilipatikana kwa ajili ya matumizi ya miradi minane, kati ya fedha hizo Sh. 7,527,273,837 zilitumika na Sh. 3,568,565,613 zilibaki kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za UNICEF zilizosalia **Jedwali Na. 3-8.**

Jedwali 3- 8: Muhtasari wa Mapato na Matumizi (Kiasi Katika Shilingi/Milioni)- UNICEF

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Shs)	Kiasi kilichotumika (Shs)	Bakaa (Shs)
1	Programu ya Kulinda Maendeleo ya Watoto	Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali	652.65	466.59	186.06
2	Programu ya Kulinda Maendeleo ya Watoto	Wizara ya Ajira, Kazi, Wazee,	486.11	429.71	56.40

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Shs)	Kiasi kilichotumika (Shs)	Bakaa (Shs)
		Wanawake na Watoto- Zanzibar			
3	Programu ya Kulinda Maendeleo ya Watoto	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Njombe	973.21	718.52	254.69
4	Programu ya Kulinda Maendeleo ya Watoto	Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi	341.41	289.98	51.43
5	Programu ya Kulinda Maendeleo ya Watoto	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Njombe	486.11	429.71	56.40
6	Ugatuaji wa Usajili wa Vizazi na vifo	Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo	3,104.84	2,935.00	169.84
7	Programu ya Utetezi wa Sera ,Uchambuzi na kusaidia Programu ya UNICEF	Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serkali za Mitaa	3,951.66	1,176.70	2,774.96
8	Stawisha Maisha - TASAF	Mfuko wa Maendelo ya Jamii - Tanzania (TASAF)	1,099.85	1,081.07	18.78
Jumla			**11,095.84**	**7,527.28**	**3,568.56**

Chanzo: *Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2020*

3.2.8 Miradi ya Sekta Mbalimbali

Miradi ya Sekta Mbalimbali inahusisha shughuli za utekelezaji wa masuala mtambuka kama vile kujenga uwezo na uhamasishaji katika masuala ya sheria, mazingira, maendeleo ya kiuchumi na masuala mengine ya maendeleo. Miradi hii ilipokea fedha kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) na Washirika wengine wa maendeleo.

Uchambuzi wangu wa taarifa 17 kwa mwaka wa fedha 2019/20 ulionesha kulikuwa na Sh. 166,013,951,257 kwa ajili ya matumizi ambapo Sh. 79,499,752,015 zilitumika na kusalia kiasi cha Sh. 86,514,199,242 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za miradi iliyosalia **(Jedwali Na. 3.9).**

Jedwali 3- 9: Muhtasari wa Mapato na Matumizi (Kiasi Katika Shilingi/Milioni)- Miradi Mingine

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika(Sh)	Bakaa (Sh)
1	Maradi wa ARU -SIDA	Chuo Kikuu cha Ardhi	1,175.00	427.88	747.12
2	Mradi Endelevu wa Kuwezesha Kuzuia na Kupambana na Rushwa - Tanzania	Ofisi ya Rais - Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri	8,735.33	5,989.80	2,745.53
3	Mradi wa Maboresho wa Huduma za Mahakama na Utoaji wa Haki kwa Wananchi	Mahakama	66,846.68	19,898.09	46,948.59
4	Msaada wa Maendeleo kwa Ukuaji Wa Takwimu Tanzania	Ofisi ya Takwimu ya Taifa	6,452.96	404.4	6,048.56
5	Mradi wa Uhamasishaji wa Raslimali za Ndani na Usimamizi Bora wa Maliasili (ISP-DRM& NRG)	Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania	11,598.60	10,349.88	1,248.72
6	Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi Vyanzo vya Maji Kihansi (KCCMP)	Ofisi ya Makamu wa Rais	1,001.47	997.1	4.37
7	Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia (NFAST)	Tume ya Sayansi na Tekinolojia (COSTECH)	3,291.27	3,119.77	171.49
8	Programu ya Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)	Wizara ya Fedha na Mipango	29,761.46	19,335.17	10,426.29
9	Mradi wa Maliasili Endelevu kwa Ukuaji (REGROW)-TANAPA	Shirika la Hifadhi za Taifa	8,692.31	3,450.46	5,241.85

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika(Sh)	Bakaa (Sh)
10	Mradi wa Maliasili Endelevu kwa Ukuaji (REGROW)	Wizara ya Maliasili na Utalii	5,942.61	423.21	5,519.40
11	Taasisi ya kuendeleza viwanda vidogo katika Kukuza Usanifu wa Maendeleo Endelevu ya Jamii na Uchumi	Taasisi ya kuendeleza viwanda vidogo (SIDO)	300.69	278.36	22.33
12	Kituo cha Kudhibiti Hewa ya ukaa Nchini (NCMC)	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine	136.93	162.55	-25.63
13	Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi na Ukuaji wa Pamoja Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFISH)	Wizara ya Mifugo na Uvuvi	8,608.74	7,140.69	1,468.05
14	Mifumo ya Majengo bora, na Utafiti Unaofaa Tanzania (SIDA)	Tume ya Sayansi na Tekinolojia (COSTECH)	2,564.12	1,740.87	823.25
15	Programu ya Ukuzaji Wa Maendeleo ya Sekta ya Biashara Tanzania	Wizara ya Viwanda na Biashara	163.39	154.57	8.83
16	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA)	Chuo kikuu cha Dar es Salaam	9,626.65	5,425.24	4,201.41
17	Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na Kuongeza Uhakika wa	Ofisi ya Makamu wa Rais	1,115.75	201.72	914.03

Na	Jina la Mradi	Mtekeleza Mradi	Kiasi kilichopo (Sh)	Kiasi kilichotumika(Sh)	Bakaa (Sh)
	Chakula katika Maeneo Kame Tanzania (LDFS)				
Jumla			**166,013.95**	**79,499.75**	**86,514.20**

Chanzo: *Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2020*

3.3 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa[7]

Hati za Ukaguzi huchukuliwa kama taarifa muhimu wakati wa kuripoti usahihi wa taarifa za kifedha kwa watumiaji. Kulingana na kifungu cha 34 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008, ninalazimika kutoa maoni ya kitaalamu, juu ya uandaaji hesabu na usahihi wa taarifa za fedha zilizowasilishwa na kuandaa ripoti ya ukaguzi. Kwa sekta ya umma, maoni yangu ya ukaguzi yanawajulisha watumiaji taarifa za kifedha kuwa taarifa za kifedha za miradi ya maendeleo zimeandaliwa kulingana na mfumo husika wa utoaji wa taarifa za kifedha kama vile Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji Hesabu katika Sekta ya Umma (IPSAS) au mfumo wa kutoa taarifa za fedha kwa madhumuni maalum na namna inavyotakiwa na Sehemu ya 25 (4) ya Sheria ya Fedha za Umma, 2001 (iliyorekebishwa 2004) na makubaliano na miongozo husika ya ufadhili wa miradi.

Katika kufanya ukaguzi wa kifedha kwenye miradi ya maendeleo, ninatoa uhakikisho kwenye maeneo maalum kulingana na mfumo unaofaa uliotumika katika kuandaa taarifa za kifedha. Maeneo haya ni pamoja na uhakikisho juu ya taarifa za kifedha, udhibiti wa ndani na uzingatiaji wa sheria na miongozo mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilifanya kaguzi wa kifedha 290 ambapo nilitoa jumla ya hati za Ukaguzi 290 juu ya taarifa za kifedha na hati za ukaguzi 21 juu ya udhibiti wa ndani ambayo yanahusiana na miradi iliyofadhiliwa na Shirika la maendeleo la

[7] Mwaka huu majina ya hati za Ukaguzi yamebadilika. Kwa miaka iliyopita, “Adverse Opinion” illiitwa “Hati Isiyoridhisha” na “Disclaimer of Opinion” iliitwa “Hati Mbaya”. Kwa mwaka huu, “Adverse Opinion” imeitwa “Hati Mbaya” na “Disclaimer of Opinion” imeitwa “Kushindwa kutoa Maoni”. Mabadiliko haya yametokea kwa kuzingatia kuwa majina mapya yanaakisi zaidi maana halisi ya hati zilizotolewa.

Umoja wa mataifa (UNDP) na Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto (UNICEF).

Katika mwaka wa fedha 2019/20, sikuripoti mapungufu yenye tija kwenye hati za Ukaguzi 21 dhidi ya udhibiti wa ndani. Maoni yanahusiana na taarifa za kifedha yamewasilishwa kwenye sura zinazofuata.

3.3.1 Maoni ya Ukaguzi Yaliyotolewa Juu ya Taarifa za Fedha

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilitoa aina mbili za hati za Ukaguzi kwenye taarifa za fedha 290, kati ya hizo nilitoa hati zinazoridhisha 275 na hati zenye mashaka 15 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 3.10.**

Jedwali 3- 10: Muhtasari wa Hati ya Ukaguzi zilizotolewa

Sekta	Hati zilizotolewa				
	Hati inayoridhisha	Hati yenye mashaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya	Jumla
Kilimo	8	0	0	0	8
Elimu	11	0	0	0	11
Nishati na Madini	18	0	0	0	18
Afya	178	15	0	0	193
Jamii	22	0	0	0	22
Uchukuzi	12	0	0	0	12
Maji	9	0	0	0	9
Miradi mingine	17	0	0	0	17
Jumla	**275**	**15**	**0**	**0**	**290**

Chanzo: *Taarifa za kaguzi za miradi ya maendeleo kwa miaka 2015/16 hadi 2019/20*

3.3.2 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi Zilizotolewa

Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa miaka mitano mfululizo yanaonesha mwelekeo unaoridhisha kuhusu miradi ya maendeleo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 3-11** na **Kielelezo 3.1**.

Hata hivyo, hati zenye mashaka zilitokana na hati za malipo kuwa na nyaraka pungufu, kuna uwezekano kwa Taasisi za Serikali kuboresha utayarishaji wa taarifa za kifedha na utunzaji wa kumbukumbu wa nyaraka za uhasibu. Hivyo basi ninahimiza Maafisa Masuuli kuwapatia mafunzo zaidi watumishi wa Serikali juu ya utunzaji wa kumbukumbu na utayarishaji wa taarifa za kifedha.

Jedwali 3- 11: Mwenendo wa Hati ya Ukaguzi zilizotolewa

Mwaka wa fedha	Hati zilizotolewa						Jumla
	Hati inayoridhisha		Hati yenye mashaka		Hati isyoridhisha		
	Na.	%	Na.	%	Na.	%	
2019/20	275	95	15	5	0	0	290[8]
2018/19	441	97	13	3	1	0.22	455
2017/18	455	97	14	3	0	0	469
2016/17	697	94	44	6	1	0.13	742
2015/16	725	91	71	9	1	0.12	797

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi mwaka 2019/20 na Ripoti kuu ya Ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa miaka iliyopita*

Kielelezo 3-1: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Miaka Mitano Mfululizo



	2019/20	2018/19	2017/18	2016/17	2015/16
Hati inayoridhisha	95	97	97	94	91
Hati yenye shaka	5	3	3	6	9
Hati isiyoridhisha	0	0.22	0	0.13	0.12

Hati inayoridhisha

Hati inayoridhisha hutolewa pale ambapo taarifa za fedha zilizowasilishwa hazikuwa na upotoshaji pia ziliandaliwa kwa kufuata mifumo ya kihasibu, ikiwa ni pamoja na Sheria na Kanuni zinazokubalika. Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilitoa hati za

[8] Kupungua kwa jumla ya Hati za ukaguzi ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/19 kulisababisha kutokujumuishwa kwa miradi iliyotekelezwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji iliyotekelezwa hapo awali na Halmashauri. Miradi hii sasa inatekelezwa na RUWASA na imejumuishwa katika ripoti kuu ya Serikali Kuu

Ukaguzi zinazoridhisha sawa na 95% ya maoni yote yaliyotolewa kwa watekelezaji wa miradi ikiwa imepungua kwa asilimia mbili ikilinganishwa na 97% kwa miaka miwili iliyopita ya kifedha mfululizo yaani 2018/19 na 2017/18.

Hati Yenye Mashaka

Hati hii hutolewa wakati mkaguzi anapokuwa amejiridhisha kuwa kuna makosa kwenye taarifa za mwisho za fedha, ama moja moja au kwa ujumla wake, ingawa makosa yaliyobainika husababisha athari sehemu maalumu tu na si taarifa nzima ya fedha.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nimetoa hati zenye mashaka 15 sawa na asilimia tano ya hati zote zilizotolewa kwa watekelezaji wa Mradi wa Mfuko wa Afya. Nilibaini kuwa taarifa za kifedha zilizopata hati zenye mashaka zilitokana na hati za malipo kuwa na nyaraka pungufu hivyo kupunguza mawanda yangu ya Ukaguzi na sikuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Taarifa ya hoja zilizosababisha kupatikana kwa hati zenye mashaka imewasilishwa katika **Kiambatisho 3-1.**

Ni maoni yangu kuwa kuwapo kwa matumizi yasiyo na viambatisho kunathibitisha udhaifu katika udhibiti wa matumizi na utunzaji wa kumbukumbu za hesabu katika miradi hiyo. Hata hivyo, mwenendo wa utoaji wa hati zenye mashaka unaonesha ongezeko la asilimia tatu katika mwaka wa fedha 2019/20 ikilinganishwa na 2018/19.

Hati Mbaya

Hati hii hutolewa pale ambapo nimejiridhisha kuwa, kulingana na ushahidi uliopatikana wakati wa ukaguzi, taarifa za fedha zilizokaguliwa zina makosa makubwa na yaliyoathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha, hivyo kupelekea taarifa hizo kutokuwa sahihi. Hii inamaanisha kuwa tofauti na hati yenye shaka, taarifa za fedha zilizoandaliwa zina makosa makubwa yatokanayo na kutokukubaliana au kushindwa kukidhi mawanda na makosa hayo hayajajikita sehemu moja bali yameathiri maeneo mengi katika taarifa za fedha na hivyo kuathiri kueleweka kwa taarifa hizo kwa watumiaji wake kwa ajili ya kufanyia maamuzi.

Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, sijatoa hati mbaya kwa miradi ya maendeleo.

Kushindwa Kutoa Maoni

Mazingira ya ukaguzi yanaweza kupelekea kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi. Hii inatokea pale ambapo nimeshindwa kupata ushahidi wa kutosha au taarifa muhimu ili kufikia malengo ya ukaguzi, na endapo madhara ya kushindwa kupata ushahidi au nyaraka hizo ni makubwa sana. Hivyo, ninaonesha kwenye ripoti yangu ya ukaguzi kuwa kutokana na ukubwa wa madhara yaliyopo au yanayoweza kutokea kutokana na kukosa ushahidi wa kutosha, nimeshindwa kutoa maoni ya ukaguzi.

Kama ilivyo kwa hati mbaya, ninaposhindwa kutoa maoni, maana yake ni kuwa sehemu kubwa ya kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha hakiaminiki hivyo taarifa za fedha zilizokaguliwa hazifai kwa ajili ya kufanyia maamuzi mbalimbali.

Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020, hakukuwa na mradi wowote niliyoshidwa kutoa maoni ya ukaguzi.

3.4 Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Fedha

Sehemu hii inatoa tathmini ya hoja muhimu za ukaguzi zinazotokana na mapungufu katika usimamizi wa fedha na udhibiti kama inavyoonekana katika taarifa za kaguzi fedha 290.

3.4.1 Usimamizi wa Bajeti Usioridhisha

a) Kutolewa kwa Fedha Pungufu kwenye Miradi ya Maendeleo Sh. Bilioni 53.37

Bajeti ni zana muhimu inayosaidia watekelezaji wa miradi katika kupanga, kudhibiti na kutathmini rasilimali walizopewa na kutumika katika utekelezaji wa shughuli za miradi. Kwa asili, inaonesha shughuli zinazotakiwa kufanywa katika mwaka husika wa kifedha na inagawanya rasilimali fedha na nyinginezo zinazohitajika kwenye shughuli maalumu zilizopangwa kwa ajili ya kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilibaini kuwa watekelezaji wa miradi walishindwa kutekeleza baadhi ya shughuli zilizopangwa

kutokana na kupokea fedha pungufu kulinganisha na bajeti iliyoidhinishwa.

Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa jumla ya Sh. 53,373,154,479.82 hazikupokelewa kutoka Hazina na Washirika wa Maendeleo kwa miradi 10 iliyotekelezwa na watekeleza miradi 144 walio chini ya sekta ya Kilimo, Elimu, Nishati na Madini, Afya, sekta Mbalimbali, sekta za Jamii na Maji kama inavyoonekana katika **Jedwali 3-12.**

Jedwali 3- 12: Kutolewa kwa fedha pungufu kwenye miradi ya maendeleo Sh. Bilioni 53.37

Sekta	Bajeti (Sh.)	Fedha Zilizotolewa (Sh.)	Kiasi Kilichopokelewa Pungufu (Sh.)
Kilimo	12,547,940,491.20	3,404,435,399.12	9,143,505,092.08
Elimu	3,495,690,481.52	1,377,416,998.98	2,118,273,482.54
Nishati na Madini	1,039,810,200	850,000,000	189,810,200
Afya	85,198,577,662	65,669,629,163.67	19,528,948,501
Jamii	1,657,324,469	364,925,546.29	1,292,398,922.51
Maji	130,874,196,057.08	110,043,632,164.29	20,830,563,893
Mbalimbali	7,770,876,480.71	7,501,222,091.71	269,654,389
Jumla	**242,584,415,841.51**	**189,211,261,364.06**	**53,373,154,480.46**

Chanzo: *Taarifa za fedha kwa mwaka 2019/20*

Sekta ya maji iliongoza kwa kupokea fedha pungufu jumla ya Sh. 20,830,563,893 ikifuatiwa na sekta ya afya Sh. 19,528,948,500.69, kilimo Sh. 9,143,505,092.08, elimu Sh. 2,118,273,482.54, sekta ya kijamii Sh. 1,292,398,922.51, miradi mingine Sh. 269,654,389 na sekta ya nishati na madini Sh. 189,810,200. Hii ilihusisha miradi 10 inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolojia, Wizara ya Nishati, Wizara ya Madini, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Wizara ya Katiba na Sheria- Zanzibar, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) na 135 Halmashauri ambazo zilitekeleza miradi wa Mfuko wa Pamoja wa Afya (HBF).

Aidha, nimebaini kuwa kutolewa kwa fedha pungufu kumesababishwa na kutekelezwa kwa miradi pasipo kufuata matakwa ya makubaliano ikiwemo ucheleweshaji wa kupeleka taarifa za utekelezaji wa miradi.

Kwa maoni yangu, kuendelea kutolewa fedha pungufu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi inaongeza uwezekano wa kutofikia malengo ya Serikali kwenye mradi husika. Pia Serikali inaweza pata hasara ya ongezeko la gharama za kutekeleza miradi na inaweza kupelekea kulipa ada ya riba kwa wakandarasi kutokana na kuchelewesha au kutowalipa wakandarasi.

Ninapendekeza Watekelezaji wa Miradi kuwasiliana na Washirika wa Maendeleo ikiwemo Serikali ya Tanzania kupitia Hazina juu ya kutolewa kwa fedha za kutosha kwa ajili ya miradi zinazolingana na bajeti zilizopangwa ili kuhakikisha Mirada hii inakamilika kwa wakati ikizingatiwa miradi hii ina muda maalumu wa kukamilishwa.

b) Malipo ya Sh. Bilioni 26.54 Yalifanyika Nje ya Bajeti

Kanuni ya 115 ya Kanuni za Fedha za Umma 2001, (iliyorekebishwa 2004) inasem kwamba "Makadirio ya bajeti yaliyoidhinishwa yanaunda msingi wa hesabu za mwaka ambazo zinahusiana na kulinganisha makadirio ya bajeti kuendana na uchambuzi na uainishaji wa hesabu za mapato na matumizi".

Kinyume na matakwa hayo, nilibaini kuwa Watekelezaji wa Miradi 12 walitumia jumla ya Sh. 26,544,881,470.18 kutekeleza shughuli za miradi ambazo hazikuwa kwenye bajeti na Mpango Kazi wa Mwaka (AWP). Sekta ya elimu ilifanya matumizi makubwa nje ya bajeti Sh. 25,621,539,386 ikifuatiwa na sekta ya usafirishaji Sh. 544,404,680.08, maji Sh. 296,272,595.88, miradi mingine Sh. 45, 393,367, kilimo Sh. 33,371,441.22 na sekta ya kijamii Sh. 3,900,000. Miradi hii ilitekelezwa Wizara ya Elimu Sayansi na Tekinolojia, Wizara ya ya Ujenzi, Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Waziri Mkuu, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Jeshi la Polisi Tanzania na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST).

Hii ilitokana na rasilimali chache zilizopo katika kufanya shughuli za miradi ambayo haikutengewa bajeti kwa sababu ya mapungufu katika uandaaji wa bajeti ya shughuli za mradi. Kwa maoni yangu, matumizi nje ya bajeti inaweza kusababisha mchakato usiofaa wa manunuzi na inaweza kuathiri kutofanikiwa kwa malengo ya miradi yaliyokusudiwa.

Ninapendekeza Watekelezaji wa Miradi hasa Wizara ya Sayansi na Teknolojia kuhakikisha mipango ya shughuli za miradi inaandaliwa kwa usahihi na kuhakikisha shughuli zote zilizopangwa zinatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha na kufuata bajeti kama nyenzo ya udhibiti wa matumizi.

c) Matumizi Yaliyolipiwa katika Vifungu Visivyostahiki Shillingi Billioni 1

Kanuni ya 115 ya Kanuni ya Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa 2004) inahitaji makadirio yaliyoidhinishwa kuunda msingi wa akaunti kwa mwaka ambao wanahusiana na uainishaji wa uchambuzi wa akaunti za mapato na matumizi lazima zilingane na makadirio hayo.

Kinyume na matakwa ya kanuni, nimebaini kuwa watekelezaji miradi 20 wanaotekeleza miradi walifanya malipo yenye jumla ya Sh. 1,009,063,103.92 kwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za miradi kupitia vifungu visivyostahili pasipokuwa na idhini ya matumizi hayo.

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa, sekta ya uchukuzi imeongoza kwa kufanya malipo kutumia vifungu visivyostahili Sh. 788,184,542.92 ikifuatiwa na sekta za afya Sh. 169,950,963 na kilimo Sh. 50,927,598 kwa miradi iliyotekelezwa na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Halmashauri 18 zinazotekeleza mradi wa HBF. Aidha, kwa maoni yangu, kushindwa kutumia vifungu husika kwenye matumizi kunaweza kuathiri shughuli zilizopangwa na inaondoa dhana nzima ya umuhimu wa bajeti kama nyenzo ya udhibiti wa matumizi.

Ninapendekeza Watekelezaji wa Mradi kuhakikisha wanaandaa bajeti yenye uhalisi na kuhakikisha kuwa matumizi yanafanyika katika vifungu husika kulingana na matakwa ya

Kanuni ya 115 ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 (iliyorekebishwa 2004).

3.4.2 Kutozingatia Matakwa ya Sheria na Kanuni za Kodi

Kodi ni malipo ya lazima ya kifedha yaliyowekwa na Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa walipa kodi (mtu binafsi au taasisi) kwa ajili ya kufadhili matumizi ya serikali na matumizi mengine ya umma. Aidha nimebaini kuwa miradi 20 inayotekelezwa chini ya sekta sita haikufuata matakwa ya sheria za kodi. Mapungufu niliyobaini yamegawanyika katika maeneo matatu, ambayo ni; kutotolewa kwa risiti za kielektroniki, Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio na kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato na malipo ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye miradi iliyosamehewa.

a) Ununuzi wa Bidhaa na Huduma bila Uthibitisho wa Stakabadhi za Kielekitroniki Sh. Bilioni 2

Kanuni ya 28 (1) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi (Stakabadhi za Kielektroniki), 2012 inawataka wanunuzi wa bidhaa na huduma kuomba na kuhifadhi stakabadhi na hati za madai za kielekitroniki ili kuonesha kwa kamishina wa kodi au afisa aliyeruhusiwa kama itahitajika.

Kinyume na matakwa ya kanuni, nimebaini kuwa Watekelezaji wa Miradi 10 walifanya malipo ya jumla ya Sh. 2,006,316,606.56 kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa na huduma pasipo kudai stakabadhi za kielekitroniki iliyosababishwa na kushindwa kufuatilia stakabadhi hizo kutoka kwa wasambazaji na watoa huduma. Kushindwa kudai na kuhifadhi stakabadhi za kielekitroniki kunahamasisha ukwepaji kodi pia inadhoofisha juhudi za Serikali katika kuongeza ukusanyaji wa kodi.

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa, sekta ya uchukuzi imeongoza kufanya malipo pasipo kudai stakabadhi za kielektroniki kwa Sh. 1,213,108,490.44, sekta ya afya Sh. 478,801,938, sekta ya elimu Sh. 180,998,285.48 na sekta ya kijamii Sh. 133,407,892.64 kwa Taasisi za Serikali zifuatazo Wizara ya Elimu Sayansi na Tekinolojia, Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa-Kagera, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa-Njombe na Halmashauri 39 zinazotekeleza miradi ya Afya (HBF).

Natoa wito kwa Watekelezaji wa Mirad kutekeleza Kanuni ya 28(1) ya Kodi ya Mapato (Vifaa vya Mfumo wa Kielektroniki), 2012 na kifungu cha 29(4) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kudai stakabadhi ya kielectronic kwa kila miamala inayofanywa kwa watoa huduma ambapo itasaidia kuongeza makusanyo za Serikali.

b) Kodi ya Zuio ya Sh. Milioni 91.79 Haikuwasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania

Kifungu 83(1) (b) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004 (Iliyorekebishwa mwaka 2008) kinataka Taasisi zote kukata kodi ya zuio kutoka kwa wazabuni wa bidhaa na huduma na kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania siku saba baada ya mwisho wa mwezi.

Ukaguzi wangu umebaini, watekeleza miradi 14 wanaotekeleza miradi tisa hawakuwasilisha malipo ya kodi ya zuio kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kiasi cha Sh. 91,795,481.09 kwa makato yaliyofanywa kwenye malipo ya wauzaji na watoa huduma hivyo Serikali ilikosa mapato yake kutokana na kodi ambazo hazikukusanywa.

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa, sekta ya elimu imeongoza kwa kutokuwasilisha kiasi cha Sh. 44,977,082.73, ikifuatiwa na sekta ya usafirishaji Sh. 17,159,363.86, miradi mingine Sh. 13,577,165.50, sekta ya afya Sh. 8,048,443 na sekta ya kijamii Sh. 8,033,426 ya miradi 14 iliyotekelezwa na Wizara na Elimu Sayansi na Tekinolojia, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (MoLF), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakala wa Serikali wa Barabara, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), Taasisi ya Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) na Halmashauri sita zinazotekeleza mradi wa Mfuko wa Afya (HBF).

Hivyo, kutowasilishwa kwa kodi ya zuio kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ilitokana na usimamizi usiridhisha wa Taaisisi husika juu ya kukatwa kwa ushuru na kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kwa maoni yangu, kutowasilishwa kwa kodi ya zuio

inakwamisha juhudi za Serikali kupata ushuru unaotarajiwa kutoka kwa vyanzo hivi kwa wakati unaofaa.

Ninapendekeza Watekelezaji wa Mradi kuimarisha udhibiti wa mifumo ya ndani na kuhakikisha kuwa sheria, kanuni, miongozo na maagizo yanayohusiana na ukusanyaji wa kodi inatekelezeka. Hii itawezesha kuongezeka kwa mapato na kuepuka uwezekano wa kulipa tozo na adhabu zitokanazo na ukiukwaji wa sheria.

c) Malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sh. Bilioni 9.88 kwa Miradi Iliyosamehewa Kodi

Nilibaini kuwa miradi sita ililipa Kodi ya Ongezeko la Thamani jumla ya Sh. 9,881,517,997.56 iliyosamehewa kinyume na matakwa ya makubaliano juu ya marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Hii ilitokana na mipango isiyoridhisha na urasimu juu ya ufuatiliaji wa idhini ya msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kutoka Serikalini. Hii inaathiri hali ya fedha za miradi na inadhoofisha juhudi za Serikali za kufuata makubaliano ya miradi.

Uchambuzi wangu umebaini kuwa, sekta ya maji imeongoza kwa kulipa malipo ya kodi ya ongezeko la thamani kwa miradi iliyosamehewa kwa Sh. 9,420,507,149.81, ikifuatiwa na sekta ya elimu Sh. 189,305,083.70 na sekta ya usafirishaji Sh. 178,928,791.26 kwa miradi sita iliyotekelezwa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Fedha na Mipango, Wakala wa Barabara Tanzania, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza (MWAUWASA), Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha (AUWSA) na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Ninapendekeza kwamba katika siku zijazo, Watekelezaji wa Miradi hasa miradi ya Sekta ya Maji kufuata matakwa ya makubaliano na wafadhili iliyosainiwa kwa kuomba msamaha wa kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania. Pia, Maafisa Masuuli wanapaswa kuwajibika kwa kiwango cha kodi ya Ongezeko la Thamani kitakacholipwa kinyume na makubaliano.

3.4.3 Mapungufu ya Udhibiti wa Matumizi Sh. Bilioni 5.99

Uanzishaji wa mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani ni moja ya majukumu ya menejimenti na utaratibu kuwa kuhakikisha malipo yote yanafanyiwa ukaguzi wa awali kabla ya kuidhinishwa. Kitengo cha ukaguzi wa awali kinahakiki iwapo udhibiti wa ndani umezingatiwa, fedha zimetengwa na zipo na viambatisho vya malipo vinatosheleza kwenye hati za malipo. Ukaguzi wangu kwenye usimamizi wa matumizi umebaini mapungufu katika udhibiti wa ndani kwenye miradi 80 yenye jumla ya Sh. 5,998,064,998 yanayotokana na malipo ambayo hayakufanyiwa Ukaguzi wa awali, malipo kufanyika bila kuwa na viambatisho na hati za malipo zilizokosekana wakati wa ukaguzi.

a) Malipo ambayo Hayakufanyiwa Ukaguzi wa Awali Sh. Bilioni 1.37

Kanuni ya 91 (6) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa 2004) inataka nakala halisi za hati za malipo kufanyiwa ukaguzi wa awali na afisa aliyeidhinishwa.

Nilibaini Watekelezaji wa Miradi 14 wanaotekeleza miradi minne walifanya malipo yenye jumla ya Sh. 1,367,361,048 kwa shughuli za miradi ya maendeleo pasipo kufanywa kwa Ukaguzi wa awali kwenye malipo hayo.

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa, miradi mingine iliongoza katika kufanya malipo pasipo Ukaguzi wa awali jumla ya Sh. 956,952,211, ikifuatiwa na sekta ya afya Sh. 309,328,837 na sekta ya kijamii Sh. 101,080,000 kwa miradi minne iliyotekelezwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa- Kagera na Halmashauri 11 zinazotekeleza mradi wa mfuko wa afya wa pamoja (HBF).

Mapungufu katika ukaguzi wa awali yanahatarisha kufanyika kwa malipo yasiyostahili ambayo inapelekea upotevu wa fedha za walipa kodi.

Ninapendekeza Watekelezaji Miradi kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa awali na kuhakikisha kuwa malipo yote yanafanyiwa Ukaguzi wa awali kabla ya kuidhinishwa.

b) Malipo Yaliyofanywa Bila kuwa na Viambatisho na Hati za Malipo Zilizokosekana wakati wa Ukaguzi Sh. Bilioni 4.57

Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (iliyorekebishwa 2004) inataka hati ya malipo ambayo ina viambatisho pungufu kutambulika kama hati ya malipo iliyokosekana wakati wa ukaguzi. Kwa kuongezea Agizo la 8 (2) (c) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linawataka wakuu wa idara pamoja na watunza hazina kutunza na kudhibiti nyaraka za fedha katika idara zao.

Ukaguzi wangu umebaini hati za malipo zenye jumla Sh. 4,565,626,453.49 yaliyofanywa na watekelezaji wa miradi 80 yalikuwa na viambatisho pungufu kama risiti za kukiri mapokezi, hati za kupokelea mizigo na ankara.

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa, miradi mingine iliongoza kuwa na hati za malipo zenye nyaraka pungufu zenye jumla ya Sh. 1,497,169,026 ikifuatiwa na sekta ya elimu Sh. 1,355,726,497.17, sekta ya afya Sh. 765,780,293, sekta ya usafirishaji Sh. 542,515,330.19, sekta ya kijamii Sh. 365,424,055,136; na Sekta ya Maji Sh. 39,011,252 kwa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Makamu wa Rais, Tume ya Mipango ya Zanzibar (ZPC), Taasisi ya Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) Mwanza, Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo na Halmashauri 44 zinazotekeleza mradi wa mfuko wa afya (HBF).

Ukaguzi wangu ulibaini watekelezaji wa miradi watatu walishindwa kuwasilisha hati za malipo wakati wa ukaguzi zenye jumla ya Sh. 65,077,497 kati ya hizo miradi mingine Sh. 54,655,697 na sekta ya afya Sh. 10,421,800 kwa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Viwanda na Biashara na Halmashauri nne. Kutowasilishwa kwa hati za malipo wakati wa ukaguzi imepunguza mawanda ya ukaguzi na sikuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Ninapendekeza Watekelezaji wa Miradi kuimarisha usimamizi wa utunzaji wa nyaraka za kihasibu na kuanzisha hatua

madhubuti ambazo zitahakikisha ukamilifu wa utunzaji wa hati za malipo pamoja na viambatisho vyake.

3.4.4 Tozo ya Riba kwa Uchelewaji wa Malipo ya Wakandarasi Sh. Bilioni 8.18

Kifungu cha 51.1 cha Sharti Kuu la Mkataba (GCC) kinamtaka Mwajiri kumlipa Mkandarasi kiasi kilichothibitishwa na Meneja wa Mradi ndani ya siku 28 tangu kupokea tarehe ya hati za madai ya wakandarasi. Ikiwa Mwajiri amecheleweshа malipo, mkandarasi atalipwa tozo ya riba kwenye malipo yanayofuata. Riba itahesabiwa kutoka tarehe ambayo malipo yalipaswa kufanywa hadi tarehe ambapo malipo yalipolipwa kulingana na kiwango cha riba kilichotolewa na Benki ya Tanzania wakati wa tarehe ya kusaini mkataba". Katika mikataba mingine kipindi hiki kinaongezwa hadi siku 56 baada ya wahandisi kupokea nyaraka muhimu.

Kinyume na matakwa ya sharti kuu la mikataba, nilibaini miradi minne chini ya sekta ya uchukuzi ilikuwa na tozo ya riba kiasi cha Sh. 8,178,283,863 kama adhabu ya kuchelewesha kulipa madai ya wakandarasi (IPCs).

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa, sekta ya uchukuzi inaongoza kuchelewa malipo ya wakandarasi ambapo Sh. 3,466,386,456.88 ilihusisha Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji (TSSP), Mradi wa Maendeleo ya Reli Tanzania (TIRDP) Sh. 2,197,609,697.74, Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kimataifa Arusha-Taveta/Holilii-Voi Sh. 1,847,308,621.55 na Mradi wa Uboreshaji Usafiri wa Mjini Dar es Salaam (DUTP) Sh. 666,979,087.41.

Nilibaini kuwa madai ya tozo ya riba yalisababishwa na ucheleweshaji wa kupokea fedha za miradi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kutokana na ufuatiliaji usioridhisha wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambayo inazuia Wakala wa Barabara Tanzania na Shirika la Reli Tanzania kulipa wakandarasi kwa wakati. Ni maoni yangu, kwamba kuchelewa kuwalipa wakandarasi kunazorotesha shughuli za miradi ya maendeleo na pia tozo za riba zinaongeza gharama za miradi kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na makadirio ya awali.

Ninapendekeza Watekelezaji wa Miradi kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kutoa fedha za kutosha za miradi kulingana na bajeti ambazo zitawawezesha watekelezaji wa miradi kulipa madai ya wakandarasi kwa wakati.

3.4.5 Mapungufu katika Usimamizi wa Masurufu Sh. Bilioni 1.99

Ninaelewa kuwa Maafisa Masuuli wanaweza kuidhinisha masurufu kwa Afisa aliyeidhinishwa kwa ajili ya matumizi rasmi ya ofisi. Masurufu yanatakiwa kutolewa endapo matumizi yanayotarajiwa yawe yametengewa bajeti. Kiwango cha chini cha masurufu kinatakiwa kidhibitishwe na Masurufu yatolewe kwa ajili ya kutimiza lengo husika.

Kwa kuongezea, Kanuni ya 103 (1-2) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa 2004) inaelekeza masurufu kurejeshwa baada kumaliza kazi iliyokusudiwa. Endapo afisa aliyepewa masurufu akishindwa kurejesha ndani ya siku 30 kabla ya mwaka wa fedha kuisha kama itavyoamriwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali, atalazimika kutakatwa mshahara au posho zake kwa kiasi ambacho hakikurejeshwa. Pia, Aya ya 5.17 ya Mwongozo wa Uhasibu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2009 inazitaka halmashauri kuanzisha rejesta ya masurufu ili kurahisisha utunzaji wa kumbukumbu na urejeshaji wa masurufu kwa usahihi na ufanisi.

Kinyume na matakwa hayo, nimebaini Watekelezaji wa Miradi 12 walikuwa na mapungufu katika usimamizi wa masurufu, ikiwa ni pamoja na kutorejesha, kuchelewa kurejesha, kutorekodiwa kwenye rejista na kukosekana kwa taarifa za maafisa husika waliopatiwa masurufu.

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa Watekelezaji wa Miradi watano walishindwa kurejesha masurufu yenye jumla ya Sh. 625,886,455.49. Pia nimebaini uchelewaji wa kurejesha masurufu baada ya kazi husika kumalizika Sh. 689,134,266 kwa watekelezaji wa miradi minne. Kwa kuongezea, nimebaini watekelezaji wa miradi wawili walishidwa kuandaa rejista ya masurufu. Zaidi ya hayo, watekeleza miradi wawili walishindwa kunipatia taarifa za maafisa husika waliopatiwa masurufu. **Jedwali Na. 3.13.**

Jedwali 3- 13: Mapungufu katika usimamizi wa masurufu Sh. 1,997,518,128.49

Na	Maelezo	Watakeleza Miradi	Kiasi (Shs)
1	Masurufu yasiyorejeshwa	5	625,886,455.49
2	Masurufu yaliyochelewa kurejeshwa	4	689,134,266.00
3	Masurufu yasiyorekodiwa kwenye rejista	1	57,885,000.00
4	Masurufu yasiyo na majina/taarifa za maafisa husika waliopatiwa	2	624,612,407.00
Total		**12**	**1,997,518,128.49.00**

Chanzo: *Hati za malipo and leja za hesabu*

Sekta zenye mapungufu katika usimamizi wa masurufu ni sekta ya kilimo Sh. 253,257,283, sekta ya kijamii Sh. 25,590,000, sekta ya usafirishaji Sh. 73,144,262.49 na miradi mingine Sh. 322,487,064. Kiasi hiki ni kwa miradi 13 iliyotekelezwa na Tume ya Mipango Zanziba (ZPC), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRGG), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Wizara ya Viwanda na Biashara (MoIT), Wizara ya Elimu Sayansi na Tekinolojia, Wizara ya Katiba na Sheria (MOCLA) na Halmashauri nane.

Mapungufu haya yanatokana na Taasisi husika kushindwa kusisitiza usimamizi na utekelezaji wa matakwa ya kanuni zinazosimamia udhibiti wa masurufu ambapo yasiposhughulikiwa yanaweza kutoa mwanya wa matumizi mabaya ya fedha za umma.

Ninapendekeza Watekelezaji wa Miradi kuweka udhibiti madhubuti unaosimamia utoaji, urejeshaji na kurekodi masurufu kwenye rejista ili kuendana na Kanuni ya 103 (1-2) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa 2004) na aya 5.17 ya Mwongozo wa Uhasibu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009.

3.4.6 Fedha za Miradi Zilizokopwa Bila Kurejeshwa Sh Bilioni 1.36

Usimamizi wa fedha za mradi ni muhimu kwa kufuata matakwa ya makubaliano yanayoelezwa kwenye hati za miradi kama Mkataba wa Fedha, Mwongozo wa Utekelezaji wa Miradi, Mkataba wa Makubaliano na Miongozo mingine inayosimamia utendaji wa miradi. Miongoni mwa maelekezo muhimu katika taarifa hizo za

miradi ni kuwataka watekelezaji wa miradi kuhakikisha fedha za miradi zinatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Nimebaini kuwa, Afisa Masuuli wa Programu ya Elimu na Ujuzi kwa Ajili ya Kazi za Uzalishaji (ESPJ) inayotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia alikopa Sh 1,360,377,044 ili kugharamia matumizi mbali mbali ya kawaida bila kurejesha fedha hizo kwenye miradi husika. Hii ilisababishwa na mapungufu ya udhibiti wa ndani katika usimamizi wa fedha. Ni maoni yangu kwamba, kutorejesha fedha hizo kunaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za miradi zilizokusudiwa.

Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha fedha za Programu ya Elimu na Ujuzi kwa Ajili ya Kazi za Uzalishaji (ESPJ) zilizokopwa zinarejeshwa ili kutoathiri utekelezwaji wa miradi iliyopangwa.

3.4.7 Malipo ya Sh. Milioni 450.96 Yasiyokubalika kwa Mujibu wa Mwongozo ya Mpango Kabambe wa Afya

Miongoni mwa madhumuni ya Mpango Kabambe wa Afya (CCHP) ni kuhakikisha kuwa mipango ya afya ya kila mwaka inaelekeza fedha katika maeneo yenye vipaumbele kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za afya na kusaidia kuidhinishwa kwa fedha hizo. Wakati huo huo, Aya 3.5 (j) ya mwongozo wa mpango kabambe wa afya CCHP 2011 inazitaka Halmashauri kutekeleza shughuli zote zilizoidhinishwa katika CCHP pasipo kugawanya fedha kwenye matumizi mengine, pia inasisitiza kuwa fedha za mfuko wa afya wa pamoja kutotumika katika matumizi ya posho ya vikao, honoraria, posho maalum ya kujikimu kwa Timu ya Usimamizi wa Afya ya Halmashauri (CHMT), Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri (CHSB) na mikutano ya kawaida ya Kamati ya Usimamizi wa Vituo vya Afya (HFGC). Pakiwa na ulazima, Halmashauri zitumie vyanzo vingine vya fedha kama vile ruzuku, mapato ya ndani n.k.

Kinyume na matakwa ya mpango kabambe wa afya, nimebaini jumla ya Sh. 450,960,762 zilitumika katika Halmashauri 33 zinazotekeleza mradi wa HBF kugharamia shughuli zinazohusiana na afya ambazo haziruhusiwi na mwongozo wa mpango kabambe wa afya CCHP. Hii ilisababishwa na mapungufu katika udhibiti wa

ndani dhidi ya bajeti ya fedha za Mfuko wa Afya wa Pamoja (HBF). Kwa maoni yangu, kufanyika kwa malipo yasiyokubalika kunaathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa lakini pia inaonesha kutofuata matakwa ya mwongozo wa mpango kabambe wa afya.

Ninapendekeza Watekelezaji wa Mfuko wa Afya wa Pamoja (HBF) kuongeza udhibiti wa malipo na kuhakikisha malipo yote yanafanywa kwa shughuli zilizopangwa.

3.4.8 Mapungufu ya Usimamizi wa Upokeaji wa Fedha za Miradi Sh. Bilioni 178.4

Upokeaji wa fedha za mradi unatarajiwa kuendana na ratiba ya utekeklezaji wa shughuli za miradi kama ilivyoidhinishwa katika Mpango wa utekelezaji shughuli za miradi wa mwaka (AWP) kwa kila mradi.

Nilibaini kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ilichelewesha kuhamisha fedha za miradi kiasi cha Sh. 167,597,672,389.01 kwa miradi miwili inayotekelezwa na Chuo cha Kilimo cha Sokoine na miradi mitatu iliyotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolojia. Uchelewaji ulisababishwa na mapungufu ya vitengo vya uratibu wa miradi katika ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa fedha zinapokelewa kwenye miradi kwa wakati na changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza Waraka wa Hazina Namba 2 unaohusiana na utaratibu wa kuomba na kuhamisha fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwenda moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo (Direct to Project Fund).

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa sekta ya elimu inaongoza kwa kuchelewa kupokea fedha za miradi Sh. 161,930,358,580.01, sekta ya kijamii Sh. 2,774,968,573, sekta ya kilimo Sh. 2,144,051,116 na miradi mingine Sh. 748,294,120.

Kwa kuongezea, nilibaini taasisi za Serikali ambazo zilichelewa kupokea fedha za miradi ni Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Elimu Sayansi na Tekinolojia kwa jumla ya Sh. 10,799,061,241 kwa utekelezaji wa shughuli za miradi zilizopangwa. Uchambuzi wangu unaonyesha kuwa sekta za kilimo na uchukuzi

zilicheleweshwa fedha kiasi cha Sh. 7,763,142,321 na Sh. 3,035,918,920, mtawalia.

Ninapendekeza Watekelezaji wa Miradi kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kutoa fedha za utekelezaji wa miradi kwa wakati kulingana na bajeti; kwa upande mwingine, ninawahimiza watekelezaji wa miradi pindi wanapopokea fedha hizo, kuziwasilisha kwa taasisi husika kwa wakati.

3.4.9 Serikali Kutochangia Sehemu ya Ufadhili wa Miradi Kiasi cha Sh. Bilioni 1.08

Mchango wa kifedha kwa Watekelezaji wa Mradi kutoka Serikalini ni jambo muhimu kwenye makubaliano yaliyosainiwa kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo yanahitaji Serikali kuchangia ufadhili wa miradi. Hii inamaanisha, Serikali pamoja na washirika wa maendeleo kutoa ufadhili kwa pamoja.

Kinyume na matakwa ya makubaliano, nimebaini kuwa Serikali haikuchangia Sh. 1,080,000,000 kwenye mradi wa Mpango wa Tanzania wa Kuzuia Mfumuko wa bei (TANIPAC).

Kwa maoni yangu, Serikali kutochangia ufadhili wa miradi kunaweza kukwamisha utekelezaji wa miradi kwa ufanisi na hivyo walengwa kushindwa kunufaika na miradi husika.

Napendekeza Serikali kuchangia kiwango cha fedha ilichoahidi kukitoa kwenye utekelezaji wa Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu kulingana na makubaliano.

3.4.10 Kuchelewa Kulipa Fidia kwa Waathirika wa Miradi Sh. Bilioni 3.95

Kifungu 26.2 cha Sharti Kuu la Mkataba pamoja na Sehemu ya 8.5 ya Mwongozo wa Utekelezaji wa Mradi wa Kuboresha Miji Tanzania (TSCP), 2017 inataka fidia kwa waathirika wa miradi kulipwa kwa wakati kabla ya utekelezaji wa mradi.

Mapitio ya usimamizi wa miradi yamebaini kuwa fedha za fidia kiasi cha Sh. 3,952,778,191.01 hazikulipwa kwa watu walioathirika na utekelezaji wa mradi wa Kuboresha Miji Tanzania (TSCP). Hii inachangiwa na Wizara ya Fedha na Mipango

kuchelewesha utoaji fedha. Hii inaweza kupelekea migorogoro ya kisheria na hivyo kuongeza gharama kwa Serikali.

Nawashauri Watekelezaji wa Miradi ya Maendeleo hasa Wakala wa Barabara Tanzania kuhakikisha kuwa wanawafidia bila kuchelewa watu walioathirika na utekelezaji wa miradi hii ili kuepusha migogoro na gharama kwa Serikali hasa pale itakaposhindwa kesi.

3.4.11 Bakaa ya Sh. Bilioni 1.27 Hazijarejeshwa kwenye Akaunti Zinazotunza Fedha za Washirika (Holding Accounts)

Kifungu cha 5.6 cha Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo katika kuunga mkono Programu ya Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) inataka fedha za miradi zilizosalia kurejeshwa kwenye Akaunti zinazotunza fedha za Washirika wa Maendeleo.

Nimebaini kuwa Sh. 1,268,939,611.07 ikiwa ni bakaa ya fedha za mradi wa Mfuko Mkuu wa Fedha za Afya hazijarejeshwa kwenye Akaunti zinazotunza fedha za Washirika wa Maendeleo (Holding Accounts) kwa muda wa miaka mitatu kutokana na maombi ya kuhamisha fedha hizo kuchelewa kupelekwa Wizara ya Fedha na Mipango.

Hii ilisababishwa na uchelewaji wa kupata idhini ya kurejesha fedha hizo. Aidha, kuchelewa kurejeshwa kwa bakaa ya fedha kwenye Akaunti zinazotunza fedha za Washirika wa Maendeleo kunaweza kuathiri mapokezi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

Naishauri Hazina kutoa kibali cha kuhamisha fedha amabazo hazikutumika kutoka katika Programu ya Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) kwenda kwenye akaunti zinazotunza fedha za Washirika wa Maendeleo ili kutimiza mkataba wa makubaliano.

3.4.12 Kucheleweshwa kwa Malipo ya Posho ya Motisha na Gharama za Kiutawala Sh. Bilioni 91.65

Aya 1.2 ya Mwongozo wa Ufadhili kwa Matokeo *(Result Based Financing)* inataka Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,

Wazee na Watoto kutoa uangalizi wa jumla wa mfumo wa Ufadhili kwa Matokeo (RBF) ili kuhakikisha utekelezaji bora. Pia, aya ya 3.18 inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha Vituo vya Afya vinapata malipo yao ya motisha ndani ya siku 28 baada ya kazi ya uthibitishaji matokeo.

Mapitio ya taarifa za utekelezaji na nyaraka nyingine za Programu ya Kuimarisha Afya ya Msingi kwa Matokeo inayotekelezwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhusu ulipaji wa motisha kwa wadau mbalimbali zinaonesha kuwepo kwa madai ya motisha kwa Bohari Kuu ya Dawa, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa na vituo vya Afya vyenye jumla ya Sh. 91,648,358,361.04. Malipo hayo yalipaswa kufanyika kabla ya tarehe 30 Juni 2020, lakini hadi wakati wa kumaliza ukaguzi huu Novemba 2020 motisha hizo hazikulipwa.

Miongoni mwa sababu zilizochangia, ni kutofuatwa kwa matakwa ya mfumo wa Ufadhili kwa Matokeo (RBF) katika utoaji wa fedha za mradi kwenda kwa watekelezaji, hii ilitokana na ufuatiliaji dhaifu wa Taasisi husika ikiwemo Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kucheleshwa kwa malipo ya motisha kunapunguza ari ya kufanya kazi kwa watumishi husika, pia kunaleta kutofikiwa kwa malengo ya programu.

Nashauri menejimenti ya Wizara Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto kwa pamoja kuhakikisha malipo ya motisha na gharama za kiutawala yanafanyika kwa wakati kwa watekelezaji wa Programu ya mfumo wa Ufadhili kwa Matokeo (RBF).

3.4.13 Fedha Zilizohamishiwa kwenda Ofisi za Uhakiki Ubora wa Shule kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi Mpya Kabla ya Utambuzi wa Eneo la Ujenzi Sh. Bilioni 10

Tarehe 24 Juni 2020 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilihamisha kiasi cha Sh. 9,999,998,861 kwenda kwa Shule 55 za

Uhakiki Ubora kupitia hundi nambari 000064 ikiwa ni kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi mpya za Uhakiki Ubora katika Wilaya na Manispaa.

Mapitio yangu ya hali ya utekelezaji wa mradi kwa Matokeo Makubwa Sasa (EPforR) nilibaini kuwa, michoro ya kimuundo na Makadirio ya Gharama za Ujenzi (BOQ's) yaliandaliwa Machi 2020 na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kabla ya utambuzi wa maeneo ya ujenzi. Ziara ya eneo la mradi iliyofanywa mwaka Oktoba 2020 ilibaini kuwa, ujenzi wa shule za Uhakiki Ubora kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati ulikuwa bado haujaanza kwa sababu ya kutopatikana kwa eneo la ujenzi.

Hali hii ilitokana na mipango isiyoridhisha kabla ya kuanza kwa mradi. Ni maoni yangu kuwa, ucheleweshaji wa kulitambua eneo la ujenzi unaweza kusababisha kuongezeka kwa muda wa kukamilisha mradi. Pia, kukosekana kwa nyaraka za umiliki kunaweza sababisha mizozo na kupoteza rasilimali zilizowekezwa.

Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha maandalizi ya utekelezwaji wa miradi ya maendeleo kwa Mradi wa Elimu ya Malipo kwa Matokeo (EPforR) yanafanywa kwa umakini ikiwa ni pamoja na kuzingatia kuwa maeneo kwa ajili ya ujenzi yanatambuliwa kabla ya fedha kupelekwa kwa watekelezaji miradi.

SURA YA NNE

USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA

4.1 Utangulizi

Usimamizi wa manunuzi na mikataba ni miongoni mwa mambo muhimu katika usimamizi wa miradi kwani inahusisha kiasi kikubwa cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya miradi na zinahusisha masuala hatarishi ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kutopata thamani ya fedha. Usimamizi wa manunuzi na mikataba inayohusiana na miradi ya maendeleo nchini Tanzania kwa kiasi kikubwa inaongozwa na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013, mikataba kati ya taasisi nunuzi na wazabuni, miongozo na waraka mbalimbali. Kwa hiyo, usimamizi wa manunuzi na mikataba ulifanyika katika ukaguzi wangu ili kujiridhisha kwamba sheria, taratibu pamoja haki na uwazi ulizingatiwa katika michakato yote ya manunuzi.

4.2 Usimamizi wa Manunuzi

4.2.1 Manunuzi ya Bidhaa na Huduma Yenye Thamani Sh. Milioni 441.17 bila Kibali cha Bodi za Zabuni

Kifungu 35(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 (Iliyorekebishwa mwaka 2016) kinakataza mtu au kampuni kusaini mkataba na taasisi yoyote ya Umma isipokuwa zabuni hiyo iwe imeidhinishwa na Bodi ya Zabuni.

Kinyume na kifungu kilichotajwa, katika kupitia nyaraka mbalimbali zinazohusiana na manunuzi ya bidhaa na huduma nilibaini kuwa miradi mitatu iliyotekelezwa na watekelezaji wa miradi 18 katika sekta za maji, jamii na afya walifanya manunuzi mbalimbali ya bidhaa na huduma yenye kiasi cha Sh. 441,166,183 bila idhini ya Bodi za Zabuni.

Manunuzi yenye thamani kubwa yaliyoidhinishwa bila kibali cha Bodi ya Zabuni ni Sh. 330,227,053 yaliyofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 16 zilizotekeleza mradi wa Mfuko wa Afya (HBF) ikifuatiwa na Programu ya Usambazaji wa Huduma ya Maji Safi Vijijini inayotekelezwa na Wizara ya Maji yenye kiasi cha Sh. 95,195,643 pamoja na Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii

(TASAF) wenye manunuzi ya Sh. 15,743,487. Miradi hii ipo chini ya sekta ya afya, maji na jamii, mtawaliwa.

Nilibaini kuwa kufanyika kwa manunuzi bila ya idhini ya Bodi za Zabuni kulisababishwa na kutozingatiwa mifumo ya udhibiti iliyowekwa na watekelezaji wa miradi katika kutatua tatizo hili. Tatizo hili haliashirii tu uwezekano mkubwa wa kutoa zabuni kwa watu wasio na uwezo, bali unapunguza pia uwazi katika mchakato mzima wa manunuzi husika.

Ninashauri menejimenti za watekelezaji wa miradi husika kufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake ili kuhakikisha kuwa manunuzi ya bidhaa na huduma yanaidhinishwa na Bodi za Zabuni husika.

4.2.2 Manunuzi ya Thamani ya Sh. Milioni 917.64 Yalifanyika Bila Kushindanisha Wazabuni

Kanuni ya 131 (5) inaelekeza taasisi za manunuzi kufanya ushindanishi wa bei katika manunuzi ya bidhaa au huduma kwa kutumia nukuu za bei angalau tatu kutoka kwa wazabuni mbalimbali; na mzabuni mwenye bei ya chini na kwa kuzingatia bei ya soko ndio atapewa mkataba wa manunuzi.

Katika kupitia mchakato wa manunuzi nilibaini kuwa watekelezaji wa miradi 25 walifanya manunuzi ya bidhaa na huduma yenye thamani ya Sh. 917,644,344.50 bila ya kushindanisha wazabuni kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 4.1. Hali hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na Maafisa Masuuli kutohimiza uwepo wa ushindani kwa manunuzi yaliyoanzishwa na Taasisi zao. Hali hiyo inatia shaka kama thamani ya fedha ilipatikana katika taasisi husika zilizofanya manunuzi hayo.

Jedwali 4- 1: Manunuzi ya thamani ya Sh. Milioni 917.64 yalifanyika bila kushindanisha wazabuni

Na.	Jina la Mradi	Mtekelezaji Mradi	Sekta	Kiasi(Sh.)
1	Mradi wa Kusaidia Elimu kwa Walimu (TESP)	Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia	Elimu	286,076,686
2	Mradi wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo (EPforR)			224,808,699.50

Na.	Jina la Mradi	Mtekelezaji Mradi	Sekta	Kiasi(Sh.)
3	Programu ya Kuimarisha Huduma ya Afya ya Msingi (SPHCforRP)	Wizara ya Afya	Afya	19,962,537
4	Mfuko wa Uchangiaji wa Afya(HBF)	Mamlaka za Serikali za Mitaa 20	Afya	219,400,038
5	Kuimarisha Upatikanaji wa Haki na Ulinzi wa Haki za Binadamu nchini Tanzania	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG)	Jamii	13,405,000
6	Kulinganisha Umaskini-Mazingira - Jinsia-Mabadiliko ya Hali ya Hewa malengo yatakayopelekea maendeleo ya kiuchumi ya ndani (LED) na Malengo ya Maendeleo Endelevu(SDG) ya ndani kwa ajili ya Maendeleo Endelevu na Kutokomeza Umaskini Tanzania	Taasisi ya Mipango ya Maendeleo Vijijini Kituo cha Kanda ya Ziwa (IRDP)		105,059,700
7	Programu ya Maendeleo katika Sekta ya Maji-Awamu ya Pili (WSDP II) - Inayofadhiliwa na Wahisani mbalimbali na Serikali ya Tanzania	Wizara ya Maji	Maji	48,931,684
Jumla				**917,644,344.50**

Chanzo: *Nyaraka za zabuni 2019/20*

Ninashauri watekelezaji wa miradi husika kuhakikisha wazabuni wa bidhaa na huduma wanachaguliwa kwa ushindani kwa lengo kupata bidhaa na huduma zenye ubora wa hali ya juu na kwa bei nafuu ili kupata thamani ya fedha katika matumizi ya fedha za Umma. Vile vile, ikiwa manunuzi yanafanyika kwa wauzaji au mtoa huduma mmoja, watekelezaji wa miradi wanapaswa kutafuta uhalali wa maamuzi hayo.

4.2.3 Manunuzi Yaliyopangwa ambayo Hayajafanyika Sh. Bilioni 104.85

Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 inataka taasisi inayofanya manunuzi kukadiria mahitaji yake ya bidhaa, huduma na kazi kwa usahihi kama zinavyoonekana katika mpango kazi wa mwaka pamoja na makadirio ya mwaka.
Kinyume na kanuni tajwa hapo juu, katika mapitio ya nyaraka za manunuzi nilibaini kuwa watekelezaji wanne wa miradi ya Elimu

wa Lipa Kulingana na Matokeo (EPforR), Programu ya Elimu na Ujuzi kwa Ajili ya Uzalishaji wa Ajira (ESPJ), Mradi wa Kuleta Mabadiliko Katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki unaotekelezwa na Wizara ya Elimu katika Taasisi ya Teknolojia – Dar es Salaam na Chuo cha Usafirishaji hawakufanya manunuzi yaliyopangwa yenye thamani ya Sh. 104,849,722,238. Rejea Jedwali Na. 4.2.

Nilibaini kuwa upungufu huu umesababishwa na kuchelewa kwa idara husika kutangaza zabuni na kutoa mikataba kwa wazabuni. Ucheleweshaji huu huongeza uwezekano wa kupanda kwa bei kwa bidhaa na huduma, hivyo menejimenti inatakiwa kuharakisha utekelezaji wa manunuzi yaliyopangwa kwa wakati ili kufikia malengo ya mradi yaliyokusidiwa.

Jedwali 4- 2: Manunuzi yaliyopangwa ambayo hayajafanyika

Na.	Jina la Mradi	Jina la Mtekelezaji wa Mradi	Sekta	Kiasi (Sh.)
1	Mradi wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo (EPforR)	Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia	Elimu	74,985,517,538
2	Programu ya Elimu na Ujuzi kwa ajili ya Uzalishaji wa Ajira-(ESPJ)	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Elimu	18,000,000,000
3	Mradi wa Kuleta Mabadiliko Katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki - Taasisi ya Teknolojia - Dar es Salaam	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Elimu	4,923,604,800
4	Mradi wa Kuleta Mabadiliko Katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki - Chuo cha Usafirishaji	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Elimu	6,940,599,900
Jumla				**104,849,722,238**

Chanzo: ***Mpango wa Manunuzi na ripoti ya manunuzi ya mwaka** 2019/20*

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha kuwa, mchakato wa manunuzi, utoaji na utekelezaji wa mikataba unafanywa kulingana na Mpango wa Ununuzi wa Mwaka. Vile vile manunuzi ambayo yalipangwa

kufanyika katika mwaka wa fedha 2019/20 yanafanywa katika mwaka wa fedha unaofuata.

4.2.4 Manunuzi Kiasi cha Sh. Bilioni 12.02 Ambayo Hayakujumuishwa Katika Mpango wa Manunuzi

Nilibaini kuwa manunuzi ya kiasi cha Sh. 12,018,961,647.40 yalifanyika katika miradi mitatu ya sekta tatu ambayo hayakujumuishwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka kinyume na Kanuni ya 69 (7) ya Kanuni za Manunuzi wa Umma ya Mwaka 2013 (Iliyorekebishwa 2016) ambayo inaitaka taasisi inayofanya manunuzi kuandaa Mpango wa Manunuzi ambao unaainisha mahitaji ambapo fedha za kutosha zitakuwa zimejumuishwa katika bajeti iliyoidhinishwa ya mwaka husika. Upungufu huu umebainika zaidi katika miradi iliyo chini ya sekta ya Elimu na Usafirishaji ikilinganishwa na sekta nyingine kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4-3.**

Jedwali 4- 3: Manunuzi ambayo hayakujumuishwa katika mpango wa manunuzi

Na.	Jina la Mradi	Jina la Mtekelezaji wa Mradi	Sekta	Kiasi(Sh.)
1	Mradi wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo EPforR)	Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia	Elimu	9,815,490,098.54
2	Mfuko wa Afya(HBF)	Halmashauri 1	Afya	39,644,223
3	Mradi wa Kusaidia Kuwajengea Wabunge Uwezo Awamu ya Pili	Ofisi ya Bunge	Jamii	34,337,900.00
4	Programu ya Maendeleo ya Mji Mkuu Dar es Salaam (DMDP)	Ofisi ya Rais-TAMISEMI	Usafirishaji	2,129,489,425.86
Jumla				**12,018,961,647.40**

Chanzo: ***Mpango wa Manunuzi na ripoti ya manunuzi ya mwaka*** *2019/20*

Manunuzi kufanyika nje ya bajeti yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na kutopitia kwa umakini na kutohuisha mpango wa manunuzi kwa wakati na watekelezaji wa miradi. Manunuzi kufanyika nje ya mpango wa manunuzi inaonesha kuwa shughuli za miradi zilifanyika bila ya kuwa na mwongozo mzuri ili kufikia

malengo yaliyowekwa ambayo yanaweza kuathiri ubora wa huduma au bidhaa zilizonunuliwa.

Ninashauri watekelezaji wa miradi husika kuhakikisha kwamba, mpango wa manunuzi unapitiwa vizuri na kuhuishwa. Vile vile ninahimiza menejimenti za watekelezaji wa miradi husika kuhakikisha kuwa manunuzi yote yanatokana na mpango wa manunuzi wa Mwaka uliodhinishwa ili kuepusha manunuzi yasiyopangwa.

4.2.5 Manunuzi Yaliyofanyika kwa Wazabuni Ambao Hawajaidhinishwa Sh. Milioni 173.21

Manunuzi ya kiasi cha Sh. 173,210,768.70 yalifanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 17 katika kutekeleza miradi ya Mfuko wa Afya chini ya sekta ya Afya kwa wazabuni ambao hawajaidhinishwa kinyume na Kanuni 131(4) (b) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma 2013((Iliyorekebishwa 2016).

Mapungufu yaliyobainika yamechangiwa na uwepo udhibiti wa ndani na uangalizi usiojitosheleza wa kitengo cha manunuzi katika taasisi husika. Ni maoni yangu kuwa kufanya manunuzi kwa wazabuni wasioidhinishwa hupunguza uwazi na kuongeza uwezekano wa kupata bidhaa na huduma chini ya viwango.

Ninashauri menejimenti za Halmashauri husika kufuata Kanuni za Manunuzi ya Umma zilizotajwa kwa manunuzi yote yanayofanyika na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika matumizi ya fedha za umma.

4.3 Usimamizi wa Mikataba

4.3.1 Malipo Yaliyofanyika Mara Mbili kwa Mkandarasi Sh. Milioni 704.16

Kanuni 243(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma mwaka 2013 (Iliyorekebishwa 2016) inaitaka taasisi iliyofanya manunuzi kuidhinisha malipo mara baada ya kupima na kuthibitisha, kwa vipindi au hatua zilizotajwa kwenye mkataba.

Katika kipindi cha mwezi Julai 2018 Wizara ya Madini iliingia mkataba wenye Kumbu Na.ME/008/SMMRP/W/12 na Kampuni Idara ya Ujenzi ya Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) kwa ajili ya kuboresha ujenzi wa ofisi za migodi zilizopo Bariadi, Musoma na

Bukoba kama vituo vya ubora kwa thamani ya mkataba ya Sh. 3,601,151,671.

Katika kupitia faili la mkataba na malipo yaliyofanyika kwa mkandarasi nilibaini kuwa, tarehe 14 Desemba 2018 Mshauri Mwelekezi Sky Architects alitoa cheti Na. 03 cha Sh. 735,314,131.69 kwa kazi iliyofanywa na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya ubora vya Bariadi, Musoma na Bukoba na kiasi kilichodaiwa kililipwa kwa mkandarasi. Hata hivyo, nilibaini kuwa cheti hicho hicho Na. 03 kilitumika kufanya malipo ya Sh. 704,155,443.20 kwa mkandarasi. Malipo yaliyobainika kufanyika mara mbili kwa mkandarasi yalisababishwa na kutokufanya uhakiki wa kutosha wa nyaraka wakati malipo yanafanyika.

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Madini kuweka mipango muhimu na mkandarasi ili kurejeshewa kiasi cha fedha kilicholipwa zaida kwa kazi ambayo haijatekelezwa.

4.3.2 Kutokuwepo kwa Uhakika wa Kulipa Shughuli za Ujenzi Ambazo Hazijakamilika Sh. Bilioni 3.09

Katika kupitia nyaraka za utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) nilibaini kuwa ufadhili wa Benki ya Dunia kwenye mradi huo ulimalizika tarehe 31 Desemba 2018 na kiasi cha fedha iliyobaki kilirudishwa Benki ya Dunia bila kubakiza fedha za wakandarasi za matazamio ambazo zilikuwa hazijalipwa kiasi cha Sh. 528,216,961.

Zaidi ya madai tajwa hapo juu, nilibaini kuwa kuna madai ambayo hayajalipwa ya kiasi cha Sh. 2,559,544,868.71 yanayohusiana na kazi mbalimbali zilizofanywa na wakandarasi sita ambapo hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya madai hayo.

Mapungufu haya kwa kiasi kikubwa yalichangiwa na uamuzi wa Wizara ya Madini kurejesha fedha za mradi Benki ya Dunia bila kuzingatia madai ya wakandarasi kwa kazi ambazo zilikuwa bado hazijalipwa. Nina maoni kwamba kutokuwa na uhakika wa fedha kwa ajili ya kulipa madai haya kutaongeza uwezekano wa kuwa na migogoro na wakandarasi nyakati za usoni.

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Madini kutoa maelezo ya mpango mkakati wenye ushahidi wa jinsi ya kulipa madeni ya wakandarasi na mhandisi mshauri na unaoainisha vyanzo vya fedha zitakazotumika. Pia kwa siku zijazo Wizara ihakikishe inafanya maamuzi sahihi kwa madai ya wakandarasi yatokanayo na utekelezaji wa miradi kabla ya kurejesha fedha kwa wafadhili.

4.3.3 Mikataba Iliyotekelezwa Bila ya Kuwepo kwa Dhamana Halali za Utendaji Sh. Bilioni 22

Katika kupitia mikataba nilibaini kuwa mikataba miwili ya ujenzi katika sekta ya elimu yenye thamani ya Sh. 22,001,132,020 ilitekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia bila dhamana za halali za utendaji. Hii ni kinyume na Kanuni ya 29 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (Ilivyorekebishwa mwaka 2016) na vifungu vya mikataba ambavyo vinamtaka mzabuni aliyefanikiwa kupata zabuni kuwasilisha dhamana ya utendaji ili kuhakikisha utekelezaji wa mkataba unafanyika kwa ukamilifu na wafanyakazi wote, wazabuni, mafundi na wakandarasi wadogo wanalipwa kwa wakati. **Jedwali Na. 4-4** linaonesha mikataba iliyotekelezwa bila uwepo wa dhamana.

Jedwali 4- 4: Mikataba iliyotekelezwa bila ya kuwapo kwa dhamana halali za utendaji

Na.	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Mkataba	Kiasi cha Mkataba (Sh.)
1	Mradi wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo (EPforR)	ME-024//2019-2020/HQ/W/06	M/s Suma JKT Construction Company Limited	17,109,576,232
2	Mradi wa Kuboresha Vyuo vya Ualimu - UTC	ME-024/CTR/HQ/2015-16/13	Afriq Engineering & Construction Ltd	4,891,555,788
Jumla				**22,001,132,020**

Chanzo: ***Nyaraka za mikataba 2019/20***

Hali hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na udhibiti dhaifu katika kufuata matakwa ya sheria za manunuzi na mahitaji ya mikataba. Kutokuwepo kwa dhamana za utendaji wa mkataba, watekelezaji wa miradi husika wanakuwa kwenye hatari ya kupoteza rasilimali kwa miradi inayoendelea endapo wakandarasi watashindwa kutekeleza kazi zilizopo kwenye mikataba.

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Sayansi na Teknolojia kuhakikisha mikataba inayotekelezwa ni salama ili kulinda maslahi ya taasisi nunuzi kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa miradi/mikataba.

4.3.4 Malipo ya Awali Yaliyofanyika Zaidi Sh. Milioni 416.44

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na SUMA JKT waliingia mkataba wa ukarabati mkubwa wa nyumba za Makazi Na. II & V katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wenye thamani ya Sh. 4,949,882,943.72 ikijumuisha na kodi ya ongezeko la thamani. Katika kupitia mkataba Namba PA/011/W/2018/2019/34 nilibaini kuwa, Kifungu cha 24 cha Masharti Maalum ya Mkataba kinaainisha kuwa malipo ya awali yanapaswa kuwa asilimia 15 ya thamani ya mkataba.

Katika ukaguzi nilibaini kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitimiza takwa la kifungu tajwa hapo juu na kililipa kiasi cha Sh. 742,482,441 kwa SUMA JKT sawa na asilimia 15 ya thamani ya mkataba. Kinyume na kifungu cha mkataba kama kilivyotajwa hapo juu, nilibaini malipo mengine ya awali ya Sh. 416,444,562.40. Hali hii ilipelekea malipo ya awali kwa ujumla kuwa asilimia 23 badala ya asilimia 15 kama ilivyoainishwa kwenye mkataba.

Mapungufu haya kwa kiasi kikubwa yametokana na jitihada za menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhakikisha kuwa mkandarasi SUMA JKT anakamilisha kazi. Ni maoni yangu kuwa, hii ni kinyume na mkataba ambapo SUMA JKT ilitakiwa kufanya kazi zilizoainishwa kwenye mkataba kwa kutumia vyanzo vingine vya mapato. Kuongeza zaidi malipo ya awali kunaweza kusababisha kushindwa kufanya malipo ya kazi iliyotekelezwa pindi cheti cha malipo kinapotolewa. Pia huweza kuathiri urejeshaji wa malipo ya awali yaliyofanyika pindi mkandarasi anaposhindwa kuteleza mkataba.

Ninashauri menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam (UDSM) kumaliza suala hili na SUMA JKT ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa mkataba huu; na katika siku zijazo kuzingatia matakwa ya masharti maalum ya mkataba.

4.3.5 Malipo ya Awali Yaliyofanyika Bila ya Dhamana ya Benki Sh. Bilioni 2.57

Katika kupitia mkataba wenye Kumbu Na. ME-024/2019-2020/HQ/W/06 kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Kampuni ya ujenzi ya SUMA JKT Construction Company Limited wenye thamani ya Sh. 17,109,576,232 kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya mfano Dodoma nilibaini kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ililipa malipo ya awali kiasi cha Sh. 2,566,436,434.80 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo "EPforR" bila ya kuwasilisha dhamana ya benki/bima. Hii ni kinyume na Kifungu cha 24 cha Masharti Maalum ya Mkataba ambacho kinaeleza kuwa, kiwango cha malipo ya awali kitakuwa asilimia 15 ya thamani ya mkataba mara baada ya kuwasilisha dhamana ya malipo ya awali chenye kiwango sawa.

Kuwepo kwa upungufu huu kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na ucheleweshwaji uliofanywa na mkandarasi katika kufuatilia dhamana ya malipo ya awali kutoka benki inayojulikana. Ni maoni yangu kuwa, upungufu huu unaweza kupelekea upotevu wa fedha za umma endapo mkandarasi atashindwa kurejesha malipo ya awali ambayo tayari yameshalipwa.

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha kuwa dhamana ya utendaji inawasilishwa kama inavyotakiwa na kanuni za manunuzi na makubaliano ya mkataba ili kulinda maslahi ya Wizara iwapo mkataba utatekelezwa bila mafanikio. Vile vile, ninahimiza menejimenti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha kuwa katika siku zijazo, malipo ya fedha za awali hayafanyiki isipokuwa dhamana halali ya malipo ya awali imewasilishwa.

4.3.6 Madai ya Wakandarasi Ambayo Hayajalipwa Sh. Bilioni 78.96

Katika kupitia ujenzi miradi minne iliyotekelezwa katika sekta za elimu na uchukuzi nilibaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 kulikuwa na madai ya wakandarasi na washauri elekezi kiasi cha Sh. 78,960,683,271.35 ambayo muda wake ulishapita kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 4-5.**

Uwepo wa madai haya ulisababishwa kwa kiasi kikubwa na kutotolewa kwa fedha na Wizara ya Fedha na Mipango hali iliyopelekea watekelezaji wa mradi kutowalipa wakandarasi kwa wakati.

Kutokufanya malipo ya madai ya wakandarasi na washauri elekezi kwa wakati kunaweza kuongeza kiwango cha deni litakalotokana na tozo ya riba. Hali hii itapelekea miradi iliyokusudiwa kukwama au kubaki bila kukamilika na hivyo kuwanyima wananchi kupata faida zilizokusudiwa kutokana na miradi hiyo.

Jedwali 4- 5: Madai ya wakandarasi ambayo hayajalipwa Sh. Bilioni 78.96

Na.	Jina la Mradi	Jina la Mtekelezaji	Kiasi(Sh.)
1.	Mradi wa Kuleta Mabadiliko Katika Ujuzi na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki - Taasisi ya Teknolojia - Dar es Salaam	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	49,185,600.00
2.	Mradi wa Kuboresha Miji Tanzania (TSCP)	Ofisi ya Rais-TAMISEMI	45,174,517,005.28
3.	Programu ya Maendeleo ya Mji Mkuu Dar es Salaam (DMDP)	Ofisi ya Rais-TAMISEMI	1,608,735,288.92
4.	Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafiri (TSSP)	Wakala wa Barabara Tanzania	32,128,245,377.15
Jumla			78,960,683,271.35

Chanzo: *Mafaili ya Mikataba ya mwaka 2019/20*

Nashauri watekelezaji wa miradi husika kuwa na tabia ya kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhusiana na utoaji wa fedha ili kuepusha ucheleweshaji zaidi na uwezekano wa kutozwa riba.

4.3.7 Mapungufu Yaliyobainika Wakati wa Kupokea Bidhaa na Huduma Kutoka kwa Wauzaji (Wazabuni)

Upokeaji wa bidhaa na huduma ni mojawapo ya hatua muhimu katika mchakato wa manunuzi kwani inahusishwa na madhara kama vile kupokea bidhaa au huduma zisizo sawa, pungufu, zilizo chini ya kiwango, kwa kuchelewa au kutopokea kabisa bidhaa na huduma zilizoagizwa. Ili kupunguza madhara haya, udhibiti unaohusiana na uagizaji, upokeaji na utoaji wa bidhaa na huduma zilizonunuliwa lazima ufanyike vyema. Wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini kasoro zinazohusiana na udhibiti usioridhisha wa upokeaji wa bidhaa na huduma zilizonunuliwa katika miradi mbalimbali kama ilivyojadiliwa katika aya zifuatazo;

a) Bidhaa zilizopokelewa na Kutumika bila Kuthibitishwa na Kamati ya Ukaguzi na kukubali Bidhaa Sh. 2.44 Bilioni

Nilibaini kuwa bidhaa zilizonunuliwa zenye thamani ya Sh. 2,443,991,727.18 kwa miradi minne inayotekelezwa na taasisi za umma 38 zilipokelewa bila kukaguliwa na Kamati ya Ukaguzi na Kupokea bidhaa kinyume na Kanuni ya 244 na 245 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 zinazomtaka Afisa Masuuli kuunda kamati ya ukaguzi na mapokezi ya bidhaa itakayowajibika kukagua, kupima bidhaa na huduma zilizopokelewa kutoka kwa wazabuni na kujiridhisha kama idadi ni sawa, zinakidhi ubora na bei ni stahiki.

Mradi wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji- Awamu ya Pili (WSDP II) iliyotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Maji ilikuwa na thamani kubwa ya bidhaa ambazo hazijakaguliwa na kamati zenye jumla ya kiasi cha Sh. 818,348,946.01 na kiasi cha Sh. 897,681,496 mtawaliwa ikifuatiwa na Sekta ya afya na jamii ambazo zilikuwa na kiasi cha Sh. 719,261,285.17 na Sh. 8,700,000 chini ya miradi ya HBF na Programu ya Kulinda Maendeleo ya Watoto, mtawaliwa.

Mapungufu ya kutokagua bidhaa zilizopokelewa ulichangiwa sana na kutokuwa makini kwa menejimenti za taasisi husika katika kusimamia udhibiti wa mifumo ya ukaguzi wa bidhaa ikiwemo kutokuunda kamati zinazohusika kwa wakati unaofaa. Ni maoni yangu kuwa kupokea bidhaa zilizonunuliwa bila kufanyiwa ukaguzi thabiti kunaweza kusababisha mapokezi ya bidhaa hafifu, zisizoendana na viwango tarajiwa na za bei ya juu kinyume na mkataba wa mauziano.

Ninashauri menejimenti za watekelezaji wa mradi husika kuhakikisha Kamati za ukaguzi na mapokezi ya bidhaa zinakagua na kutoa ripoti ikiwa bidhaa zilizonunuliwa vinakidhi viwango vilivyowekwa na ubora unaohitajika.

b) Bidhaa na Huduma Zilizonunuliwa Lakini Bado Kupokelewa Sh. Bilioni 1.87

Mapitio yangu ya mihamala na nyaraka za manunuzi kwa miradi minne ambayo ni Mradi wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo

(EPforR), Usafi wa Maji na Mazingira Shuleni (SWASH), Mradi Endelevu wa Kuwezesha Kuzuia na Kupambana na Rushwa - Tanzania (BSAAT) na Mradi wa Maboresho wa Huduma za Mahakama na Utoaji Haki kwa Wananchi inayotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Makamu wa Rais na Mahakama. Miradi hii ilifanya malipo ya jumla ya kiasi cha Sh. 1,865,730,431.72 kwa wazabuni mbalimbali (pamoja na kiasi cha Sh. 83,389,299.38 kwa huduma ya mfumo mtandao zilizotolewa na Kampuni ya Mawasiliano Tanzania (TTCL) katika utekelezaji wa mradi wa Maboresho ya Huduma za Mahakama na Utoaji Haki kwa Wananchi) kabla ya kuletwa kwa bidhaa na huduma. Nilibainisha pia bidhaa ambazo hazijaletwa zenye thamani ya kiasi cha Sh. 649,851,366 kwa Halmashauri 33 zinazotekeleza Mradi wa Mfuko Afya. Bidhaa hizi zilikuwa bado hazijaletwa ingawa malipo yalikuwa tayari yamekwisha fanyika kwa wazabuni.

Hii ni kinyume na Kanuni ya 242 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 ambayo inataka taasisi za umma zinazonunua bidhaa kuwa na taarifa za mapokezi ya bidhaa zilizowasilishwa kulingana na mkataba ambayo inapelekea kuidhinisha malipo kwa wazabuni husika.

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa miradi ya sekta mbalimbali ilikuwa inaongoza kwa bidhaa na huduma ambazo hazikupokelewa zenye thamani ya Sh. 1,124,514,876.72 ikifuatiwa na sekta za Afya na Elimu ambazo zilikuwa na kiasi cha Sh. 649,851,366 na Sh. 91,364,189 mtawalia.

Ninashauri menejimenti za watekelezaji wa miradi husika kufanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa bidhaa zilizonunuliwa zinafikishwa na kutumiwa kama ilivyopangwa kwa maslahi ya umma.

c) Bidhaa na Vifaa vya Matibabu Ambavyo Havijatolewa na Bohari kuu ya Dawa Kiasi cha Sh. Bilioni 11.28

Nilibaini bidhaa na vifaa vya matibabu vyenye thamani ya Sh. 11,277,099,476 havikupokelewa na Ofis ya Raisi-TAMISEMI inayotekeleza Programu ya Kusaidia Sekta ya Afya (HSPS) kutoka

Bohari Kuu ya Dawa (MSD) licha ya malipo kufanyika tangu tarehe 7 Agosti 2019.

Hii ilisababishwa kwa kiasi kikubwa kutokuwepo kwa makubaliano ya kimkataba kati ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Bohari Kuu ya Dawa inayoelezea haki na wajibu kwa kila mhusika. Ni maoni yangu kuwa kuchelewesha kupeleka bidhaa na vifaa vya matibabu kunainyima jamii iliyokusudiwa kufurahia faida zinazotarajiwa kutoka kwa Serikali kwa wakati unaofaa, na hivyo kusababisha utoaji huduma za afya usioridhisha.

Ninashauri menejimenti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha kuwa usafirishaji wa shehena nzima ya vifaa tiba na dawa inapelekwa kwa walengwa waliokusudiwa bila kuchelewa zaidi.

4.3.8 Mali na Vifaa ambavyo Havijaingizwa kwenye Leja ya Vifaa Kiasi cha Sh. Milioni 814.37

Ili kuwa na uangalizi mzuri wa mali na vifaa, mtekelezaji wa mradi anapaswa kutunza leja ya vifaa na mali ili kuwa na kumbukumbu ya kila kifaa kilichotunzwa, idadi na thamani ya vifaa vilivyonunuliwa, vilivyotolewa na vilivyosalia. Kanuni ya 220 ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inataja kuwa "vifaa vilivyopokelewa baada ya kukaguliwa ikilinganishwa na hati ya mapokezi vinapaswa viingizwe bila kuchelewa kwenye folio inayofaa ya leja ya vifaa.

Manunuzi ya bidhaa yenye thamani ya Sh. 814,365,066.90 yaliyofanywa na taasisi za umma 39 zinazotekeleza miradi minne katika sekta ya Afya, Elimu na Maji hazikuingizwa katika leja husika ili kutunza kumbukumbu ya vifaa husika. Uchambuzi wangu unaonesha kuwa Halmashauri 36 zilizotekeleza mradi wa mfuko wa Afya zilikuwa na vifaa vyenye thamani ya Sh. 486,041,041.06 ambavyo havikuingizwa katika leja ya vifaa na kufuatiwa na mradi wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo (EpforR) vyenye thamani ya Sh. 297,987,025.90 na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji –II vyenye thamani ya Sh. 18,377,000. Miradi hii inatekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Technolojia na Wizara ya Maji.

Udhaifu huo unatokana na upungufu katika udhibiti wa ndani juu ya uwekaji kumbukumbu wa bidhaa zilizonunuliwa. Hii inasababishwa na ufuatiliaji usioridhisha wa Afisa Masuuli katika taasisi husika. Kukosekana kwa kumbukumbu za leja ya vifaa na hati ya kutolea vifaa, usahihi na ukweli wa vifaa vilivyonunuliwa haukuweza kuthibitishwa; kwa hiyo kuna uwezekano wa matumizi mabaya ya fedha za umma.

Ninashauri menejimenti ya watekelezaji wa miradi husika kuanzisha udhibiti wa kutosha katika uwajibikaji kwa bidhaa zilizonunuliwa na kuhakikisha kuwa bidhaa zote zilizonunuliwa na kupokelewa zinaingizwa katika vitabu vya stoo kama ushahidi wa uwajibikaji wao.

4.3.9 Kuanza kwa Miradi Miwili ya Ujenzi Bila Kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira

Kanuni ya 241(3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inasema, "taasisi inayofanya manunuzi inatakiwa kutathmini athari ya mazingira ya kazi yoyote katika hatua za maandalizi ya mradi na kabla ya kuanza mchakato wa manunuzi". Pia, Kifungu cha 81(2) ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (EMA), 2004 inahitaji tathmini ya athari za kimazingira kuwa inafanyika kabla ya kupanga fedha au kuanza kwa mradi.

Kinyume na matakwa yaliyotajwa, nilibaini miradi miwili katika sekta ya elimu yenye thamani ya Sh. 27,058,101,894 ilianzishwa bila kufanya tathmini ya athari za mazingira. Hii ni pamoja na Programu ya Elimu na Ujuzi kwa Ajili ya Kazi na Uzalishaji (ESPJ) ambapo kiasi cha Sh. 9,948,525,662 kilitumwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Ofisi za Wilaya 25 za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ambapo ujenzi ulianza bila kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA). Hali kadhalika, kiasi cha Sh. 17,109,576,232 kilipangwa kutumika katika mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya mfano Dodoma chini ya mradi wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo (EpforR) bila kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira.

Kasoro hii imesababishwa na maandalizi yasiyojitosheleza kabla ya kuanza kwa mradi unaohusiana na kubadilika kwa eneo la

mradi katika utekelezaji wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Dodoma.

Utekelezaji wa miradi bila kufanya tathmini ya athari za mazingira zinawaweka walengwa katika hatari ya kupata madhara yatokanayo na mazingira na zinaweza kusababisha upotevu wa rasilimali za umma katika kuchukua hatua za kukabiliana na madhara hayo.

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha kuwa katika siku zijazo Tathmini ya Athari za Mazingira inafanywa kabla ya kuanza miradi ili kuepuka hatari zitokanazo na kutofanya tathmini.

4.3.10 Kushindwa Kuhuisha Hati ya Dhamana ya Utekelezaji Iliyokwisha Muda Wake Inayohusiana na Mikataba ya Ujenzi kiasi cha Sh. Bilioni 16.98

Kifungu cha 50.1 cha mkataba Na. ME 012 2018-19/ERPP/W/64-68 kati ya Wizara ya Kilimo na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Upanuzi wa Uzalishaji wa Mpunga (ERPP) inahitaji dhamana ya utekelezaji itolewe kwa Mwajiri kabla ya tarehe iliyoainishwa kwenye barua ya kukubali mkataba katika utekelezaji mradi wa Upanuzi wa Uzalishaji wa Mpunga (ERPP).

Katika kupitia mafaili ya mikataba inayohusiana na utekelezaji wa mradi wa ERPP nilibaini kuwa, kulikuwa na ongezeko la muda wa mikataba mitano yenye thamani ya Sh. 16,984,618,292.25 bila kuongeza muda wa dhamana ya utendaji ambao ni kinyume na kifungu kilichotajwa hapo juu. Nilibaini kuwa wakandarasi bado walikuwa kwenye eneo la ujenzi wakati dhamana za utendaji zilikuwa zimekwisha muda wake kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 4-6**.

Jedwali 4- 6: Orodha ya wakandarasi ambao dhamana zao za utendaji ziliisha

Na	Zabuni Na.	Mkandarasi	Tarehe ya Kukamilisha Mkataba	Tarehe ya kuisha kwa Dhamana ya Utendaji	Thamani ya Mkataba (Sh.)
1	ME 012/2018-19/ERPP/W/64-NJAGE-Kilombero	NAKUROI Investment Co Ltd. S.L.P 19716 DSM	Miezi 13 21/07/2020	Aprili, 2020	4,469,208,362.39
2	ME 012/2018-19/ERPP/W/65-Msolwa Ujamaa-Kilombero	Ms Confi Eng Ltd S.L.P 31211 DSM	30/12/2020	Februari 2020	3,378,875,168.35
3	ME 012/2018-19/ERPP/W/66-Mvumi-Kilosa	Ms White City International Ltd S.L.P 62189 DSM	30/07/2020	Machi 2020	1,973,651,503.01
4	ME 012/2018-19/ERPP/W/67-Kigugu-Mvomero	Ms GOPA contractor (T) Ltd S.L.P 33259 DSM	30/12/2020	Machi 2020	1,734,190,959.58
5	ME 012/2018-19/ERPP/W/68-Kilangali Seed Farm-Kilosa	Ms Lukolo co Ltd. S.L.P 75028 DSM	15/01/2021	April 2020	5,428,692,298.92
Jumla					**16,984,618,292.25**

Chanzo: *Mikataba na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo 2019/20*

Upungufu huuo ulitokana na ufuatiliaji duni juu ya uhalali wa hati za mikataba wakati wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi. Kwa kukosekana kwa dhamana za utendaji, Watekelezaji wa Miradi husika walikuwa kwenye hatari ya kupoteza rasilimali kwa miradi inayoendelea endapo wakandarasi wangeshindwa kutekeleza kazi zilizoanishwa kwenye mkataba.

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Kilimo kuhakikisha kuwa, inaongeza ufuatiliaji wa mikataba kwa kuhakikisha kuwa

dhamana za utendaji zilizokwisha muda zinahuishwa kama inavyotakiwa na mikataba.

4.3.11 Kukosekana kwa Idhini ya Kuongezwa kwa Tarehe ya Kumaliza Mkataba

Ukaguzi wangu wa faili la mkataba ulibaini kuwa, Mradi wa Kuboresha Vyuo vya Ualimu (UTC) uliotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia uliongezewa muda wa kukamilisha mkataba kutoka 5 Aprili 2018 hadi 11 Oktoba 2020 kwa ukarabati wa Chuo cha Ualimu Shinyanga fungu namba 2 kwa bei ya mkataba wa kiasi cha Sh. 4,891,555,788. Hata hivyo, ongezeko la muda wa kukamilisha haukuidhinishwa na Katibu Mkuu licha ya Mhandisi Mshauri kuomba suala hili kupitia barua yenye Kumbukumbu Na. AFRIQ/SHY/MOEST/2020/6, AFRIQ/SHY/MOEST/2020/11 na ARU/A.538/SF.221/217 ya tarehe 21 Septemba 2020. Hii ni kinyume na Kanuni ya 111 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 ambayo inataka ongezeko la muda wa utekelezaji wa kazi za mkataba liidhinishwe na Afisa Masuuli peke yake. Kwa sasa mkandarasi anaendelea na kazi za ujenzi na ukarabati.

Upungufu huu ulichangiwa na usimamizi usioridhisha wa mikataba kwani Afisa Masuuli anayo mamlaka ya kukubali au kukataa pendekezo la ongezeko la muda katika utekelezaji wa mkataba kutoka kwa mshauri elekezi. Ni maoni yangu kwamba endapo mkandarasi atakiuka masharti ya makataba hakutakuwa na msingi wa hatua itakayotakiwa kuchukuliwa ili kuinufaisha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha kuwa, inaimarisha udhibiti wa usimamizi wa mikataba na pia kutathmini utendaji wa mkandarasi pamoja na sababu za kuchelewesha kumaliza kazi na ikionekana inafaa, itoe idhini ya kuongeza muda au kuchukua hatua zinazohitajika ili mradi ukamilike kwa wakati.

4.3.12 Manunuzi ya Vifaa Tiba vyenye Thamani ya Sh. Milioni 402.61 Bila Idhini ya Bohari Kuu ya Dawa

Nilibaini kuwa Halmashauri 27 kupitia sekta ya Afya zilinunua vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. 402,609,089.08 kutoka kwa

wazabuni binafsi bila idhini ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kinyume na Kanuni ya 140 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013

Udhaifu huu ulichangiwa na kukosekana kwa mawasiliano madhubuti kuhusu ukosefu wa vifaa tiba kati ya taasisi za umma na Bohari Kuu ya Dawa. Kutokuwapo kwa ushahidi wa kukosekana kwa bidhaa kutoka Bohari Kuu ya Dawa inapelekea hatari ya kupata vifaa vya matibabu kwa gharama ya juu.

Ninashauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuhakikisha kwamba ununuzi wote wa vifaa tiba haufanyiki kwa wazabuni binafsi isipokuwa kuna ushahidi unaojitosheleza kuwa dawa/vifaa hizo hazipo katika Bohari Kuu ya Dawa.

SEHEMU YA TATU

MAPITIO YA UTENDAJI WA MIRADI

Sehemu ya tatu ya taarifa hii inajumuisha sura saba zinazoonesha muhtasari wa matokeo ya kaguzi za kiufundi zilizofanyika kwenye miradi 13 katika mwaka wa fedha 2019/20. Uwasilishaji wa Matokeo ya kaguzi 13 za miradi ya kiufundi umefanyika kulingana na kipindi kilichoangaziwa katika mawanda ya ukaguzi husika. Muhtasari ya matokeo ya kaguzi sita zenye mawanda yanayolenga zaidi ya kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20 umewasilishwa kwenye sura zinazojitegemea wakati kaguzi saba zinazolenga mwaka wa fedha 2019/20 zimejumuishwa katika sura moja.

Hivyo, sura ambazo zimewasilishwa kwa kujitegemea na zinajumuisha vipindi zaidi ya mwaka wa fedha 2019/20 ni hizi zifuatazo: Sura ya Tano: Mradi wa Reli Ya Kisasa (SGR); Sura ya Sita: Mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere; Sura ya Saba: Mradi wa Mabasi ya Yaendayo Haraka Dar es Salaam; Sura ya Nane, Mradi wa Upanuzi wa Barabara ya Morogoro; Sura ya Tisa: Mradi wa Uboreshaji wa Usambazaji Maji Same-Mwanga na Korogwe; na Sura ya 10: Mradi wa Uzalishaji Sukari Mbigiri.

Sura ya 11 inajumuisha uchambuzi wa matokeo ya kaguzi za kiufundi zilizofanyika kwenye miradi saba iliyotekelezwa na Wakala wa Barabara, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka - Arusha na Shirika la Umeme Tanzania. Kaguzi hizi zilijikita kwenye shughuli za mradi zilizotekelezwa kwenye mwaka wa fedha 2019/20. Aidha, sura ya 12 imejikita kwenye masuala yanayohusiana na hali ya utekelezaji wa miradi kama yalivyobainika kwenye kaguzi nyingine mbali na kaguzi 13 za kiufundi zilizoelezewa hapo juu.

SURA YA TANO

UJENZI WA RELI YA KISASA (SGR) KUTOKA DAR ES SALAAM HADI MAKUTUPORA KIPANDE CHA KWANZA NA CHA PILI

5.1 Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Reli, inafanya juhudi kupanua na kuboresha miundombinu ya reli nchini. Miongoni mwa juhudi hizo ni utekelezaji wa ujenzi wa njia mpya ya reli ya kisasa iitwayo "Standard Gauge Railway" (SGR). Awamu ya kwanza ya mradi huu ni kujenga reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.

Reli ya kisasa imesanifiwa kutumia nishati ya umeme kuendeshea treni (locomotive) zitakazotoa huduma. Baada ya mradi kukamilika, treni za abiria zitasafiri kwa mwendokasi wa kilometa 160 kwa saa wakati treni za mizigo zitasafiri kwa mwendokasi wa kilometa 120 kwa saa. Ujenzi wa awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza unajumuisha vipande vitano ambavyo ni: Kipande cha 1 kutoka Dar es Salaam-Morogoro (Km 300), Kipande cha 2 Morogoro-Makutupora (Km 422), Kipande cha 3 Makutupora-Tabora (Km 294), Kipande cha 4 Tabora-Isaka (Km 130) na Kipande cha 5 Isaka-Mwanza (Km 249).

Lengo kuu la kujenga reli ya kisasa ni kuboresha ufanisi wa usafirishaji katika sekta ya reli Tanzania.

5.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi

Kwa ujumla, lengo la ukaguzi wa kiufundi lilikuwa ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa mradi unaosimamiwa na Shirika la Reli Tanzania, hususani mipango ya utekelezaji wa mradi, usanifu na hatua za utekelezaji, pamoja na kutathmini ubora wa kazi na maendeleo ya mradi ili kujiridhisha na kuwapo kwa thamani ya fedha.

Mkaguliwa mkuu ni Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa sababu ndiye mtekelezaji mkuu wa mradi. Hii ni kutokana na jukumu lake la kuendeleza, kusimamia, kukuza na kudumisha miundombinu ya reli na kutoa huduma za usafirishaji kwa njia ya reli kupitia ubia au makubaliano.

Ukaguzi ulihusisha kipande cha kwanza ambacho ni kutoka Dar es-Salaam hadi Morogoro na kipande cha pili ambacho ni kutoka Morogoro hadi Makutopora. Kipande cha tatu hadi cha tano hakikuhusishwa kwa kuwa utekelezaji wake ulikuwa bado haujaanza wakati wa kupanga utekelezaji wa ukaguzi huu. Kwa ujumla, ukaguzi huu ulihusisha uchunguzi kwenye masuala sita ambayo ni: usimamizi wa fedha, manunuzi na mkataba, masuala ya kiufundi, masuala ya mazingira, afya & kijamii, pamoja na rasilimali watu.

Nilitembelea mikoa mitano na wilaya 11 ambazo mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa unapita. Mikoa na wilaya zilizotembelewa ni: Dar es Salaam (Ilala), Pwani (Kisarawe na Kibaha), Morogoro (Morogoro vijijini, Mororgoro mjini, Mvomero na Kilosa), Dodoma (Mpwapwa, Dodoma mjini na Chamwino) na Singida (Manyoni).

Ukaguzi ulihusisha kipindi cha kuanzia mwezi Mei 2017 hadi Januari 2021. Kipindi kilichohusishwa kiliwawezesha wakaguzi kutathmini kiwango cha utekelezaji wa mradi ambao ulipangwa kutekelezwa kuanzia mwezi Mei 2017 hadi Novemba 2019 kwa kipande cha kwanza, na kutoka Februari 2018 hadi Februari 2021 kwa kipande cha pili.

5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi hususani katika: Uandaaji wa mipango, usanifu na nyaraka za zabuni, manunuzi ya mkandarasi na mshauri elekezi, masuala ya Afya, Usalama na Mazingira, pamoja na Usimamizi wa Mkataba. Matokeo haya ya ukaguzi yamefafanuliwa zaidi hapa chini:

5.3.1 Kulikuwa na Usimamizi Usioridhisha wa Mkataba wa Kipande cha Kwanza na cha Pili

Sehemu hii inatoa matokeo yanayohusiana na usimamizi wa mikataba. Kimahususi, matokeo yanahusisha: usimamizi wa rasilimali watu, usimamizi wa muda wa mkataba, usimamizi wa fedha, pamoja na usimamizi wa ubora.

a) Usimamizi Duni wa Rasilimali Watu

Nilibaini udhaifu mbalimbali katika usimamizi wa rasilimali watu kama ilivyoelezwa hapa chini:

(i) Sio Raia Wote wa Kigeni Wana Vibali vya Kufanya Kazi Nchini

Kifungu cha 9 (2) (a) cha Sheria za Ajira za Raia wa Kigeni ya mwaka 2015 kinataka TRC isiajiri mtu yeyote asiye raia, isipokuwa ana kibali halali cha kufanya kazi katika kazi maalum.

Mapitio ya Ripoti ya Maendeleo ya kazi ya Mwezi wa Novemba 2020 yalibaini kuwa, jumla ya raia wa kigeni 586 kati ya 924 walioajiriwa kwenye kipande cha kwanza cha ujenzi wa reli ya kisasa hawakuwa na vibali vya kufanya kazi. Hali hii pia ilibainika kwenye kipande cha ujenzi cha pili; ambapo ilibainika kuwa jumla ya raia wa kigeni 952 kati ya 1,484 hawakuwa na vibali vya kufanya kazi.

Mahojiano zaidi na maafisa wa TRC yalionesha kuwa, Idara ya Uhamiaji ilitoa idhini ya raia hao wa kigeni kutumia visa ya biashara kuendelea kufanya kazi wakati maombi yao ya vibali vya kazi yakishughulikiwa.

Hata hivyo, ilielezwa wazi katika barua hiyo kwamba kutolewa kwa Visa ya Biashara hakikuwa kisingizio cha kutokuwa na vibali vya kufanya kazi kwa raia hao wa kigeni walioajiriwa katika mradi wa SGR.

Kutozingatiwa kwa kupata vibali vya kazi kulisababisha kutolipwa kwa ada ya vibali vya kazi inayofikia Dola za Marekani 1,538,000 ambazo ni sawa na Sh. 3,537,400,000 (kiwango cha ubadilishaji kilichotumika ni 2,300).

Ninapendekeza Menejimenti ya Shirika la Reli kutoruhusu ajira kwa watu wasio raia wa Tanzania ambao hawana kibali halali cha ajira ili kufuata matakwa ya Kifungu cha 9 (2a) cha Sheria za Kanuni za Ajira kwa watu wasio Raia, za mwaka 2015.

(ii) Raia wa Kigeni Kutokuwa na Vyeti vya Kitaaluma

Kifungu cha 10 (3) cha Sheria ya Ajira za Raia wa Kigeni ya Mwaka 2015 kinataka mtu ambaye si raia aliyeajiriwa katika kazi yoyote kuwa na sifa na ujuzi unaohitajika kwa utendaji wa kazi ambayo kibali cha kazi kinatolewa.

Mapitio ya Ripoti ya Maendeleo ya kazi ya mwezi wa Novemba 2020 yalibaini kuwa, jumla ya raia wa kigeni 1,026 wanaofanya kazi katika mradi wa SGR (kwa vipande vyote viwili) walikuwa hawana vyeti vya sifa zao za masomo. Ripoti ya Maendeleo ya kazi ya mwezi wa Novemba 2020 ilionesha kuwa, vyeti vyao vilikuwa vikiendelea na michakato anuwai ya uthibitishaji. Hata hivyo, asilimia 83 kati yao bado walikuwa wakisubiri kwa sababu ilibainika waombaji hawakuwa na vyeti halisi vya masomo na walikuwa wakingojea kuvipokea kutoka Uturuki.

Ninapendekeza Shirika la Reli kuhakikisha watu wasio raia walioajiriwa katika kazi yoyote kuwa na sifa, ujuzi na ustahiki unaohitajika kwa utendaji wa kazi ambayo kibali cha kazi kinatolewa kwa kufuata Kifungu cha 10 (3) Sheria za Ajira kwa watu wasio raia za mwaka 2015.

(iii) Wataalamu Wengine Kutosajiliwa na Bodi za Usajili wa Wataalamu

Kifungu kidogo cha 6.12 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kilihitaji Kampuni kujisajili na Bodi ya Usajili ya Wakandarasi na Wahandisi wake kujisajili na Bodi ya Usajili ya Wahandisi wa Tanzania mara moja na wataalamu wengine kujisajili na Bodi zao za taaluma.

Kwa upande wa ujenzi wa kipande cha kwanza (1) ilibainishwa kuwa, wafanyakazi watano hawakuwa wamesajiliwa na Bodi zao za Utaalamu. Wafanyakazi watano ambao hawajasajiliwa walikuwa ni Mhandisi wa Udhibiti Ubora, Mhandisi wa Miamba, Mhandisi wa Miundo ya Ujenzi (*Structural Engineer*), Mhandisi Msanifu wa Njia za Reli na Daktari wa Tiba. Mapitio ya Taarifa ya Maendeleo ya kazi ya mwezi wa Novemba 2020 inaonesha kuwa, wafanyakazi watano hawakusajiliwa na Bodi zao za Utaalamu kwa sababu maombi manne yalikuwa kwenye Bodi ya Usajili wa

Wahandisi na ombi moja lilikuwa likisubiri Baraza la Matabibu la Tanganyika kwa uhakiki zaidi.

Kwa kuongezea, ukaguzi wa Ripoti ya Maendeleo ya kazi ya mwezi wa Novemba 2020 kwa ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha pili (2) ilibainisha kuwa, wafanyakazi 272 hawajasajiliwa na Bodi zao za Utaalam. Kada za wafanyakazi wasiosajiliwa ni pamoja na: Madaktari wa Tiba 3; Kada mchanganyiko 197 na Wahandisi 72. Mapitio ya Ripoti ya Maendeleo ya mwezi wa Novemba 2020 yanaonesha kuwa, kushindwa kusajili wafanyakazi hawa kulisababishwa na kutokuwa na vyeti na kulazimika kuviagiza nchini Uturuki.

Makosa haya yanaweza kusababisha kuwa na wataalamu walioajiriwa kwenye mradi ambao wanakosa ujuzi, maarifa na umahiri unaohitajika.

Ninapendekeza Shirika la Reli kuhakikisha wakandarasi chini ya mradi wa SGR wamesajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi Tanzania mara moja na wataalamu wengine wasajiliwe na bodi zao za kitaalamu ili kuleta imani kwamba wataalamu walioajiriwa katika mradi wa SGR wana ujuzi, maarifa na umahiri unaohitajika.

b) Usimamizi Hafifu wa Mkataba

Nilibaini udhaifu katika kusimamia mkataba kama inavyooneshwa hapa chini:

(i) Usimamizi Hafifu wa Muda wa Kumaliza Mradi

Kifungu cha 1.1.3.3 cha mkataba kati ya Shirika la Reli (TRC) na Kampuni ya ujenzi ya Yapi Merkez yenye ubia na kampuni ya MOTA Engil kilihitaji usanifu na ujenzi wa SGR kipande cha 1 kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kukamilika ndani ya miezi 30 kuanzia Mei 2017 hadi Novemba 2019. Pamoja na hayo, nilibaini kuwa, kufikia Desemba 2019 maendeleo ya mradi yalikuwa 88.39% dhidi ya 95.96% iliyopangwa.

Pia, nilibaini kuwa, kipande cha 2 kilitarajiwa kukamilika ndani ya miezi 36 kutoka Aprili 2018 hadi Februari 2021. Pamoja na hayo, ukaguzi wa ripoti ya maendeleo ya mradi ulionesha kuwa,

hadi Desemba 2020 mkandarasi alifikia 52.2% badala ya 98.7% kama ilivyopangwa. Nilibaini maendeleo yasiyoridhisha katika ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) yalisababishwa na:

- **Ucheleweshaji katika Kuleta Vifaa/Mitambo ya Ujenzi**

Nilibaini kuwa, mkandarasi wa kipande cha 1 hakuleta vifaa 69 muhimu vilivyoelezwa wakati wa kuwasilisha mpango wa kazi. Pia, hali hiyo ilikuwepo wakati wa utekelezaji wa kipande cha 2 ambapo jumla ya mitambo na vifaa 351 kati ya 721 na vifaa vya lazima havikuletwa na mkandarasi ndani ya miezi 20 baada ya kuanza kwa mkataba wa kipande cha 2.

- **Ucheleweshaji katika Ujenzi wa Shughuli Kuu**

Kifungu cha 8.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kinahitaji mkandarasi kuanza kusanifu na kutekeleza kazi bila kuchelewa. Mpaka mwezi Aprili 2019 nilibaini kuwa, sanifu za miundo 124 kati ya 315 zilizoidhinishwa sawa na 39% hazijajengwa hadi wakati wa ukaguzi huu (Januari 2021). Pia maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya reli 57 haikuwa ya kuridhisha. Mpaka Septemba 2020, sanifu za miundombinu ya reli 620 kati ya 792 zilizopangwa ziliidhinishwa. Kati ya hizo, miundombinu ya reli 325 imekwishajengwa na 56 iliyobaki ilikuwa inaendelea wakati 239 ilikuwa bado haijaanza kujengwa.

- **Mkandarasi Kukosa Mbinu ya Kupunguza Ucheleweshaji wa Kazi**

Nilibaini kuwa, mkandarasi hakuwasilisha mpango wa kazi ulioboreshwa ili uendane na muda wa kukamilisha mkataba. Hii ilikuwa kinyume na Kifungu cha 8.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (FIDIC[9]-GCC) kinachomtaka mkandarasi kuwasilisha mpango wa kazi ulioboreshwa kwa msimamizi wa mradi muda wowote kama maendeleo halisi hayaendani na programu iliyoidhinishwa awali.

[9] Federation International des Ingenieurs Conseils (French)

- **Kucheleweshwa Kuanza kwa Usanifu na Ujenzi wa km 3 za kwenda Bandarini**

Kulingana na programu ya njia ya reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro iliyoidhinishwa tarehe 30 Aprili 2020, usanifu na ujenzi wa 3 Km kwenda bandarini ulitakiwa kuanza Januari 2019 na kukamilika Aprili 2019.

Nilibaini kuwa, kuanzia Aprili 2019 kazi ilikuwa haijaanza. Ilibainika kuwa, nyongeza ya muda ilitolewa mara tatu ambayo ilifanya tarehe ya kukamilika kwa mradi huo kuwa Aprili 2021 (yaani miezi 18 baadaye). Hata hivyo, ilibainika zaidi kuwa, licha ya kuongezwa kwa muda usanifu wa njia ya reli kwenda bandarini haukufanyika. Hadi tarehe 1 Desemba 2020, usanifu na ujenzi wa njia ya kwenda bandarini ulikuwa haujaanza licha ya sehemu hiyo kuwa tayari imekabidhiwa kwa mkandarasi tangu 21 Aprili 2017. Hii huweza kusababisha ucheleweshaji katika kukamilika kwake, hivyo kuathiri faida za mradi zinazotarajiwa kupatikana.

Nilibaini kuwa, ucheleweshwaji wa maamuzi ya kusanifu km 3 za kwenda bandarini ndiyo sababu kuu ya kutoweza kuanza ujenzi wa kiungo cha Bandari. Mawasiliano kati ya mkandarasi na mhandisi mshauri yalionesha kuwa, ucheleweshaji wa uamuzi juu ya usanifu wa km 3 kwenda bandarini ulionekana kuwa mgumu kutokana na usanifu wa awali. Kulingana na mkandarasi, usanifu wa awali uliofanyika kulingana na mahitaji ya mwajiri ulionekana kuwa ngumu kutekelezeka. Kulingana na mahojiano na wafanyakazi wa shirika la reli Tanzania, ilibainika kuwa ugumu wa km 3 kwenda bandarini umetokana na ujenzi wake kuhusisha miradi mingine ya kiufundi kama ujenzi wa daraja la gerezani, uendeshaji na ujenzi wa Reli ya Zamani ya Kipimo cha Mita (MGR) na upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam.

Kifungu cha 1.9 na 5.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinamtaka mkandarasi kutoa taarifa kwa mhandisi mshauri juu ya makosa yasiyotarajiwa na kasoro katika mahitaji ya mwajiri ndani ya siku 14 baada ya tarehe ya kuanza ujenzi. Mahojiano na wafanyakazi wa Shirika la reli Tanzania yalibainisha kuwa, mkandarasi hakumjulisha mwajiri makosa hayo ndani ya muda tajwa hapo juu. Hii inamaanisha kuwa, lilikuwa ni jukumu la

mkandarasi kusanifu na kujenga kilometa 3 kwenda Bandarini kulingana na mkataba.

Kwa kuongezea, kulingana na kikao cha majadiliano kilichofanyika tarehe 21-24 Januari 2017 kuhusu uingiaji wa bandari ya Dar es Salaam wakati wa ujenzi, walikubaliana na kuthibitishwa kuwa mzabuni atasanifu miundombinu ya reli inayohitajika ndani ya Bandari ya Dar es Salaam bila gharama yoyote baada ya kupokea taarifa ya upembuzi iliyoandaliwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na taarifa nyingine zinazohitajika kisha kupendekeza gharama ya ujenzi kwa mtoa zabuni ili aweze kuamua. Pamoja na hayo, hadi tarehe 1 Desemba 2020 hakukuwa na uamuzi wowote uliokuwa umefanyika juu ya kubadili mapendekezo ya njia ya awali ya km 3 ya kuunganisha na bandari.

c) Usimamizi wa Masuala Fedha na Gharama Usioridhisha

Udhaifu ulionekana kwenye maeneo ya utoaji wa fedha na matumizi, ulipaji fidia, kodi ya zuio na urejeshaji fedha na marejesho ya kodi kama inavyoelezwa hapa chini:

(i) Faini ya Dola za Marekani 1,286,913.23 kama Riba Kutokana na Ucheleweshwaji wa Malipo ya Mkandarasi (IPC's) katika Ujenzi wa Kipande cha Kwanza (fungu la 1).

Ilibainika kuwa wakandarasi walikuwa hawalipwi ndani ya muda uliokubaliwa wa siku 56 baada ya mhandisi mshauri kupokea nyaraka za madai na vielelezo vya malipo. Riba iliyotozwa na mkandarasi kwa kucheleweshewa malipo ilikuwa Dola za Marekani 1,286,913.23 sawa na Shilingi za Tanzania 2,983,064,867.14[10] ambazo ziliidhinishwa na Shirika la Reli kulipwa kama malipo ya riba ndani ya hati ya malipo namba 41 (IPC 41).

Ucheleweshaji wa malipo ya mkandarasi ulisababishwa haswa na ucheleweshwaji wa fedha kutolewa.

---

[10] Kiwango cha kubadilisha fedha cha Benki Kuu ya Tanzania mwezi Novemba 2020 (Dola 1 ya Marekani = Shilingi 2318 ya Tanzania)

Ninapendekeza Shirika la Reli Kuwasiliana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ili Kuhakikisha Wakandarasi na Washauri Elekezi Wanalipwa kwa Wakati ili Kuepuka Ongezeko la Gharama za Miradi Inayotokana na Tozo ya Riba.

(ii) Ongezeko la Dola za Marekani 11,222,653 kama Gharama za Usimamizi wa Mradi Kipande cha Kwanza (fungu la 1) Baada ya Mradi Kuchelewa Kukamilika

Mapitio ya Ripoti ya Maendeleo yalibaini kuwa, shughuli za ujenzi wa mradi wa SGR kipande cha 1 zilitakiwa kuchukua miezi 30 kuanzia tarehe 2 Mei 2017 na kuisha tarehe 01 Novemba 2019. Mbali na hayo, kutokana na ucheleweshaji wa muda utekelezaji, tarehe ya kukamilisha mradi ilibadilishwa hadi tarehe 21 Aprili 2021 ambayo ni nyongeza ya miezi 18.

Ongezeko la miezi 18 limepelekea gharama ya ziada ya mhandisi mshauri kufikia Dola za Marekani 11,222,653.00 (sawa Sh. 26,025,332,307[11]).

(iii) Kutotambuliwa kwa Gharama Zilizotumika

Sehemu ya 14.3 ya Kanuni za Fedha na miongozo ya kihasibu ya shirika la Reli inahitaji kuanzishwa kwa taratibu za mwisho wa mwaka ili kuhakikisha usahihi na ulinganifu wa uandishi wa taarifa za mwezi na taarifa za malipo na fedha zilizopokelewa.

Mapitio ya hati za malipo ya mkandarasi na vocha za malipo yalibaini kuwa malipo ya hati 2 kwenda kwa mkandarasi na 2 za mhandisi mshauri yalitambuliwa kwenye vitabu vya akaunti wakati fedha zinalipwa lakini sio wakati matumizi yalipopatikana kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 5-1** hapa chini.

Table 5- 1: Kutotambuliwa kwa gharama zilizotumika (Hati za malipo ya mkandarasi na mhandisi mshauri)

Kielelezo	Kipande (Lot)	Maelezo	Zilitambuliwa Ndani ya	Badala ya Mwaka wa Fedha	Dola za Marekani

[11] Kiwango cha kubadilisha fedha cha Benki Kuu ya Tanzania mwezi Desemba 2020 (Dola 1 ya Marekani = Shilingi 2,319 ya Tanzania)

			Mwaka wa Fedha		
Hati namba 10 (Mkandarasi)	1	Hati ya Malipo ya Mkandarasi ya tarehe 19/06/2018	2018/19	2017/18	14,044,557.14
Hati namba 2 (Mhandisi mshauri)	2	Hati ya Mhandisi Mshauri ya tarehe 21/06/2018	2018/19	2017/18	823,457.00
Hati namba 6 (Mhandisi mshauri)	1	Hati ya Mhandisi Mshauri ya tarehe 1/11/2017	2018/19	2017/18	823,674.00
Hati namba 22 (Mkandarasi)	2	Hati ya Malipo ya Mkandarasi ya tarehe 30/05/2020	Haitambuliki	2019/2020	31,721,191.76
Jumla					**47,412,879.90**

Chanzo cha taarifa: *Hati za malipo ya mkandarasi, hati za malipo ya mhandisi mshauri, Leja ya Jumla, Vocha za Malipo na Stakabadhi.*

Kutoka **Jedwali Na. 5-1**, inaonyeshwa kuwa Dola za Marekani 31,721,191.76 zilitambuliwa wakati pesa zilipolipwa na siyo wakati matumizi yalipopatikana. Ilibainika kuwa, taasisi haikuona kutofuatwa kwa taratibu ndani ya mwaka mzima wa fedha. Hii inaweza kusababisha tafsiri isiyo sahihi ya taarifa za fedha.

(iv) Kutofautiana kwa Viwango vya Kubadilishia Fedha Wakati wa Malipo ya Mkandarasi

Sehemu ya 5 ya makubaliano yaliyosainiwa tarehe 3 Februari, 2017 inahitaji 65% ya bei ya mkataba kulipwa kwa Dola ya Marekani na 35% kulipwa kwa Shilingi ya Tanzania.

Hata hivyo, ilibainika kuwa, 35% ya sehemu ya Shilingi ya Tanzania ya hati nambari 10 ya malipo ya mkandarasi ya kipande cha kwanza ilibadilishwa kwa kutumia bei ya kununulia siku ya kupokea malipo, wakati katika hati namba 11 hadi 16 sehemu ya 35% ilibadilishwa kwa kutumia kiwango cha ununuzi katika tarehe ya uthibitisho badala ya kiwango cha kuuza cha Benki Kuu ya Tanzania (BOT). Hali hii ya kutumia kiwango cha ununuzi badala ya kiwango cha kuuza ni hatari inayoweza kuleta migogoro kwa sababu ya ukosefu wa ufanano juu ya matumizi ya viwango vya ubadilishaji kama ilivyoainishwa katika mkataba.

(v) Ucheleweshaji wa Kuondoa Kodi ya Zuio

Kifungu cha 84 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kinamtaka kila wakala anayetoza kodi ya zuio kulipa kwa Kamishna Kodi yoyote ya mapato iliyozuiwa ndani ya mwezi husika katika kipindi cha siku saba baada ya mwezi wa kalenda kuisha.

Mapitio ya hati za malipo ya mkandarasi na vocha za malipo yalibaini kuwa, ushuru wa zuio ulikatwa kwenye malipo yaliyofanyika kwa awamu nane kwa wakandarasi na wahandisi washauri. Pamoja na hayo, malipo yao hayakupelekwa TRA kwa wakati. Ilibainika kuwa, ucheleweshaji wa hali ya juu zaidi ulikuwa kwa CFP 6 ya kipande cha kwanza cha ujenzi. Malipo haya yalicheleweshwa kwa siku 82, yakifuatiwa na ya hundi namba 17 ya malipo ya mhandisi mshauri kwa kipande cha kwanza yaliyocheleweshwa kwa siku 76.

(vi) Kutotolewa kwa Kodi ya Zuio Kutoka Kwenye Hati ya Malipo Namba 20 (IPC 20)

Uhakiki wa hati za malipo ya mkandarasi ulibaini kuwa, kodi ya zuio ya hati namba 20 ya malipo kwa mkandarasi yenye thamani ya Sh. 2,290,493,768.97 ilipunguzwa kutoka kwenye vocha ya malipo namba 19428 ya tarehe 8 Mei 2020. Hata hivyo, kodi hiyo haikutolewa TRA. Hii ilitokana na ukweli kwamba, Shirika la Reli Tanzania liligundua kuwapo kwa malipo mara mbili kwenye mfumo wa TRA katika Hati Na. 19. Kutokana na hili, TRC wanafanya mazungumzo na TRA kuhamisha ushuru wa ziada uliowekwa ili uongezwe kwenye hati namba 20.

Ninapendekeza Shirika la Reli lihakikishe kwamba, zuio la kodi linalokatwa kutoka kwenye malipo kwa wakandarasi na Wahandisi washauri linawasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ndani ya muda unaokubalika kisheria.

d) Udhaifu Ulibainika Katika Kusimamia Ubora wa Kazi

Upitiaji wa mambo ya kiufundi ya mradi ulibaini udhaifu katika usanifu wa majengo kama ilivyoelezwa hapa chini:

(i) Uzingatiaji Hafifu wa Matumizi ya Nishati

Nilibaini kuwa, usanifu wa majengo ya abiria katika vituo vya abiria vya Dar es Salaam na Morogoro haukuzingatia hali ya matumizi ya nishati. Pia, haukuzingatia uwezekano wa kukatika kwa umeme na hali za dharura wakati wa uendeshaji. Ilibainika kuwa, majengo yote mawili yalisanifiwa kutegemea tu viyoyozi na hakukuwa na madirisha ya uingizaji hewa ya asili pindi umeme ukikatika.

(ii) Uwekaji wa Miundombinu Isiyozingatia Njia za Kiusalama na Uokoaji Wakati wa Dharura

Wakati wa ziara kipindi cha ukaguzi ilionekana kuwa usanifu na ujenzi wa kituo cha abiria cha Morogoro haukuzingatia uwekaji wa njia salama za kutoroka wakati wa dharura. Jengo limejengewa ngazi nyembamba na lifti kama njia pekee ya kuwezesha kupanda/kushuka; na halijazingatia uwekaji wa njia za kupandia kama njia mbadala ya watumiaji, haswa walemavu. Hii inaweza kuleta shida kwa watumiaji ikitokea dharura, umeme ukikatika na changamoto zinazohusiana na jenereta, hasa masuala ya matengenezo na matumizi endelevu. Njia za kupandia husaidia watu wenye mahitaji mbalimbali kama vile wagonjwa, walemavu na wazee kuweza kutoka ghorofa moja kwenda nyingine na kushuka chini wakati wa dharura na kusaidia kipindi wanahitaji uokoaji.

(iii) Matokeo ya Vipimo vya Kuhakiki Kuzingatiwa kwa Ubora wa Kazi

Nilitembelea maeneo mbalimbali ya mradi wa Reli ya kisasa (SGR) kuanzia tarehe 23 hadi 24 Januari 2021 kwa lengo la kutathmini ubora wa kazi zilizofanyika. Aidha, ulifanyika uchunguzi wa ubora wa sehemu za reli zilizoungwa kwa kuchomelewa kwa njia ya "Ultrasoniki" pamoja na kukusanya sampuli za reli na za nondo kwa ajili ya kuzifanyia vipimo vya kimaabara. Nilichukua sampuli za reli na za nondo kwa kipande cha pili (Lot 2) kutoka katika kambi ya Kilosa, wakati kwa kipande cha mwanzo (Lot 1) zilikusanywa kutoka kambi za Soga na Ilala. Kwa ujumla, vipimo vilivyofanyika maabara kwa sampuli zote zilizokusanywa kutoka maeneo mbalimbali ya mradi vilikidhi viwango vya ubora vilivyoanishwa kwenye mikataba husika.

Pia, nilitembelea maeneo mbalimbali ya mradi wa Reli ya kisasa (SGR) kuanzia tarehe 22 hadi 28 Januari 2021 kwa lengo la kutathmini ubora wa kazi zilizofanyika. Ukaguzi ulihusisha upimaji wa kiwango cha ushindiliaji (field density), uwezo wa zege pamoja na mataruma ya zege kuhimili mkandamizo kwa kutumia kifaa maalum. Pia, nilikusanya kokoto maalum kwa ajili ya ujenzi wa reli, kokoto ndogondogo na mchanga na sampuli za maji kwa ajili ya kuzifanyia vipimo vya kimaabara. Upimaji na uchukuaji wa sampuli ulifanywa kwenye maeneo maalum ya mradi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma. Kwa ujumla, matokeo ya vipimo vya kimaabara vilivyofanyika kwa sampuli zote zilizokusanywa kutoka maeneo mbalimbali ya mradi yalikidhi viwango vya ubora vilivyoanishwa kwenye mikataba husika.

Napendekeza Shirika la Reli kuendelea kusimamia mradi huu kwa ipasavyo.

5.3.2 Usimamizi Usioridhisha wa Mazingira, Afya, Usalama na Masuala ya Kijamii

Nilibaini udhaifu ufuatao:

a) Mradi wa SGR Ulianza Kabla ya Kufanyika kwa Tathmini ya Uharibifu wa Kimazingira (EIA)

Sehemu ya 81 (2) ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (EMA) inahitaji Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA) kutekelezwa kabla ya kuanza au kufadhili mradi.

Nilibaini kuwa, kazi ya ujenzi wa mradi wa SGR Kipande cha 1 ulianza tarehe 2 Mei 2017, wakati Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA) ilifanywa Novemba 2018; na iliyorekebishwa ilikuwa Februari 2019. Hii inamaanisha kuwa, tathmini ya athari ya mazingira ilifanywa mwaka mmoja baada ya mradi wa SGR ukiwa umekwishaanza utekelezaji.

Pia nilibaini kuwa, Shirika la Reli (TRC) lilianza kufuatilia utendaji wa mkandarasi kuelekea kushughulikia masuala yanayoweza kuathiri mazingira mnamo Novemba 2018. Ilibainika kuwa, katika kipindi hicho TRC iliratibu utendaji kazi wa mkandarasi katika kuzuia uharibifu wa mazingira kwa kutegemea mpango wa

usimamizi wa kuzuia uharibifu wa mazingira na kijamii ulioandaliwa na mkandarasi. Hata hivyo, TRC haikuweza kuwasilisha Ripoti za Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Robo mwaka za kipindi hicho ili kuthibitisha kama ilikuwa imefuatillia utendaji kazi wa Mkandarasi; vilevile ili kuweza kujua kwamba mkandarasi anafuata Viwango vya Mazingira vya Kitaifa na Kimataifa wakati ambapo hakukuwa na ripoti ya ESIA.

Ninapendekeza Shirika la Reli kuhakikisha kuwa Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (ESIA) inafanywa kabla ya kuanza kutekeleza Mradi wowote wa ujenzi ambao unaweza kuwa na athari mbaya kwa mazingira.

b) Utupaji Holela wa Maji Taka Kutoka Kambi za SGR

Ziara iliyofanywa katika eneo la utupaji wa maji taka ilibaini kuwa, hakukuwa na uchujaji/utibiwaji bora wa maji taka; badala yake, maji taka yalitupwa tu kwenye dimbwi (Tazama Picha 5.1). Licha ya ukweli kwamba, bwawa hili lilikuwa na lengo la kutibu maji taka lakini ilibainika kuwa bwawa halikuwa na seli zinazoshauriwa kitaalumu kuruhusu kuondolewa kwa vimelea vya magonjwa.

Kuwapo kwa maji taka yasiyotibiwa kunahatarisha uhai wa wanyama na viumbe vingine vilivyo kwenye misitu. Hii ni kwa sababu maji taka yaliyotajwa hapo juu yana mkusanyiko mdogo wa oksijeni. Hivyo, wakati viumbe hai vikiwa ndani ya majitaka hayo vinaweza kufa.

Picha 5.1: Utupaji wa maji taka yasiyotibiwa kutoka kambi za SGR kwenda kwenye bwawa (Picha ilichukuliwa tarehe 29 Januari 2021).

c) Ufuatiliaji Usioridhisha Juu ya Ubora wa Maji Taka Yanayotiririshwa kwenye Mazingira

Kulingana na ripoti za tathmini ya athari za Kimazingira na kijamii (ESIA) moja ya majukumu ya TRC ni kutekeleza kila mwezi ufuatiliaji wa mambo ya uchafuzi wa mazingira yanayotokana na mradi wa SGR na kuhakikisha ubora wa maji kwa kuyapima maji mara kwa mara, hasa katika maeneo nyeti ya vyanzo vya maji katika eneo la mradi.

Ilibainika kuwa majitaka yanayotoka kwenye mitambo iliyojengwa ya kutibu mafuta na grisi yalikuwa yanapimwa, ila sio mara kwa mara kama inavyotakiwa na tathmini ya athari ya mazingira. TRC ilitegemea matokeo ya upimaji yaliyotolewa na mkandarasi. Ilibainika zaidi kuwa, TRC haijawahi kufanya au kuthibitisha kuwa matokeo yanayotolewa na mkandarasi kila wakati yanakidhi kiwango.

Ninapendekeza Shirika la Reli lihakikishe kwamba maji taka kutoka kambi za mradi wa ujenzi wa Reli za Kisasa (SGR) yanatibiwa vyema na kutolewa kwa njia inayofaa kuelekea kwenye mazingira ili kulinda maisha ya wanyama na viumbe vingine vinavyoishi ndani ya maeneo ambayo majitaka hutiririshwa.

d) **Utekelezaji Usio wa Kuridhisha wa Hatua za Kudhibiti Mrundikano wa Mchanga na Mmomonyoko**

Sharti C(V) (29/4/2019) linataka kibali kiwe kinatolewa na Mamlaka ya Bonde ya Maji la Ruvu/Wami; na kwamba, hatua za udhibiti lazima ziwe zinachukuliwa mara moja katika eneo la kazi ambapo udongo huwa katika hali ya kuweza kusababisha mmomonyoko. Vivyo hivyo, sharti E (I) linahitaji hatua za kudhibiti uhamaji wa mchanga kabla ya mabadiliko hayajaanza kutokea na kundeleza hatua hizi kwa kipindi chote cha wakati wa mabadiliko.

Katika mlima wa Pugu, ukaguzi uligundua njia tofauti zinazosababisha mmomonyoko. Ukaguzi uliofanywa kwenye maeneo ya mlima wa Pugu ulibaini kuwa urudishiaji wa maeneo yaliyoathirika na mradi (24 + 100km 6) kuja kwenye hali yake ya awali haukufanyika vizuri. Hii ni kwa kuwa mkandarasi alipanda nyasi katika maeneo machache wakati maeneo mengine hayakupandwa. Ukaguzi pia uligundua kuwa, sehemu ya mchanga ulio wazi ilikuwa inamomonyoka, hasa wakati wa mvua, kutokana na kutokuwapo kwa miundombinu ya kuzuia mmomonyoko wa udongo.

Athari inayotokana na kuwapo kwa mmomonyoko wa udongo ni kuongezeka kwa tope au mchanga kwenye mito na vyanzo vingine vya maji vilivyopo bondeni mwa mlima Pugu kutokana na maji yanayotiririka kuishia kwenye mito. Pia, uwezekano wa kuongezeka kwa tope na mchanga ukiwa umechanganyika na maji katika Mto Msimbazi ni mkubwa. Zaidi ya hayo, kwa kuwa Mto Msimbazi unavuka ardhi oevu ya asili ya Jangwani karibu na kituo cha mabasi ya yaendayo haraka (DART), hii pia itachangia kuongezeka kwa mchanga katika ardhi oevu.

e) **Kucheleweshwa Kurejeshwa katika Hali ya Awali kwa Mlima Pugu na Mashimo Makubwa**

Hadi wakati wa kufanya ukaguzi huu, maeneo yaliyoathiriwa ya Pugu Hill na Misitu ya akiba ya Ruvu iliyoathiriwa na ujenzi wa SGR yalikuwa hayajarejeshwa vya kutosha. Ilibainika kuwa, ili kurejesha mlima wa Pugu na pori la Akiba la Ruvu Kusini msaada ulihitajika kutoka kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFSA). Zaidi, ilibainika kuwa kuna mkataba wa makubaliano

(MoU) kati ya TRC na TFSA juu ya ushirikiano wa shughuli za mpango wa utekelezaji wa bioanuwai kurejesha maeneo yaliyoathiriwa. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi huu hakukuwa na ushahidi kwamba pande hizo mbili zimeanza kutekeleza memoranda hiyo.

Kwa upande mwingine, ukaguzi uligundua kuwa, shimo namba 225 lililoko Mkata Ranchi ya Morogoro bado halijarejeshwa katika hali yake ya awali. Ilifafanuliwa zaidi kuwa mkandarasi aliacha kuchukua vipuli vya ujenzi kutoka katika shimo hilo. Ilibainika zaidi kuwa, hadi wakati wa ukaguzi huu sehemu ndogo sana ya shimo ilianza kufukiwa, na sehemu iliyobaki ilibaki kwa takribani mwaka mmoja.

Mahojiano na maafisa kutoka TRC yalionesha kuwa, shimo hilo halikufukiwa kwa sababu kulikuwa na mazungumzo kati ya Ranchi ya taifa na Mkandarasi kuhusiana nalo. Barua ya tarehe 22 Januari 2019 kutoka kwa Kampuni ya Ranchi ya Taifa kwenda kwa Mkandarasi ilimtaka Mkandarasi asijaze shimo hilo badala yake liachwe kwa ajili ya kuhifadhia maji (DAM) kwa matumizi ya ranchi na jamii za mifugo. Jibu kutoka kwa Mkandarasi kupitia barua ya tarehe 22 Desemba 2020 ilifafanua kwamba, mkandarasi hakukubali ombi hilo kwa sababu za kiafya na usalama. Ilibainika kuwa shimo hilo limeendelea kubaki kama lilivyo bila kujazwa kwa miezi 14 hadi wakati wa ukaguzi huu.

Kwa kuongezea, nilibaini kuwa, shimo hilo halikuwa limezungushiwa alama kwa kuzingatia masuala ya usalama kwa wanyama/mifugo. Pia, hakukuwa na ishara za onyo katika sehemu za kuingilia kuelekea ndani ya shimo hilo.

Ninapendekeza Shirika la Reli kuhakikisha mazingira yaliyoathiriwa na miradi yanarudishwa kwa wakati kwenye hali ya awali.

f) Athari kwa Jamii Kutokana na Mafuriko

Wakati wa ziara ilionekana kuwa kulikuwa na mafuriko kwenye eneo la 194 + 000km ndani ya Manispaa ya Morogoro ambapo daraja la urefu wa mita 80 limejengwa. Hii ilikuwa kwa sababu,

wakati wa ujenzi wa tuta la reli hakukuwa na mfereji wa kuhifadhi na kuondoa maji kutoka kwa jamii.

Ukaguzi pia uligundua kuwa, kalvati lililowekwa kenye barabara ya dharura lilikuwa dogo sana kiasi cha kulishindwa kuhimili mkusanyiko mkubwa wa maji. Hivyo, lilipelekea maji kurudi kwenye makazi ya watu na kuleta athari kama kuathiri mali za watu na baadhi ya nyumba kubomoka kwa jamii yote inayoishi katika eneo hilo ambalo huwa na mito ya misimu.

Licha ya kuwa na uelewa wa majira ya mvua, ujenzi wa matandiko chini ya daraja haukuzingatiwa kama jambo la dharura ili kuruhusu mtiririko rahisi wa maji kutoka upande wa mto na kuepuka mafuriko. Hii imeoneshwa kwenye Picha 5.2 hapa chini

Picha Na. 5.2 Eneo lililoathiriwa na ujenzi unaoendelea wa SGR. Picha ilipigwa Km.194 ndani ya Manispaa ya Morogoro (Picha imechukuliwa tarehe 29/1/2021).

Ninapendekeza Shirika la Reli kuweka miundombinu ya kutosha kwa kuruhusu mtiririko rahisi wa maji ili kupunguza hatari ya mafuriko kwa jamii.

SURA YA SITA

UJENZI WA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE

6.1 Utangulizi

Ujenzi wa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP) ambao awali ulijulikana kwa jina la Mradi wa Umeme wa Maji Rufiji (RHPP) ni moja miongoni mwa miradi ya kimkakati inayotekelezwa na serikali. Mradi huu upo kwenye mto Rufiji. Malengo ya mradi huu ni kuzalisha nishati ya umeme itokanayo na maji, kudhibiti mafuriko kwenye maeneo yaliyopo chini ya mto Rufiji, kuanzisha miradi ya kilimo cha umwagiliaji, kusambaza maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, pamoja na kuongeza udhibiti wa mazingira na uhifadhi wanyama pori. Zaidi, lengo la mradi ni kuzalisha umeme wa mega-wati 2,115, ambapo mara mradi utakapokamilika inatarajiwa kuzalisha kiwango cha nishati cha giga wati 5,920 kwa mwaka.

Mradi huu unatekelezwa na Shirika la Usambazaji wa Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kupitia kitengo cha (TECU) ambaye ni mhandisi mshauri anayesimamia mradi. Shirika la Umeme Tanzania ilisaini mkataba Na. ME/008/2017-2018/HQ/W/03 na kampuni ya Kandarasi ya Ubia wa Pamoja (JV-ACEE) baina ya Mkandarasi M/S Arab Contractors "Osman A. Osman & Co." (AC) na kampuni ya Misri El Sewedy Electric (EE) wenye thamani ya kiasi cha Sh. Trilioni 6.558 (sawa na Dola za Marekani milioni 2,900). Fedha hizi zinalipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muda wa utekelezji wa mradi huu ni miezi arobaini na mbili (42), ikiwa ni pamoja na kipindi cha a miezi sita (6) kwa ajili ya maandalizi kutokea tarehe ya kusaini mkataba ambayo ni tarehe 15 Desemba 2018. Mradi unatarajiwa kukamilika tarehe 14 Juni 2022.

6.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi

Lengo la ukaguzi huu ilikuwa ni kutathmini ikiwa Shirika la Umeme Tanzania lilikuwa linasimamia ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere kwa kuzingatia muda, gharama na ubora (kulingana na viwango vilivyobainishwa) kwa shabaha ya kufikia malengo ya mradi.

Ukaguzi wangu ulihusisha uzingatizi wa muda wa mradi, upangaji, masuala ya fedha, manunuzi, usimamizi wa mikataba, masuala ya kiufundi, masuala ya mazingira, pamoja na athari za mradi kwa kwa jamii. Ukaguzi wa kiufundi pia ulifanyika kuhusiana na namna mradi ulivyopangiliwa, ulivyosanifiwa, manunuzi yalivyofanyika na mradi ulivyotekelezwa kwa kuzingatia viwango vilivyotumika, vipengele vya ubora pamoja na utendaji kazi uliodhihirishwa.

Zaidi, Ukaguzi wa kiufundi ulihusisha miaka mitatu ya fedha, kuanzia 2017/18 hadi 2019/20. Hii ni kwa sababu Shirika la Umeme Tanzania ilianza kutekeleza mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP) kwa vipengele vya msingi kuanzia kwenye usanifu na maendeleo yaliyofanyika wakati wa utekelezaji wake.

6.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya Ukaguzi kuhusu usimamizi wa ujenzi wa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP) kwa kuzingatia muda, gharama na ubora (kulingana na viwango vilivyobainishwa) ili kuhakikisha malengo ya mradi yanafikiwa. Matokeo ya Ukaguzi yamegawanywa kulingana na vipengele muhimu vinavyounda mchakato wa mradi ambayo inajumuisha upangaji, usanifu, manunuzi, usimamizi wa mikataba, pamoja na uzingatizi wa mazingira, afya, usalama na jamii.

6.3.1 Upangaji na Usanifu wa Mradi

Jukumu la kuhakikisha muundo wa mradi unaendana na mahitaji ya mteja unafanywa na TANESCO kupitia TECU. Hata hivyo, kupitia ukaguzi wa usanifu wa awali, usanifu wa kina na mahitaji ya mwajiri, nilibaini mapungufu kadhaa kwenye upangaji na muundo kama ilivyoelezwa hapa chini:

a) Kutokuwapo kwa Upembuzi wa Kina Uliohuishwa

Mradi wa umeme wa JNHPP una malengo mengi kwa ajili ya matumizi ya maji. Hivyo basi, utekelezaji wake unapaswa kufuata Sheria ya Umeme ya mwaka 2008, Sheria ya Umwagiliaji ya Kitaifa ya mwaka 2013[12], Sheria za Usimamizi ya Vyanzo vya Maji ya mwaka 2009 na

[12] Vifungu 20(2) na 20(3) Sheria ya Umwagiliaji ya Kitaifa 2013

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya 2004. Sheria hizi zote zinaelezea uhitaji wa kuwapo kwa upembuzi yakinifu kabla mradi haujafadhiliwa na kutekelezwa. Kwa hali hii, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupitia Mhandisi Mshauri na Msimamizi wa Mradi (TECU) kama mwakilishi wa mwajiri lilitarajiwa kupitia upya na kuhuisha upembuzi yakinifu uliofanyika hapo awali na kupata mapitio mapya ili kuitumia taarifa hiyo katika kuandaa usanifu wa kina wa kila shughuli ya Mradi wakati wa ujenzi.

Hata hivyo, nilibaini kuwa, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilishindwa kuhuisha vipengele vyote vya upembuzi yakinifu uliofanyika awali. Badala yake, lilitegemea upembuzi yakinifu ambao ulifanywa katika miaka ya 1970 na 1972 na kampuni ya M/S Norconsult (ya Norway) pamoja na Mpango mtambuka wa mradi na ripoti ya uchunguzi wa kiufundi uliofanywa na kampuni ya M/S Hafslund na M/s Norplan (wote kutoka Norway) ambayo iliweza kuhuisha vipengele vya taarifa ya upembuzi yakinifu. Hii ilifanyika miaka ya 1980.

Vipengele vikuu vilivyohuishwa ni pamoja na tathmini ya athari za mazingira (EIA), usanifu wa kiufundi na utafiti wa jiolojia na utafiti wa kiutaalamu wa ufanisi wa miamba. Vipengele ambavyo havikufanyiwa mapitio na kuhuishwa ni pamoja na utafiti wa kiuchumi na kifedha wa mradi, tafiti za kuwepo kwa maji na uendeshaji endelevu wa mradi.

Maafisa waandamizi kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na TECU walieleza kwamba, upembuzi yakinifu uliofanyika katika miaka ya 1970 ulionesha kwamba mradi unawezekana kitaalamu, kiuchumi na kifedha. Maafisa waliongeza kuwa kutokana na uharaka wa kuanza utekelezaji wa mradi, taarifa za upembuzi za awali hazikuweza kupitiwa upya zote ili kuzihuisha. Sehemu ya tafiti ambazo hazikupitiwa upya ni pamoja na zile za kiuchumi na kifedha, upatikanaji endelevu wa maji, tabia ya miamba na usanifu wa kiuhandisi.

Yapata takribani miaka 50 tangu tafiti za upembuzi yakinifu zilipofanyika mwaka 1970. Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilipaswa kufanya stadi za upembuzi yakinifu ili zitoe mwongozo kwenye usanifu wa ujenzi wa mradi unaoendelea kutekelezwa. Ingawa mradi ulitambulika kuwa unatekelezeka, unafaa na

endelevu, kutokuwepo kwa upembuzi yakinifu wa kina uliohuishwa hakutoi uhakika kwamba mradi utatekelezeka, una manufaa na utasaidia katika kuongeza uchumi katika taifa. Inakuwa ni vigumu kuthibitisha juu ya uendelevu wa mradi, hasa kwa upatikanaji wa vyanzo vya maji, ili kusaidia mradi kuzalisha umeme kwa misimu yote ya mwaka.

b) Kutowekwa kwa Mfumo wa Kutoa Uchafu Kwenye Bwawa na Kwenye Njia za Maji Kuelekea Kwenye Mitambo ya Kuzalisha Umeme

Kifungu 10.11.2(2) cha Matakwa ya Mwajiri Juzuu ya II ya Desemba 2017 kilimtaka Mkandarasi kuweka mfumo wa kutoa uchafu. Vivyo hivyo, Kifungu 9.2 cha Usanifu Mkuu wa Awali Juzuu ya I na Kifungu 8.1.2 c. na 8.2.4 ya Matakwa ya Mwajiri Juzuu ya II vinahitaji kuwapo kwa valvu au matundu mawili sehemu ya chini kwenye bwawa (2 butterfly Valves) na reki mbili za kuchuja uchafu kwa ajili ya ekolojia. Vivyo hivyo, aya ya pili ya Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na maswala ya Kijamii (ESMP) kwa ajili ya usimamizi/uhifadhi wa mto na kingo za mto Udhibiti wa Mafuriko, kuimarisha miinuko, inataka Shirika la Umeme Tanzania(TANESCO) kuandaa na kutekeleza hatua zinazofaa za kuzuia uharibifu wa kingo za mto. Kwa upande wake, aya ya 5 inataka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kudhibiti uchafu kutuama ndani ya bwawa la hifadhi ya maji kwa kuweka mifumo ya kuruhusu uchafu kutiririka nje ya bwawa la maji.

Nilibaini kuwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) halikuhakikisha kwamba mkandarasi anaweka mifumo ya kutoa uchafu kwenye bwawa kupitia matundu ya chini na kuyatiririsha ndani ya mkondo wa chini wa mto kwa ajili ya mazingira/ekolojia kipindi cha ujazwaji wa bwawa. Vivyo hivyo, usanifu wa mkandarasi haukuwa na mifumo ya kutolea uchafu kwenye mkondo wa kuchepusha maji kwenda kwenye mtambo wa kufulia nishati (Headrace Power Tunnels) na kurudisha uchafu ndani ya mto.

Maafisa kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) waliwaelezea wakaguzi kuwa, mfumo wa kusafisha uchafu hautumiki kwa mabwawa makubwa kwa sababu hatari itokanayo na kutuama kwa uchafu ni ndogo. Hata hivyo, Ukaguzi una maoni kwamba, kwa kuwa ilitajwa katika Matakwa ya Mwajiri kwa lengo la kuzuia mmomonyoko upande wa chini ya mto na kwa ajili ya kuongeza uimara wa bwawa, uamuzi

huu wa TECU ulifanywa bila tathmini ya kutosha juu ya athari ya muda mrefu ya mkusanyiko wa uchafu kwenye mitambo na kuzingatia athari ya uharibifu kama inavyooneshwa katika Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Masuala ya Kijamii (ESMP).

Ukosefu wa mifumo ya kutoa uchafu kunaashiria hatari ya kuathiri uimara wa bwawa kwa sababu ya mmomonyoko wa msingi wa bwawa na kuongezeka kwa kina cha mkondo wa chini wa mto. Pia, huweza kufanya umwagiliaji kuwa mgumu kwa maeneo yaliyo baada ya bwawa. Kwa kuongezea, uchafu unaweza kuingia kwenye njia za maji yanayoenda kwenye mtambo ya kufua umeme, Hatimaye, hali hii huweza kusababisha athari kama vile kulika kwa mapanga ya mitambo ya kufua umeme (turbine), kupunguza ufanisi wa mtambo wa kufua umeme na kusababisha gharama kwa ajili ya kubadilisha mapanga ya mara kwa mara ya mitambo pamoja na athari nyingine zinazoambatana nazo.

c) Ujenzi wa Mkondo Mmoja Badala ya Mikondo Miwili, kinyume na Ilivyoainishwa Kwenye Matakwa ya Mwajiri na Usanifu wa Awali wa Mradi

Ukaguzi wangu wa Maelelezo ya Mkandarasi kuhusu Ujenzi wa mikondo ya kuchepushia maji ya mto Rufiji ili kupisha shughuli za ujenzi wa eneo la bwawa kuu ulibaini kuwa, Mkandarasi alijenga mkondo mmoja wenye uwezo wa kupitisha maji kiasi cha mita za ujazo kwa sekunde 6,170 badala ya mikondo miwili kwa ajili ya kuchepusha maji yenye uwezo wa kupitisha maji kiasi cha mita za ujazo kwa sekunde 7,000 (main dam). Hii ni kinyume na Kifungu cha 12.3 cha Matakwa ya Mwajiri Juzuu ya II ya Desemba 2017 kinachomtaka Mkandarasi kujenga mikondo miwili kwa ajili ya kuchepusha maji yenye uwezo wa kupitisha maji kiasi cha mita za ujazo kwa sekunde 7,000.

Hii inamaanisha kuwa, ujenzi wa mkondo mmoja badala ya miwili, umepunguza uwezo wa kupitisha maji kwa kiwango cha 11.9% (kutoka mita za ujazo kwa sekunde 7,000 kama ilivyokusudiwa hapo awali hadi kufikia mita za ujazo kwa sekunde 6,170 ambazo ndizo zilizojengwa).

Hali hii ilipelekea ucheleweshaji wa mradi kwa miezi mitano (5) kutokana na tuta-kingo la kuzuia maji kugharikishwa, kisha maji kufurika ndani ya mkondo wa kuchepushia maji ya mto. Athari hii ingeweza kuepukika iwapo utekelezaji wa Usanifu wa Mradi wa Awali

ungezingatiwa kwa kujenga mikondo miwili kwa kuanza kuchimba mkondo mmoja baada ya mwingine. Hii ni kwa sababu kabla ya eneo hilo kujaa maji, kiwango cha kazi kilikadiriwa kuwa cha kutosha kukamilisha uchimbaji wa mkondo mmoja mfupi (wa urefu wa mita 497 na uwezo wa mita za ujazo kwa sekunde 3,500) ili kuruhusu sehemu ya maji ya mafuriko kupita. Hivyo, wakati maji yaliyokuwa yamefurika yangekuwa yamepita kwenye mkondo mmoja uliokamilika baada ya tuta kingo la muda kugharikishwa, ujenzi wa mkondo mwingine ungekuwa ukiendelea. Janga lilidumu kwa takribani miezi mitano ya ucheleweshwaji wa kazi za mradi, hivyo basi, iliwezekana kuepukika ikiwa umakini ungezingatiwa katika kutekeleza mikondo miwili ya kuchepushia maji.

Aidha, uamuzi uliofanywa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) katika kuidhinisha usanifu wa mkandarasi wa kujenga mkondo mmoja badala ya mikondo miwili kulingana na Usanifu wa Mradi wa Awali haukuzingatia vya kutosha ukubwa wa mafuriko kulingana na taarifa za kihistoria za haidrolojia. Picha Na. 6.1 (a) na (b) zinaonesha mkondo wa kuchepusha maji uliojengwa kama nilivyoshuhudia wakati wa ziara katika eneo la mradi.

Kielelezo 6.1(a): Muonekano wa mbele wa Mkondo. Picha ilipigwa tarehe 15 Desemba 2020	Kielelezo 6.1 (b): Mtazamo wa Nyuma wa mkondo. Picha ilipigwa tarehe 15 Desemba 2020

Maafisa kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) walielezea kuwa, waliridhia Mkandarasi kujenga mkondo mmoja badala ya miwili kama ilivyokusudiwa awali, kwa sababu walitaka kuharakisha maendeleo ya kazi, kwani kujenga mkondo wa kuchepusha maji ilikuwa kazi iliyo kwenye shughuli ya lazima katika mradi. Kwa kuwa mbinu ya utekelezaji iliyopendekezwa na Mkandarasi ilikuwa na faida

ikilinganishwa na muda wa utekelezaji wa mradi. Maafisa hao waliongeza kuwa, ikiwa wangeruhusu kufuata mpango wa awali ingeweza kuchukua hadi miaka mitatu kukamilika. Hata hivyo, TECU haikuzingatia teknolojia na mbinu za uchorongaji mwamba zilizotumiwa na Mkandarasi ambazo pia zingesaidia utekelezaji wa ujenzi wa mikondo miwili ya kuchepusha maji ndani ya muda uliopangwa.

d) Matakwa ya Mwajiri Kutokuwa na Viwango vya Kutosha vya Mbinu za Kuzuia Kutu Kwenye Vyuma

Ninatambua kuwapo kwa viwango vingine vya kulinda miundombinu ya chuma ambavyo huwekwa juu ya ardhi ambavyo pia vinahitaji kulindwa dhidi ya kutu kama ilivyoahinishwa katika Kipengele cha 7.33 cha Matakwa ya Mwajiri. Hata hivyo, niligundua kwamba waraka wa mahitaji na Matakwa ya Mwajiri haukuainisha namna ya kulinda chuma kinachozikwa au kinachokuwa kimezamishwa kwenye maji dhidi ya kutu kama ilivyokuwa imeshauriwa na Chama cha Kimataifa cha Viwango cha Wahandisi wa Kutu (National Association of Corrosion Engineers (NACE)). Kutokana na viwango vya kuzuia kutu vilivyooneshwa kwenye miongozo ya chama hicho cha wataalamu wa kutu, mfumo wa kuzuia kutu hutumia umeme (Cathodic electic current) kupaka chuma rangi kwa ajili ya kuzuia kutu ambayo ni njia au mfumo bora wa kuzuia na kupambana na kutu kwenye chuma kilichozikwa chini au kuzamishwa kwenye maji.

Matokeo yake, Mkandarasi hakutumia njia sahihi ya kuzuia kutu katika baadhi ya vyuma vilivyozikwa chini na kuzamishwa kwenye miamba na maji. Hii imeshuhudiwa na mimi kwa kujihakikishia kilichofanyika kwa kutembelea mradi pale ambapo timu iliona mabomba makubwa ya chuma ya chini ya kutolea maji kwenye tuta kuu la bwawa la umeme hayakulindwa kwa njia sahihi dhidi ya kutu.

Kutokutumia njia sahihi za kulinda chuma kilichozikwa chini au kuzamishwa ndani ya maji kunaweza kusababisha hatari ya kutokufikia maisha marefu ya chuma yaliyosanifiwa kutokana na tatizo la kutu. **Picha Na. 6-2** inaonesha mabomba makubwa ya chuma ya chini yaliyozikwa katika tuta kuu la bwawa yakiwa hayajalindwa kisahihi dhidi ya kutu.

Picha Na. 6.2: Mabomba Makubwa ya Chuma ya Chini ya Tuta Kuu

Picha Na. 6-2 inaonesha mabomba makubwa ya chuma ya chini ya Tuta kuu la Bwawa yatakayozikwa yakiwa hayajalindwa kwa njia sahihi dhidi ya kutu.

Maafisa kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na TECU walifafanua kwamba katika mkataba wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi (EPC) Mkandarasi anaruhusiwa kupendekeza njia za ujenzi zenye kuongeza thamani kama ilivyoonesha sehemu ya 7.3.1 katika andiko la nakala ya Matwakwa ya Mwajiri. Maafisa hao walieleza zaidi kuwa tuta kuu la zege lililoshindiliwa litakalozika chuma na mabomba ya chuma ni sawa na viwango vya Kimataifa vya NACE. Kwa mujibu wa Maafisa hao, Tuta kuu la zege linatoa madhara madogo madogo ya mabomba ya chuma yaliyozikwa chini ya ardhi au kuzamishwa kwenye maji. Nina mtazamo kwamba, TANESCO bado wanahitaji kutumia njia sahihi iliyopendekezwa kulinda mabomba yatakayozikwa chini au yaliyozamishwa kwenye maji.

Ili kuboresha Usanifu na Mipango ya Utekelezaji wa Mradi, nashauri manejimenti ya Shirika la Usambazaji Umeme Tanzania (TANESCO) linatakiwa kufanya yafuatayo:

(a) Kuhakikisha kuwa ripoti ya upembuzi yakinifu iliyohusihwa inakuwepo kwa lengo la kuweka uwazi na kuufanya mradi utekelezeke; pia kuhakikisha inatumika kwa ajili ya muundo wa ujenzi kwa maeneo ya mradi ambao ujenzi wake unaendelea;

(b) Kuhakikisha kwamba Mwakilishi wa Mwajiri anahakiki vizuri muundo wa Mkandarasi na mbinu za utekelezaji (method statement) na kusisitiza utumiaji wa vipimo

vilivyopendekezwa ikiwa ni pamoja na vipimo vya NACE vilivyopendekezwa kwa ajili ya kuzuia kutu kwa vyuma viliyozikwa na kuzamishwa ardhini;

(c) Kurekebisha mabadiliko ya muundo kutoka mikondo miwili kuwa mkondo mmoja kwa kuanzisha uchambuzi wa kina katika mabadiliko ya muundo na mapendekezo yoyote yanayofanana na hili au mapungufu mengine katika utekelezaji wa mradi. Hidrolojia na taarifa nyingine zote ambazo ni msingi wa kazi za mradi katika hatua anuwai ikiwa ni pamoja na muundo, utekelezaji au ujenzi na mtambo ujao wa umeme na operesheni ya hifadhi inapaswa kutumiwa vyema ili kufanikisha malengo ya mradi; na

(d) Kupitia upya muundo uliobadilishwa ili kuzingatia ujumuishaji wa mashapo yanayotiririka kwenye mtiririko wa mto na nje ya mtiririko kwenda kwenye njia za umeme ili kulinda ubora na kulinda bwawa kwa muda mrefu (upande wa chini) kwa kuingizwa kwa mashapo kwenye mtiririko uliotolewa kutoka kwenye hifadhi na kutoa maji kuelekea kwenye mtambo wa umeme. Tathmini inapaswa kujumuisha uchambuzi wa vihatarishi ili kuhakikisha vinakuwa vidogo na kuzuia kwa muda mrefu dhidi ya uharibifu wa vifaa vya injini ya maji (turbines) vya mtambo wa nguvu za umeme na mchanga, kwa kuhakikisha mchanga unaondolewa katika mtiririko unaopelekwa kwenye injini ya maji.

6.3.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Masuala ya Manunuzi

Ninatambua jitihada zilizofanywa na TANESCO kupitia kwa Mhandisi Mshauri wake (TECU) katika kuhakikisha mkandarasi anafuata matakwa ya mkataba kwa kutumia zaidi vifaa vya ujenzi vinavyozalishwa hapa nchini katika ujenzi wa mradi. Baadhi ya vifaa hivyo vya ujenzi ni kama vile saruji, nondo, mabati na kadhalika. Hata hivyo, nilibaini mapungufu yanayohusu manunuzi kama ifuatavyo:-

a) TANESCO hawakufuata Matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 katika manunuzi ya Mwakilishi wa Mwajiri

Nilibaini kuwa, TANESCO hawakufuata taratibu za manunuzi ya Umma kama zinavyoelezwa katika kifungu cha 78(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni ya 253 ya Sheria

ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013, na marekebisho yake ya mwaka 2016, ambapo kwa pamoja vinaeleza namna ya kumpata mhandisi mshauri wa mradi (Mwakilishi wa Mwajiri). Hii ilithibitishwa na kukosekana kwa nyaraka[13] zote za manunuzi katika mchakato wa kumpata mhandisi mshauri ambazo zilipaswa kuwepo kama utaratibu ungefuatwa. Hii ilikuwa ni kinyume na kifungu cha 61(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 ambacho kinataka nyaraka zote za manunuzi kuhifadhiwa kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (5) tangu tarehe ambayo mkataba wa manunuzi ulimalizika. Pia, nyaraka hizo ziwasilishwe ikiwa zitahitajika kwa Waziri wa Fedha na Mipango au Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kukosekana kwa nyaraka hizo za manunuzi hakutoi uhakika kama TANESCO ilifuata taratibu za manunuzi katika mchakato wa kumpata mhandisi mshauri wa mradi kwa mujibu wa sheria ya manunuzi ya umma.

Hii inamaanisha kuwa hakuna nyaraka yoyote ile inayoonesha mchakato wa manunuzi ambao ulipelekea kupatikana kwa TECU kuwa mwakilishi wa TANESCO katika mradi huu.

b) TANESCO Haikuomba Idhini ya Bodi ya Zabuni Kabla ya Kuingia Makubaliano na "TANROADS Engineering Consulting Unit (TECU)" kuwa Mhandisi Mshauri (Mwakilishi wa Mwajiri)

Kifungu cha 35(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 kinasema kuwa "hakuna mtu yeyote au kampuni itakayosaini mkataba na taasisi ya umma, mpaka makubaliano hayo yatakapoidhinishwa na bodi ya zabuni ya Taasisi ya Umma husika".

Maofisa wa TANESCO walibainisha kuwa, TANESCO hawakuomba idhini ya bodi ya zabuni yao kabla ya makubaliano na TANROAD Engineering Consulting Unit (TECU) kutoa huduma ya kiushauri katika kazi ya ujenzi wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP). Hii ilibainishwa na ukweli kuwa TANESCO hawakuweza

[13] Mpango wa manunuzi, hati ya maombi ya kununua (Fomu na. 2), muhtasari wa kikao kilichopitisha njia ya manunuzi, muhtasari wa kikao cha kufungua zabuni za mapendekezo, ombi la Pendekezo ("Request For Proposal"), barua ya uteuzi wa kamati ya tathmini, ripoti ya tathmini ya mapendekezo, mapendekezo ya pendekezo lililoshinda, mpango wa majadiliano na mshindi, muhtasari wa kikao cha kabla ya majadiliano, na timu ya majadiliano na nyinginezo.

kuwasilisha nyaraka zilizohusika katika mchakato huo kama vile mihutasari ya vikao vya bodi ya zabuni vilivyoidhinisha njia ya manunuzi iliyotumika, hadidu za rejea, ombi la mapendekezo ya zabuni na ripoti ya tathmini. Kukosekana kwa idhini ya bodi ya zabuni kunafanya makubaliano hayo kuwa batili kwa mujibu wa kifungu cha 35 (3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011.

TANESCO iliingia makubaliano ya hiari badala ya mkataba na TECU kupitia kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) katika manunuzi yenye kiasi cha Sh. 8,910,704,500. Hii ni kinyume na kifungu cha 60(7) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 ambacho kinataka wakati ambapo taasisi ya umma imefikia muafaka wa makubaliano na mkandarasi, muuzaji au mtoa huduma yeyote ni lazima mkataba rasmi usainiwe baina ya pande mbili na kazi/huduma ifanyike kwa mujibu wa makubaliano hayo.

Nilibaini kuwa, TANESCO waliingia makubaliano ya hiari na TECU badala ya mkataba rasmi. Makubaliano hayo yalikuwa hayaziwajibishi kisheria pande zote mbili. Pia ilibainika kuwa tarehe 17 Aprili 2019 TANESCO ilisaini makubaliano ya hiari na Wakala wa Barabara kwa ajili ya huduma ya ushauri katika ujenzi wa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Julius Nyerere kwa thamani ya Sh. 8,910,704,500. Thamani hii inajumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani, kinyume na matakwa ya sheria ya manunuzi ya umma.

Makubaliano ya hiari (MoU) kati ya TANESCO na TECU kupitia TANROADS siyo mkataba kwa sababu hayalazimishi pande mbili kutekeleza majukumu yao kisheria, kinyume na kipengele cha 3.1 cha Masharti ya jumla ya mkataba (GCC) isipokuwa kwa kuendana na Kipengele cha 15 cha Masharti ya jumla ya mkataba (GCC). Kwa kuwa makubaliano ya hiari hayafungi kisheria, mhandisi mshauri na mwajiri wake hawalazimishwi kisheria kufanya au kutofanya majukumu yao. Hii inahatarisha kutokuwapo kwa uwajibikaji na majukumu wakati wa utekelezaji wa mradi.

c) **Makubaliano ya Hiari Baina ya TANESCO na TECU Hayakulazimisha Uwajibikaji wa Kitaalamu Baina ya Pande Hizo**

Pia nilibaini kuwa kifungu cha 7 cha makubaliano ya hiari baina ya TANESCO na TECU kinaeleza kuwa hakutakuwa na kuwajibika kwa aina yoyote ikiwa kuna dai linatokea katika mkataba, fidia, kufanya kosa (ikiwamo uzembe), dhima kubwa, au vinginevyo. Hakuna atakayewajibika kwa mwingine chini ya makubaliano ya hiari (MoU) kufuatia hasara, upotevu wa mapato, upotevu wa uzalishaji, au uharibifu wowote.

Kwa kuzingatia kifungu tajwa hapo juu uwajibikaji wa kitaalamu kwa mhandisi mshauri haukuwepo. Hivyo basi, madhara yanayoweza kujitokeza kwa pande mbili za makubaliano ya hiairi hayawezi kuzuilika.

d) **TANESCO Hawakuhakikisha Kuwa Sehemu Kuu za Mradi Zinatekelezwa na Mkandarasi Mkuu**

Kifungu cha 4.4 cha Masharti ya jumla ya mkataba (GCC), kinamtaka mkandarasi awe na uwezo wa kutekeleza sehemu kubwa ya mradi; na asitoe kazi zote za mradi kwa wakandarasi wasaidizi. Pia, kazi atakazogawa kwa wakandarasi wasaidizi zisizidi 50% ya thamani ya mkataba wa kazi yote kwa ujumla.

Katika kupitia ripoti ya utekelezaji wa mradi ya mwezi Desemba 2020, ilibainika kuwa jumla ya wakandarasi 21 na Wahandisi washauri 9 walikuwa wamepewa kazi katika maeneo muhimu ya mradi.

Hata hivyo, mahojiano na maafisa wa TANESCO na TECU yalionesha kuwa, mkandarasi mkuu hakuwa tayari kuweka wazi taarifa za malipo aliyoyafanya kwa kazi zinazotekelezwa na wakandarasi wasaidizi. Juhudi zilifanyika kuhakikisha taarifa hizo zinapatikana. Nilibaini kuwa, Mkandarasi mkuu aliandika barua[14] kwa TECU kuwajulisha kuwa hadi kufikia tarehe 24 Julai 2020, jumla ya kazi walizopewa wakandarasi wasaidizi zilikuwa na thamani ya 36.7% ya gharama ya mkataba, ambayo ilikuwa ndani

[14] Barua yenye kumbukumbu Na. 7000-JVP-TEC-NLT-000641 ya tarehe 24 Julai 2020

ya ukomo wa 50% wa gharama ya mkataba, kwa mujibu wa kifungu cha 4.4 cha maelekezo maalumu ya mkataba. Pia, ilibainika kuwa wakandarasi wasaidizi waliidhinisha bila kujua thamani ya kazi waliyopewa. Hivyo basi, TANESCO hawajaweza kuhakikisha kazi muhimu zinafanywa na mkandarasi mkuu, licha ya ukweli kuwa katika mikataba ya EPC hatari kuhusu ubora wa kazi ipo kwa mkandarasi, lakini kazi nyingi muhimu kufanywa na wakandarasi wasaidizi huhatarisha ubora wa kazi hizo.

e) Kiwango cha Juu cha Gharama Iliyowekwa Katika Mkataba ili Kufidia Uharibifu Hakikuwa Sahihi

Kanuni ya 112(3) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inaeleza kuwa "kiwango cha gharama kinachowekwa katika mkataba ili kufidia uharibifu kinapaswa kuwa sawa na kiwango cha juu cha gharama kinachowekwa kama dhamana ya kuhakikisha utekelezaji wa kazi unafanyika kwa mujibu wa mkataba".

Nilibaini kuwa, kiwango cha gharama kilichowekwa katika mkataba ili kufidia uharibifu kilikuwa kinyume na Kanuni ya 112(3) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016). Kwa mujibu wa mkataba, kifungu cha 8.7 fidia ya uharibifu ilikuwa 0.1% ya gharama ya mkataba kwa siku, na ukomo wake ni 0.5% ya gharama ya mkataba. Kwa mujibu wa kifungu 4.2 cha maelekezo ya jumla ya mkataba, kiwango cha juu cha gharama kilichowekwa kama dhamana ya kuhakikisha utekelezaji wa kazi ni 10% ya gharama ya mkataba. Hivyo basi, kuna hatari ya kushindwa kufidia gharama ya hasara inayoweza kujitokeza ikiwa mradi utachelewa kukamilika.

Kuhusu suala hili, maafisa wa TANESCO na TECU walibainisha kuwa hadi kufikia 2018, mamlaka ya ununuzi wa umma Tanzania haikuwa na Muongozo wa mikataba ya EPC. Pia walibainisha kuwa kuweka kiwango kikubwa cha gharama ya kufidia uharibifu katika mkataba kunaweza kuongeza gharama za mradi. Maofisa pia walionesha mtazamo wao kuwa katika mikataba ya EPC hatari ya utekelezaji wa mradi ipo kwa mkandarasi; hivyo kiwango cha kufidia uharibifu hakina madhara yoyote kwenye utekelezaji wa mradi.

Ili kuboresha kufuata taratibu za manunuzi na michakato ya mikataba, nashauri manejimenti ya Shirika la Usambazaji Umeme Tanzania (TANESCO):

(a) Kuingia mkataba rasmi na TECU kwa utoaji wa huduma za ushauri (Mwakilishi wa Mwajiri) kwa muundo, kupitia usimamizi wa ujenzi na usimamizi wakati wa ujenzi, upimaji na wajibu katika mradi na usimamizi wa shughuli katika kipindi cha matazamio cha mradi ili kuzingatia ufuatiliaji wa mahitaji ya Sheria ya Manunuzi ya Umma na kuepuka hatari zinazoweza kutokea kwa kukosa makubaliano rasmi; na

(b) Kusahihisha mapungufu yaliyobainika kwa kuandaa na kusaini makubaliano ya nyongeza ili kiwango cha juu cha tozo kwa ucheleweshaji wa mradi kiwe 10% ya bei ya mkataba kulingana na matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016).

6.3.3 Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Mkataba

a) Hadi Kufikia Desemba 2020, Shughuli za Mradi Zilikuwa Zimechelewa kwa Miezi Sita

Licha ya kwamba Mwakilishi wa Mwajiri (TECU) alikuwa na mifumo madhubuti ya kuweza kusimamia muda wa mradi, hakuweza kutosha kusimamia vya kutosha uekelezaji wa shughuli za mradi ndani ya muda uliopangwa. Mpaka tarehe 31 Desemba 2020 maendeleo ya utekelezaji wa mradi yalikuwa ni asilimia 28.61 ikilinganishwa na asilimia 46.93 ya mpango au programu ya awali ya utekelezaji wa mkataba. Kwa ujumla, shughuli za mradi zilikuwa zimechelewa kwa asilimia 18.32 ambayo ni sawa na siku 200 (miezi 6.7) kwenye jumla ya siku 1,095 za ujenzi wa mradi. Hii ni kinyume na kifungu cha 8.6 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC). Kifungu hiki kinatoa masharti ya ujumla kwamba kwa muda wote: (a) kasi ya kumaliza mradi ndani ya muda ikiwa ndogo sana, (b) ikiwa maendeleo ya utekelezaji wa mradi yatakuwa nyuma ya mpango wa utekelezaji uliopo, Mwajiri anatakiwa kumtaarifu Mkandarasi kupitia upya njia/mbinu za utekelezaji alizokwisha kupendekeza na kushauri jinsi gani ataweza kufikia malengo ya kufidia muda alioupoteza na kukamilisha mradi ndani ya muda wa utekelezaji uliopangwa.

Ucheleweshaji wa mradi ulichangiwa na kuchelewa kuanza kwa baadhi ya shughuli au kazi muhimu (kazi changizi) kama; mkondo wa kuchepushia maji ya mto Rufiji, mikondo ya njia za maji ya kuzalisha umeme, nyumba ya kuzalishia umeme, kingo za kuzuia maji na kingo kuu ya bwawa. Kuchelewa kuanza kwa shughuli hizi ilikuwa kuanzia siku 42 hadi siku 514 ikilinganishwa na mpango wa utekelezaji wa awali kama inavyoonekana kwenye **kielelezo Na. 6-1** hapa chini.



Kielelezo Na. 6. 1: Kiwango cha ucheleweshwaji wa kuanza kwa kazi za ujenzi katika shughuli kuu za ujenzi wa Mradi.

Kielelezo Na. 6-1 hapo juu kinaonyesha kazi zilizochelewa kuanza kwa ujenzi katika shughuli tano za ujenzi. Shughuli hizo zinajumuisha: tuta kubwa la bwawa, njia za maji (mahandaki) kwa ajili ya uzalishaji umeme, matuta mkingamo manne kwa ajili ya kuzuia maji yasitoroke na nyumba ya kuzalishia umeme. Ucheleweshaji mkubwa wa kuanza kazi ulionekana kwa upande wa tuta kuu la bwawa na njia za maji (handaki) kwa ajili ya uzalishaji umeme ambayo yalichelewa kwa takribani siku 110.

Sababu nyingine zilizochangia ucheleweshaji wa kuanza kwa kazi za ujenzi wa mradi ni: TANESCO kuchelewa kuanza matengenezo ya barabara za kuingia na kutoka kwenye mradi kwa kiwango cha changarawe ambazo zingechangia mradi kuanza mapema, pamoja na mabadiliko ya kiwango cha uzalishaji wa umeme yaliyofanywa kutoka Megawati 2100 kwenda Megawati 2115. Mabadiliko haya yalisababisha kuchelewa kuanza kwa uchoraji na usanifu wa michoro kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa kwa zaidi ya miezi 15.

b) Kuchelewa Kuanza Utekelezaji wa Miradi Shirikishi ya Uwajibikaji wa Kijamii (CSR)

Nilibaini kuwa TANESCO ilisaini makubaliano na Mkandarasi kutekeleza miradi ya kijamii katika sekta ya afya na elimu kwa gharama ya 4% ya gharama zote za mradi wa Bwawa la uzalishaji umeme. Hata hivyo, utekelezaji wa miradi hiyo ulikuwa haujaanza mpaka muda wa ukaguzi huu. Sababu zilizochangia kuchelewa kuanza mapema kwa utekelezaji wa miradi hii ni pamoja na: kutowasilishwa kwa wakati makubaliano ya kina kwa muda wa miezi 14, kuchelewa kwa Mkandarasi kutoa maoni kwenye makubaliano ya kina kwa muda wa miezi saba (7). Sababu nyingine ilikuwa ni pamoja na muda wa uandaaji wa makubaliano ya kina na pamoja na kupendekeza miradi uliokadiriwa wa mwezi mmoja haukuwa na uhalisi wa kutosheleza kutekeleza hayo.

Ucheleweshaji pia ulisababishwa na madai ya Mkandarasi kuwa miradi iliyopendekezwa haikushabihiana na makubaliano kuwa miongoni mwa sekta ya elimu na ya afya. Mkandarasi alifikiri kuwa, miradi iliyochaguliwa ya ujenzi wa barabara na uwanja wa michezo haikuangukia katika sekta ya afya na elimu. Miradi iliyochaguliwa ilikuwa ni ujenzi wa kilometa 35 za barabara ya kutoka Fuga stesheni (Kituo cha gari moshi) hadi Stigo (eneo la mradi wa Bwawa la umeme) na Ujenzi wa uwanja wa michezo wa Dodoma. Kuchelewa kuanza kwa miradi hii kumesababisha jamii kuchelewa kunufaika na miradi hii.

c) Mwakilishi wa Mwajiri Hakuwa na Mfumo Madhubuti Unaotosheleza kwa Ajili ya Usimamizi wa Ubora wa Kazi za Mradi Zinazotekelezwa

Nilibaini kuwa Mwakilishi wa Mwajiri hakuwa na mfumo wa uthibiti na usimamizi wa ubora unaojitosheleza ili kuweza kusimamia na kujihakikishia ubora wa kazi za mradi zinazoendelea. Ilibainika kuwa Mwakilishi wa Mwajiri hakuhakikisha kuwa Mkandarasi anaandaa na kuwasilisha mpango wa kuhakiki na kusimamia ubora wa kazi zinazofanyika katika mradi. Hii ilikuwa ni kinyume na kifungu kidogo cha 4.9 cha Masharti ya Ujumla ya Mkataba (GCC). Mpaka Desemba 2020 Mkandarasi alikuwa hajawasilisha mpango wa uhakiki na uthibiti ubora pamoja na kiwanda cha majaribio ya vipimo katika eneo la ujenzi kwa Mwakilishi wa Mwajiri anayesimamia mradi (TECU) kama ilivyoainishwa katika sehemu ya 11 ya Matakwa ya Mwajiri. Kutokuwepo kwa mfumo na mpango huu kunaleta mashaka au kunaondoa kabisa uhakika wa kuwa Mkandarasi atazingatia vigezo vyote vya ubora wa kazi anazofanya.

Vilevile, nilibaini kwamba TANESCO hawakujenga maabara ya kujitegemea kwa ajili ya Mwakilishi wa Mwajiri (TECU) katika eneo la mradi. Hivyo basi, Mwakilishi wa Mwajiri alikuwa akitumia maabara ya Mkandarasi. Hii ni kinyume na Kifungu cha 4 cha Makubaliano ya Hiari (MOU) kati ya TECU na TANESCO kinachotaka TANESCO kujenga maabara yenye vifaa kamili kwa ajili ya kupima na kukagua ubora wa kazi za mradi zinazofanywa na Mkandarasi zinazoendelea na kukamilika. Shabaha ya hili ni kuhakikisha kwamba Mwakilishi wa Mwajiri anatimiza wajibu wake kama ilivyoelezewa katika Sehemu ya 2.2.2.5 (v) ya nyongeza ya MoU iliyotiwa saini tarehe 30 Agosti 2019. Sehemu hii inamtaka TECU kudhibiti ubora na taratibu za upimaji bora zilizofanyika katika muda wote wa ujenzi ili kuthibitisha vigezo vya ubora, taarifa za njia na viwango vya vifaa vilivyotumika katika miundo na shughuli zote za mradi na utoaji wa Hati za Kukubali ubora wa kazi iliyokamilika.

Katika kujibu hili, Maafisa wa TANESCO na TECU waliohojiwa walieleza kuwa wanategemea maabara ya Mkandarasi, ingawa wanapokuwa na shaka na matokeo ya vipimo vya ubora wa vifaa vilivyotumika katika vipimo husika, hutuma vifaa au bidhaa kwenda kupimwa katika maabara ya nje ya mradi zinazoaminika. Zaidi, walithibitisha kuwa huwa wanafanya ukaguzi wa pamoja na Mkandarasi wa kila siku kukiwa na kazi ya ujenzi inayoendelea.

Maelezo haya yanakinzana na ufanisi wa udhibiti wa ubora kama inavyohitajika katika Matakwa ya Mwajiri.

d) TANESCO Kufanya Malipo kwa Mkandarasi kwa Wakati

Nilibaini kuwa TANESCO iliweza kumlipa Mkandarasi kwa wakati kama ilivyoainishwa katika mkataba. Kati ya maombi ya malipo 14, TANESCO ilichukua muda wa siku 44 kukamilisha malipo kati ya siku 56 zilizoainishwa katika mkataba uliosainiwa kati ya TANESCO na Mkandarasi M/S Arab Contractors na kutoka Misri kwa ushirikiano na Mkandarasi M/S Elsewedy Electric (S.A.E). TECU ilibainika kufanya vizuri katika kudhibiti gharama kwa kupitia, kukagua maombi ya malipo ndani ya muda (IPC) hadi idadi ya hati 14 zilizoombwa hadi Desemba 2020. Kwa kuongezea, TECU ilionesha utendaji mzuri katika kujibu madai yaliyotolewa hadi sasa na Mkandarasi na hivyo kudhibiti gharama za mradi.

Hata hivyo, TANESCO inahitaji kuongeza juhudi zaidi katika kujibu kwa wakati madai ambayo yameonesha kuwa na viashiria vya hatari ya kuweza kuongeza gharama ya mradi. Kwa kuongezea, niligundua kuwa ushuru au kodi ya zuio imelipwa kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru au Kodi ya Mapato na ongezeko la thamani ya mwaka 2019 na imewasilishwa kwa Mamlaka inayohusika (TRA) kwa wakati unaofaa. Hii ni kwa sababu TANESCO imeweza kukata na kutoa kodi ya zuio kwa TRA kulingana na masharti ya mkataba.

e) TANESCO Ilichelewesha Malipo ya Ada ya Mwakilishi wa Mwajiri Kinyume na Makubaliano (MoU)

Kifungu cha 3 (5) fungu la 2 la Marekebisho ya Kwanza ya Makubaliano kati ya TANESCO na Mwaklishi wa Mwajiri kuhusu ada na malipo kinaonesha kwamba Mwajiri (TANESCO) atalipa katika Akaunti ya Benki ya Mwakilishi wa Waajiri (TECU) malipo yake katika ankara hizo ndani ya siku thelathini (30) baada ya kupokea maombi kutoka kwa Mwakilishi wa Mwajiri.

Ripoti za malipo ya ushauri zilizopitiwa zilionesha ucheleweshaji wa malipo yaliyotolewa kwa Mwakilishi wa Mwajiri kwa kipindi kinachoanzia siku 1 hadi 130, licha ya ankara hizo kuwasilishwa kwa wakati kila mwezi. Ankara 15 za jumla ya Sh. 1,932,247,487 zilikuwa bado hazijalipwa hadi Januari 2021.

Hali hii, kwa kiasi kikubwa, ilitokana na kuchelewa kutolewa kwa fedha kutoka Wizara ya Nishati kwenda TANESCO kuwezesha malipo ya Mwakilishi wa Mwajiri. Fedha zilizotolewa kutoka Wizarani zilichelewa kwa zaidi ya Miezi 6. Matokeo yake, TANESCO ililazimika kutumia fedha kutoka katika vyanzo vyake vingine vya ndani kulipia ada ya Ushauri kwa Mwakilishi wa Mwajiri. Kwa mfano, tarehe 21 Novemba 2019 kupitia Hati za Malipo ya Nambari 4602697, TANESCO ililipa Sh. 549,759,584.00 kwa TECU kupitia chanzo chake; na vivyo hiyo ilirudishwa kwa TANESCO Januari na Juni 2020. Pia, Julai 2020 TANESCO ililipa ada ya ushauri kwa Mshauri wa mradi (TECU) kiasi cha Sh. 650,000,000 kupitia ankara zenye hati namba 10 - 16 (Februari hadi Agosti 2020). Hata hivyo, hiyo haijarejeshwa kwa TANESCO hadi Januari 2021.

Kwa hivyo, ucheleweshaji wa malipo yaliyotolewa kwa Mshauri anaweza kuharibu sifa ya Shirika, na unaweza kusababisha ucheleweshaji wa utekelezaji.

Ili kuboresha usimamizi wa mikataba, nashauri manejimenti ya Shirika la Usambazaji Umeme Tanzania (TANESCO):

(a) Kuhakikisha hatua za kuchukua zinaandaliwa na kusimamia utekelezaji wake ili kuharakisha utekelezaji au kufidia muda uliopotea na kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati uliopangwa;

(b) Kuhakikisha Mfumo wa kuhakiki Ubora na Mpango wa Kudhibiti Ubora wa Mradi unaandaliwa na utekelezaji wake unasimamiwa kama matakwa ya Mwajiri yanavyotaka pamoja na Masharti ya jumla ya Mkataba;

(c) Kuhakikisha kwamba Mwakilishi wa Mwajiri anaanzisha eneo la maabara huru katika eneo la mradi; na

(d) Makubaliano ya Uwajibikaji katika Jamii (CSR) yanasainiwa ili kuruhusu kuanza mara moja utekelezaji wa miradi ya kijamii. Katika siku zijazo kwa miradi inayofanana kutenga muda halisi ambao unazingatia muda unaohitajika kwa ajili ya utambuzi wa miradi ya Uwajibikaji katika Jamii na uandaaji wa makubaliano.

6.3.4 Matokeo Kuhusu Usimamizi wa Rasilimaliwatu

Nilibaini kuwa, Mwakilishi wa Mwajiri (Mshauri Msimamizi wa Mradi) alizingatia kifungu kidogo cha 6.1 cha Matakwa Maalumu ya Mkataba kinachosisitiza kwamba Mkandarasi kwa namna inavyowezekana kwa kiasi kikubwa kutumia wafanyakazi wenye ujuzi, uzoefu na sifa zinazohitajika kutoka Tanzania. Zaidi, mchakato wa ajira unapaswa kufanyika kwa kuzingatia matakwa ya sheria za nchi ya Tanzania. Nilibaini kwamba, hadi kufikia mwezi Desemba 2020 kulikuwa na raia wa Tanzania 5,361 walioajiriwa kwenye mradi kati ya jumla ya wafanyakazi 6,130 wa mkandarasi. Hii inamaanisha kwamba asilimia 87.5 (87.5%) ya wafanyakazi wa mkandarasi walikuwa raia wa Tanzania.

Licha ya mafanikio hayo, nilibaini mapungufu kama yalivyoainishwa hapa chini:

a) Asilima 87 ya Wataalamu Wabobezi wa Mkandarasi Hawakusajiliwa na Bodi Husika za Kitaaluma

Kanuni ya 118(4) ya tangazo la Gazeti la Serikali namba 446 ya 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) inamtaka mzabuni wa kigeni kabla hajasaini mkataba awe amesajiliwa au kuleta ushaidi wa ustahiki wa kusajiliwa na bodi ya kitaaluma iliyowekwa kisheria.

Katika kupitia taarifa za Usimamizi wa Rasilimali Watu kutoka kwa Mkandarasi iligundulika kuwa, wafanyakazi wabobezi 167 kati ya 209 (sawa na 87%) waliokuwepo sehemu ya mradi (wazawa na wageni) hawakusajiliwa na Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB) pamoja na Bodi ya Usajili ya Wasanifu na Wakadiriaji Ujenzi (AQRB). Wafanyakazi 97 ambao hawakusajiliwa (sawa na 58%) walikuwa wafanyakazi wa kigeni na waliobaki 70 ni wafanyakazi wazawa.

Hii ni kinyume na kifungu kidogo namba 13(1) cha Sheria ya Bodi ya Usajili ya Wasanifu na Wakadiriaji Ujenzi (AQRB) ya mwaka 2010 ambayo inamtaka msanifu na mkadiriaji majengo kutokufanya kazi kama msanifu na mkadiriaji majengo isipokuwa akiwa amesajiliwa katika sheria hii na kifungu 14(1) cha Sheria ya Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB) ya mwaka 1997 kinaeleza kuwa

hakuna mtu atakayeajiri au ataendelea kuajiri mtaalamu mhandisi ambaye hajasajiliwa na Bodi ya Waandisi.

Katika kujibu hili, Mwakilishi wa Mwajiri alikiri kwamba kushindwa kusajiliwa kwa baadhi ya wataalamu bobezi kwenye bodi za kitaaluma kulichangiwa na mchakato wa usajili kuwa mrefu na muda uliopangwa na bodi husika. Maafisa kutoka Mwakilishi wa Mwajiri (TECU) wameonesha kwamba inachukua muda wa miaka miwili hadi mitatu kupata usajili wa bodi husika. Hii inahusisha muda wa kupata kibali cha kazi, ikifuatiwa na ithibati ya cheti toka TCU, kisha usajili wa bodi husika, hata hivyo wengi bado wanasubiri vibali vitolewe.

Usimamizi usiotosheleza wa utekelezaji wa masharti na vigezo vya kusajiliwa na bodi husika za kitaaluma ni moja ya sababu kubwa ya kutosajiliwa kwa idadi kubwa ya wafanyakazi wabobezi wa Mkandarasi. Matokeo yake, wafanyakazi wote wabobezi wanafanya kazi zao za kitaaluma bila kuzingatia takwa la kisheria. Hii ilipelekea kukosa mapato kwa makadirio ya Sh. 3,580,000 na Dola za Marekeni 107,000 ambazo zingeweza kukusanywa kama ada ya usajili.

b) Nafasi 21 kati ya Nafasi za Chini 56 za Timu ya Usanifu na ya Utekelezaji ya Mkandarasi Zilijazwa na Wafanyakazi wa Kigeni

Kifungu kidogo cha 6.1 cha Masharti Maalum ya Mkataba kinasema kwamba, mfanyakazi yeyote asiyekuwa na ujuzi wa juu akihitajika na Mkandarasi ni lazima atoke ndani ya nchi kupitia Mawakala wa Kazi na Ajira kwa kuzingatia sheria za Tanzania. Kinyume chake, nilibaini kwamba, wafanyakazi wa kigeni 21 kati ya 56 waliajiriwa katika nafasi za utaalamu wa wapima vifaa (Materail Test), wapima ardhi, mafundi mchundo wa maabara, mafundi mchundo wa mpimaji, mkadiriaji ujenzi, mhandisi ujenzi na mhandisi miundo mbinu, nafasi ambazo zingeweza kujazwa na watanzania. Wataalam kutoka kwa Mwakilishi wa Mwajiri (TECU) walibainisha kwamba, iliwalazimu kuhusisha wafanyakazi wa kigeni mwanzoni mwa utekelezaji wa mradi kwa ajili ya kutoa mafunzo ya mitambo na vifaa vyenye kutumia teknolojia ya hali ya juu pamoja na kuwapa elimu wafanyakazi Watanzania.

Hakukuwa na uthibitisho wa kutosha kwa nafasi iliyojazwa ambayo isingeweza kupatikana ndani ya nchi. Hii ilitokana na ukweli kwamba kuna idadi ya vyuo na vyuo vikuu nchini vinavyotoa wahitimu wenye ujuzi na taaluma sawa na mahitaji ya nafasi hizo.

Sababu kubwa zilizochangia nafasi hizi kujazwa na wageni ilikuwa ni pamoja na uratibu duni kati ya Taasisi za Kiserikali na uhakiki duni wa vibali vya kazi. Pamoja na hayo, mkandarasi alikuwa anatoa matangazo ya kazi kupitia tovuti ya "Zoomtanzania" na 'Bright Monday' ambapo matangazo hayo yalikuwa hayawafikii Watanzania. Hii, kwa kiasi kikubwa, iliwapa ugumu raia wengi na kushindwa kuomba nafasi hizo.

c) Kutokulipa Fidia kwa Wategemezi wa Wafanyakazi Waliofariki Mahali pa Kazi

Zaidi nilibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Desemba 2020, kulikuwa na idadi ya vifo vitatu vilivyotokea mahala pa kazi. Hata hivyo, hapakuwa na fidia iliyotolewa kwa wategemezi wa wafanyakazi waliofariki kulingana na matakwa ya kimkataba na Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi. Kifungu kidogo cha 19(1) cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 2008 na kifungu kidogo 18.3 (b) cha Masharti Maalum ya Mkataba (PCC) vimeainisha kiasi cha fidia kuwa kisiwe chini ya Dola za Marekani 100,000 kwa kifo cha mtu yeyote katika mradi. Hivyo basi, Mwakilishi wa Mwajiri hakuwa na ushahidi kama Mkandarasi aliweza kulipa fidia kwa wategemezi wa wafanyakazi waliofariki kama inavyotakiwa na vifungu vilivyonukuliwa hapo juu.

Sababu iliyotolewa kwa kutokulipwa kwa fidia kwa wategemezi watatu wa wafanyakazi waliokufa ni pamoja na kuchelewa kwa malipo ya Bima zote za hatari za Mkandarasi (CAR) za Shirika la Taifa la Bima. Bima hizi hutumika kufidia wategemezi wa waajiriwa waliokufa. Sababu nyingine ni ufuatiliaji duni wa Mwakilishi wa Mwajiri kuhakikisha Shirika la Bima (NIC) linalipa kwa wakati.

d) Asilimiia 51 ya Wafanyakazi Muhimu wa Mkandarasi Hawakuwa na Vibali Halali Vya Kazi

Kanuni ndogo namba 10(1) ya Kanuni ya Ajira kwa Wafanyakazi Wasio Raia wa Tanzania inasema kwamba, “Mtu yoyote anayetaka kuhusisha au kuajiri mfanyakazi wa kigeni katika ajira anatakiwa kuomba kibali kutoka kwa Kamishna wa Kazi kabla ya Mfanyakazi huyo wa kutoka nchi za kigeni kuingia nchini.” Zaidi, kanuni ndogo namba 10(2) inataka maombi ya kibali yaambatane na malipo ya ada kama ilivyoelezewa kwenye Jedwali la sita ya sheria ya wafanyakazi wasio raia.

Mapitio ya Taarifa za Rasilimali watu zilizotolewa kwa ajili ya ukaguzi na Mwakilishi wa Mwajiri yalionesha kwamba, wafanyakazi muhimu (bobezi) wa kigeni wa Wakandarasi 46 kati ya 91 ambao ni sawa na 51% walikuwa wanatumia visa ya biashara badala ya kibali cha kazi kama inavyotakiwa na Kanuni ndogo namba 10 (1) ya Kanuni za Ajira kwa Wafanyakazi wa Kigeni ya mwaka 2015. Mchanganuo wa idadi ya wafanyakazi wa kigeni wa Wakandarasi waliokosa kibali cha kisheria/halali cha kufanya kazi nchini ni kama ulivyooneshwa katika **Jedwali Na. Na 6-1.**

Jedwali 6- 1: Muhtasari wa Wafanyakazi wa Kigeni wa Mkandarasi waliokosa Vibali vya Kisheria/Halali vya Kufanya kazi Nchini

Timu za utekelezaji kwa kila Shughuli ya Mradi	Idadi ya wafanyakazi waliokuwepo kwenye Mradi mpaka mwezi Desemba 2020	Idadi ya wafanyakazi waliokosa vibali vya kazi kisheria	Asilimia ya wafanyakazi waliokosa kibali cha kazi	Makadirio ya upotevu wa mapato ya Dola za Marekani 550 kwa kila mtu mmoja
Timu ya usanifu ya Mkandarasi	16	7	44	**3,850**
Timu ya utekelezaji (Ujenzi) wa mradi ya mkandarasi	75	39	52	**21,450**
Jumla	91	46	51	**25,300**

Chanzo cha Taarifa: *Uchambuzi wa Wakaguzi wa taarifa za usimamizi wa Rasilimali watu ya Mradi (Desemba 2020)*

Kutokuwepo kwa utaratibu wa kuhakikisha kuwa kibali cha kufanya kazi kinashughulikiwa kabla ya kuwasili kwa raia wa kigeni kushiriki katika mradi huo ni kinyume na matakwa ya Kanuni ya 10 (2), ambayo inataka ushughulikiaji wa kibali ufanyike kabla ya kuwasili kwa wafanyakazi wanaotarajiwa. Kuchelewa kuomba vibali vya kufanya kazi kwa watu wengi wasio raia wanapendelea kuanza kushughulikia

vibali vyao vya kazi baada ya kuhakikishiwa / kuwa na uhakika kuwa watahusika katika mradi.

Zifuatazo ni sababu kubwa zilizotolewa na Mwakilishi wa Mwajiri za kushindwa kutafuatilia vibali vya kazi kwa 51% ya wafanyakazi wa kigeni wa Mkandarasi:

(a) Ukosefu wa utaratibu wa kuhakikisha kwamba vibali vya kazi vinashughulikiwa kabla ya wafanyakazi wa kigeni wanaotegemewa kufanya kazi katika Mradi kuwasili nchini kulingana na matakwa ya kanuni namba 10(2) ambayo inataka kibali kishughulikiwe kabla ya kuwasili kwa mfanyakazi wa kigeni anayetarajiwa kushiriki ujenzi kwenye mradi;

(b) Raia wengi wa kigeni kuchelewa kuomba vibali vya kazi kwa kuwa hawapendi kuanza kufuatilia kibali mpaka wapate uhakika au kuhakikishiwa kipindi ambacho watashiriki katika mradi huo; na

(c) Ukosefu wa uratibu na ushirikiano mzuri kati ya Mwakilishi wa Mwajiri na Taasisi za Serikali zinazohusika na kutoa idhini na vibali vya wafanyakazi wa kigeni kufanya kazi nchini.

Nilibaini kuwa Serikali inaingia kwenye hatari ya kukosa mapato kutokana na kutokulipwa kwa malipo yaliyoamriwa ya kuomba kibali cha kazi yenye thamani ya fedha za kigeni Dola za Marekani 500 kwa kila mfanyakazi mmoja wa kigeni mwenye taaluma maalum na fedha za kigeni Dola za Marekani 1,000 kwa kila mfanyakazi wa kigeni kwa taaluma zingine. Kwa ujumla, kwa makadirio serikali ilikosa jumla ya fedha za kigeni Dola za Marekani 25,300 kama mapato ambayo yangetokana na maombi vibali vya kazi.

e) Ufuatiliaji Usiotosheleza Katika Kukahikisha Mkandarasi anatimiza Masharti ya Mkataba Kuhusu Uwasilishaji wa Mishahara ya Wafanyakazi wa Mkandarasi

Kifungu cha 6 (e) cha Masharti Maalum ya Mkataba wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi kimeainisha kwamba, Mkandarasi, wakati wa hatua za mwanzo za shughuli, atawasilisha, kulingana na mpango wa utekelezaji, nyaraka zinazohusiana na upangaji wa kazi kulingana na idadi ya mikataba kati yao na nguvukazi inayopendekezwa pamoja na mshahara wa msingi inaotarajiwa kulipwa kwa kila mfanyakazi, kila kada na aina ya kazi.

Ushahidi uliopatikana kwenye mapitio ya majibizano ya barua na kazi za kila siku kati ya Mwakilishi wa Mwajiri na Mkandarasi yenye kumbukumbu nambari TECU//AC-EE-JV/783 ya tarehe 4/11/2020; ilionesha kwamba TECU hakuhakikisha kwamba Mkandarasi anakidhi Matakwa ya kifungu cha 6 cha Masharti Maalum ya Mkataba kwa kuwasilisha mishahara inayolipwa kwa kila aina ya mfanyakazi na kada yake au utaalamu wake (mfano fundi mchundo, Waendesha mitambo na wahandisi), haswa kwa wafanyakazi wa kigeni wanaoshiriki kwenye mradi. Maafisa kutoka TANESCO walieleza kwamba Mkandarasi alikuwa akidai kuwa mishahara ni miongoni mwa taarifa za siri, hivyo hakuona ulazima wa kuziwasilisha kwa Mwakilishi wa Mwajiri. Hii ilitokana na Mkandarasi kutotii Masharti ya Mkataba. Kutokana na hayo, Timu ya wakaguzi imekutana na changamoto ya kushindwa kuthibitisha endapo Mkandarasi amekidhi mahitaji ya sheria yanayohusu viwango vya malipo yanayotakiwa kulipwa kwa wafanyakazi wazawa na wafanyakazi wa kigeni.

Ili kuboresha usimamizi wa rasilimali watu nashauri manejimenti ya Shirika la Usambazaji Umeme Tanzania (TANESCO):

(a) Kushirikiana na bodi za kitaalam kuhakikisha mradi, mkandarasi, wasaidizi wa wakandarasi, washauri welekezi wasaidizi na wafanyakazi wataalam wanahusishwa katika utekelezaji wa mradi na wanasajiliwa na bodi husika za kitaalam; na

(b) Kushirikiana na taasisi zinazohusika za Serikali na kuandaa utaratibu ambao utarahisisha mchakato wa kupata kibali cha kufanya kazi ili kuhakikisha kuwa wageni wote wanaofanya kazi kwenye Mradi wana vibali sahihi vya kufanya kazi na hivyo kuiwezesha Serikali kukusanya mapato yaliyotarajiwa.

6.3.5 Matokeo ya Ukaguzi Kuhusu Bajeti na Utoshelevu wa Mfumo wa Udhibiti Fedha za Mradi

a) TANESCO Haikuwa na Taarifa za Kutosha za Bajeti Iliyotengwa kwa Ajili ya Mradi

TANESCO ilitarajiwa kuwa na taarifa za kutosha kuhusu kiasi cha bajeti iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kabla ya utekelezaji wake. Uchambuzi wetu wa bajeti ya TANESCO ya

mwaka 2017/18 hadi 2019/20 pamoja na mahojiano yaliyofanyika baina ya wakaguzi na Mratibu wa Mradi na Mhasibu ilibainika kuwa TANESCO haikuwa na taarifa za kutosha juu ya mfuko wa mradi uliotengwa kwa miaka miwili ya kwanza ya utekelezaji wa mradi. **Jedwali Na. 6-2** linawasilisha bajeti ya kila mwaka ya utekelezaji wa mradi kwa kipindi cha 2017/18 - 2020/21:

Jedwali 6- 2: Bajeti ya mradi kutoka mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2020/21(Amount in TZS/Milioni)

Mwaka wa Fedha	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Kiasi Kilichotengwa	Hakuna Taarifa	Hakuna Taafifa	1,443,264	1,440,000

Chanzo: *Bajeti ya TANESCO ya Nukuu ya Mradi Na. 3001-3172 na Nukuu ya Mradi Na 3001-3172).*

Jedwali Na. 6-2 linaonesha kuwa, kulikuwa na bajeti kwa miaka miwili ya kifedha, yaani 2019/20 na 2020/21 (Rejea bajeti ya TANESCO 2019/20 kuhusu mradi na Nukuu ya Mradi Na. 3001-3172 na Nukuu ya Mradi 3001-3172) ambapo bajeti iliyotengwa ikiwa ni Sh. 1,443,264,000,000 na Sh 1,440,000,000,000 mtawalia, na Mfadhili akiwa Serikali ya Tanzania.

Bajeti ya 2017/18 na 2018/19 haikutolewa kwa ajili ya ukaguzi. Hii ni licha ya maombi kadhaa na mahojiano yaliyofanywa na Mratibu na Mhasibu wa Mradi. Pamoja na kuwakumbusha mara kadhaa kuhusu kunipatia bajeti ya Ujenzi wa Mradi wa umeme kwa uthibitisho wa ukaguzi, sikupatiwa hadi ukaguzi ilipomalizika. Hii inamaanisha kuwa TANESCO haikuwa na ushahidi wa kuhalalisha upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi au bajeti ya Ujenzi wa JNHPP.

Ukosefu wa taarifa za kutosha kuhusu bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mradi huweza kuleta hatari ya kushindwa kuwalipa wakandarasi kwa wakati, na TANESCO inashindwa kudhibiti gharama za mradi na kuishauri Serikali juu ya utoshelevu wa bajeti, pamoja na kuchukua hatua stahiki za kudhibiti gharama.

b) Kiasi cha Malipo Kilichofanyika Kinawiana na Kiwango cha Kazi Iliyofanyika

Katika kudhibiti gharama za mradi, TANESCO kupitia TECU ilitarajiwa kuhakikisha kuwa malipo yanalingana na maendeleo ya kazi zilizotekelezwa. Nililinganisha kiwango halisi cha malipo

kilichofanywa kwa Mkandarasi dhidi ya maendeleo ya mradi uliofanywa. Matokeo ya ulinganisho yalionesha kuwa kiwango cha kazi halisi zilizokamilika ni 27.87% wakati malipo yakiwa yamefanyika kwa asilimia 25.30. Hii inamaanisha kuwa Sh. 497,793,408,143 na Dola za Marekani 516,949,764.52 (ambazo kwa jumla yake ni sawa na asilimia 25.30) zililipwa hadi kufikia Novemba 2020. Hii inamaanisha kuwa kiasi kilicholipwa kinalingana na maendeleo ya kazi zilizofanyika. Hata hivyo, Mwakilishi wa Mwajiri alikuwa hajafanya uchambuzi wa kutathmini kuwa shughuli zilizobaki za mradi zitaweza kukamilika kwa kutumia fedha zilizobaki za mradi. Badala yake, maafisa walionesha kuwa kwa sababu hawajapokea taarifa yoyote ya madai kutoka kwa Mkandarasi ambayo yanaashiria hatari zinazohusiana na gharama za mradi, hivyo basi wanaamini kuwa shughuli zilizobaki zitatimizwa katika bajeti iliyopangwa.

Hata hivyo, kwa kuwa shughuli zilizobaki zinajumuisha ununuzi wa mitambo na vifaa vya elektroniki (Mitambo ya kufua umeme (Turbine), Jenereta n.k.), TANESCO inapaswa kufanya uchambuzi zaidi kutathmini endapo fedha zilizopangwa zinaweza kukamilisha shughuli zote za mradi zilizobaki.

c) Hakuna Viashiria Hatarishi Vya Mabadiliko ya Gharama Yatokanayo na Viwango vya Kubadilisha Fedha

Nilibaini kuwapo kwa viashiria vya hatari kuhusiana mabadiliko ya bei kwa kiasi kidogo. Hii ni kwa sababu TANESCO ilikuwa imeweka masharti kuhusu mabadiliko ya bei kwenye mkataba ambayo ilichukua tahadhari ya kupunguza athari za mabadiliko ya bei. Masharti hayo yalioneshwa katika Kifungu cha 14.15 cha Masharti ya Mkataba ambayo yalibainisha kwamba bei ya mkataba inapaswa kulipwa kwa sarafu au sarafu zilizotajwa katika Masharti ya Mkataba, isipokuwa kama itatamkwa vinginevyo katika Masharti Maalum ya Mkataba, ikiwa ni zaidi ya sarafu zaidi ya moja.

Kwa kuongezea, Kifungu cha 14.15 cha Masharti ya Mwisho ya Mkataba kinasema kuwa, bei ya Kimkataba inapaswa kulipwa kwa kutumia sarafu ya ndani ambayo ni Shilingi za Tanzania asilimia 30 ya Mkataba na sarafu ya kigeni ambayo ni Dola za Marekani (asimilia 70). Nilipitia Mkataba na kubaini kuwa kiwango cha ubadilishaji kilipangwa hadi

Dola za Marekani 2,224 kwa malipo ya sehemu ya fedha za kigeni kama kilivyobainishwa kwenye mkataba, wakati kiwango cha ununuzi wa Dola ya Marekani kikiwa ni cha kuridhisha sawa na kile cha Benki Kuu ya Tanzania. Hata hivyo, nilibaini kuwa kiwango cha kununua kwa Dola ya Marekani kilikuwa juu. Kwa hivyo, mara nyingi kulikuwa na faida iliyopatikana wakati malipo yalipofanywa kwa Mkandarasi; na kwa hivyo, TANESCO walipata faida kwa sababu ya kiwango cha ubadilishaji.

d) Kutokuwapo kwa Akaunti ya Maalum ya Fedha za Mradi Katika Benk Kuu ya Tanzania (BOT)

Katika kupitia kumbukumbu za Usimamizi wa Fedha za Mradi, nilibaini kuwa TANESCO ina akaunti mbili ambazo ni akaunti za fedha za Tanzania na fedha za kigeni kwa malipo yaliyolipwa kwa Mkandarasi wa mradi. Akaunti hizi hupokea fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Wizara ya Nishati. Fedha za Kigeni (Dola za Marekani) zinatunzwa katika Benki ya kuu ya Tanzania (BOT) iliyoitwa kama akaunti ya Ruzuku ya Serikali, na hupokea na kutoa fedha zote za Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere kwa ajili ya pesa za Mkandarasi.

Akaunti nyingine ya Benki ni ya sarafu ya ndani, inayotunzwa kwa kutoa sehemu fedha za Kitanzania kwa Mkandarasi kulingana na Mkataba uliosainiwa kati ya TANESCO kwa niaba ya Serikali ya Tanzania na Mkandarasi M/S Arab Contractors.

Hata hivyo, mapitio ya usimamizi wa fedha yaligundua kuwa, akaunti iliyotunzwa kwa ajili ya Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere katika BoT inajumuisha fedha nyingine za miradi mingine mbalimbali inayosimamiwa na TANESCO. Kwa hivyo, ni vigumu kufuatilia matumizi na mchanganuo wa fedha zilizopokelewa, zilizolipwa na salio lililobaki kwa mwaka. Kwa mfano, katika ukaguzi wangu (uliofanyika Julai 2019 - Desemba 2020) nilibaini kuwa taarifa za Wahasibu wa Miradi zilionesha kuwa kulikuwa na faida ya kubadilishana na fedha za kigeni za Mradi wa Umeme wa JNHHP jumla ya Sh. 284,659,603.85 zilizopatikana katika risiti za malipo na madai ya Mkandarasi mpaka tarehe 30 Desemba 2020 ambayo ingeweza kutumika kwa ajili ya miradi mingine kwa kuwa akaunti hiyo hiyo ilitumika kwa ajili ya mradi na fedha nyingine za TANESCO.

Bila uwepo wa utaratibu wa kifedha wa ufuatiliaji na usimamizi wa Miradi wa Ujenzi wa Umeme wa Julius Nyerere(JNHPP) fedha za mradi katika Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi ya TANESCO, ingepelekea upotevu wa Sh. 284,659,603.85, ambayo ni faida inayotokana na ubadilishaji wa fedha za Mradi wa JNHPP kutumika katika miradi mingine iliyoko chini ya TANESCO.

e) Ukosefu wa Utaratibu Sahihi wa Kuhifadhi kumbukumbu, Utunzaji na Mfumo wa Kuripoti wa Mfuko wa Fedha za Mradi wa JNHPP

TANESCO kama taasisi inayotekeleza Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Umeme wa Julius Nyerere, iliunda kitengo cha Utekelezaji wa Mradi (PIU) kwa ajili ya ufuatiliaji, kusimamia na kutekeleza mradi ambao ulianza ujenzi toka tarehe 12 Desemba 2018. Pamoja na shughuli zingine, Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi (PIU) kinawajibika kuanzisha na kuchakata malipo ya Mkandarasi, kushauri na kuomba msamaha wa Kodi kutoka kwa TRA kwa niaba ya Mkandarasi.

Katika kipindi cha ukaguzi (2018 - 2020), nilifanya tathmini juu ya utaratibu wa kurekodi, kuhifadhi kumbukumbu za malipo, kukiri, kutunza na kuripoti katika mfumo wa taarifa kuhusu masuala ya mradi unavyotekelezwa na Kitengo cha Uratibu wa mradi cha TANESCO (PIU) na kubaini kuwa hakuna utaratibu rasmi/mzuri wa kurekodi, kutunza kumbukumbu, kwa kupitia mfumo wa ukarabati na utoaji wa taarifa kwa shughuli za kifedha za kila siku. Uchunguzi zaidi ulibaini kuwa, Mhasibu wa Mradi amekuwa akitumia mkeka wa hesabu (Microsoft Excel) kuweka kumbukumbu za akaunti kama vile vyeti vya malipo, fedha zilizopokelewa na kulipwa kwa Mkandarasi.

Kwa kuongezea, nilishindwa kufuatilia taratibu za kudhibiti zilizopo kwa ajili ya uhakiki na uidhinishaji wa cheti cha malipo ya kazi za PIU zilizopokelewa kutoka kwa Mkandarasi (M/s Arab Contractor) na Mshauri wa Mradi (TECU).

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa hakukuwa na uthibitisho wa kukiri kupokelewa kwa malipo ya Mkandarasi pamoja na Mshauri wa Mradi. Hii inaweza kusababisha mzozo ikiwa Mshauri wa Mradi au Mkandarasi katika tukio hilo ataleta madai ya kutolipwa kwa usahihi au matumizi mabaya au kutolewa kwa fedha pungufu au kupunguzwa kwa fedha na mwajiri.

Zaidi, ilibainika kuwa hakukuwa na mfumo wa kuripoti kuhusu utayarishaji wa taarifa za kifedha au ripoti maalum za mradi. Mapungufu haya yaliyobainika yalichangiwa na ukosefu wa taratibu zilizopangwa za kuhifadhi, kukiri kupokea na kukubali malipo, utunzaji kumbukumbu na kuripoti fedha za mradi na TANESCO kwa utekelezaji wa mradi. Ukosefu wa utaratibu wa kuhakiki vielelezo na nyaraka (kama vile kitabu cha mahudhurio) na kumbukumbu nyingine kunaweza kusababisha taarifa mbaya na matumizi mabaya ya fedha za mradi.

Ili kuimarisha Udhibiti wa ndani wa fedha za Mradi, nashauri manejimenti ya Shirika la Usambazaji Umeme Tanzania (TANESCO):

(a) Kuhakikisha kuwa kunakuwa na akaunti ya Mradi wa Ujenzi wa Bwala la Umeme wa Julius Nyerere(JNHPP) kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi mzuri wa fedha za mradi zinazopokelewa kutoka Serikalini; na

(b) Kuhakikisha kuwa kuna utaratibu mzuri wa kurekodi, kupokea na mfumo wa kutoa taarifa kwa ajili ya ufuatiliaji sahihi wa fedha za mradi.

6.3.6 Matokeo ya Ukaguzi Kuhusu Uendelevu wa Mradi na Muunganiko na Wadau

a) Wadau Kutokushirikishwa vya Kutosha katika Kujenga Uwezo Juu ya Mradi

Nilibaini kuwa, TANESCO haijafanya juhudi za kutosha katika kuhakikisha wafanyakazi wake wazawa wanajengewa uwezo katika hatua zote za mradi. Hii ni kwa sababu TECU haikuhakikisha kwamba Mkandarasi anaandaa mpango madhubuti wa mafunzo ambao utaongoza katika kujenga uwezo wa wafanyakazi wa hapa nchini, na kwa njia hiyo kuhamisha maarifa na utaalam. Ilibainika kuwa TANESCO haikuwa na mpango wa kutosha wa kurithishana ujuzi (succession plan) wa kuwawezesha wafanyakazi wake katika kusimamia mradi, na kuweza kusimamia uendeshaji wa Mtambo wa kuzalisha umeme baada ya kukamilika kwa ujenzi wa mradi na kukabidhiwa kwa TANESCO. Hii ilidhihirishwa na:

(i) Ukosefu wa Mpango Madhubuti wa Mafunzo

Nilibaini kwamba Mkandarasi hakuwa na mpango madhubuti wa mafunzo kwa ajili ya wafanyakazi wa mwajiri (TANESCO) kulingana na takwa la Kanuni ya 7 (2) ya Ajira ya Wazawa ambayo inamtaka TANESCO kuanzisha mpango wenye ufanisi wa mafunzo ili kuweza kuzalisha waajiriwa wazawa watakaotekeleza majukumu ya wafanyakazi wasio wazawa walioajiriwa kwenye mradi. Hii ni kwa sababu kifungu kidogo cha 2.2.4 cha Mahitaji ya Mwajiri kilikuwa kimeelezea mafunzo ya Mkandarasi ambayo yalilenga zaidi kwenye kuunganisha mitambo ya umeme na kimakenika na vifaa vya ukaguzi wa mtambo wa kufua umeme.

Hata hivyo, mpango wa kina wa mafunzo ulioainisha jinsi Mkandarasi atakavyotekeleza mafunzo na kuweza kukidhi mahitaji ya Mwajiri haukutolewa kwa ukaguzi ili kujiridhisha. Mpango huo ungeweza kuthibitisha dhamira ya Mkandarasi katika kukidhi Mahitaji ya Mwajiri kuhusu mafunzo.

Kufuatana na mazungumzo zaidi na maofisa husika, ilibainika kuwa mafunzo hayo yalikusudiwa katika nyanja ya kuunganisha vifaa vya umeme na Mitambo (E&M) ambayo utekelezaji wake ulikuwa haujaanza. Maofisa pia walionesha kozi za mafunzo zilizopangwa au zilizokusudiwa kufanyika katika nchi zinazotengeneza mitambo ya chuma ya umeme wa maji (Hydraulic Steel Structures). Kozi hizo zingejumuisha mafunzo ya kuunganisha mitambo hiyo, shughuli ambayo utekelezji wake ungefanyika katika hatua za mwisho.

Hii ilitokana na kutokujumuishwa kwa mahitaji ya mafunzo ya kina miongoni mwa Mahitaji ya Mwajiri, ambayo yangetolewa kwa wafanyakazi wa Mwajiri katika hatua zote za mradi, na siyo maeneo kadhaa kama ilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha 2.2.4 cha Mahitaji ya Mwajiri. Kutokuwapo kwa programu kamili ya mafunzo kunaweza kusababisha kutokufuatiliwa vya kutosha kwa mahitaji ya mafunzo ambayo mwishowe kutasababisha upungufu wa ujuzi kwa wafanyakazi wa mwajiri wa namna ya kuendesha na kufanya matengenezo huko mbeleni.

(ii) Ukosefu wa Mpango wa Urithishaji wa Ujuzi

Pamoja na kwamba kulikuwa na nafasi mbalimbali zilizoshikiliwa na Wafanyakazi Muhimu wa Mkandarasi kwenye timu zote za Usanifu na Utekelezaji, wafanyakazi wa TANESCO hawakutoa ushahidi wa kutosha unaoonesha mpango wa kuandaa watakaochukua nyadhifa hizo baadaye. Hii ilikuwa kinyume na Kanuni ya 7 (1) ya Kanuni ya Ajira za Wazawa ambayo inasema kwamba mtu yeyote mwenye nia ya kuajiri mtu ambaye si raia wa Tanzania (mgeni) atatayarisha mpango ulioelezewa vizuri wa kurithisha ujuzi au utaalamu wa mgeni kwa raia wa Tanzania muda wote wa ajira yake.

Ukosefu wa mpango wa kurithisha ujuzi ulitokana na usimamizi duni wa TECU katika kuhakikisha kuwa Mkandarasi anaandaa mpango mzuri wa mafunzo ili kuandaa wafanyakazi wa Mwajiri kuchukua majukumu ya wataalamu wa kigeni baada ya kukamilika kwa mradi. Matokeo yake, Watanzania hawatapata ujuzi wa kutosha kuweza kutekeleza miradi mingine ya aina hiyo hapo baadaye.

Kwa kuongezea, ujenzi wa mradi wa umeme unaotokana na maji unajumuisha maeneo mengine ya utaalamu kama vile mabwawa, majengo, njia za maji, barabara na madaraja. Wataalamu kutoka kwa taasisi nyingine za serikali zinazoshughulika na maeneo hayo hapo juu kama vile Wakala wa Uchimbaji na Ujenzi wa Visima na Mabwawa (DDCA) na Wakala wa maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) hawakuwa wamehusika licha ya kuwa wakala wa serikali wanaoshughulika na ujenzi wa mabwawa na maji.

Maafisa kutoka TANESCO na TECU wanakiri kwamba hawakuzingatia katika hatua hii ya awali, ijapokuwa wanaona ni muhimu sana kwa wadau hao kushiriki katika shughuli zinazoendelea.

Ili kuhakikisha kuwa kuna Uendelevu wa Mradi na Uratibu na Wadau, nashauri manejimenti ya Shirika la Usambazaji Umeme Tanzania (TANESCO):

(a) Kushirikiana na taasisi za Serikali kama vile vyuo vikuu na vyuo vingine vya elimu ili kuweka utaratibu ambao utarahisisha

wazawa wenye sifa za kitaalamu zinazohitajika kushiriki katika fursa za ajira ili kuepusha kuajiri wageni katika nafasi ambazo zinaweza kuchukuliwa na wazawa. Utaratibu wa kuruhusu uwazi na kufikia sehemu kubwa ya wazawa unatoa nafasi sawa kwa wafanyakazi wote waliohitimu na wenye sifa; na

(b) Kuhakikisha kuwa Mkandarasi anaandaa mpango wa mafunzo ili kuwezesha kufanikisha Mahitaji ya Mwajiri kwa kuwashirikisha watanzania katika kila hatua ya mradi ili waweze kujifunza na kupata maarifa ambayo yatatumika wakati wa uendeshaji na uangalizi wa mradi na kutekeleza mradi kama huo hapo baadaye. Mpango huo unapaswa kuwajumuisha wafanyakazi wa Mwajiri kama wasaidizi wa wafanyakazi muhimu kama njia ya kuhamisha maarifa.

6.3.7 Kuna Uwezekano Mkubwa wa Mradi Kufikia Lengo Lililokusudiwa

Kulingana na tathmini iliyofanywa hadi sasa, nilibaini kuwa hakuna udhaifu mkubwa wa kiufundi ambao unaweza kuzuia mradi kufikia malengo mahususi yaliyokusudiwa. Kwa kuwa TANESCO ilikadiria kiwango cha chini cha uwezo wa mradi wa Uzalishaji wa Nishati wa Mwaka kwa kutumia 'Nishati thabiti' (Firm Energy) ya GWh 6307 badala ya ' Nishati ya Wastani ' (Nominal Energy) ya GWh 10300, ni wazi kuwa uwezekano wa kufikia kiwango kilichotajwa cha umeme ni mkubwa endapo TECU atahakikisha kwamba Mkandarasi anatekeleza kwa kuzingatia Usanifu na viwango vya ubora vya mradi vilivyoainshwa.

SURA YA SABA

MRADI WA MIUNDOMBINU YA MABASI YAENDAYO HARAKA JIJINI DAR ES SALAAM

7.1 Utangulizi

Mradi wa Miundombinu wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili Jijini Dar es Salaam unahusisha ujenzi wa miundombinu ambayo inajumuisha kilometa 20.3 za barabara zinazojitegemea za mabasi yaendayo haraka na miundombinu ya usafiri kwa vyombo visivyo vya moto katika Ukanda wa barabara ya Kilwa na baadhi ya sehemu ya barabara ya Kawawa. Mradi unaanzia eneo la Mbagala katika wilaya ya Temeke hadi katikati ya Jiji ambapo unaungana na awamu ya kwanza ya mradi wa mabasi yaendayo haraka eneo la Kituo cha Kariakoo.

Makadirio ya jumla ya gharama ya mradi pasipo kodi ni Dola za Marekani Milioni 159.32 (Sh. 285.1 billioni). Mradi unafadhiliwa kwa umoja kati ya Benki ya Kimaendeleo ya Afrika (61.1%), Mfuko wa Pamoja wa Ukuaji wa Afrika (27.8%) na Serikali ya Tanzania (11.1%). Mradi ulitarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka minne (2016-2020). Hata hivyo, kutokana na kuchelewa kwa awamu za usanifu na manunuzi, tarehe ya kukamilika kwa mradi kwa sehemu ya kwanza ni tarehe 5 Mei 2022 na kwa sehemu ya pili ni 28 Februari 2021.

7.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa kutathmini kama Wakala wa Barabara (TANROADS) walisimamia ujenzi wa awamu ya pili ya mradi wa miundo ya mabasi ya yaendayo haraka kwa kuzingatia kama ujenzi huo umefanyika kwa muda, gharama na ubora uliopangwa kulingana na miongozo na viwango vya ubora wa kazi ili kuwezesha mwendo stahiki wa vyombo vya usafiri na kuondoa vikwazo kwa mtiririko wa vyombo vya usafiri kuelekea sehemu mbalimbali za katikati ya jiji zenye shughuli za kiuchumi.

Wakala wa Barabara chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ni mkaguliwa mkuu kwa sababu ni mtekelezaji mkuu wa mradi huu. Kwa upande mwingine, Wakala wa Mabasi yaendayo haraka (DART) pia ni mkaguliwa kwa mradi huu kwa sababu, DART

inahusika na ununuzi wa huduma kwa ajili ya mzabuni wa uendeshaji huduma za usafiri kupitia mabasi, ukusanyaji wa nauli na mifumo yake na kusimamia uendeshwaji wa mfumo wa mabasi yaendayo haraka . DART ilihusika katika manunuzi na usimamizi wa huduma za kishauri kwa ajili ya usanifu wa km 42.9 za mfumo wa mabasi yaendayo haraka awamu ya pili na ya tatu katika jiji la Dar es Salaam.

Vipengele viwili vinavyohusiana na shughuli za ujenzi vilikaguliwa, navyo ni kazi za ujenzi na huduma za ushauri kihandisi. Kipande cha kwanza kilihusisha kazi za barabara ikiwemo barabara ya Kilwa, barabara ya Gerezani, barabara ya Chang'ombe, sehemu ya barabara ya Kawawa na sehemu ya barabara ya Sokoine yenye kilometa 20.3, ikijumuisha madaraja ya juu mawili na vituo vya mabasi barabarani. Kipande cha pili kilijumuisha Kazi za Majengo: Kituo kikuu kimoja, vituo vya mabasi viwili na vituo vitatu vilivyo nje ya barabara kwa ajili ya kupeleka abiria kwenye vituo vilivyo barabarani.

Ukaguzi wangu uliangalia kazi za mradi tangu kuanzishwa kwa mradi na upembuzi yakinifu hadi hatua ya ujenzi iliyofikiwa kipindi ukaguzi wangu unafanyika Januari 2021. Nilipitia kazi zote za mradi zilizotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ya fedha iliyopita kuanzia 2016/17 hadi 2020/21. Hii ni kwa sababu hiki kilikuwa kipindi ambacho Wakala wa Barabara (TANROADS) na Wakala ya Mabasi yaendayo haraka (DART) walijikita katika utekelezaji wa mradi.

7.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi kwenye kazi za ujenzi wa miundombinu na majengo. Inajumuisha masuala ya upangaji, usanifu na uandaaji wa nyaraka za zabuni, manunuzi, usimamizi wa mkataba, masuala ya fedha, masuala ya ubora wa kazi zilizofanyika, pamoja na usimamizi wa rasilimali watu.

7.3.1 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Mipango, Usanifu na Uandaaji wa Nyaraka za Zabuni

a) Huduma za Uhandisi Elekezi kwa Ajili ya Usanifu wa Kilomita 42.9 wa Mabasi Yendayo Haraka - Awamu ya 2 na 3 katika Jiji la Dar es Salaam

Mhandisi Mshauri Alicheleweshа Kazi kwa Miaka Minne
Mkataba wa Mradi wa Miundombinu wa Mabasi yaendayo haraka ulisainiwa tarehe 25 Februari, 2011 na kuanza baada ya siku 28, na ulitarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miezi kumi na mbili. Mkataba ulitarajiwa kuisha tarehe 25 Machi, 2012. Tarehe 25 Januari 2012 Mhandisi Mshauri aliomba kuongezewa muda kwa miezi miwili ambayo ilitolewa na Wakala wa Mabasi yaendayo haraka. Ingawa, Mhandisi Mshauri hakumaliza kazi kama ilivyokubaliwa na kuchelewa kukabidhi kazi kamili ya usanifu na nyaraka za zabuni kwa zaidi ya miaka minne (hadi kufikia 15 Aprili 2016). Kuchelewa kwa usanifu kuliathiri kuanza kwa mradi na mpango wa ufadhili. Kuchelewa kulisababishwa kwa kiasi kikubwa na mapitio ya usanifu yaliyofanywa na Wakala wa Mabasi yaendayo haraka ambayo yalisababishwa na utoaji wa maelekezo mapya ambayo yalihitaji marekebisho ya usanifu . Sababu ya pili ilikuwa kuchelewa katika kushughulikia fidia.

b) Kipande cha Kwanza: Huduma ya Uhandisi Ushauri Elekezi kwa Kazi za Barabara

(i) Ripoti ya Mapitio ya Usanifu Ilicheleweshwa kwa Miezi Saba
Kwa mujibu wa Kifungu cha 8.3 cha Mkataba wa Huduma ya Uhandisi Ushauri Awamu ya 2, Kipande cha kwanza, Mhandisi Mshauri alitakiwa kuwasilisha taarifa ya mapitio ya usanifu miezi minne baada ya kuanza kwa kazi. Kuanza kwa kazi hii ilitakiwa iwe tarehe 27 Machi, 2017; kwa hiyo, ripoti ya mapitio ya usanifu ilitakiwa iwe imefanyika kabla ya tarehe 27 Julai, 2017.

Hata hivyo, mapitio ya mafaili ya mawasiliano ya kikazi yalionesha kwamba, taarifa ya usanifu iliwasilishwa tarehe 27 Februari, 2018 ambayo ni kuchelewa kwa miezi saba. Kushindwa kuwasilisha taarifa ya usanifu kwa wakati hakukuweza kufikisha maoni ya Mhandisi Mshauri, na maboresho yaliyofanywa kwenye

usanifu yalichelewesha mchakato wa ununuzi wa mkandarasi kwa wakati.

(ii) Taarifa Kamili ya Usanifu wa Kina na Nyaraka za Zabuni kwa Mabadiliko ya Mkataba Na. 1 Ilicheleweshwa kwa Miezi Nane

Sehemu ya tisa ya Hadidu za Rejea kwa ajili ya mabadiliko ya mkataba Na. 1 kwa huduma zilizoongezeka ikiwemo usanifu wa daraja la juu ukanda wa Bandari –na barabara ya gerezani zilihitaji Mhandisi Mshauri kuwasilisha taarifa kamili ya usanifu miezi mitatu baada ya kuanza kwa kazi. Kazi ilitakiwa ianze tarehe 17 Februari, 2018; na kwa hiyo, taarifa kamili ya usanifu ilitakiwa ikamilike kabla ya tarehe 18 Mei, 2018.

Hata hivyo, mapitio ya mafaili ya mawasiliano ya kikazi yalionesha kwamba, taarifa kamili ya usanifu iliwasilishwa tarehe 17 Januari, 2019 huku ikiwa imechelewa kwa miezi nane. Uwasilishaji wa mapema wa taarifa kamili ya usanifu pamoja na nyaraka za zabuni ungewezesha ujumuishaji wa mabadiliko stahiki katika zabuni ya mkandarasi na mapatano kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya 2, Kipande cha kwanza kwa kazi za barabara. Sababu ya kuchelewesha mabadiliko ya mkataba Na. 1 ilikuwa majadiliano marefu kati ya Shirika la Reli (TRC) na Wakala wa Barabara (TANROADS), kuhusiana na kuondoa miundombinu ya reli iliyopo au kubakiza kimo chake kutoka usawa wa bahari pasipo kuathiri usanifu .

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa kushirikiana na menejimenti DART kuimarisha usimamizi wa muda ili kuhakikisha usanifu na mapitio ya udhibiti wa ubora wa rasimu za usanifu zinafanyika kwa wakati muafaka.

(iii)Kukosekana kwa Mpangilio wa Mipango Miji Yakinifu Kulisababisha Mabadiliko ya Sh. Bilioni 28.05 (Bila Kodi ya Ongezeko la Thamani) kwa Ajili ya Ujenzi wa Daraja la Juu Ukanda wa Bandari - Barabara ya Gerezani.

Kwa mujibu wa kifungu cha 7 (Sehemu ya 5.1- Mapitio ya Usanifu na Huduma kabla ya Mkataba), Mhandisi Mshauri alitakiwa kupitia taarifa za usanifu wa kina wa kiuhandisi ikijumuisha taarifa za usanifu, ramani na michoro, kuthibitisha usahihi wa taarifa za

utafiti wa eneo la ujenzi na tafiti za kipindi cha nyuma (kama zilikuwepo) pamoja na kuhuisha taarifa ya usanifu wa kina wa kiuhandisi.

Hata hivyo, mapitio ya nyaraka za mradi yalionesha kwamba, hakukuwa na mapitio ya upembuzi yakinifu kwa mradi wa Mabasi yaendayo haraka iliyofanyika mwaka 2005. Hii ilitokana na kukosekana kwa taarifa juu ya mipango ya serikali katika kuanzisha miundombinu kama vile reli. Matokeo yake, wakati maandalizi ya zabuni kwa ajili ya sehemu ya kwanza ya mradi yalipokuwa yamefika mbali, kulikuwa na mabadiliko ya usanifu yaliyoletwa katika Daraja la juu la Reli katika eneo la Bandari ambayo yalihitaji kupandisha kimo cha reli kutoka usawa wa bahari kwa ajili ya Reli ya Kisasa (SGR). Mabadiliko haya yaliathiri mwinuko wa barabara inayokaribia daraja la juu na kuingia katika barabara na reli inayopita eneo la bohari ya mafuta. Matokeo yake, kazi hii iliingizwa kwenye mkataba wa mwanzo wa Kipande cha Kwanza kama mabadiliko ya mkataba Na. 1 yenye gharama ya Sh. 28,047,114,893.02.

Mabadiliko haya ambayo yalisababisha usanifu kwa mara nyingine kwenye daraja la juu la pili yalisababishwa na kukosekana kwa mpango mkuu wa kina wa mipango miji kwa miaka 10 kutoka muda usanifu ulipofanyika ambao ulitakiwa kuandaliwa na Wizara ya Ardhi.

c) Kipande cha Pili: Huduma ya Ushauri wa Kiuhandisi Kwenye Kazi za Majengo

(i) Taarifa ya Kamili ya Mapitio ya Usanifu Ilichelewa kwa Siku 80

Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 8.3 cha Mkataba wa Huduma ya Ushauri wa Kiuhandisi, Mhandisi Mshauri alitarajiwa kuwasilisha mapitio ya taarifa ya usanifu kamili miezi minne baada ya kuanza kwa kazi. Taarifa ya usanifu ilitarajiwa kuwasilisha maoni ya Mhandisi Mshauri kutoka kwa mapitio ya usanifu , na maboresho yaliyofanyika. Kazi hiyo ilitarajiwa iwe tarehe 24 Machi, 2017; kwa hiyo, taarifa ya mapitio ya usanifu kamili ilitakiwa iwe tarehe 24 Julai, 2017.

Hata hivyo, mapitio ya nyaraka yalionesha kwamba, taarifa ya usanifu kamili iiliwasilishwa tarehe 12 Oktoba, 2017 ambapo ni

ucheleweshwaji ya taarifa hii kwa siku 80. Hii ilisababishwa na mabadiliko ya eneo la kazi, kwani eneo la kazi lilifidiwa kwa sehemu tu wakati wa usanifu. Pia, taarifa ya mapitio ya usanifu kamaili ilichelewa kwa sababu mapitio ya rasimu ya taarifa ya usanifu haikufanyika kwa wakati na Wakala wa Barabara na wadau wengine kama vile Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka, Shirika la Reli ya Kati, na Mamlaka ya Bomba la Mafuta kati ya Tanzania na Zambia (TAZAMA). Kuchelewa kwa taarifa kamili ya mapitio ya usanifu kulisababisha kuchelewa kwa mchakato wa ununuzi wa mkandarasi na kuanza kazi za ujenzi.

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa kushirikiana na menejimenti ya Mabasi yaendandayo Haraka (DART) kuimarisha ushirikiano wa sekta mbalimbali na taasisi za umma wakati wa maandalizi ya mipango mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kuna ujumuishaji wa kutosha kwa lengo kupunguza marekebisho mapya na ongezeko la kazi za ujenzi.

7.3.2 Matokeo ya Ukaguzi Katika Mchakato wa Manunuzi

a) Kipande cha 1: Kazi za Ujenzi

(i) Wazabuni Walioshindwa Hawakupewa Muda wa Kutoa Malalamiko yao

Sehemu ya 60(3) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 (ikisomwa na marekebisho yake ya Mwaka 2016) inataka Afisa Masuuli kutoa taarifa ya kuonesha dhamira ya kutoa kandarasi kwa wazabuni wote walioshiriki katika zabuni, huku ikitoa siku saba za kuwasilisha malalamiko yao, kama yapo.

Hata hivyo, mapitio ya mchakato wa manunuzi hayakuonesha kama wazabuni wote walitaarifiwa. Kushindwa kutoa muda kwa wazabuni walioshindwa kuwasilisha malalamiko yao kuliwanyima nafasi ya kujua sababu za kushindwa kwao. Hivyo ina athari katika kufanya maboresho katika ushiriki wao wa mchakato wa zabuni kwa siku zijazo.

(ii) Kuchelewa kwa Miezi Minne kuwafahamisha Wazabuni Walioshindwa

Sehemu ya 60(14) ya Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2011 (ikisomwa na marekebisho yake ya Mwaka 2016) inamtaka Afisa Masuuli ndani ya siku thelathini baada ya kutoa taarifa ya kumpa kazi mzabuni aliyeshinda, kuwafahamisha wazabuni walioshindwa jina la mzabuni aliyeshinda. Hata hivyo, mapitio ya nyaraka za manunuzi yalionesha kwamba, barua ya kupewa kazi ilipelekwa kwa mzabuni aliyeshinda (Sinohydro Corporation Limited) tarehe 19 Novemba, 2018 na mkataba ulisainiwa tarehe 10 Desemba, 2018, wakati barua za kuwafahamisha wazabuni walioshindwa zilitumwa tarehe 20 Machi, 2019, miezi minne mbele. Kuchelewa kuwajulisha wazabuni walioshindwa kunaweza jenga dhana miongoni mwa wadau kwamba, mchakato wa manunuzi ya mkandarasi haukuwa wa haki na uwazi.

7.3.3 Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Mkataba

a) Kipande cha Kwanza: Huduma za Ushauri Kihandisi kwa Kazi za Ujenzi

(i) Wakala wa Barabara hakupeleka Watumishi kwa Wahandisi Washauri kwa Ajili ya Mfunzo wakati wa Usimamizi wa Kazi.

Kifungu cha 5.2 (xxiv) cha Hadidu Rejea kwa Huduma za Ushauri wa Kiuhandisi kilitaka Mhandisi Mshauri kuandaa na kutoa mafunzo kazini kwa watumishi wa Wakala wa Barabara (TANROADS). Ilifikiriwa kwamba, TANROADS ilitakiwa kupeleka walau wahandisi wawili kwa Mhandisi Mshauri wakati wa usimamizi wa kazi.

Nilibaini kwamba, hakukuwa na kifungu katika makisio ya gharama za ujenzi (BoQ) kwa wafanyakazi wa TANROADS. Haikuwekwa wazi kama TANROADS alikubaliana na Mhandisi Mshauri wakati wa hatua za awali za mkataba kuondoa kifungu hicho. Afisa wa Wakala wa Barabara aliyehojiwa alibainisha kwamba, kukosekana kwa kifungu hicho kwenye makisio ya gharama za ujenzi kulitokana na kutokukijumuisha kifungu hicho kwa ajili ya mafunzo ya watumishi katika bajeti ya mradi.

Kushindwa kuwapeleka wafanyakzi wa Wakala wa Barabara kwenye mradi kuliwanyima wahandisi wa TANROADS kupata elimu kwenye maeneo mbalimbali yanayohusu usimamizi wa miradi. Hii

hujumuisha masuala yote yahusuyo usimamizi wa mkataba wa kazi za ujenzi wa barabara, upangaji wa kazi, matumizi ya mifumo ya programu mbalimbali za komputa, udhibiti wa viwango vya ubora kwa kazi zilizokamilika, upangaji na upimaji, ikijumuisha maandalizi ya michoro ya kazi kadri ilivyojengwa na taarifa kamili za ujenzi.

(ii) Mhandisi Mshauri Hakuandaa na Kuwasilisha Mwongozo wa Usimamizi wa Mradi

Kwa mujibu wa mkataba wa ushauri wa kihandisi kwa ajili ya mapitio ya usanifu na usimamizi wa ujenzi wa awamu ya pili ya mabasi yaendayo haraka, mhandisi mshauri alitakiwa kuandaa Mwongozo wa Usimamizi. Mwongozo huu ungekuwa umeweka taratibu za kufuata wakati wa utekelezaji wa kazi. Nilibaini kwamba, Mwongozo wa Usimamizi uliandaliwa na kuwasilishwa kwa Wakala wa Barabara (TANROADS). Hata hivyo, haukuwa wa kina kuelezea namna ambavyo usimamizi ungetakiwa kufanyika. Mhandisi mshauri aliagizwa kuboresha mwongozo wa usimamizi. Zaidi, hadi kuisha kwa ukaguzi huu, mwongozo wa usimamizi haukuwa tayari kwa ajili ya kuwasilishwa tena.

(iii) Mkandarasi Alichelewa Kuwasilisha Dhamana ya Utendaji kwa Siku 63

Kwa mujibu wa kifungu cha 4.2.2 cha Masharti ya Mkataba (GCC), mkandarasi alitakiwa kuwasilisha Dhamana ya Utendaji kwa Mwajiri ndani ya siku 28 baada ya kupokea barua ya kukubalika kupewa kazi na kuwasilisha nakala kwa Mhandisi.

Nilibaini kwamba, barua ya kukubalika kupewa kazi ilitumwa kwa mkandarasi tarehe 19 Novemba, 2018 na Dhamana ya Utendaji ilitakiwa iwasilishwe kwa mwajiri sio zaidi ya tarehe 17 Desemba, 2018 (ndani ya siku 28). Hata hivyo, iliwasilishwa kwa mwajiri tarehe 17 Februari, 2019 (takribani miezi miwili baadaye).

Kuchelewa kuwasilisha Dhamana ya Utendaji kwa mwajiri kulisababisha kuchelewa kuanza kwa kazi kwa takribani miezi miwili.

Nashauri Wakala wa Barabara kuboresha usimamizi wa miradi kwa kuhakikisha matakwa ya mkataba yanatekelezwa ikiwemo uwasilishaji wa dhamana za kiutendaji.

7.3.4 Usimamizi wa Fedha

a) Kipande cha Kwanza: Kazi za Ujenzi Barabara

(i) Kutokukokotolewa kwa Fedha Kiasi cha Dola za Marekani 52,951.80

Uchambuzi wangu ulibaini rasimu ya mapitio ya usanifu kwa awamu ya pili yalichelewa kwa siku 11 wakati mapitio ya taarifa kamili ya usanifu yalichelewa kwa siku 215 na kufanya jumla ya ucheleweshaji wa taarifa hizi kuwa siku 226. Nilibaini kwamba, mwajiri aliidhinisha na kulipa zaidi ya vyeti vya malipo 20 vilivyotolewa na mhandisi mshauri bila kukata fedha zinazotokana na ucheleweshaji wa kuwasilisha taarifa kiasi cha Dola za Marekani 52,951.80 ambayo ni sawa na Sh. 120,610,962.45. Hii ilikuwa kinyume na kifungu cha 8.9 ya kiambatisho A cha Mkataba kati ya Wakala wa Barabara na Mhandishi Mshauri M/S. Botek Bosphorus Consulting Corporation.

(ii) Malipo ya Dola za Marekani 300,645 Yalifanyika kwa Mhandisi Mshauri bila Bima

Nilibaini kwamba, bima dhidi ya hatari iliwasilishwa na mhandisi mshauri tarehe 20 Februari, 2019 kwa kutumia barua yenye kumbukumbu namba Na. TZ/3210/EG/70. Hata hivyo, kabla ya uwasilishaji wa bima, malipo yalikuwa yameshafanyika mara nne kupitia hati ya malipo Na. 1 hadi 3 ikiwa na jumla ya Dola za Marekani 233,145 (bila Ongezeko la Kodi ya Thamani)[15] na hati namba nne ya kiasi cha Dola za Marekani 67,500 (bila Ongezeko la Kodi Thamani) kama 50% ya malipo ya kazi ya mabadiliko ya mkataba Na.1.

Kufanya malipo bila bima ni kinyume na kifungu cha 24.1 GCC cha Masharti ya Jumla ya Mkataba na kifungu cha 12 (SCC) cha

[15] Kama ilivyooneshwa kwenye SCC 20 kama malipo wakati wa awamu ya mapitio ya usanifu kwa malipo ya 20%, 50% na 30% ya jumla ya gharama yote ya awamu ya mapitio ya usanifu .

Masharti Maalumu ya Mkataba ambavyo vinataka bima dhidi ya hatari kuwasilishwa kabla ya kuanza kwa huduma kwa ajili ya kuwafidia walengwa hadi kiasi cha Sh. Milion 10 kwa kiwango cha chini na zile bima za madai yanayohusiana na masuala ya uweledi yenye fidia kwa walengwa sawa na thamani ya mkataba. Hii ingeweza sababisha upotevu wa fedha za Serikali endapo kungetokea kushindwa kwa Mhandisi Mshauri.

(iii) Ucheleweshaji wa Malipo kwa Mhandisi Mshauri Yamesababisha Riba ya Adhabu Dola za Marekani 23,834.38

Kwa mujibu wa Kifungu cha 46.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC), kama mwajiri anachelewesha malipo zaidi ya siku kumi na tano baada ya tarehe iliyooneshwa, riba inatakiwa kulipwa kwa mhandisi mshauri kwa kiasi chochote atakacholipwa, lakini kisilipwe kwa tarehe hiyo kwa kila siku ya kuchelewesha kwa kiwango cha mwaka kilichowekwa katika Masharti Maalum ya Mkataba (SCC).

Wakati wa ukaguzi, tarehe 20 Oktoba, 2020, nilibaini kwamba Ankara mbalimbali kutoka kwa mhandisi mshauri zililipwa kwa kuchelewa, na baadhi hazikulipwa kabisa katika tarehe iliyotajwa ya ukaguzi. Nilibaini kuwa, kuchelewa kulisababishwa na mchakato wa kuthibitisha na kuidhinisha kiasi cha kulipwa kutoka Wakala wa Barabara kwenda Wizara ya Fedha na Mipango na kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda kwa Mfadhili wa mradi. Ucheleweshwaji huu wa malipo utamgharimu mwajiri adhabu ya fidia kiasi cha Dola za Marekani 23,834.38, ambacho ni sawa na Sh. 54,288,759.05.

(iv) Dola za Marekani 4,315.84 Zilitozwa Zaidi Katika Cheto cha Malipo Na 23

Kwa mujibu wa Masharti Maalumu ya Mkataba kifungu namba 22 (SCC 22), malipo yanatakiwa kufanyika kwa kila mwezi kwa kazi zilizofanyika kulingana na Hadidu Rejea, zikijumuisha ada kwa ajili ya wafanyakazi walioidhinishwa na malipo yaliyoidhinishwa.

Katika mapitio ya hati ya malipo namba 23 nilibaini kwamba, kiasi kilichoidhinishwa bado hakijalipwa, vocha ya malipo namba 000005235 ya Benki ya Maendeleo ya Kiafrika (AFDB) ilikuwa Dola za Marekani 53,998.66 na vocha ya malipo 000005236 ya AGTF

ilikuwa Dola za Marekani 24,487.76. Kiasi hiki cha fedha kilichooneshwa kwenye vocha hizi mbili za Malipo kilikuwa juu kuliko kiasi kilichoidhinishwa kwa Dola za Marekani 2,969.3 kwa hati ya AFDB na Dola za Marekani 1,346.54 kwa hati ya AGTF. Ilibainika kwamba, ongezeko lilitokea kwa sababu mhasibu aliandaa malipo kwa kutumia kiasi cha Ankara badala ya kiasi kilichoidhinishwa. Hii humaanisha kukosekana kwa umakini kwa mhasibu na kutofuata taratibu za mfumo wa uthibiti wa malipo uliopo TANROADS ambao unataka malipo yafanyike kwa kutumia kiasi kilichoidhinishwa. Kuzidishwa kwa malipo kunapelekea matumizi yasio na tija.

b) Kipande cha Kwanza: Kazi za Ujenzi - Ujenzi wa Barabara

(i) Mhandisi Mshauri na Mwajiri Walichelewa Kuwasilisha Cheti cha Malipo Na. 1

Kifungu cha 14.6.1 cha Masharti ya Jumla ya mkataba kinahitaji Mhandisi ndani ya siku 28 baada ya kupokea taarifa na nyaraka za uthibitisho kuwasilisha kwa mwajiri cheti ya malipo ambayo itaonesha kiasi ambacho mhandisi mshauri anaona inafaa kulipwa.

Hata hivyo, nilibaini kwamba katika cheti cha malipo Na. 1, mkandarasi aliwasilisha maombi ya fedha na nyaraka za uthibitisho tarehe 21 Desemba, 2019 wakati mhandisi mshauri amewasilisha cheti cha malipo Na. 1 kwa Wakala wa Barabara tarehe 27 Januari, 2020. Badala ya siku 28 kama inavyotakiwa kwenye Kifungu cha 14.6.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba, ilichukua siku 36 kwa Mhandisi kuidhinisha cheti cha malipo. Hii iliathiri siku nyingine 28 za mwajiri na kumwacha mwajiri na siku 20 tu kukamilisha malipo kwa mkandarasi ambapo siku ya malipo ilikuwa tarehe 15 Februari 2020. Hivyo, hati ya malipo Namba 1 ililipwa tarehe 29 Aprili, 2020, huku ikiwa imechelewa kwa siku 73.

(ii) Riba Kwenye Malipo Yaliyochelewa Yafikia Sh. 30.3 Milioni

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14.8.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba wa Kazi za Barabara Kipande cha kwanza, kinaeleza "kama mkandarasi hatolipwa kwa wakati kwa mujibu wa Kifungu cha 14.7, atastahili kupokea gharama za kifedha zinazoongezeka

kwa mwezi kama tozo kwa kiasi ambacho hakijalipwa kwa wakati kwa kipindi chote cha ucheleweshwa kwa malipo husika. Mapitio ya vyeti vya malipo Na. 1 na 2 yanaonesha kwamba malipo yalicheleweshwa kwa siku 73 kwa cheti Na. 1 na yalicheleweshwa kwa siku 33 kwa Hati namba 2 hadi tarehe ya ukaguzi tarehe 19 Oktoba 2020 na kutoa jumla ya gharama ya Sh. milioni 30.3.

(iii) Kukosea Ukokotoaji Kulikofanywa na Mhandisi Mshauri Kuliongeza Riba kwa Sh. Milioni 13.14

Kifungu cha 14.7.1 (b) cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinahusu ukomo wa idadi ya siku za malipo; ambapo kiwango cha juu ni siku 56 kwa cheti cha malipo kwa Mhandisi Mshauri na Mwajiri ambazo huhesabiwa kutoka siku baada ya Mhandisi kupokea taarifa ya malipo na vithibitisho vya maombi ya malipo kutoka kwa mkandarasi.

Hata hivyo, wakati wa kupitia hati ya malipo Namba 1 ilibainika kwamba, Mhandisi alikokotoa riba ya kuchelewesha malipo kwa kuanza kuhesabu siku baada ya uidhinishwaji wa vyeti vya malipo ambayo ni kinyume na matakwa ya Kifungu cha 14.7.1 cha mkataba. Zaidi ya hilo, kwa mujibu wa Kifungu cha 14.8.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba, gharama za malipo zitakokotolewa kwa kiwango cha mwaka cha asilimia tatu zaidi ya kiwango cha benki kuu katika nchi yenye aina ya fedha ambayo malipo husika hufanyika au kama haipo basi kiwango kutoka benki nyingine inatoa kiasi kinachofanana na malipo yatalipwa kwa aina ya fedha ya nchi hiyo. Hata hivyo, ilibainika kwamba, Mhandisi alitumia riba ambayo inatofautiana na matakwa ya mkataba kwa viwango vya fedha za Kitanzania na Dola za Marekani.

Nilibaini kwamba, Mhandisi alitumia kiwango cha punguzo kutoka Benki Kuu cha asilimia saba cha aina ya fedha za ndani ya nchi kwa aina zote za fedha bila kujumlisha asilimia tatu kwa ajili ya fedha za ndani. Zaidi ya hilo, Benki Kuu haikuwa na kiwango cha punguzo kwa Dola za Marekani. Hata hivyo, Mhandisi hakutumia kiwango cha benki cha kubadilisha fedha cha kimataifa (*interbank rate*), bali alitumia kiwango cha punguzo kwa aina ya fedha za ndani. Mapungufu haya yalisababisha utozwaji wa Sh. 13,143,232.97 kama kiwango cha riba kwa cheti cha malipo Na. 1.

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara (a) Kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kujitahidi kupunguza muda wa kupitia ankara ili kuhakikisha ankara ambazo zimesalia zinalipwa kwa wakati ili kuepusha riba ya inayotokana na ucheleweshaji wa malipo. (b) Kurudia kukokotoa kiwango cha riba kilicholipwa na kurejesha Serikalini kiwango kilicholipwa zaidi kwa mkandarasi.

c) Kipande cha Pili: Kazi za Majengo

(i) Kuchelewa kwa Malipo Kulisababisha Riba Kiasi cha Sh. Milioni 49.26

Kifungu cha 14.8.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinasema kwamba, kama mkandarasi hapokei malipo kwa mujibu wa Kifungu cha 14.7, mkandarasi atastahili kupokea riba inayoongezeka kwa kila mwezi kwenye kiasi cha fedha ambacho hakijalipwa wakati wa ucheleweshaji wa malipo.

Nilibaini kwamba, kulikuwa na ucheleweshaji wa vyeti vya malipo Na. 1,2,3,4 na 5 kwa kampuni ya ujenzi ya China Civil Engineering Construction Corporation ambayo kama ingedaiwa na mkandarasi, mwajiri ataingia gharama ya malipo ya riba ya Sh. 49,263,362.87 kwa mujibu wa tathmini yangu ambayo itaongeza gharama ya mradi bila faida yoyote au faida kutokana na ongezeko la gharama husika.

Nilibaini kwamba, kuchelewa kulipa cheti cha malipo Na. 3, kwa siku 78 hadi kipindi cha ukaguzi, kulisababishwa na mfadhili wa mradi (AFDB) kwa kutolipa kwa wakati. Hata hivyo, gharama za ucheleshaji zitalipwa na Serikali ya Tanzania.

d) Kipande cha Pili: Huduma za Kiushauri Katika Kazi za Majengo

(i) Kuchelewa kwa Malipo Kulisababisha Riba Kiasi cha Sh. Milioni 9.78

Kwa mujibu wa kifungu cha 46.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba, kama mwajiri atachelewesha malipo zaidi ya siku 15 baada ya tarehe ya malipo iliyopangwa, riba inatakiwa kulipwa kwa mhandisi mshauri kwa kiasi chochote kinachotakiwa kulipwa. Ikiwa hakitalipwa tarehe hiyo, kiasi hicho kitakuwa

kinaongezeka kadri kitakavyooneshwa kwenye Masharti Maalum ya Mkataba.

Nilibani kwamba, malipo kwa kampuni ya "M/s Intercosult" yalicheleweshwa katika Ankara mbalimbali; ambapo Ankara zilitoa jumla ya Sh. 9,789,534.31 kama zingedaiwa na mhandisi mshauri. Ankara Na. 9 hadi 18 ambazo zilikuwa bado kulipwa hadi kipindi cha ukaguzi huu zitaendelea kuongezeka kama hazitolipwa, hivyo kuongeza gharama zisizo za lazima kwa mwajiri.

Mapitio ya barua zilizowasilishwa baina ya pande zinazohusika katika mkataba yalibaini kuwa ucheleshwaji huu ulisababishwa na Wizara ya Fedha na Mipango, Wakala wa Barabara na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.7-1.**

Jedwali 7- 1: Riba Kutokana na Malipo Yaliyocheleweshwa kwa M/s Interconsult

Ankara	Kiasi Kilichoidhinishwa	Siku Zilizocheleweshwa	Riba (Sh.)
Ankara Na. 2	61,235,000	103	1,764,375.89
Ankara Na. 3	36,141,000	38	330,774.28
Ankara Na. 6	126,850,000	103	1,368,894.69
Ankara Na. 7	32,745,000	66	378,016.58
Ankara Na. 8	36,875,000	39	183,346.75
Ankara Na. 9	36,875,000	246	1,288,551.37
Ankara Na. 10	36,875,000	202	1,059,721.75
Ankara Na. 11	36,875,000	153	787,727.31
Ankara Na. 12	36,875,000	153	787,727.31
Ankara Na. 13	41,418,000	120	734,503.56
Ankara Na. 14	42,078,800	91	510,985.82
Ankara Na. 15	43,070,000	62	376,371.00
Ankara Na. 16	43,070,000	36	218,538.00
Jumla			**9,789,534.31**

Chanzo: *Mawasiliano ya kazi*

7.3.5 Matokeo ya Ukaguzi Hatua ya Ujenzi

a) Kipande cha Kwanza: Ushauri kwenye Kazi za Ujenzi

(i) Adhabu Kutokana na Kuchelewesha Kuwasilisha Taarifa ya Maendeleo ya Kazi kwa Kila Mwezi

Kwa mujibu wa Kifungu cha 8.9 cha Hadidu Rejea, mhandisi mshauri alitakiwa kuandaa taarifa za maendeleo ya kazi kwa kila mwezi katika kipindi cha utekelezaji mkataba. Taarifa zilitakiwa kumfikia Mwajiri sio zaidi ya siku 15 baada ya mwisho wa mwezi unaotolewa taarifa. Mapitio ya taarifa za maendeleo yalionesha kwamba, mhandisi mshauri hakuzingatia kwa ukamilifu matakwa kuhusu uwasilishaji taarifa kwa wakati na kwa ukamilifu kulingana na matakwa ya mkataba. Hii ni kwa kuwa kulikuwa na ucheleweshwaji wa taarifa ambao ulikuwa kati ya siku moja hadi 37. Nilibaini kuwa, taarifa 11 kati ya 19 za maendeleo ya kazi ya kila mwezi 19 hazikuwasilishwa kwa wakati kwa mwajiri.

Kwa mujibu wa kifungu cha 8.9 cha Hadidu Rejea, kushindwa kuwasilisha taarifa za ujumla au za kipindi cha utekelezaji wa hatua mbalimbali za mradi kwa kipindi kilichopangwa kulitarajiwa kusababisha gharama za uchelewaji ambacho ni sawa na moja ya elfu moja (1/1000) ya thamani ya mkataba wa mhandisi mshauri kwa awamu husika kikilipwa kwa kila siku ya ucheleweshaji kazi hadi kufikia 15% ya gharama ya mkataba wa mhandisi mshauri.

Nilifanya makadirio kwamba mwajiri hakukata gharama za ucheleweshaji kazi kama adhabu kwa mhandisi mshauri kiasi cha Dola za Marekani 309,200.55 ambayo ni sawa na Sh. 704,281,552.76. Kuchelewa kuwasilisha taarifa za maendeleo ya kazi kwa kila mwezi hakukumpa nafasi Mwajiri kujua maendeleo ya mradi na kufanya maamuzi kwa wakati ili kutatua masuala ambayo yangeweza kuathiri utekelezaji wa mradi.

b) Kipande cha Kwanza: Kazi za Ujenzi- Ujenzi wa Barabara

(i) Maendeleo Hafifu ya Kazi Yatokanayo na Mkandarasi

Kwa mujibu wa taarifa ya Utekelezaji namba 18 ya Maendeleo ya Kazi kwa mwezi Desemba 2020, maendeleo ya kazi za ujenzi

yanayotekelezwa na mkandarasi yalikuwa asilima tisa dhidi ya 49% kama yalivyopangwa na kusababisha kuchelewa kwa 40%. Japokuwa kumekuwa na taarifa za kumkumbusha mkandarasi kuhusu maendeleo hafifu za utekelezaji wa mradi kutoka kwa Wakala wa Barabara (TANROADS) kwenda kwa mkandarasi, bado hatua stahiki za kuunusuru mradi hazikuchukuliwa. Maendeleo hafifu ya mradi yalisababishwa na mambo yafuatayo: mkandarasi kutokuwa na utayari, mlipuko wa Ugonjwa wa Homa ya Mapafu unaosababishwa na virusi vya Korona (UVIKO-19), kusimamishwa kwa kazi ili kupisha uchunguzi dhidi ya ubora wa kazi, marekebisho ya usanifu, pamoja na kubadilisha wafanyakazi ambako kuliathiri weledi wa kazi.

(ii) Matatizo ya Ubora Kwenye Tabaka la Zege Lililojengwa Kwenye Njia ya Mabasi Yaendayo Haraka

Kwa mujibu wa michoro na miongozo ya viwango vya ubora, tabaka la zege kwa ajili ya njia ya Mabasi yaendayo haraka lilitakiwa kuwa na unene wa milimita 220, upana wa mita 3.5 kwa tabaka la saruji la kiwango C1 na tabaka lililoboreshwa la udongo kiwango cha G15. Nilibaini kwamba, barabara zilizojengwa zilikuwa na nyufa kutoka katikati ya barabara kuja pembezoni kati ya kilomita 6.40 hadi kilomita 8.910.

Wakala wa Barabara iliamua kuchunguza ili kufahamu sababu ya kukosa ubora kwa zege lililowekwa katika barabara hii. Kwa mujibu wa taarifa ya uchunguzi, sababu kuu za kasoro hizo kwenye barabara ya zege zilihusishwa na ubebaji duni wa zege kutoka kwenye sehemu inayohusika na uzalishaji hadi mahali pa kazi. Kutoka sehemu ya uzalishaji, zege lilisafirishwa kwa gari maalumu la kubebea zege mpaka sehemu ya kazi kisha lilibebwa kwa gari maalumu lenye mtambo wa kuchimbia ardhini (*excavator*) na kuweka kwenye mtambo wa kusambaza na kushindilia zege. Hivyo, taratibu za ubebaji huu wa zege ulisababisha kutengana kwa zege. Sababu nyingine zilizohusishwa na zege hilo kutoa nyufa zilijumuisha:

- Mkandarasi hakutoa kwa kiwango cha kutosha udongo wa mfinyanzi na uchafu uliotokana na masalia ya mimea katika mchanga. Hii ilisababisha idadi kubwa ya mashimo kwa juu na ndani ya barabara ya zege.

- Mkandarasi hakusimamia ipasavyo malighafi zinazotumika katika kutengeneza zege kutoka sehemu zilipokusanywa na kuhifadhiwa hadi sehemu ya kumwaga zege hilo. Hii ilisababisha mchanganyiko usiofanana wa zege ambao baadaye ukatengeneza nyufa. Uchunguzi ulibaini kwamba, mkusanyiko wa malighafi hizo za ujenzi, utengenezaji wa kokoto za saizi kubwa na ubebaji wa mara kwa mara wa zege kabla ya kulimwaga kama sababu kuu zinazohitaji zitatuliwe.

Nilibaini kuwa, aina za nyufa zilizoenea upana wote wa barabara pasipo kudhibitika na nyufa zilizozama ndani kati ya maungio ya kuruhusu kutanuka vilitokana na kuchelewa kukatwa kwa maungio (contraction joints). Hata hivyo, nilibaini kwamba, Wakala wa Barabara haukuchukua hatua kali na stahiki kwa mkandarasi licha ya matatizo ya ubora yaliyojitokeza.

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara kuchukua hatua stahiki kwa mkandarasi kwa Kipande cha kwanza kwa kazi zote zenye ubora duni alizozifanya. Pia, kuhakikisha kuwa mkandarasi anatoa mwongozo mpya wa mpango wa kufidia wakati uliopotea na kuondoa mapungufu yaliyojitokeza.

c) Kipande cha Pili: Ushauri wa Kihandisi kwenye Kazi za Majengo

(i) Wakala wa Barabara Haukupeleka Wahandisi kwa Ajili ya Mafunzo ya Vitendo Kazini kwa Mhandisi Mshauri

Kwa mujibu wa mapitio ya mafaili ya mradi, nilibaini kwamba, Wakala wa Barabara hakupeleka walau wahandisi wawili kwa mhandisi mshauri kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kazini ili kupata uzoefu wa stadi za usimamizi wa miradi. Nilibaini zaidi kwamba, TANROADS haikuweka kifungu katika makisio ya gharama za ujenzi kwa ajili ya mafunzo ya wahandisi wake. Hii ilikuwa kinyume na Kifungu cha 5.2 (xxiv) cha Hadidu za Rejea kwa ajili ya kazi za Ushauri Elekezi ambazo zilihitaji mhandisi mshauri kupanga na kutoa mafunzo ya vitendo kazini kwa wahandisi wake wenye vigezo.

Kwa sababu hii, wahandisi wa Wakala wa Barabara hawakunufaika kutoka kwenye mafunzo yaliyopangwa ambayo yalitarajiwa kujumuisha masuala yote ya usimamizi wa mikataba ya kazi za

barabara. Kwa mujibu wa mahojiano na maafisa wa Wakala wa Barabara, ofisi ilikuwa na kiwango cha chini cha rasilimali watu na hapakuwa na wahandisi waliokuwa huru kwa ajili ya kujiunga katika mafunzo ya vitendo kazini.

(ii) Mhandisi Mshauri Hakuandaa na Kuwasilisha Mwongozo wa Usimamizi wa Mradi

Mapitio ya mkataba wa mhandisi mshauri kwa ajili ya mapitio ya usanifu na usimamizi wa ujenzi wa awamu ya pili wa mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam yalibaini kwamba, Kifungu cha 5.2 (xxii) cha Hadidu Rejea kwa ajili ya kazi ya Ushauri wa Kihandisi kilimtaka mhandisi mshauri kuandaa mwongozo wa usimamizi ambao ungekuwa umeainisha hatua za kufuatwa wakati wa utekelezaji wa kazi. Uchambuzi wangu ulibaini kuwa wahandisi washauri hawakuandaa na kuwasilisha kwa Wakala wa Barabara mwongozo wa usimamizi wa mradi. Kuwapo kwa Mwongozo wa Usimamizi kungewezesha usimamizi kufanyika ipasavyo, na kutoa msingi wa mafunzo ya vitendo kazini kwa watumishi wa Wakala wa Barabara na kwa wanafunzi wote ambao wanaotembelea wakati wa utekelezaji wa mkataba wa ujenzi.

d) Kipande cha Pili: Kazi za Majengo

(i) Fremu Sita za Vituo vya Abiria Hazikujengwa Kama Michoro Ilivyoelekeza Katika Kituo cha Mabasi Kariakoo

Ziara yangu katika Kituo cha Mabasi Kariakoo ilibaini kwamba, fremu sita kwa ajili ya kituo cha mabasi hazikujengwa kama michoro ilivyoonesha kwa kubadilisha fremu aina “A” kwa kuweka aina “B”. Matokeo yake, ilisababisha malipo ya ziada ya Sh. 234,371,760. Katika ukaguzi huu sikuona maelekezo yoyote ya mhandisi kwa ajili ya mabadiliko au marekebisho. Kuchepuka kutoka kwenye michoro ya kihandisi ilitokana na usimamizi na ukaguzi duni uliofanywa na mhandisi mshauri wakati wa ujenzi na uwekaji wa fremu. Baada ya kubaini malipo ya ziada yalifanyika, mhandisi mshauri aliamua kurejesha malipo yaliyozidi kwa kupunguza fedha hizo katika malipo ya mkandarasi.

Kwa mujibu wa cheti cha malipo Na. 8 ambayo kilitolewa tarehe 22 Desemba, 2020, sehemu ya malipo ya ziada katika fremu aina “A” yalipunguzwa kutoka kwenye hati hii ya malipo. Hivyo,

malipo ya ziada yaliyobaki kwa ajili ya fremu aina “A” ni Sh. 103,477,920.

(ii) Nguzo za Kituo cha Mabasi Kariakoo Zilikuwa Fupi Kuliko Kimo cha Usanifu, Hivyo Kusababisha Malipo ya Ziada ya Sh. Milioni 91.14

Ziara yangu ya ukaguzi katika kituo cha mabasi Kariakoo ilibaini kuwa nguzo zilizojengwa zilikuwa fupi kuliko kimo kilichotakiwa kwenye michoro ya usanifu na michoro ya kina. Kwa mujibu wa mchoro namba T497-BRT L2-KRK-TSA-ST-06 wa kituo cha mabasi kwa ajili ya fremu aina A, nguzo zilitakiwa kuwa na vipimo ya sehemu mkato vya 200mm x 20mm x 52 mm na kimo cha 5,305 mm. Hata hivyo, matokeo ya vipimo vya pamoja yalionesha kwamba, nguzo zilikuwa na urefu wa 3,700 mm ambayo inaonesha tofauti ya 1,605 mm.

Kwa mujibu wa makisio ya gharama za ujenzi, nguzo yenye urefu wa 5305 mm ilitakiwa kuuzwa kwa Sh. 3,586,180 ambayo ni sawa na Sh. 676,000 kwa urefu wa mita moja. Hii inamaanisha kwamba, urefu wa 1,605 mm unaopungua, sawa na Sh. 1,084,980 kwa nguzo moja, ambayo ni sawa na Sh. 15,189,720 kwa kituo kimoja kilichokamilika. Hii ilisababisha malipo ya ziada jumla ya Sh. 91,138,320 kwa vituo vyote sita vya mabasi yaendayo haraka ndani ya kituo cha Kariakoo. Wakati wa ukaguzi huu, ilibainika kwamba Wakala wa Barabara ulizungumzia kurudisha kiasi kilichozidi. Kwa mujibu wa cheti cha malipo namba nane kilichotolewa tarehe 22 Desemba, 2020, kulikuwa na marekebisho kwenye malipo kwa kurejesha fedha za malipo ya ziada yaliyofanywa kwenye cheti za malipo namba nne kwa kupunguza Sh. 83,430,816 kati ya Sh. 91,138,320. Hii humaanisha kwamba kiasi kilichobaki kurejeshwa ni Sh. 7,707,704.

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara kukata tozo ya kuchelewesha kazi pamoja na kulipa malipo yaliyozidishwa kwa mhandisi mshauri.

7.3.6 Matokeo ya Ukaguzi kwenye Masuala ya Usimamizi wa Udhibiti Ubora

a) Kipande cha Kwanza: Kazi za Ujenzi wa Barabara

(i) Kifusi cha Udongo Uliorundikwa Haukukidhi Viwango vya Ubora

Kipimo cha ubora kwa ajili ya kutambua uwezo wa udongo kuhimili uzito (*California Bearing Ratio, CBR*) kilifanyika ili kutafuta uhusiano kati ya kiasi cha unyevu kilichopo, tungamo na uimara wa udongo (CBR) kwa udongo uliokusanywa sehemu moja. Matokeo haya yalionesha kwamba, kipimo cha uimara ya kifusi hiki ulikuwa ndani ya kiwango kinachokubalika cha chini ya asilimia moja, lakini uimara wa kifusi hiki ulishuka toka asilimia 95% mpaka 25% baada ya kuwekwa kwenye maji kwa siku nne. Matumizi ya udongo wenye kiwango pungufu cha uimara chini ya 25% huleta madhara kwenye uimara wa tabaka la udongo lenye kuchanganywa na saruji hivyo tabaka hilo halitoweza kuhimili mzigo utakaopita juu yake.

(ii) Sampuli Nne za Udongo Hazikukidhi Kiwango cha Kipimo cha Uimara wa Tabaka la Udongo Lililochanganywa na Saruji na Kushindiliwa (*Unconfined Compressive Strength*)

Nilichukua sampuli za tabaka la udongo uliochanganywa na saruji kwa ajili ya kutathmini uimara wa tabaka hilo kuona kama lilikidhi viwango. Kwa mujibu wa viwango vya ubora, kipimo cha kila sampuli kilitakiwa kisipungue 90% ya kiwango cha chini kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 3802/2 la kwenye Mwongozo wa Viwango vya Ubora wa Barabara wa mwaka 2000 (yaani, kiwango kisipungue 0.9 Mpa). Hata hivyo, sampuli nne kati ya 20 zilizofanyiwa vipimo zilikuwa na matokeo yenye kiwango pungufu ya 0.9 Mpa.

Sababu za kuwa na kiwango pungufu kwa maeneo hayo yaliyochukuliwa sampuli ni pamoja na kutumika kwa barabara pasipo ruhusa kutoka kwa wakala wa Barabara, na kuwa wazi kwa tabala la barabara lililochanganywa udongo na saruji pasipo kufunikwa. Sehemu zilizokuwa na kiwango pungufu huenda zikasababisha uimara kulingana na matumizi yaliyokusudiwa ya barabara husika.

(iii) Tabaka la Udongo Uliochanganywa na Saruji Lilikuwa na Kiwango kidogo cha Ushindiliaji

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Viwango vya Ubora wa Kazi za Barabara wa Mwaka 2000, kiwango cha chini cha tungamo la

udongo uliochanganywa na saruji barabarani (C1) kinatakiwa kuwa 95% (*95% BS Heavy*). Ilibainika kwamba, sehemu 9 kati ya 23 zilizopimwa zilikuwa na matokeo yaliyo chini ya viwango vya ubora wa barabara kwani kiwango cha ushindiliaji wa hizo sehemu ulikuwa chini kwa asilimia 83 hadi 94.

Hali ya sehemu hizo kuwa na matokeo ya chini ya kiwango cha ushindiliaji huenda ikawa imesababishwa na magari kupita pasipo kuruhusiwa kwa sababu ya sehemu hiyo kuachwa wazi.

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara kuhakikisha kuwa mkandarasi anasahihisha sehemu ambazo hazikufikia viwango vinavyohitajika kabla ya kuweka lami ngumu kwenye tabaka lililoimarika na kuhakikisha kuwa tabaka hilo linakingwa ili kuepusha hatari ya watumia barabara kupita na kuharibu ubora wa tabaka hilo.

7.3.7 Matokeo ya Ukaguzi kwenye Usimamizi wa Rasilimali Watu

a) Kipande cha Kwanza: Huduma za Ushauri kwenye Kazi za Barabara

(i) Wasimamizi Wawili Walikuwa Wakifanya Kazi Bila Kibali cha Kazi

Mapitio ya vibali vya kazi yalionesha kwamba, wafanyakazi wanne kati ya sita ni wa kigeni; na mmoja wao, aliyeshika nafasi ya Mhandisi Mkazi, hakuwa na kibali cha kazi. Pia, mfanyakazi Mhandisi Ujenzi alikuwa na kibali kilichokwisha muda wake wa matumizi ulioidhinishwa.

Mahojiano yaliyofanywa na afisa wa mkandarasi yalibainisha kuwa, Mhandisi Mkazi hakuwasilisha vyeti vya masomo ya chuo kikuu na elimu ya sekondari kwenda Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kwa ajili ya uhakiki. Kushindikana kuwasilisha nyaraka hizo kwa Tume ya Vyuo Vikuu kulisababishwa na ugumu wa mawasilano kutoka nchini kwake kwa sababu ya mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Korona (UVIKO-19). Kukosa kibali cha kazi kwa Mhandisi Mkazi huenda kukawa na athari katika utekelezaji wa mradi, kwani Mhandisi Mkazi huenda akakosa vigezo vinavyohitajika kwa ajili ya kazi.

(ii) Leseni za Wahandisi Zilizotolewa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi kwa Wafanyakazi Watatu wa Kigeni kwa Mhandisi Mshauri Ziliisha Muda Wake

Kifungu cha 6.1 cha Mkataba wa mhandisi mshauri kinamtaka mhandisi mshauri kuweka wasimamizi wa ngazi ya juu wenye sifa stahiki ili kukidhi malengo ya usimamizi wa mradi. Hata hivyo, mapitio ya sifa za kielimu na usajili wa kitaalamu yalionesha kwamba wasimamizi wa ngazi ya juu walikidhi kiwango cha chini kilichotakiwa kwa ajili ya usimamizi wa mradi. Nilibaini kwamba, wasimamizi wa ngazi ya juu walikuwa na sifa za kielimu, uzoefu na usajili wa bodi za kitaalamu kwa ajili ya usimamizi wa miradi. Hata hivyo, leseni za wahandisi wasimamizi watatu ngazi ya juu wa kigeni zilikuwa zimeisha muda wake.

b) Kipande cha Kwanza: Kazi za Ujenzi wa Barabara

(i) Wafanyakazi Wawili Walikuwa Wakifanya Kazi Pasipo Kukamilisha Vibali vya Kazi

Kwa mujibu wa Sheria Na. 1 ya Wahamiaji (Kanuni za Ajira), ya mwaka 2015 inaleza kuwa "Mhamiaji haruhusiwi kujihusisha katika ajira yoyote kwa ajili ya kupata ujira, faida au pasipo faida isipokuwa tu awe ana kibali cha kazi ambacho kinamruhusu kujihusisha na ajira iliyoainishwa katika vibali vya kazi vinavyotumika".

Nilitembelea ofisi ya mkandarasi (M/S Sinohydro Corporation Ltd) tarehe 31 Desemba 2020 na kupitia Vibali vya Kazi Daraja C (Kwa ajili ya watumishi wa makampuni). Nilikagua uhalali wa vibali kwa kila mfanyakazi wa ngazi ya juu katika mradi na kubaini kwamba, wafanyakazi walikuwa wakifanya kazi pasipo kukamilisha vizuri taratibu za vibali vya kazi.

Nilibaini kwamba, nafasi za wasimamizi 11 kati ya 12 zilikuwa za kigeni wakati nafasi iliyobaki (Afisa Usalama, Jamii na Mazingira) ilikuwa ya Mtanzania. Nilibaini kuwa, kati ya wafanyakazi 11 wa ngazi ya juu, sita walikuwa na vibali vya kazi vilivyo halali, na wapo kwenye mradi; wafanyakazi watatu walikuwa na vibali vya kazi vilivyo halali lakini walikuwa likizo; na wafanyakazi wawili hawakuwa na vibali. Nilifahamishwa kuwa, vibali vya wafanyakazi wawili ambao hawakuwa na vibali vya kazi vilikuwa kwenye

mchakato wa maombi ya vibali na wafanyakazi hao walikuwa likizo.

(ii) Wafanyakazi Tisa wa Kampuni ya Sinohydro Hawakuwa Wamesajiliwa na Bodi za Kitaalamu za Tanzania

Nilipitia sifa za kielimu na usajili wa bodi za kitaalamu kwa wafanyakazi wa ngazi ya juu waliobadilishwa na kubaini kuwa, sio wafanyakazi wote walisajiliwa na bodi ya kitaalamu ambayo ni Bodi ya Wahandisi (ERB). Nilibaini kwamba, wafanyakazi 11 kati ya 12 walikuwa wa kigeni na mmoja alikuwa Mtanzania. Kati ya wafanyakazi 11 ambao walikuwa wa kigeni, watatu walikuwa na usajili ulio halali wa bodi za kitaalamu, wanane hawakuwa wamesajiliwa na bodi za kitaalamu za Kitanzania. Pia, mfanyakazi Mtanzania hakuwa na usajili wa bodi ya kitaalamu.

Kukosa usajili na bodi ya kitaalamu ya Kitanzania hakutoi uhakika kwa serikali kwamba mradi unakuwa katika mikono ya wataalamu ambao wako vizuri kwa kazi. Pia, hakutoi uhakika wa ubora wa kazi zilizofanyika.

c) Kipande cha Pili: Kazi za Majengo

(i) Wafanyakazi wa Ngazi ya Juu Wanne Walikuwa Wakifanya Kazi Bila Vibali vya Kazi

Nilitembelea ofisi ya mkandarasi tarehe 31 Desemba, 2020 na kupitia Vibali vya Kazi Daraja C (Kwa watumishi wa Makampuni) na kuangalia uhalisi wao kwa kila mfanyakazi katika mradi. Nilibaini kwamba, kulikuwa na wafanyakazi waliokuwa wakifanya kazi angali vibali vyao vya kazi vimekwisha muda.

Nilibaini kuwa wafanyakazi wanne kati ya sita wa kigeni hawakuwa na vibali vya kazi. Kukosekana kwa vibali vya kazi kwa wafanyakazi wageni ni uvunjifu wa sheria za nchi na kuondoa haki za wafanyakazi kupata huduma muhimu kusaidia maisha ya wafanyakazi kama vile kufungua akaunti ya benki na huduma za kiafya.

(ii) Si Wafanyakazi Wote Walikuwa na Sifa za Kielimu na Kitaalamu za Kiwango cha Juu au Zilizofanana Katika Mkataba Uliosainiwa

Mkataba wa Ujenzi ulimtaka mkandarasi kuwa na wafanyakazi wenye vigezo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Zaidi, mkataba ulitaka endapo kuna mabadiliko ya wafanyakazi, wafanyakazi wapya sharti wawe na vigezo vinavyofanana au vilivyozidi ya vile vilivyoanishwa kwenye mkataba.

Mapitio ya taarifa za maendeleo ya kazi kwa kila mwezi na mawasiliano ya mradi yalionesha kwamba, wafanyakazi wote walioorodheshwa katika mkataba uliosainiwa walibadilishwa wakati wa utekelezaji wa mradi na kuajiri wafanyakazi wapya kushika nafasi zao.

Nilipitia sifa za kielimu na usajili katika bodi za kitaalamu kwa wafanyakazi wapya ili kutathmini kama walikuwa na vigezo vilivyotakiwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Nilibaini kwamba, sio wafanyakazi wote wapya walisajiliwa na bodi za kitaalamu ambazo ni Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) na Bodi ya Usajili wa Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Ujenzi (AQRB). Nilibaini kwamba, wafanyakazi wa kigeni sita hawakukidhi vigezo vya chini vilivyotakiwa. Mfanyakazi wa kigeni mmoja hakuwasilisha vyeti vya elimu na vigezo vya kitaalamu kwani aliwasilisha wasifu tu (CV), hivyo hakukuwa na uhakika kama anafaa kwa nafasi hiyo.

Kwa wafanyakazi wawili wa Kitanzania, mmoja (Mhandisi) alikidhi vigezo vya chini vilivyowekwa. Hata hivyo, leseni ya kihandisi iliisha muda wake tarehe 3 Desemba, 2020, wakati mfanyakazi mwingine alikuwa na sifa za elimu zilizohitajika, lakini usajili na bodi ya kitaalamu bado ulikuwa kwenye mchakato. Kukosekana kwa vigezo kamili (vya kielimu na usajili wa bodi za kitaalamu) hakutoi uhakika wa kutosha kwa mfanyakazi kufaa katika nafasi hiyo. Hii inaweza kuathiri ubora wa kazi itakayofanywa na mfanyakazi husika.

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara kuhakikisha;
(a) Wafanyakazi raia wa kigeni wanaosimamia miradi ya ujenzi nchini wana vyeti sahihi na wanamiliki vibali halali vya kufanya kazi. Hii ni pamoja na kuwasiliana na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ili kutatua changamoto zinazokabili maombi ya vibali vya kufanya kazi na wafanyakazi muhimu;

na (b) wafanyakazi wote muhimu wana sifa zinazohitajika za kielimu, usajili wa bodi za kitaalam na wanamiliki leseni halali ya kufanya kazi.

7.3.8 Afya, Usalama na Mazingira

Mpango wa Usimamizi wa Mazingira haukukaguliwa kiasi cha kutosha kuendana na Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Masuala ya Kijamii (ESMP)

Kifungu cha 1.2 cha Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Masuala ya Kijamii (ESMP) kinahitaji ukaguzi wa mazingira kwa mradi kwa vipindi ili kutambua mapungufu yoyote katika utendaji kimazingira na kushauri hatua za kuchukuliwa kutatua masuala hayo. Mpango wa usimamizi mazingira ulitaka ukaguzi ufanyike kila baada ya miezi sita. Pia, Kifungu cha 1.2 cha Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Masuala ya Kijamii kilimtaka mkandarasi kuandaa taarifa za mazingira kwa kila mwezi ambayo itaelezea kwa kifupi masuala yalivyofanyiwa kazi kutoka kwa taarifa iliyopita ili kuonesha kama masuala haya yalikuwa yametatuliwa au yalikuwa yakiendelea na pia kuonesha masuala mapya yakiibuka.

Nlibaini kuwa, kutoka mwanzo wa mradi hadi wakati ukaguzi huu ukifanyika ni taarifa moja tu ya ukaguzi wa mazingira ya mwezi Desemba 2020 ililetwa kwa ukaguzi. Kukosekana kwa taarifa za ukaguzi wa mazingira kwa vipindi vilivyopita kulimzuia mwajiri kuwa na taarifa kuhusu ubora wa mazingira ya mradi, hususani uchafuzi wa maji na udhibiti, uchafuzi wa hewa, usimamizi wa taka ngumu na masuala ya usalama kama vile udhibiti wa ajali, nakadhalika.

Ninashauri Menejimenti ya Wakala wa Barabara kuimarisha utaratibu wa usimamizi wa mkataba ili kuhakikisha kuwa mradi unazingatia ratiba iliyoidhinishwa ya Kazi. Pia, kuhakikisha Mpango wa Usimamizi wa Mazingira unatekelezwa. Zaidi, kuhakikisha nyaraka zote za Mkataba zimeandikwa vizuri.

SURA YA NANE

UPANUZI WA BARABARA YA MOROGORO KIPANDE CHA (KIMARA-KIBAHA)

8.1 Utangulizi

Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) anatekeleza mradi wa Upanuzi wa Barabara ya Morogoro unaotegemea kupunguza muda wa kusafiri kutoka masaa matatu hadi dakika 30 kati ya Kibaha mpaka Kimara. Upanuzi huu utaongeza moja kwa moja na kuboresha mwendo wa magari; hivyo, kupunguza vikwazo vya foleni kwenye maeneo muhimu yenye shughuli nyingi za kiuchumi.

Wakala wa Barabara Tanzania aliingia mkataba wa miezi 30 tarehe 13 Julai, 2018. Gharama ya mkataba wa mradi huu ilikuwa shilingi za Tanzania bilioni 140.45, na unafadhiliwa moja kwa moja na Serikali ya Tanzania. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya Ujenzi ya Estim na kusimamiwa na Kitengo Cha Ushauri wa Kihandisi cha TANROADS (TECU).

8.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi

Lengo la ukaguzi huu ilikuwa ni kutathmini mchakato na utelekelezaji wa mradi. Ukaguzi uliangalia ukamilifu wa usanifu wa mradi na nyaraka za zabuni, michakato wa manunuzi, vigezo na michoro, ubora wa kazi za ujenzi zilizofanyika, udhibiti wa gharama, usimamizi wa muda na hali halisi ya utekelezaji wa mradi kwa ujumla wake. Mawanda ya mradi ni kujega kilometa 19.2 njia nane za magari pamoja na madaraja sita, makalavati 36, daraja la juu moja, mitaro ya kando kando ya barabara na Miundombinu mingine ya uchukuzi na vituo vya mabasi na maegesho ya magari.

8.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi kupitia vipengele vifuatavyo: upangaji, usanifu na uandaaji nyaraka za zabuni, mchakato wa manunuzi, usimamizi wa mikataba, hatua za ujenzi, usimamizi wa fedha, udhibiti wa ubora, na usimamizi wa rasilimali watu.

8.3.1 Matokeo Ukaguzi Kwenye Maeneo Yanayohusu Mipango, Usanifu na Uandaaji wa Nyaraka za Zabuni

a) Kuanzishwa kwa Kituo Kipya cha Basi Huko Mbezi-Mwisho Hakukujumuishwa Katika Muundo na Usanifu wa Mradi Huu kwa Hivyo Kuna Uwezekano wa Kuongeza Msongamano Katika Makutano Wakati wa Utekeleazaji Wake

Kulingana na mahojiano na maafisa wa Wakala wa Barabara na jinsi tulivyoona kwenye eneo la mradi, nilibaini kuwa mradi wa Upanuzi Barabara ya Morogoro haupo kwenye mwelekeo wa kufikia malengo yake ya kupunguza msongamano wa vyombo vya usafiri kutokana na ujenzi wa kituo cha Mabasi cha Mbezi Mwisho. Ujenzi huu ulianzishwa wakati mradi wa upanuzi unaendelea. Kwa hivyo, kituo cha mabasi hakikujumuishwa katika mpango na usanifu wa mradi huu. Zaidi ya hayo, uendeshaji wa kituo cha mabasi mbali na kusababisha msongamano wa magari unaweza kusababisha changamoto zaidi kwenye makutano yanayoingia barabara ya Morogoro. Kituo hiki cha mabasi kinatarajiwa kuhudumia mabasi 700 kila siku. Wakati, Wakala wa Barabara ulikua unaandaa mikakati ya upanuzi wa barabara ya Morogoro, TAMISEMI nao, kupitia Mamlaka za Manispaa ya Jiji la Dar es Salaam, zilikuwa pia zikipanga mikakati ya ujenzi wa kituo cha Mabasi huko Mbezi-Mwisho. Mipango hii miwili ilifanywa bila ushirikiano kati ya taasisi hizi za serikali. Ukosefu wa mpango mkuu jumuishi wa kisekta baina ya taasisi za umma ndio chanzo kikuu cha tatizo hili.

b) Makadirio ya Gharama Hayakuakisi Uhalisi

Kulingana na Kanuni za 69 (5), (6) na 238 ya 2013 za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 Wakala wa Barabara Tanzania anatakiwa kuandaa makadirio ya mahitaji kulingana na bei za soko na fedha zilizopo. Hata hivyo, nilibaini kuwa makadirio ya gharama ya mradi huo hayakuakisi hali halisi ya mahitaji ya mradi.

Mapitio yangu ya mahitaji ya mwajiri na kabrasha la zabuni nilibaini kuwa vitu muhimu vilikuwa na makadirio ya chini. Mfano wa vitu hivi ni pamoja na: fidia ya ardhi; ujenzi wa ofisi ya mhandisi; gharama ya udhibiti wa VVU/UKIMWI na magonjwa ya zinaa na gharama ya kuhamisha miundombinu ya utoaji huduma kama nguzo za umeme, mabomba ya maji n.k. Kwa kuwa mambo

haya ni muhimu, wakati mradi ukiwa unaendelea, yalijumuishwa kwa uhalisia na hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za mradi. Mifano ya masuala ambavyo yaliyokuwa yamekadiriwa bajeti ndogo ni:

- Jumla ya Sh. milioni 10 ilitengwa kwa ajili ya kampeni ya kupinga maambukizi ya VVU wakati gharama halisi ilikuwa zaidi ya Sh. milioni 100; na
- Jumla ya Sh. milioni 200 zilikadiriwa kwa ajili ya uhamishaji wa miundombinu mbalimbali, wakati gharama halisi ilikuwa zaidi ya Sh. bilioni sita.

c) Vigezo Muhimu vya Kufuzu ili Kushinda Zabuni Viliondolewa Kwenye Nyaraka ya Tahmini ya Zabuni

Mapitio ya nyaraka za zabuni yalionesha kuwa, taarifa muhimu kuhusu vigezo vya kufuzu ili mkandarasi aweze kushinda zabuni viliondolewa kwenye nyaraka ya tathmini ya zabuni. Hii ilikiuka Kanuni ya 184 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 ambayo inaitaka taasisi nunuzi kuandaa nyaraka za zabuni ambazo zina vigezo vyote muhimu vya kuwawezesha wazabuni wanaotarajia kuwasilisha zabuni zao. Taarifa zilizokosekana ni pamoja na uzoefu wa mkandarasi, vifaa, sifa na uzoefu wa wafanyakazi muhimu, kiwango cha mapato kwa mwaka, pamoja na uwezo wa kifedha wa mzabuni. Mapungufu haya kwa sehemu yalisababishwa na kukosekana kwa umakini katika kuhakiki nyaraka za zabuni wakati zilipotengenezwa kwa mara ya kwanza. Ukosefu huu ulisababisha ugumu kwa timu ya tathmini kutathmini uwezo wa mkandarasi.

Ninashauri menejimenti kuendeleza utaratibu na mipango ya kuimarisha mchakato wa ukaguzi wa ubora wa mipango, muundo na hati za zabuni ili kuhakikisha kufuata matakwa.

8.3.2 Matokeo ya Ukaguzi Kwenye Vipengele vya Manunuzi

a) Mapungufu Yaliyobainika Kuhusiana na Maswala ya Manunuzi

Ukaguzi wangu ulibaini mapungufu kadhaa yanayohusiana na kutotekeleza masharti ya Sheria ya Manunuzi na kanuni zake kama ifuatavyo:

(i) Bajeti ya zabuni ya mradi huu ilikuwa Sh. bilioni 170. Kiasi hiki kinahitaji utaratibu wa manunuzi wa zabuni wa ushindani wa kimataifa (ICT). Hata hivyo, utaratibu wa manunuzi uliotumika ni

wa Zabuni ya Ushindani wa Kitaifa (NCT) ambao ukomo wake ni wa zabuni zenye thamani ya hadi Sh. bilioni 15. Hii ni kinyume na Kanuni ya 151(2) (c) ya Kanunuzi za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016). Kushindwa kutumia zabuni ya ushindani wa kimataifa kunanyima Serikali faida ya kupata ushiriki mpana wa zabuni ambao ni pamoja na kupata bei ya ushindani na fursa ya kupata teknolojia mpya kutoka kwa wazabuni wa nje.

(ii) Kulingana na nyaraka za manunuzi zilizopitiwa, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) haukutoa Tangazo la Manunuzi ya Jumla (GPN) wakati wa mwaka wa fedha 2017/18. Maafisa wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) walithibitisha kuwa, hii ilisababishwa na hali ya dharura ya mradi huo na kipindi kifupi cha manunuzi. Kwa hiyo, taarifa juu ya zabuni haikuwa kwenye Tangazo la Manunuzi ya Jumla (GPN). Sikupata nyaraka zozote za kuonyesha kuwa manunuzi haya yalikuwa ya dharura, ambayo yangeweza kufuata taratibu za manunuzi ya dharura. Kushindwa kutoa Tangazo la Manunuzi ya Jumla (GPN) kungepelekea kuathiri ushindani.

(iii) Mapitio ya kifungu cha tatu (b) cha muhtasari wa kikao cha mazungumzo ya kukubaliana na gharama za mkataba yalionyesha kuwa Wakala wa Barabara Tanzania ulibadilisha kiwango cha riba kutoka kiwango cha riba wakati wa kusaini mkataba hadi kiwango cha riba cha Benki Kuu ya Tanzania (BoT). Marekebisho haya ni kinyume na Kanuni ya 183 (4) ya Kanununi za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016) ambayo inasema kwamba mabadiliko yoyote katika nyaraka za zabuni za kawaida yatafanyika tu kupitia karatasi za data za zabuni, au kupitia masharti maalumu ya mkataba. Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) haukuangalia vya kutosha ili kufuata kanuni hii wakati wa mazungumzo ya mapatano. Kwa sababu hiyo, mabadiliko yanaweza kusababisha ukosefu wa haki kwa washindani wengine.

Nashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara: (a) Iboreshe usimamizi wa mfumo wa manunuzi kwa kuhakikisha nyaraka zote zinapitiwa kwa kina kabla ya kupelekwe kwenye hatua nyingine za maamuzi; na (b) Irekebishe kiwango cha riba ili kilingane na kiwango kilichotumika wakati wa kusaini mkataba.

b) Manunuzi ya Huduma Bila Kushindanisha ya Sh. 100,370,800

Manunuzi ya mzabuni wa kutoa huduma kwa ajili ya uzinduzi na uwekaji rasmi wa Jiwe la Msingi la Mradi haukuwa na ushindani. Hii ni kwa kuwa, mzabuni mmoja tu ndiye aliyealikwa kuwasilisha zabuni. Hata hivyo, iligundulika kuwa huduma aliyotoa haikuwa maalumu kiasi cha kutumia manunuzi ya mzabuni mmoja. Manunuzi hayo yalifikia Sh. 100,370,800 ambayo yalilipwa kupitia Hati ya ya Malipo Na. PV-00005337 ya tarehe 19 Februari, 2019. Kwa upande mwingine, ilibainika kuwa manunuzi haya hayakuwa na idhini kutoka kwa Bodi ya Zabuni ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Ukosefu wa kuruhusu ushindani unaweza kufanya gharama ya kupata huduma au bidhaa kwa bei ya ghali kama ingetumiwa njia ya ushindani.

Ninashauri menejimenti kutumia njia sahihi ya kuchagua mzabuni na kufuata mchakato wa tathmini na utoaji wa mkataba na kuhakikisha kuwa usimamizi na ukaguzi unaimarishwa ili kupata huduma na bidhaa vinavyokidhi ushindani wa vigezo vilivyoanishwa kwenye mkataba.

8.3.3 Matokeo ya Ukaguzi Kuhusu Usimamizi wa Fedha

a) Posho na Mishahara Iliyolipwa Ilizidi Bajeti Iliyoidhinishwa kwa Sh. 252,798,980

Kulingana na mapitio ya bajeti, bajeti iliyoidhinishwa kwa mishahara na posho za usimamizi wa mradi huu ilikuwa Sh. 1,110,350,000[16] kwa kipindi cha tarehe 21 Julai 2018 hadi 21 Januari 2021. Hata hivyo, ukaguzi wa hati za malipo na nyaraka zinazoambatana nazo, malipo ya posho na mishahara yalizidi kiwango cha bajeti kilichoidhinishwa ambacho ni Sh. 252,798,980 ambayo ilikuwa karibu asilimia 23 ya bajeti. Hii ni ishara ya kwamba kulikuwa na mapungufu katika udhibiti wa ndani ambao pia unaweza kuonyesha bajeti isiyo ya uhalisi. Kwa sababu hii, shughuli zinazogharimu Sh. 252,798,980 zinaweza kuathiriwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

[16] Barua yenye Kumb Na. TRD/D/R.043/VOL.V/89 ya tarehe 3 Septemba 2018

Ninashauri menejimenti kuboresha mpango wake na bajeti ili kuhakikisha makadirio sahihi ya mahitaji ya bidhaa, huduma na kazi ili kupunguza tofauti wakati wa utekelezaji wa mpango wa kazi

b) Malipo Yaliyocheleweshwa Kupelekea Malipo ya Riba ya Jumla ya Sh. 304,244,580.35

Nilibaini kuwa malipo kwa Mkandarasi yalicheleweshwa. Hii ilikuwa kinyume na Kifungu cha 14.7 (a) cha Masharti ya Jumla ya mkataba, ambacho kinamtaka mwajiri kumlipa mkandarasi kiasi kilichothibitishwa na meneja wa mradi ndani ya siku 56 baada ya meneja wa mradi kupokea taarifa na nyaraka zinazoambatishwa kama vithibitisho. Zaidi ya hayo, Kifungu cha 14.8 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba na Kifungu cha III (b) cha Muhtasari wa Kikao cha Majadiliano ya Makubaliano ya Mkataba kilielezea kwamba ikiwa Mwajiri atafanya malipo kwa kuchelewa, mkandarasi atalipwa riba katika malipo mengine yanayofuatia. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa ucheleweshaji wa malipo ulikuwa kati ya siku 2 hadi 72 kwa ucheleweshwaji wa wastani wa siku 32 na hivyo kupelekea malipo ya riba ya jumla ya Sh. 304,244,580.35 hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2020. Ucheleweshaji wa malipo unapelekea kuathiri mtiririko wa fedha wa mkandarasi na inaweza kusababisha kuchelewesha kukamilika kwa mradi na kuongezeka kwa gharama ya mradi kwa sababu ya malipo ya riba.

Ninaishauri menejimenti ya Wakala wa Barabara kuhakikisha inafanya maombi ya fedha kwa wakati kutoka kwa Wizara ya Fedha na Mipango na ufuatiliaji wa karibu ili kuharakisha mchakato wa kupatiwa idhini ya malipo ili kuepusha upotezaji wa fedha za umma zinazotokana na tozo ya riba kwa kuchelewesha malipo.

8.3.4 Masuala ya Udhibiti wa Ubora

Sehemu hii inaelezea matokeo juu ya masuala ya ubora wa kiufundi ikiwemo usanifu, majaribio ya matokeo ya upimaji wa kazi, ukaguzi wa eneo la mradi ambao umejikita katika mambo maalum yafuatayo: upangaji na usanifu wa kihandisi ulioidhinishwa kuendana na mahitaji ya mwajiri, kuhakiki kazi iliyofanyika eneo la mradi kufuatana na uhalisia, pamoja na na masuala ya kudhibiti ubora.

a) **Unene wa Tabaka la Lami Ulifuata Vipimo**

Ili kupima ubora wa tabaka la lami, wakati wa ukaguzi nilikata tabaka la lami katika maeneo kumi ndani ya barabara ambapo vipande vya lami vyenye kipenyo cha milimita 150 vilichukuliwa kupimwa. Matokeo yalionyesha kuwa unene wa wastani wa vipande vyote ulikuwa milimita 53.4 ambayo ni zaidi ya ulioainishwa kwenye michoro na usanifu (milimita 50), na wastani wa ujazo wa lami kutoka katika kipande cha tabaka lami ulikuwa asilimia 5.6. Vigezo hivi vilizingatia Usanifu na vipimo vilivyoidhinishwa.

b) **Maabara ya Mkandarasi Haikuwa na Vifaa vya Kutosha**

Kifungu SS.1305 cha Vipimo Maalum vya mkataba kilihitaji mkandarasi kuwa na maabara yake binafsi wakati wote wa kipindi cha mkataba. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi maabara ya mkandarasi haikuwa na vifaa vya kufanyia vipimo vilivyoainishwa kwenye mkataba. Matokeo yake, vipimo vyote vya Mkandarasi vilifanywa katika Maabara ya Mhandisi Mshauri wa mradi ambaye ni TECU. Hii itapelekea vifaa vya maabara vya TECU kuchakaa mapema na kuongeza gharama zaidi ya matengenezo kwa mwajiri.

c) **Ukosefu wa Idhini ya Bodi ya Zabuni Kuruhusu Ujenzi wa Aina Nyingine ya Tabaka za Lami**

Matabaka ya lami yaliyobainishwa katika taarifa kamili ya usanifu hayakuzingatia Mahitaji ya Mwajiri. Hii ni kwa sababu Mahitaji ya Mwajiri yalihitaji zege la lami aina ya "Asphalt Concrete", lakini usanifu wa mwisho ulibainisha zege la lami aina ya "Stone Mastic" Asphalt kwa tabaka la mwisho. Sikupata nyaraka zinazoonyesha idhini ya Bodi ya Zabuni juu ya mabadiliko haya ya usanifu. Licha ya kushindwa kupata idhini ya Bodi ya Zabuni, nilibaini kuwa kuanzishwa kwa aina hii ya zege ya "Stone Mastic" ulikuwa uamuzi wa busara kwa kuwa aina hii inaleta ufanisi zaidi katika ujenzi wa barabara. Hii ni kulingana na uzoefu, kwani zege aina ya "asphalt Concrete" ilionyesha kutofanya vizuri katika barabara nyingi zilizojengwa.

d) **Sh. Milioni 185 Zililipwa kwa Ajili ya Jengo la Muda Mfupi Liliojengwa kwa Ajili ya Ofisi ya Mhandisi**

Ukaguzi umebaini kwamba, Mkandarasi alijenga jengo la muda la ofisi ya Mhandisi lakini alilipwa Sh. milioni 185 ambayo ni asilimia 50 ya gharama za ujenzi. Hata hivyo, Wakala wa Barabara (TANROADS) ililipa kiasi hiki bila kufanya tathmini yoyote ya gharama halisi. Kwa kufanya hivi, hawakufuata matakwa ya Mwajiri. Kulingana na kifungu SS.1404.01 kichohusiana na viwango maalum vinavyotakiwa kimkataba, jengo la ofisi ya mhandisi lilitakiwa kuwa na vyumba vifuatavyo: ofisi tano za mtu mmoja mmoja, chumba kimoja cha mkutano, ofisi nne za watu wawili wawili na vyumba viwili vya stoo. Pia, jengo hilo linapaswa kuwa la kudumu na urefu wa ndani kuwa mita 2.8. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi, vipimo vilichukuliwa ili kujua kama utekelezaji ulifuata mkataba. Matokeo yalionesha kuwa, upangaji wa vyumba vya ofisi ya Mhandisi haukuzingatia mahitaji ya Mwajiri. Pia, urefu wa ndani ulikuwa ni mita 2.4 badala ya mita 2.8. kwa vyumba vyote. Hivyo, urefu wa vyuma haukukidhi viwango.

Nashauri Wakala wa Barabara kupata uthibitisho wa gharama wa kujenga jengo la ofisi ya mhandisi kutoka kwa mkandarasi na kumtaka arejeshe fedha zote ambazo hazikutumika katika kazi hii.

8.3.5 Matokeo ya Ukaguzi Kwenye Vipengele Vinavyohusu Afya, Usalama na Mazingira

a) Tathmini ya Athari za Mazingira Haikufanyika

Ukaguzi umebaini kuwa, Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) haikufanywa kulingana na Kifungu cha 81 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004. Sheria hii inahitaji tathmini hiyo ifanyike na kupitishwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kabla ya mradi kuanza. Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) haukupanga muda wa kutosha kwa ajili ya kufanya Tathmini ya Kina ya Athari za Mazingira, kwani shughuli za ujenzi zilihitajika kuanza ndani ya muda mfupi. Kwa hiyo, hakukuwa na wakati wa kutosha wa kufanya uchunguzi wa kina. Matokeo yake, TANROADS ilishindwa kuandaa au kutambua njia mbadala za kutatua matatizo ya kimazingira kwa haraka ambayo yangeweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi. Ukosefu wa Uchunguzi wa Athari za Mazingira uliathiri

utayarishaji wa makadirio ya gharama zinazohusiana na kupunguza uharibifu wa mazingira. Hii inaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama wakati wa utekelezaji wa mradi.

b) Mkandarasi Hakuchukua Tahadhari Dhidi ya Kuenea kwa VVU/UKIMWI

Kulingana na nyaraka zilizopitiwa pamoja na uhalisi ulioshuhudiwa wakati wa ukaguzi, inaonesha kuwa mkandarasi hakuchukua tahadhari zote za kudhibiti VVU/UKIMWI. Hapakuwa na rekodi za kina za idadi ya kondomu zilizotolewa, na mipango mingine ya uhamasishaji wa kujikinga na VVU/UKIMWI kama sehemu ya tahadhari havikuwekwa katika kumbukumbu za kimaandishi. Kulingana na mahojiano na maafisa husika, nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) haukuyapa kipaumbele maeneo haya. Hii ilidhihirishwa na ukweli kwamba bajeti ya mipango ya uhamasishaji ilipunguzwa kwa kiasi kikubwa kutoka Sh. milioni 100 hadi milioni 10. Ukosefu wa uwekezaji katika udhibiti wa VVU/UKIMWI unaweza kusababisha kudhoofisha nguvu kazi iwapo ugonjwa huu utaenea kati ya wafanyakazi na jamii inayozunguka mradi.

c) Mkandarasi Hakuweka Alama za Barabarani za Muda Mfupi Kudhibiti Magari Kulingana na Mahitaji ya Mkataba

Kulingana na Kifungu SS.1503.01 kichohusiana na viwango maalum vinavyotakiwa kimkataba, mkandarasi alitakiwa kuweka alama zenye ujumbe ulioandikwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza (Kiswahili juu ikifuatiwa na tafsiri yake kwa Kiingereza chini). Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa ujumbe uliowekwa katika alama za barabarani kwa ajili ya kudhibiti na kuongoza watumiaji wa barabara wakati wa ujenzi ziliandikwa kwa lugha ya Kiingereza tu. Kwa hiyo, ujumbe uliokusudiwa haukueleweka kwa watumiaji wote wa barabara; hivyo ungeweza kusababisha mkanganyiko, na pengine ajali.

d) Mkandarasi Hakutoa Maji Safi na Salama kwa Wafanyakazi

Kifungu SS.1715 kichohusiana na viwango maalum vinavyotakiwa kimkataba kilihitaji mkandarasi kutoa maji safi ya kunywa kwenye maeneo ya kazi. Wakati wa ukaguzi, ilionekana kuwa mkandarasi hakutoa maji safi na salama. Maji yalitolewa kwa kutumia tenki la plastiki (Simtank) lililofunikwa na ubao na

kuwekwa nje katika mazingira yasiyo safi na salama. Hii ilihatarisha afya na usalama wa wafanyakazi, kwani maji yanayotumiwa kwa kunywa yangeweza kuchafuka kwa urahisi.

e) Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Haukuweka Mahitaji ya Vyoo Katika Eneo la Maegesho ya Malori Eneo la Mbezi Kibanda cha Mkaa

Wakati wa ukaguzi, nilitembelea eneo la mradi. Nilibaini kuwa, kwenye maegesho ya malori katika eneo la Kibanda cha Mkaa hakukuwa na huduma ya vyoo. Maegesho haya yamejengwa kati ya Kilomita 4.7 hadi Kilomita 5.1 upande wa kulia wa barabara. Pia, ilibainika kuwa Mahitaji ya Mwajiri hayakuwa wazi na hayakuhusisha ujenzi wa huduma ya vyoo katika eneo hili la maegesho ya malori. Eneo hili la maegesho lina uwezo wa kuhudumia madereva 80 kila siku. Kulingana na mahojiano na maafisa wa TANROADS, vyoo vilisahaulika kwenye mpango wa mwanzo wa usanifu na ilihofiwa kuwa kama vyoo vingeongezwa wakati mradi unaendelea ingeweza kuongeza bajeti ya mradi. Hata hivyo, maoni yangu ni kwamba, kwa kuzingatia umuhimu wa afya ya watumiaji wa maegesho haya, ya vyoo ni muhimu kuwepo ili kupunguza hatari ya magonjwa ya mlipuko.

Ninashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara kuboresha usimamizi wa mkandarasi ili kuhakikisha kuwa anazingatia kikamilifu sheria na kanuni za afya na usalama kwa kumuamuru kutekeleza masharti kama ilivyoainishwa katika Masharti Maalum na ya Jumla ya Mkataba.

8.3.6 Matokeo ya Ukaguzi Kuhusiana na Vipengele vya Usimamizi wa Rasilimali Watu

Wafanyakazi Muhimu wa Mradi Walipewa Ajira za Muda Mfupi, Kinyume na Mahitaji ya Muudo wa Usimamizi wa Mradi

Kulingana na muundo wa utawala na majukumu ya usimamizi wa mradi uliopitishwa, Meneja wa Wakala wa Barabara mkoa wa Dar es salaam alipaswa kuwa Meneja wa Mradi. Pia, Mhandisi wa Mradi na Mhandisi Mkazi walitakiwa kutoka ofisi ya Wakala wa Barabara mkoa wa Dar es Salaam.

Kulingana mapitio ya majalada ya mradi wakati wa ukaguzi iligundulika kuwa Meneja wa Mkoa wa Dar es salaam alikuwa Meneja wa Mradi, hii ilizingatia mahitaji ya muundo wa mgawanyo wa majukumu ulioidhinishwa. Hata hivyo, iligundulika kuwa Meneja wa Mkoa pia alikuwa akitumikia nafasi ya Mhandisi Mkazi. Hii ni kinyume na mahitaji ya muundo kuhusu mgawanyo wa majukumu.

Kuendelea kushika nyazifa zote mbili kulisababishwa na usimamizi duni wa mabadiliko yaliyotokea katika mradi huo, kipindi ambapo baadhi wafanyakazi muhimu walihamishwa au kuondoka kutoka katika mradi huo. Kwa kutumikia nafasi zote mbili ilipelekea ugumu na kupunguza usawa katika kufanya maamuzi kuhusu mradi.

Kwa upande mwingine, ilibainika kuwa wafanyakazi wengine kwenye mradi huu walitakiwa kuwa maafisa wa kudumu walioajiriwa katika mradi ambapo wangetumia muda wao kwenye mradi huu. Hata hivyo, muundo wa utawala na majukumu ya usimamizi wa mradi ulioidhinishwa ulionesha kuwa Mhandisi anayehusika na kusimamia viwango vya ubora wa ujenzi wa barabara hakuwa mfanyakazi wa kudumu wa mradi huu. Mhandisi huyo alikuwa mfanyakazi wa kudumu wa Maabara kuu ya ujenzi ya serikali (CML) na alitumia muda wake mwingi nje na mradi huu. Kulingana na mahojiano na maafisa wa mradi, majukumu yote ya kuidhinisha matokeo ya upimaji wa viwango vya ubora yalikabidhiwa kwa mafundi mchundo wa maabara. Hii ilikiuka matakwa ya mradi kwani ukaimishaji huo ungewezasababisha usimamizi duni na ucheleweshaji wa maamuzi ikiwemo kuchukua hatua stahiki.

Ninashauri Menejimenti kutenganisha wafanyakazi muhimu waliopewa miradi mbali na mahitaji ya kazi nyingine.

SURA YA TISA

MRADI WA USAMBAZAJI MAJI SAME, MWANGA NA KOROGWE

9.1 Utangulizi

Serikali ya Tanzania imetenga kiasi cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa usambazaji wa maji katika wilaya za Same, Mwanga na Korogwe kama mojawapo ya miradi ya kimkakati. Mradi huu umetengewa jumla ya kiasi cha Sh. bilioni 450.3 kutoka serikali ya Tanzania pamoja na Washirika wa Maendeleo wengine kama Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Uchumi Afrika (BADEA), Mfuko wa Maendeleo ya Kimataifa wa Jumuiya ya Nchi Zinazozalisha Mafuta Duniani (OFID), Mfuko wa Kuwaiti kwa ajili ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Nchi za Kiarabu (KFD) pamoja na Mfuko wa Maendeleo wa Sudan (SFD).

Shabaha ya kutekeleza mradi huu ni kuwezesha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wa wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mradi huu unahusisha ujenzi wa chanzo cha maji, miundombinu ya kutibu maji, matenki ya kuhifadhi maji, pampu za kusukuma maji, kutandaza mabomba kwa ajili ya kusafirisha maji na kuunganisha maji kwa kaya.

Utekelezaji wa mradi ulianza mwaka 2013/14 kwa kufanya mapitio ya usanifu uliosimamiwa na Wizara ya Maji. Ujenzi wa mradi huu ulipangwa kufanyika kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilikuwa kujenga chanzo cha maji kwa kuchukua maji kutoka mto Pangani chini ya Bwawa la Nyumba ya Mungu, ulazaji wa mabomba ya kusafirisha maji, ujenzi wa matenki ya kuhifadhia maji, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji na kuunganisha maji kwa wananchi wa Wilaya za Mwanga na Same. Awamu hii ilipangwa kuwa na mikataba minne (mikataba namba I, II, III na IV).

Awamu ya pili ilikuwa kwa ajili ya kusafirisha maji kutoka Wilaya ya Same mpaka Wilaya ya Korogwe na kusambaza maji kwenye vijiji vinavyopitiwa na bomba kuu linalosafirisha maji. Awamu ya kwanza ilikuwa ipeleke maji kwenye vijiji tisa vinavyozunguka chanzo cha maji, ikiwa ni pamoja na kupeleka maji katika miji ya

Same na Mwanga. Awamu ya pili ilipangwa kupeleka maji katika vijiji 29 vilivyoko katika wilaya ya Korogwe. Kutokana na changamoto za kifedha, utekelezaji ulianza kwa kutekeleza miradi ya awamu ya kwanza bila kuhusisha vijiji tisa vinavyozunguka chanzo cha Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Utekelezaji wa Mradi Awamu ya Kwanza

Utekelezaji wa awamu ya kwanza uligawanyika katika mikataba minne ambayo ni:

Mkataba namba I: Mkataba huu alipata mkandarasi anayejulikana kwa jina la M.A. Kharafi and Sons kutoka nchini Misri wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 41.36. Mawanda ya kazi yalihusisha ujenzi wa chanzo, Ujenzi wa kituo cha kusukuma maji ghafi, Kutandaza mabomba kutoka chanzo cha maji mpaka kituo cha kutibu maji ghafi, ujenzi wa kituo cha kutibu maji, ujenzi wa kituo cha kusukuma maji safi, kutandaza mabomba ya chuma yenye ukubwa wa DN900 kwa umbali kilometa 9.25 kutoka kituo cha kutibu maji hadi tenki la kuhifadhia maji la Kisangara, pamoja na ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji lenye ukubwa wa mita za ujazo 2000 katika eneo la Kisangara. Mkataba ulianza tarehe 17 Februari 2014 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 16 Julai, 2017 lakini hadi wakati huo ulikuwa bado haujakamilika. Mpaka kufikia Kipindi cha Desemba 2020, mradi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 64% tu, ilhali muda wa kutekeleza mradi ulikuwa umekwisha. Mradi huu unasimamiwa na kampuni ya ECG kutoka Misri kwa kushirikiana na ATKINS ya Tanzania.

Mkataba namba II: Mkataba huu mawanda yake yalikuwa kutandaza mabomba ya kusafirisha na kusambaza maji kwa vijiji tisa vinavyozunguka Bwawa la Nyumba ya Mungu. Kutokana na changamoto za kibajeti, mkataba huu haukutekelezwa.

Mkataba namba III: Mkataba huu ulipata mkandarasi anayejulikana kwa jina BADR East Africa Limited kutoka Tanzania kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 36.08. Mawanda ya kazi yalihusisha: ujenzi wa kituo cha kusukuma maji safi eneo la Kisangara na kufunga pampu 11 za kusukuma maji zenye uwezo wa 126L/s, kwa kimo cha 234m, Ujenzi wa Tenki la maji eneo la Vodoi lenye ukubwa wa mita za ujazo 6,000 katika mji wa Mwanga, na kutandaza bomba la chuma (ductile iron) la ukubwa

wa milimita 900 kwa ajili ya kusafirisha maji kutoka Kisangara hadi tenki la Kiverenge kwa umbali wa kilometa 18. Zaidi, mkataba ulihusisha: ulazaji wa bomba la kusambaza maji kwa njia ya mtiririko kutoka tenki la Kiverenge hadi matenki ya Mwanga kwa kutumia mabomba ya chuma yenye vipenyo vya milimeta 600 (kilometa 4.55) na milimeta 500 (kilometa 11.95), ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji katika mji wa Mwanga kwa kutumia mabomba ya plastic (HDPE Pipes) yenye vipenyo vya ukubwa wa kati ya milimita 90 mpaka milimita 630 na kutandazwa umbali wa kilometa 95, kutandaza mabomba ya ukubwa kipenyo cha 32mm kwa ajili ya kuunganisha maji kwenye makazi ya watu kwa umbali wa 10km na mita za maji 5000, pamoja na kukarabati matenki manne ya maji yaliyopo katika mji wa Mwanga. Mkataba ulianza tarehe 28 Agosti 2018 na ulitarajiwa kumalizika tarehe 4 Machi 2021. Mpaka kufikia mwezi Desemba 2020, mradi ulikuwa umekamilika kwa 60.35%, ikilinganishwa na muda uliokuwa umeisha wa 86%. Mradi huu unasimamiwa na kampuni ya Don Consult Ltd kutoka Tanzania.

Mkataba namba IV: Mkataba huu alipata mkandarasi anayejulikana kwa jina la BADR East Africa Limited kutoka Tanzania kwa gharama ya Dola za Marekani 35.25 Milioni. Mawanda ya kazi yalihusisha: ujenzi wa tenki la maji la Kiverenge lenye ukubwa wa meta za ujazo 7,500, likiwa pamoja na chumba cha dawa kwa ajili ya kutibu maji (Chlorination System) katika mlima Kiverenge, ujenzi wa mfumo wa kutibu maji wenye ukubwa wa meta za ujazo 9,000, ikiwa na mfumo wa kutibu maji, ujenzi wa karakana katika mlima wa Kavambughu, ujenzi wa matenki mawili ya chini yenye ukubwa wa meta za ujazo 300, katika mji wa Same, kutandaza bomba la kusafirisha maji umbali wa km 34.7 kwa kutumia mabomba ya chuma (DI-Pipe) yenye ukubwa wa DN mm900, 800mm na 500mm na bomba la plastiki (HDPE PN 16), kutandaza mabomba ya kusambaza maji katika mji wa Same ikiwa na umbali wa 100km kwa mabomba ya plastiki (HDPE pipes), ununuzi na ufungaji wa mabomba ya kuunganisha maji kwa wananchi aina ya plastiki (HDPE) yenye kipenyo cha meta 12,120 pamoja na viambatisho vyake na kuleta mita za maji 7500 pamoja na viambatisho vyake. Mkataba ulianza tarehe 1 Juni, 2017 na ulitarajiwa kumalizika tarehe 30 Julai 2019. Mpaka kufikia Desemba 2020, mradi ulikuwa umekamilika kwa asilimia

87%, wakati mkataba wa utekelezaji ulikamilika mwezi Julai 2020. Mradi huu unasimamiwa na kampuni ya Don Consult Ltd kutoka Tanzania.

9.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi

Lengo na Mawanda ya Ukaguzi ni kutathmini mchakato na namna mradi unavyotekelezwa kwa ufanisi kwa kuzingatia vipengele vya: usimamizi wa muda, gharama na thamani ya fedha ili kuwezesha utolewaji wa maji safi na salama katika eneo la mradi kama ilivyokusudiwa. Ukaguzi ulilenga kubainisha maeneo yaliyotakiwa kuboreshwa katika utekelezaji wa mradi ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa. Zaidi, ukaguzi ulilenga kutathmini utoshelevu wa usanifu na nyaraka za zabuni, mchakato wa manunuzi, michoro, ubora wa ujenzi na sifa za watendaji, udhibiti wa gharama, uhalisi wa maendeleo ya mradi. Asasi kuu iliyokaguliwa ni Wizara ya Maji. Katika utekelezaji wa mradi huu, Wizara hii inawajibika katika kuunda sera zinazohusiana na sekta ya maji nchini, kusimamia utekelezaji (ikiwamo kuthibitisha sanifu na malipo yanayofanyika katika kila hatua ya utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi ulihusisha shughuli zote kuanzia upembuzi, usanifu hadi utekelezaji wake hadi kipindi cha ukaguzi (Desemba 2020). Ukaguzi wangu ulihusisha vipengele muhimu vya: masuala ya fedha, manunuzi, usimamizi wa mikataba, masuala ya kiufundi, pamoja na masuala ya mazingira, usalama na athari za mradi kwa jamii. Hii ilihusisha upitiaji na tathmini ya mchakato na jinsi mradi ulivyopangiliwa, ulivyosanifiwa, manunuzi yalivyofanyika na mradi ulivyotekelezwa kwa kuzingatia viwango vilivyotumika, vipengele vya ubora, utendajikazi uliodhihirishwa pamoja na hali halisi ya mradi.

9.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa Mradi wa Maji wa Same, Mwanga na Korogwe kupitia vipengele vifuatavyo: upangaji, usanifu na nyaraka za zabuni, manunuzi, usimamizi wa mikataba, hatua za ujenzi, usimamizi wa fedha, udhibiti wa ubora, na usimamizi wa rasilimali watu.

9.3.1 Mipango, Usanifu na Uandaaji wa Zabuni

Nilibaini kuwa mipango na usanifu wa Mradi wa Maji wa Same-Mwanga na Korogwe haukufanywa ipasavyo. Hii ilidhihirishwa na: (a) Ubainishaji wa mahitaji ya maji yasiyojitosheleza, (b) Usanifu duni wa miundombinu ya maji, (c) kukosekana kwa upembuzi yakinifu kwa mkataba namba III, (d) Usanifu wa miundombinu ya miradi haina thamani ya fedha, na (e) Utayarishaji usiojitosheleza wa zabuni.

Maelezo ya kina kwa mapungufu yaliyobainishwa kuhusiana na uandaaji wa mipango na usanifu yameelezewa hapa chini:

a) Ukadiriaji wa Mahitaji ya Mradi wa Maji Usiojitosheleza

Sura ya 1.1.4.3 (e) ya Mwongozo wa Usanifu wa Miradi ya Maji wa Wizara ya Maji wa mwaka 2009 inataka idadi ya watu kuwa sehemu kuu ya kutumia wakati wa ukadiriaji mahitaji ya maji na hivyo unahitaji kupewa umakini wa hali ya juu.

Wakati wa usanifu wa mradi, idadi iliyotumika ilitokana na sensa ya idadi ya watu ya 2002 kwa wilaya za Same, Mwanga na Korogwe; ambapo maeneo haya yalikadiriwa kuwa na watu 127,796. Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, kiwango cha ukuaji wa mkoa wa Kilimanjaro maeneo ya vijijini na mijini kilikuwa 1.8% na 4.01 % na kwa mkoa wa Tanga vijijini ilikuwa 2.2%.

Mapitio ya taarifa ya usanifu nilibaini kuwa kiwango cha uongezekaji wa watu kilichotumiwa kilikuwa asilimia tano kwa maeneo ya mijini ya eneo la mradi na hivyo kupata makadirio ya watu 456,930 hadi ifikapo mwaka 2038. Kwa kutumia kiwango cha uongezekaji wa watu kama kilivyotolewa na Ofisi Taifa ya Takwimu, idadi ya watu ilikadiriwa kuwa 287,989 ifikapo mwaka 2038. Hii inaonesha kuwa, idadi halisi ya watu waliokadiriwa hadi 2038 itakua kwa 63% ya idadi ya watu wanaokadiriwa kwenye mradi huu.

Matumizi ya kiwango kisicho sahihi cha uongezekaji wa watu yamepelekea usanifu miundombinu ya mradi kufanywa kwa kutumia idadi ya watu 456,930 badala ya watu 287,989 (63%). Hii imepelekea mahitaji ya maji yaliyokadiriwa kufikia mwaka 2038 kuongezeka na kuwa meta za ujazo 101,600 kwa siku badala ya

meta za ujazo 60,708.52 kwa siku, ambayo ni sawa na lita 702.64 kwa sekunde (67% zaidi). Hii imesababisha gharama za kusanifu pampu na bomba kuwa kubwa zaidi ya ambazo zingetakiwa kutumika kwenye Mradi.

Naishauri Menejimenti ipitie upya ukadiriaji wake wa mahitaji ya maji ili kuendana na idadi ya makadirio ya watu; hatimaye kuepuka uwezekano wa kuongeza au kupunguza makadirio ya mahitaji ya pampu na mabomba ili kuondoa uwezekano wa kuongezeka kwa gharama za mradi.

b) Usanifu Usiojitosheleza wa Miundombinu ya Maji

(i) Usanifu Usiojitosheleza wa Miundombinu ya Kutibu Maji

Sura ya 3.3.1.4-B na C na 3.3.2.1 ya Mwongozo wa Usanifu wa Miradi ya Maji wa Mwaka 2009 ya Wizara ya Maji inasema kwamba, muda wa maji kukaa kizuizini (detention time) kwa kukusanya taka za mseleleko (gravitational flocculation) ni dakika 20 hadi 30. Pia inataka kasi ya maji katika theluthi mbili (2/3) ya kwanza ya vyumba vya kukusanya taka (flocculator) kuwa na kasi ya 0.5 hadi 0.6, na theluthi moja (1/3) ya chumba cha mwisho cha maji kuwa na kasi ya 0.3 –0.4m/s.

Mapitio yangu ya taarifa ya usanifu yanaonyesha kuwa muda wa maji kukaa kizuizini (dentetion time) kwenye kikusanya taka (flocculator) unapaswa kuwa dakika 30.6 na maji kwenda kwa kasi ya 0.2 m/s. Hata hivyo, baada ya kufanya mahesabu kulingana na vipimo vilivyooneshwa kwenye mchoro namba SMK-WTP-SET-CIV-504, wa kikusanya taka (flocculator), ilibainika kuwa maji ghafi yanayoingia ni meta za ujazo 103,680 kwa siku na yanakaa dakika 13.23 kwenye kikusanya taka na kasi ya juu ni 0.052m/s, dhidi ya muda zuio wa chini uliopendekezwa wa kuwekwa kizuizini (dentetion time) kwa muda wa dakika 20 na kasi ya chini ya 0.5 m/s.

Athari za miundombinu isiyojitosheleza wa mtambo wa kutibu maji ni kwamba, kuna uwezekano kwamba utendaji wa kikusanya taka kilichopendekezwa kisifanye kazi yake kama ilivyokusudiwa. Hivyo, kupelekea maji yaliyokuwa yazalishwe na mtambo wa kutibu maji kutokutibiwa kisawasawa na kupelekea maji kutokuwa salama na hatari kwa matumizi ya binadamu. Hii ni kwa

sababu maji bado yatakuwa yana kemikali zilizowekwa kwa ajili ya kutibu maji; pia baadhi ya wadudu bado watakuwemo kwenye maji. Hii ni kutokana na kwamba kazi ya kukusanya taka itakuwa haikufanyika vizuri na kusababisha maji kupita yakiwa bado na taka.

Naishauri Menejimenti ifanye upembuzi wa haraka ili kuunda mtambo wa uhakika wa kutibu maji kwa ajili ya kuzuia uwezekano wa mafuriko kwenye kituo cha awali cha kusukuma maji na kuchakata uzalishaji wa maji safi. Nashauri hii ifanyike kabla ya kutafuta mkandarasi mpya ili kuepusha uwezekano wa migogoro kwa wakati ujao.

(ii) Matenki Yasiyokuwa ya Lazima Kwenye Mtambo wa Kutibu Maji

Katika kupitia michoro ilibainika kuwa, katika kituo cha kutibu maji kulikuwa na matenki matatu kati ya nyumba ya kusukuma maji safi na chujio la mchanga; ambapo matenki mawili yana ukubwa wa meta za ujazo 200 na moja lina ukubwa wa meta za ujazo 2,000.

Mzunguko wa mtiririko wa maji kutoka kwenye chujio hadi nyumba ya kusukuma maji ulikuwa kama ifuatavyo: kutoka kwenye chujio (filter) la maji pembezoni kuna tenki lenye ukubwa wa meta za ujazo 200 ambalo hupokea maji kutoka kwenye chujio, maji husafirishwa kwa mseleleko hadi tenki la ukubwa wa meta za ujazo 2,000 ambalo hulisha tenki lingine la ukubwa wa meta za ujazo 200 lililo pembezoni mwa nyumba ya pampu ya maji safi.

Hapakuwa na ulazima wa kuweka tenki la kupokea maji kutoka kwenye chujio, na tenki la pembezoni mwa ukuta wa nyumba ya pampu ya maji safi katika mzunguko wa maji. Hii ni kwa sababu tenki la ukubwa wa meta za ujazo 2,000 lilitosha kutumika kama tenki la kuleta msawazo kwenye mtiririko wa maji kati ya maji yaliyochujwa na kituo cha kusukuma maji safi.

Uchambuzi wa usanifu wa pampu na mabomba kutokana na kuzidisha kwa makadirio ya idadi ya watu umewasilishwa katika **Jedwali Na. 9-1** ambalo linaonesha gharama za ufungaji na gharama za uendeshaji wa tenki, mabomba na pampu.

Jedwali 9- 1: Uchambuzi wa Gharama juu ya Athari za kuzidisha idadi ya watu

Na.	Kitu	Gharama kwenye Mkataba (Dola za Marekeni)	Gharama Iliyorekebishwa kulingana na Bei ya Mkataba (Dola za Marekani)	Kiasi ambacho kingeweza kuokolewa (Dola za Marekani)	Maoni
1.	Pampu ya Maji ghafi katika chanzo kilichopo Nyumba ya Mungu	467,280	233,640	233,640	-
2.	Mabomba ya Maji ghafi toka bwawa la Nyumba ya Mungu Mpaka eneo la chujio la Maji	1,506,507	931,348	575,159	Bomba la ukubwa wa DN900 daraja la C30 limepunguzwa na kuwa DN800 daraja la C20
3.	Mobomba toka eneo la chujio la maji hadi Kisangara	5,312,578	4,313,445	999,133	Bomba la ukubwa wa DN900 daraja la C30 limepunguzwa na kuwa na ukubwa wa DN800 daraja la C30
4.	Bomba toka Kisangara hadi Kiverenge	6,912,276	4,812,630	2,099,646	Bomba la ukubwa wa 900mm lilipunguzwa na kuwa la 600mm na kwa sasa ipo kwenye mchakato wa manunuzi
3.	Pampu za Kisangara	1,760,000	279,064	1,480,936	-
5.	Tenki la Kiverenge	3,708,067		3,708,067	Tenki halikupaswa kuwepo
Jumla		**19,666,708**	**10,570,127**	**9,096,581**	

Chanzo: *Nukuu za Makadirio ya Ukubwa wa Kazi na Bei, Taarifa za maendeleo ya Mradi na Mikataba*

(iii)Eneo Lisiloridhisha Ilipowekwa Pampu ya Kusafishia Chujio

Wakati wa kutembelea eneo ulipo mtambo wa kutibu maji (chujio la maji), ilibainika kuwa pampu za kusafishia chujio (Backwash pump) ziliwekwa eneo ambalo kulikuwa hakuna dirisha la kuingiza hewa kwa ajili ya kupoza mota. Kukosekana kwa mzunguko wa hewa kwenye pambu ya kusafisha chujio kunaweza kusababisha kuharibika mapema kwa pampu na kupelekea gharama kubwa ya matengenezo ya pampu mara kwa mara.

(iv)Kiasi cha Maji Kinachoingia Katika Tenki la Maji la Kiverenge ni Kidogo kuliko Kiasi cha Maji Kinachotakiwa

Katika kupitia taarifa ya usanifu wa mradi ilionyesha kuwa kiwango cha maji kinachoingizwa kwenye tenki la Kiverenge ni kidogo kulinganishwa na kiwango cha maji kinachopaswa kusambazwa katika miji ya Same na Mwanga kutoka tenki la Kiverenge. Taarifa ya usanifu wa kina wa awamu ya kwanza kipande cha 2 (lot 2), ilionyesha kuwa, maji yatakayoingizwa kwenye tenki la Kiverenge ni lita 1008 kwa sekunde wakati maji yatakayotoka tenki la Kiverenge kwenda Mwanga na Same ni lita 1313 kwa sekunde. Hii inaonesha upungufu wa lita 305 kwa sekunde; na italeta uwezekano wa kuwa na mgawo wa maji.

Uchambuzi uliofanywa na Wakaguzi juu ya athari za kuzidisha usanifu wa miundombinu ulibaini kuwa, imeongeza gharama zaidi kwa Dola za Marekani 27,967,539.78 ambazo ni sawa na Jumla ya Sh. bilioni 61.57. Fedha hizi zingeokolewa kama usanifu ungefanyika vizuri kulingana na idadi halisi ya watu iliyokadiriwa hapo awali.

Jedwali 9- 2: Uchambuzi wa Gharama za Uendeshaji Kutokana na Kuwa na Moundombinu Mikubwa Zaidi

Maelezo	Gharama za Umeme kulingana na usanifu wa kwenye mkataba (Sh./Siku)	Gharama za Umeme kulingana na usanifu uliofanywa na wakaguzi (Sh./Siku)	Kiasi ambacho kingeokolewa (Sh./Siku)
Gharama ya umeme kwa ajili ya kusukuma maji ghafi toka bwawa la Nyumba ya Mungu	5,427,562.97	2,796,330.71	2,631,232.26

Maelezo	Gharama za Umeme kulingana na usanifu wa kwenye mkataba (Sh./Siku)	Gharama za Umeme kulingana na usanifu uliofanywa na wakaguzi (Sh./Siku)	Kiasi ambacho kingeokolewa (Sh./Siku)
Pampu za kusukuma maji kwenye mtambo wa kutibu maji	2,265,217.68	1,006,763.41	1,258,454.27
Gharama ya umeme kwa ajili ya kusukuma maji safi toka Mtambo wa kutibu maji	23,236,484.78	12,948,223.82	10,288,260.96
Gharama za Umeme pampu za Kisangara	16,344,520.07	2,554,927.78	13,789,592.29
Jumla	**47,273,785.50**	**19,306,245.72**	**27,967,539.78**

Chanzo: *Nukuu za Makadirio ya Ukubwa wa Kazi na Bei na repoti ya usanifu wa mradi*

(v) Kuzidisha Usanifu wa Tenki la Majitaka na Nyumba za Watumishi

Kutokana na mapitio ya michoro, ilibainika kuwa tenki la maji taka lilisanifiwa kujengwa kwa kuta za zege zikiambatana na nondo (Mchoro namba S-I7-002) bila kuwa na uthibitisho wowote wa kiusanifu. Kwa kuzingatia uwezo wa tenki la Maji taka, nina maoni kwamba, kutumia ukuta wa zege na wenye nondo ndani badala ya tofali za zege ni upotezaji wa rasilimali bila sababu za msingi; hii ni kwa sababu tofali za zege zingeweza kutosheleza.

Pia ilibainika kuwa nyumba za wafanyakazi ambazo si za ghorofa zilijengwa kwa kutumia nguzo nyingi. Kwa mfano, jengo moja ambalo si la ghorofa lilijengwa na nguzo 18 za ukubwa wa milimeta 300x400 na mikanda ya msingi (ground beam) ya ukubwa milimeta 300x400 (Tazama **Kielelezo Na. 9-1** hapa chini) kupitia Mkataba namba I mchoro namba. S-I7-002). Hii inaonesha kuwa, mradi umesanifiwa zaidi kwani hakuna mzigo mkubwa unaohitaji nguzo nyingi kwa kiasi hiki kwa jengo ambalo si la ghorofa. Hii imepelekea upotevu wa fedha, kinyume na kanuni namba 4 (1) na 5 (1) ya Kanuni za Manunuzi wa Umma ya mwaka 2013.

Kielelezo Na. 9-1: Kinaonesha Tenki la Majitaka na Nyumba za Watumishi Zikiwa Zimesanifiwa Zaidi ya Inavyotakiwa



Tenki la Maji Tanka



Idadi ya nguzo ni nyingi mno kwa jengo ambalo si la ghorofa

Nyumba ya watumishi aina ya B Mchoro namba S-18-002	yumba ya watumishi aina ya D \choro namba S-19-001

Kielelezo Na. 9-2: *Michoro ikionesha Tenki la maji taka na nyumba za watumishi zikiwa zimesanifiwa zaidi ya inavyotakiwa*

Kutumia Dari la Zege kwenye Jengo Ambalo Siyo Ghorofa na Limefunikwa kwa Bati

Wakati wa ziara ya kutembelea mradi na kupitia michoro namba SMK-WTP-SWP-MECH-422 na namba CW-00-801 iligundulika kuwa, usanifu ulipendekeza kufunika jengo kwa kutumia paa la mabati katika jengo la kusukuma maji ghafi na katika jengo la kusukuma maji yaliyokusanywa kutokana na kufurika iliyokuwa imepewa jina la “clear water pit”. Nilibaini kuwa, pamoja na majengo haya kufunikwa kwa bati pia yalikuwa na dari la zege kwa baadhi ya maeneo yaliyohitaji kuwa na dari la kawaida. Huu ni upotevu wa rasilimali kwa kuwa dari la zege ni ghali zaidi kulinganisha na kutumia dari la gypsum. Hii ni kinyume na Kanuni za 4 (1) na 5 (1) za Kanuni za Ununuzi wa Umma Mwaka 2013.

Picha Na. 9-1: Dari la Zege kwenye jengo ambalo si la ghorofa na lililofunikwa na bati juu

	Paa lililofunikwa kwa bati juu pamoja na dari la zege katika nyumba	
Jengo lenye shimo la kuhifadhia maji yaliyosafishwa	Nyumba ya kuhifadhia pumpu ya kusukuma maji	

Picha 9-1: Dari la Zege katika nyumba ambayo si ya ghorofa na lililoofunikwa kwa bati juu (Picha ilichukuliwa na wakaguzi tarehe 21 Desemba 2020)

c) Kutokuwepo kwa Upembuzi Yakinifu Kwenye Mkataba Na. III

Nilibaini kuwa hakukuwa na upembuzi yakinifu wa kazi za Mkataba Na. III. Mkataba huu ni sehemu ya mradi wa Same-Mwanga-Korogwe ukiwa na upembuzi yakinifu ulioandaliwa na kampuni ya SEURECA kwa kushirikiana na NETWAS Tanzania Ltd mwezi Aprili 2009.

Nilibaini kuwa katika usanifu wa bomba la njia linalosafirisha maji (kutoka kituo cha kusukuma maji kilichopo Kisangara hadi tenki la Kiverenge na bomba la kusafirisha maji kutoka Kiverenge hadi

matenki ya Mwanga kuna bomba la chuma la K9 lenye ukubwa wa DN900, DN600 na DN500 ambayo kulingana kwa unene wake yanaweza kuhimili shinikizo la mgandamizo wa kiwango cha 31.2, 35.7 na 38.4. Mabomba ya usambazaji kwa mji wa Mwanga yenye kipenyo kutoka DN600 hadi milimeta DN125 yamebainishwa kama PN16 (yenye uwezo wa kuhimili mkandamizo wa kiwango cha 16) na mabomba ya plastiki yenye kipenyo cha mm 90 yameainishwa kuwa na viwango vya PN10 (kuhimili shinikizo la mgandamizo wa kiwango cha 10).

Katika ukaguzi niliofanya nilibaini kuwa, Kifaa cha Modeli ya Usambazaji wa Maji (Distribution Hydraulic Model) kilizingatia kipindi cha nyakati za usiku ambapo hakuna mtiririko wa maji, hiki ni kipindi ambapo mkandamizo wa mabomba huwa mkubwa. Nilibaini kuwa mkandamizo wa juu zaidi ulikuwa wa kiwango cha 195 (19.5 bars) ambapo mabomba ya PN16 (yanayohimili mkandamizo wa kiwango cha 16) na PN10 (yanayohimili mgandamizo wa kiwango cha 10) hayawezi kuhimili. Kwa hiyo, bomba zilikuwa hazijasanifiwa vizuri kuweza kuhimili mkandamizo wa maji utakaozalishwa. Hii itapelekea mabomba kupasuka mara kwa mara, na kusababisha uvujaji wa maji; hatimaye kuwa hasara kwa umma kutokana na matengenezo ya mara kwa mara.

Pia ukaguzi ulipofanyika kwa mabomba yanayosafirisha maji toka tenki la Kiverenge hadi matenki ya Mwanga, nilibaini kuwa kuna maeneo ambayo mkandamizo unazidi kiwango cha 30 bars. Pia, kuna maeneo unakuwa chini ya kiwango cha 30 bar hadi chini ya 20 bar. Hii inaonesha kuwa, maeneo ambayo mkandamizo ni zaidi ya kiwango cha 30 mabomba yatakuwa yanapasukapasuka. Aidha, maeneo ambayo katika mgandamizo ulio chini ya kiwango cha 20 usanifu wake ulizidisha viwango na hivyo kupelekea kupoteza fedha za umma.

Hivyo, naishauri menejimenti ichukue hatua za kimkataba kwa wahandisi washauri ambao walishindwa kumshauri vizuri mwajiri kwenye masuala mbalimbali yaliyopelekea makosa kwenye kituo cha awali cha kusukuma maji na kusababisha matukio ya mafuriko.

d) Usanifu wa Muundo wa Mradi Usio na Tija

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa, kuna mipango isiyo na tija kwa baadhi ya miundombinu ya maji; ambapo mingine bei zilikuwa juu kulinganishwa na bei za sokoni.

Nilibaini kuwa kulikuwa na tathmini iliyofanywa na kampuni ya DON Consult Ltd (Msimamizi wa Mradi) juu ya muundo wa mradi). Mapitio hayo yalibadilisha njia za kupita mabomba, idadi ya mabomba, eneo la kujenga tenki na usanifu wa tenki kwa kuweka kuta katikati.

Licha ya mapitio ya usanifu uliofanywa na Msimamizi wa Mradi, pia ilibainika kuwa wakati wa utekelezaji wa mkataba, kulikuwa na masuala ya kiusanifu ambayo hayakubainishwa wakati wa mapitio ya mradi. Mambo ya kiusanifu yaliyobainishwa yalipelekea mradi kuchelewa kukamilika na kuongezeka kwa gharama za ujenzi kwa Wizara ya Maji.

Baadhi ya mambo yaliyobainika wakati wa kutembelea eneo la mradi na baada ya kupitia nyaraka ni kama ifuatavyo:

(i) Ukarabati wa Matenki ya Maji na Njia za Kuingia

Njia kama ukarabati wa matenki madogo manne ya maji, ikiwemo njia ya kuingia kwenye matenki hayo ambapo gharama yake ilikuwa juu kufikia Dola za Marekani 580,0000 (sawa na Sh. bilioni 1.28). Kulingana na uchambuzi, kiasi hiki cha fedha kingetosheleza kujenga matenki mapya manne yenye ujazo wa mita za ukubwa 500 kila moja. Kwa kawaida, tenki la ukubwa kama huu hugharimu Dola za Marekani 14,000 (Sawa na Sh. milioni 30).

(ii) Usanifu wa Chumba cha Kemikali

Chumba cha kemikali, ilibainika kuwa jengo la kawaida la ukubwa urefu wa mita 10.9 na upana wa mita 5.5 na kimo cha mita 3.9 na yenye ukuta mrefu kwenye miisho ya jengo kwa mita 4.25 (gable end height of 4.25m) uligharimu Dola za Marekani 185,380.10 ambayo ni sawa na Sh. milioni 408 za Tanzania.

Ilibainika kuwa, hali ya bei kuwa juu ni kukosekana kwa makadirio ya gharama ya Wahandisi ambayo yangeweza kusaidia timu ya tathmini kufanya ulinganifu wa bei zilizoletwa na wazabuni na makadirio yaliyoletwa na mhandisi ili kupata bei nafuu zaidi ya jengo.

Hayo yote yaliyobainishwa hapo juu yalichangia kuongezeka kwa bei ya mkataba. Gharama hiyo iliyoongezeka ingeweza kuhifadhiwa na kutumiwa kwa shughuli nyingine za mradi.

(iii)Usanifu wa Njia ya Mabomba Usio na Tija

Nilifanya tathmini na kubaini kuwa, kiwango cha bomba la C30 ambalo lilisanifiwa ili litumike kwenye njia yote kusafirishia maji lilipitiliza viwango vya usanifu (overdesigned). Mabomba haya yalikuwa na jumla ya urefu wa mita 20,583.58 kwenye mkataba kwa gharama ya Dola za Marekeni 5,762,615.6. Kulingana na tathmini yangu, nilibaini kuwa njia mbadala na yenye tija ambayo ina urefu wa mita 15,129.9 na gharama yake ni Dola za Marekani 3,908,364.4 ingeweza kuokoa karibu urefu wa mita 5,358 ambayo gharama yake ni sawa na Dola za Marekani 1,854,251.2 sawa na Sh. bilioni 4.

(iv)Mabadiliko ya Michoro Wakati wa Utekelezaji wa Mradi Bila Sababu za Msingi

Pia, nilibaini kuwa mchoro wa zabuni uliotumika kwenye matenki ya Same na Kiverenge iliyotolewa na M/S DON Consult Ltd Machi 2014 (Mchoro namba S-92-201 Tenki la Kiverenge) lilioneshwa kuwa kuna kuta za katikati kwa ajili ya kugawa tenki.

Hata hivyo, tathmini iliyofanywa na Mshauri mwelekezi (M/S DON Consult ltd) huyohuyo baada ya mkataba kusainiwa, mshauri alikubali kubadilisha usanifu na kuongeza kiungo kwa ajili ya upumuaji (expansion joint) kwa gharama ya nyongeza ya Dola za Marekani 15,652.75. Mbali na gharama, mabadiliko haya yalisababisha kuchelewa kwa ujenzi kwa sababu ya kusubiria kibali au ruhusa ya kuendelea na utekelezaji. Hakukuwa na uthibitisho wowote unaoonesha Wizara ya Maji kuhoji sababu ya kubadilisha usanifu wake uliopelekea gharama ya utekelezaji kuongezeka kama ilivyo Kanuni ya 5 (1) za Sheria za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 na masharti ya jumla ya mkataba (GCC) kifungu cha 3.5 (a) juu ya kuwajibika Kitaaluma.

(v) Ubora na Ukamilifu wa Taarifa ya Upembuzi Yakinifu Usiojitosheleza

Katika kupitia taarifa ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi ilibainika kuwa, taarifa ya upembuzi yakinifu iliyopo ya mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe iko katika rasimu. Wizara ya Maji ilianzisha utekelezaji wa Mradi kwa kuzingatia rasimu ya taarifa ya upembuzi yakinifu, kinyume na matakwa ya Kanuni ya 239 (8) ya Kanuni za Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2013.

Pia, ripoti ya Upembuzi yakinifu ilikosa taarifa muhimu kuifanya iwe kamili na inayokubalika. Baadhi ya taarifa zilizokosekana ni pamoja na: Tathmini ya awali ya Mazingira na namna ya kuzuia uharibifu wa mazingira, uchambuzi wa gharama, faida na tija ya mradi endapo kama utatekelezwa, njia mbalimbali za kutekeleza mradi, usanifu kulingana na mabadiliko ya tabia ya nchi mfano kutumia takwimu za Mafuriko kwenye chanzo kwa kutumia takwimu za miaka 30 au zaidi. Hii ni kinyume na Sehemu 1.1.3, 1.1.4.3 na 1.4.2 ya kanuni za usanifu za Wizara ya Maji ya Mwaka 2009 na Kanuni namba 5; 241 (3) na 321 (1) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

Naishauri menejimenti iwasiliane na msimamizi mshauri wa mradi kwa ajili ya kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa hapo juu. Pia, ihakikishe kuwa vipengele vyote vya mkataba vinatekelezwa kikamilifu.

e) Maandalizi Hafifu ya Nyaraka za Mchakato wa Manunuzi

Nilibaini kuwa, hati ya nukuu ya gharama ya vifaa na huduma haikuandaliwa ipasavyo. Yafuatayo ni mapungufu yaliyoonekana katika nukuu ya gharama ya vifaa na huduma:

(i) Mkandarasi Alipaswa Kujaza Bei kwa Ajili ya Kuwasilisha Dhamana kwa Ajili ya Malipo ya Awali na Utendaji Kazi

Kanuni ya 29(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 inaitaka Taasisi inayofanya manunuzi kuhakikisha kuwa mshindi wa zabuni anawasilisha dhamana ya utendaji wa kazi ili kuweka imani ya utendaji katika mkataba na malipo ya vibarua, watoa huduma, mafundi na wasaidizi wa mkandarasi kama itataka hivyo.

Kifungu 4.2 cha masharti ya jumla ya mkataba kinasema kwamba "Mkandarasi kwa gharama yake atapaswa kupata hati ya dhamana ya utendaji wa kazi kwa ajili ya kuhakikisha utendaji unaotakiwa, kwa kiasi, mfumo wa fedha uliotajwa katika kiambatisho kilicho katika tenda. Endapo kiasi hakijatajwa katika kiambatisho cha tenda, kipengele hiki hakitahusika". Kiasi kilichotajwa katika kiambatisho kilikuwa ni 10% ya kiasi kilichokubaliwa kwenye bei ya mkataba.

Nilipitia vipengele vya nukuu ya gharama za vifaa na huduma vinavyohusu kazi za awali ukurasa wa 1 kati ya kurasa 6. Vipengele Na. 3 na 4 vilionesha kuwa Mkandarasi alitakiwa kujaza dhamana ya malipo ya awali na dhamana ya kuaminisha utendaji wake wa kazi. Mkandarasi alijaza bei ya vipengele hivyo na akalipwa na Wizara katika Hati za Malipo yaliyofuata. Zaidi ya hayo, kuongezeka kwa vipengele hivi ni sehemu ya mabadiliko yaliyofanyika katika mkataba. **Jedwali Na. 9-3** hapo chini linaonesha kiasi kilichojazwa kwa ajili ya fedha ya awali na dhamana ya utendaji kazi wa mkandarasi.

Jedwali 9- 3: Vipengele Ambavyo Havikupaswa Kujazwa Katika Nukuu ya Gharama za Vifaa na Huduma

Kipengele	Gharama za Awali (Dola za Marekani)
Ukurasa wa 1 kati ya kurasa 6 Kipengele cha 3 Dhamana ya Malipo ya Awali	10,620
Ukurasa wa 1 kati ya kurasa 6 kipengele cha 4 Dhamana ya Utendaji kazi wa Mkandarasi	796,500
Jumla	**807,120**

Chanzo Cha Taarifa: *Nyaraka za mkataba, Hati ya kuthibitisha Malipo Namba 21 na Taarifa ya Tathmini ya Mkataba Namba 1*

Jedwali Na. 9-3 linaonesha kuwa gharama za kupata dhamana ya utendaji na malipo ya awali kiasi cha Dola za Marekani 807,120 (sawa na Sh. bilioni 1.8) zimejumuishwa kwenye gharama ya mkataba ambayo haikutakiwa kuwa miongoni mwa vitu vya kulipiwa, kutokuwa na bei. Matokeo yake, wakati wa utekelezaji gharama za vitu hivi ziliidhinishwa kulipwa kupitia Cheti Nambari 1 na kulipwa. Kiasi hiki cha pesa kingeweza kutumika katika shughuli nyingine za serikali.

(ii) Mapungufu Katika Ujazaji wa Nukuu ya Gharama za Vifaa na Huduma

Ukaguzi wa kipengele cha awali katika nukuu ya gharama za vifaa na huduma ilionesha kuwa, wakandarasi walipaswa kujaza nukuu ya gharama za vifaa kwa ajili ya kukamilisha kazi zote zilizofafanuliwa katika nyaraka mbalimbali za mkataba zinazoeleza ukubwa wa kazi katika mradi. Hii haikutakiwa ijazwe kwa sababu hakukuwa na maelekezo katika nukuu ya gharama za vifaa na huduma iliyokuwa inataka kuzikamilisha kazi za mradi

kwa kuzingatia michoro na vigezo. Hii ni kwa sababu haya yalikuwa maelekezo tu kwa wakandarasi.

Zaidi ya hayo wakati wa kikao cha kabla ya wakandarasi kujaza nukuu, hoja Namba 8 iliibuliwa na mkandarasi ili kutaka ufafanuzi. Hii inaonesha kuwa kulikuwa na ugumu katika kukijaza kipengele hicho; na walipendekeza kiondolewe na badala yake iongezwe 10% katika kipengele cha fedha ya dharura kwenye sehemu ya majumuisho ya nukuu ili kuwezesha kufanyika kwa kipengele hiki na vingine ambavyo vingejitokeza pasipo kutarajiwa.

Ilibainika kuwa, Wizara ya Maji walijibu kuwa ujazaji uzingatie maelekezo yaliyomo katika nyaraka zilizoandaliwa kujazwa na wakandarasi, ikiwemo nukuu ya gharama ya vifaa na huduma. Matokeo ya hii ni kuwa kipengele hiki kilijazwa bei ya Dola za Marekani 295,000 (sawa na Sh. milioni 649) ambayo zililipwa kupitia Hati za Malipo zilizofuata. Haya yalikuwa matumizi mabaya ya mali za umma. Hii ni kwa sababu, kipengele hiki kiliongeza gharama ya mkataba isiyotakiwa ambayo ingeelekezwa katika kazi nyinginezo.

Pia nilibani kuwa, kulikuwa na kipengele cha dhamana ya utendaji wa mkandarasi katika nukuu ya gharama ya vifaa na huduma ambacho kililipwa kwa mkandarasi, jumla ya kiasi cha Dola za Marekani 200,000. Hiki kilichofanyika kilikuwa kinyume na Masharti ya ujumla ya mkataba kipengele 4.4.1 ambacho kinamtaka mkandarasi kupata dhamana ya utendaji wake wa kazi kwa gharama zake mwenyewe kwa kiasi ambacho kimetajwa katika masharti maalumu na kwa namna ya fedha ilivyopendekezwa katika mkataba au katika namna ambayo fedha zinaweza kubadilishwa bila gharama inayokubalika na Mwajiri.

Pia kipengele Namba 7 cha mkataba kinaelekeza “Kodi mbalimbali zilizotajwa zinazotakiwa kulipwa kwa mujibu wa sheria za serikali ya Tanzania” kilikuwa hakijatajwa au kufafanuliwa katika kipengele 01770 cha Maelezo ya Kiufundi. Kipengele hiki hakikueleweka, kwani mradi huu ulikuwa na msamaha wa kodi. Mkandarasi alilipwa kumwezesha kulipa kodi, wakati kulikuwa na msamaha wa kodi katika mkataba.

Naishauri Wizara ya Maji ihakikishe mkandarasi anarejesha kiasi cha pesa kilicholipwa kama kodi kwenye vifaa vyenye msamaha wa kodi.

(iii)Ujazaji kwa Zaidi ya Mara Moja wa Vipengele Katika Nukuu ya Gharama ya Vifaa na Huduma

Katika kupitia kipengele cha awali cha nukuu ya gharama za vifaa na huduma, ilionekana kuwa kulikuwa na baadhi ya vipengele vilivyojazwa zaidi ya mara moja. **Jedwali Na. 9-4** linaonesha vipengele vilivyojazwa kwa zaidi ya mara moja.

Jedwali 9- 4: Vipengele vilivyoonekana mara mbili katika nukuu ya gharama ya vifaa na huduma

Jina la kipengele kilichoonekana mara ya kwanza	Jina la kipengele kilichoonekana mara ya pili	Gharama kwa kipengele kilipoonekana mara ya kwanza (Dola za Marekani)	Gharama kwa kipengele kilipoonekana mara ya pili (Dola za Marekani)
Mkataba Namba I			
Ukurasa wa 1 kati ya 6 kipengele 7: Wafanyakazi wa kusimamia utekelezaji wa mradi	Ukurasa wa 3 kati kurasa 6 kipengele cha 3: Utawala na wafanyakazi	792,511.60	84,960
Ukurasa wa 1 kati ya 6 kipengele 8: Mhandisi Msimamizi wa kazi ya Ujenzi	Ukurasa wa 3 kati kurasa 6 kipengele cha 5: Fundi mkuu, Fundi wa ujumla na Wasimamizi	217,002.00	124,006.02
Ukurasa wa 1 kati ya 6 kipengele 11: Vitendea kazi vya kutosha kuwezesha maendeleo ya kukamilisha kazi kwa mujibu wa kipengele 01320	Ukurasa wa 1 kati ya kurasa 6 kipengele cha 12: Mhandisi wa kupanga na kuratibu kazi	24,780.00	47,200
	Ukurasa wa 1 kati ya kurasa 6 kipengele cha 12: Mhandisi wa kupanga na kuratibu kazi Ukurasa wa 1 kati ya kurasa 6 kipengele cha 13: Uratibu, uhuishaji		18,290

	na marekebisho ya kazi		
Ukurasa wa 3 kati ya kurasa 6 kipengele cha 8: Huduma za muda kwa Mwajiri na Mhandisi kwa mujibu wa kipengele 01510 na 1590 ambavyo vinajumuisha alama za mradi,	Ukurasa wa 4 kati ya kurasa 6 kipengele cha 2: Alama za mradi	161,660	5,900
	Ukurasa wa 1 kati ya kurasa 6 kipengele cha 3: Utambulisho wa mradi		5,900
Ukurasa wa 4 kati ya kurasa 6 kipengele cha 1: Kuondoa huduma zote katika eneo la baada ya mradi kukamilika	Ukurasa wa 4 kati ya kurasa 6 kipengele cha 5: Kazi za kufunga mradi kwa mujibu wa kipengele 01770	64,900	23,600
Mkataba namba III			
Huduma za muda Kipengele 01510 - Huduma ya simu - Usafiri - Ofisi kwa matumizi ya Mhandisi - Vifaa kwa ajili ya kupimia na kufanyia vipimo kucheki ubora - Alama katika eneo la mradi Kipengele 01590 - Huduma ya umeme - Huduma ya maji - Matengenezo Vifaa kwa ajili ya mawasiliano ikijumuisha kompyuta, mashine ya kutolea nakala, huduma za simu	Kipengele cha 2 Kazi na huduma za kuwezesha mradi kuanza: Magari 3 kwa ajili ya Mhandisi Mshauri na Mwajiri Kazi na huduma za kuwezesha mradi kuanza: Kipengele cha ujumla Na. 10 komputa na mashine ya kutolea nakala Kazi na huduma za kuwezesha mradi kuanza: Malazi/ofisi za muda, huduma Kipengele Na. 12 kuleta na kuweka bango la kutambulisha mradi kwenye eneo la mradi	800,000.00	480,000.00 21,000.00 1,900.00
Kazi na Huduma za Awali Kipengele cha Ujumla Na. 3: Alama ya Mradi	Huduma za Awali Kipengele cha ujumla 2: Alama	6,000.00	6,000.00

	ya kutambulisha mradi		
Kazi na Huduma za Awali Ratiba za kuendeleza kazi kipengele cha 12: Mhandisi mratibu na muandaaji	Kazi na Huduma za Awali Ratiba za kuendeleza kazi kipengele cha 13: Uratibu, uhuishaji na kufanya mapitio ya kazi.	50,000.00	25,000.00
Jumla		**2,116,853.60**	**843,756.02**

Chanzo: *Uchambuzi wa wakaguzi kutoka katika Mabadiliko ya Mkataba namba 1 (Kazi na Huduma za Awali eneo la mradi).*

Uchambuzi katika **Jedwali Na. 9-4** hapo juu unaonesha kuwa katika nukuu ya gharama ya vifaa na huduma kulikuwa na vipengele vilivyoonekana mara mbili. Vipengele hivyo vikipangiliwa katika mpangilio wa kwanza na wa pili vinaonesha kuwa viligharimu Dola za Marekani 2,116,853.60 na 843,756.02, mtawalia. Hii inaonesha kuwa kama gharama za mara ya kwanza zingechaguliwa na kuachana na ile ya pili kingeokolewa kiasi cha Dola za Marekani 843,756.02 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 1.9.

Naishauri Wizara ya Maji ijiridhishe kwa kupitia upya gharama za vifaa ambavyo vililipwa kimakosa mara mbili kisha kuwasiliana na Mkandarasi ili arejeshe fedha hizo zilizolipwa mara mbili.

(iv)Kutoeleweka kwa Kipengele cha Kazi na Huduma za Awali katika Nukuu ya Gharama za Vifaa na Huduma

Ilibainika kuwa, katika Nukuu ya Gharama za vifaa na huduma kulikuwa na vipengele ambavyo havieleweki kama vile "Mengineyo yanayohitaji ufafanuzi" ambavyo vilikuwa havina maelezo ya nini hasa kililengwa, na endapo mzabuni au mkandarasi asingefafanua wangefanya nini kuweza kuitumia hiki kipengele katika hatua ya kutafuta mkandarasi.

Zaidi ya hayo, wakati wa tathmini na makubaliano ili kumpata mkandarasi, Wizara ya Maji haikusaka ufafanuzi kutoka kwa wazabuni ili kuthibitisha ukubwa wa kazi katika kipengele 7 na 10 cha kazi na huduma za awali kwenye kitabu cha kujaza bei kuwa

kile kilichoitwa "Mengineyo yenye kuhitaji ufafanuzi". Jambo hili ni kinyume na matakwa ya kanuni namba 5(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013.

Njia bora ingekuwa kuviondoa hivi vipengele katika Nukuu ya Gharama za Vifaa na Huduma kama hawakufafanua walichoweka wakati wa mchakato wa kumpata mkandarasi. Hata hivyo, ilibainika kuwa Mhandisi Mshauri amepitisha kwa ajili ya malipo ya vipengele hivi vyenye kiasi cha Dola za Marekani 1,936,062.54, sawa na fedha za kitanzania Sh. Bilioni 4.2 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-5.**

Jedwali 9- 5: Vipengele vilivyojazwa bei na mkandarasi bila Kufafanua kazi katika kipengele cha kazi na huduma za awali

Kipengele Na.	Jina la Kipengele	Jumla ya gharama za awali (Dola za Marekani)	Jumla ya Gharama zilizoongezeka na kuidhinishwa kwa malipo wakati wa utekelezaji
Ukurasa wa 1 kati ya kurasa 6 kipengele cha 10	Mengineyo (yanayohitaji kufafanuliwa)	756,297.4	1,199,069.03
Ukurasa wa 3 kati ya kurasa 6 kipengele cha 7	Mengineyo (yanayohitaji kufafanuliwa)	464,849.20	736,993.51
Jumla		**1,221,146.60**	**1,936,062.54**

Chanzo cha Taarifa: *Nyaraka za Mkataba na Hati za kuidhinisha Malipo*

Jedwali Na. 9-5 linaonesha kuwa vipengele vyenye thamani ya Dola za Marekani 1,221,146.60 katika mkataba havikufafanua kazi zilizotakiwa kufanyika. Hii ilisababisha ongezeko la gharama isiyo ya lazima. Mapitio ya tathmini ya hati ya kuidhinisha malipo namba 21 yalibainisha kuwa wakati wa utekelezaji wa mradi kutokana na kuongeza muda gharama iliongezeka kufikia kiasi cha Dola za Marekani 1,936,062.54.

Zaidi ya hilo, kupitia mahojiano na Timu ya Wakaguzi, Mfanyakazi wa Mkandarasi alitoa maelezo ya vipengele vilivyotajwa "Mengineyo yenye kuhitaji ufafanuzi" kuwa ni malazi, ukarimu, mawasiliano, kompyuta na viambatisho vyake, kupata ushauri wa kitaalamu, usafiri, ofisi na vifaa vya ofisini, leseni na vyeti, vifaa, gharama ya pango la mkandarasi, na umeme.

Kwa vile wakandarasi hawakufafanua kipi kingefanyika wakati wa mchakato wa kumpata mkandarasi, ilisababisha mkandarasi kutafuta kila namna ya kuweza kulipwa; hivyo ilisababisha ongezeko lisilo la lazima kwa kazi hiyo.

Naishauri Wizara ya Maji ijiridhishe kubaini uhalali wa malipo ya kipengele cha "other specify" kama kinavyooneshwa kwenye makisio ya gharama za ujenzi (BoQ), aidha ikibainika malipo hayo si sahihi mawasiliano yafanyike ili Mkandarasi arejeshe fedha zilizolipwa kama "other specify".

(v) Kutokuwa na Mfanano Katika Nyaraka za Manunuzi ya Wakandarasi

Nilibaini kuwa Wizara ya Maji haikuangalia kutokuwa na mfanano kwa nyaraka za manunuzi. Hii ni kinyume cha kanuni ya 185(2) ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 ambayo inataka Timu ya Tathmini kuwa na nyaraka zote za kufanyia zabuni, ikijumuisha nukuu ya gharama za vifaa na huduma, matakwa ya kiufundi na michoro. Pia hii ilikuwa kinyume na matakwa ya kanuni 239(8) ya Kanuni za Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 ambayo inasema kuwa "Taasisi Nunuzi haitapaswa kualika wazabuni kwa ajili ya kazi, isipokuwa tu pale ambapo Michoro na matakwa ya kiufundi vitakuwa viko kamili na makadirio ya gharama yameandaliwa". Kuendeleza zabuni na kuanza kazi ya ujenzi kwa kutumia michoro na matakwa ya kiufundi visivyo kamili vilipelekea kuwa na mabadiliko ya kubadili eneo la kazi, nyongeza au punguzo la uwingi. Ilibainika kuwa ongezeko la mabadiliko limepanda hadi kufikia gharama ya Dola za Marekani 1,110,816.94 sawa na Sh. bilioni 2.4

Naishauri Wizara ya Maji ihakikishe kwamba makabrasha ya zabuni yanaandaliwa kwa ukamilifu kabla ya kualika wazabuni.

(vi) Kutoendana kwa Matakwa ya Kiufundi na Viwango

Wizara iliandaa nyaraka za mkataba (maelekezo kwa wazabuni na matakwa ya kiufundi) kwa kufuata viwango vya kigeni na matakwa ya kiufundi ambayo hayatumiki Tanzania. Mchanganuo wenye msimbo Na. 02300 unahusishwa kwenye viwango vya

Kimarekani[17]. Viwango hivi vyote si sawa kuvitumia kwenye miradi ya ujenzi wa mabomba ya maji ambayo ni kinyume na matakwa ya Mwongozo wa kusanifu wa Wizara ya Maji wa mwaka 2009. Viwango ambavyo vinatumika zaidi ni vya Shirika la Viwango vya Kimataifa[18] kwa ulazaji wa mabomba ya DI[19] na HDPE[20] ambavyo vinatumika nchini Tanzania. Hii inamaanisha kwamba kulikuwa na kutoendana kwa nyaraka katika matakwa ya kiufundi na viwango. Madhara ya kutumia matakwa ya kiufundi na viwango visivyo sahihi yalibainika katika ufukiaji na ushindiliaji wa mabomba ambapo ubora wake uliathiriwa pia hali kuwa endelevu kwa baadaye.

Niashauri Wizara ya Maji ipitie na kuhuisha viambatisho vyote vya mkataba (kama vile maelekezo ya zabuni, taratibu za mkataba, makadirio ya gharama za vifaa, michoro na majedwali ya mikataba) ili kuondoa vipengele vyenye matatizo, vipengele vinavyokinzana. Pi, ili kuboresha vipengele ambavyo vinaendana na mazingira ya Tanzania.

(vii) Uwekwaji wa Barua Iliyoboresha Nyaraka za Zabuni Pasipo Kufuata Taratibu

Sehemu ya 29.1 ya maelekezo kwa wazabuni inaeleza kuwa wazabuni wasifute kipengele chochote kwa kukata katika nyaraka ya kufanyia zabuni au chochote kati ya usanifu wa kiufundi na matakwa ya kiufundi au kufanya badiliko lolote ndani yake. Mabadiliko ya aina mbalimbali hayatazingatiwa. Endapo mzabuni atahitaji kuweka masharti maalum au kuingiza mabadiliko ya kiufundi au njia mbadala, inabidi ziwasilishwe katika bahasha tofauti iliyoambatishwa na zabuni yake kwa mujibu wa kifungu cha 26 cha nyaraka ya mkataba. Wakati huohuo, ifanyike rejea katika fomu ya zabuni na Mwajiri/Mhandisi anayo haki kukubali au kukataa mabadiliko, upindishaji au mibadala mbalimbali itakayotolewa.

---

[17] The standards of American Society of State Highway and Transport Officials (AASHTO), American Society of Testing and Materials (ASTM) and NEMA
[18] ISO Standards
[19] Ductile Iron
20 HDPE

Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa waraka wa mkataba ulijumuisha barua za mkataba ambazo ziliingizwa katika nyaraka kuu za zabuni bila kufuata utaratibu; na zikaruhusu wazabuni kutoa masharti maalum au kuingiza mabadiliko ya kiufundi au mibadala ambayo ilibadilisha kwa kiasi kikubwa masharti na matakwa muhimu ya mkataba. Barua za zabuni ni kama zilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-6** hapo chini:

Hii ilikuwa kinyume na matakwa ya kanuni ya 4, sehemu 2(d) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 ambayo inatoa umuhimu wa uadilifu, uwajibikaji na ukweli na uwazi katika mchakato wa manunuzi; ambapo kanuni 5(1), 78(1) na 79(3) zinazuia kutoka katika viwango vya utendaji wa mara kwa mara. Hiyo pia ni kinyume cha kifungu kidogo 83(1) na kifungu cha masharti ya jumla ya mkataba 15.6.3 kinachozuia kujihusisha na vitendo vya udanganyifu katika manunuzi na utekelzaji wa mradi.

Hii ilipelekea kuwapo kwa migogoro mikubwa miwili iliyokuwa katika mabomba ya DI na malipo ya vifaa vilivyopo katika eneo la mradi. Mabomba ya DI yalilazimisha Wizara ya Maji kuondoa mabomba ya DI katika mkataba mkuu ili kutafuta mkandarasi mwingine kwa kazi zilizoondolewa.

Jedwali 9- 6: Orodha ya barua za zabuni zenye utata katika mkataba wa III

Namba ya Rejea ya Barua	Yaliyomo katika barua	Mapungufu yaliyobanika
Rejea Na. BDR/0309/31 12/2017	Kipengele cha kazi na huduma za awali bei za ujumla kwa kutumia kanuni ya FIDIC kwa kuzingatia malipo yanayopaswa kupitishwa na Mwajiri kwa vipengele ambavyo vinaanza kufanywa na mkandarasi	Kanuni ya FIDIC kwa bei ya ujumla haikuwa sehemu ya mkataba
Rejea Na. BDR/0392/3112/2017	Aina ya malipo ya awali kwa mujibu wa vifungu vya FIDIC, mkandarasi anaomba kiasi chote kinachopaswa kupitishwa kwa ajili ya malipo bila makato yoyote baada ya mkandarasi kufanya maandalizi ya awali katika eneo la utekelezaji mradi	Kanuni ya FIDIC kwa bei ya ujumla haikuwa sehemu ya mkataba
Rejea Na. BDR/0391/3112/2017	Kwa kuzingatia kwamba manunuzi ya vifaa vya mradi huu (mkataba Na. III) unaozidi 50% ya jumla ya kiasi cha mradi. Mkandarasi anaomba malipo ya	Ulegezaji wa matakwa muhimu ya zabuni kwa mzabuni mmoja kitu ambacho kinaonesha kutokuwepo kwa usawa

Namba ya Rejea ya Barua	Yaliyomo katika barua	Mapungufu yaliyobanika
	awali si chini ya 25% ya jumla ya bei ya mradi	kwa wazabuni wengine. Wakati katika nyaraka za zabuni ilikuwa imewekwa kuwa 10% ambayo baadaye ilikubaliwa kupitia makubaliano iwe 20%
Rejea Na. BDR/0313/3112/2017	Kuwapo kwa kipengele cha 15% ya fedha ya makato kuwa mbadala kwa makato ya kila Hati ya Kuidhinishia Malipo	Ulegezaji wa matakwa muhimu ya zabuni kwa mzabuni mmoja kitu ambacho kinaonesha kutokuwapo kwa usawa kwa wazabuni wengine. Ambapo wakati wa mchakato wa zabuni ilipaswa kuwa inarejeshwa katika kila Hati ya Kuidhinishia malipo
Rejea Na. BDR/0309/3112/2017	Maombi ya malipo kwa vifaa vilivyopo katika eneo la kazi kufanyika kwa 70% ya gharama ya iliyowekwa katika nukuu ya gharama ya vifaa na huduma, na mitambo na vifaa vidogovidogo kuwekwa katika 70% ya gharama iliyowekwa katika nukuu ya gharama ya vifaa na huduma	Ulegezaji wa masharti kwa sababu endapo Mwajiri alilipa kwa kuzingatia alivyoombwa kuna uwezekano wa kupoteza fedha kwa baadhi ya kazi za ufungaji mitambo zilizofanyika endapo mkandarasi ataondolewa katika mkataba wa kutekeleza mradi.
Rejea Na. BDR/0377/3112/2017	Mkandarasi alimjulisha Mwajiri kuwa mahali ambapo yangewekwa makazi ya malazi, ofisi, karakana na ghala	Mkandarasi alikuwa na uwezo wa kutambua eneo la kuweka makazi kabla ya hatua za kiserikali za kuomba ardhi kutajwa Uwezekano wa barua ya zabuni kufanyiwa maboresho yalielekezwa kwa mzabuni aliyejulikana kabla ya hatua sahihi za manunuzi hazijaanzishwa. Hiki kingeweza kuitwa udanganyifu na kula njama kwa mujibu wa matakwa ya ujumla ya mkataba sehemu 15.6.3 (ii)&(iii).

Namba ya Rejea ya Barua	Yaliyomo katika barua	Mapungufu yaliyobanika
Rejea Na. BDR/0376/3112/ 2017	Vipengele vya nukuu ya gharama za vifaa na huduma mkandarasi alimjulisha Mwajiri kuwa hakukuwa na vipengele kwa ajili ya kusafisha eneo, Uchimbaji wa mitaro kwa ajili ya kulaza bomba, uchimbaji wa sehemu zenye mawe na kazi ya ufukiaji wa njia kubwa na njia ya ugawaji bomba za maji na alipendekeza lijadiliwe gharama ya kuzifanya kazi hizo katika kikao cha makubaliano.	Matakwa ya makataba yaliyojumuishwa katika kipengele 02620 na 02621 kazi zote zimetajwa lakini mkandarasi alidai kuwa hazikuwemo. Mkandarasi aliomba mabadiliko na Mwajiri akakubali na kulipa kazi ya kusafisha eneo la ujenzi wa mradi na uchimbaji wa mitaro ya kulaza bomba
Rejea Na. BDR/0380/3112/ 2917	Kutoka katika vipengele vya nukuu ya gharama ya vifaa na huduma maelezo yaliyotolewa na Mkandarasi ni kuwa Daraja ubora wa mabomba aliloweka katika zabuni yake kwa vile haikuwa imefafanuliwa vizuri katika nyaraka za zabuni. Mabomba aina ya DI yenye kipenyo DN500 daraja la ubora C25, Mabomba ya chuma aina ya DI yenye kipenyo DN600 na kipenyo DN900 daraja la ubora C20.	Mkandarasi alibadili matakwa ya kiufundi kutoka K9 ambayo ni sawa na daraja la ubora C30 na katika barua yake ya zabuni alisema kuwa alijaza bei ya K9 ambayo ni sawa na daraja la ubora C25 na C20 Wakati wa maelekezo kwa ajili ya kujaza bei suala hili lilitajwa na mkandarasi kwa kuonesha kuwa mabomba ya ubora daraja K na viambatisho vyake vilikuwa vimepitwa na wakati lakini wanazalisha mabomba yenye ubora daraja C viwandani yanakozalishwa mabomba aina ya DI. Mwajiri alijibu kwa kuahidi kuwa suala hilo lingetatuliwa katika hatua nyingine ya manunuzi mbeleni jambo ambalo halikufanyika.

Chanzo: *Mikataba ya ujenzi wa mradi wa maji wa Same-Mwanga na Korogwe*

Naishauri menejimenti ichukue hatua za kisheria dhidi ya mkandarasi na wote waliohusika kwenye vitendo vya ulaghai

kuhusiana na barua za zabuni, garantii za malipo ya awali, na garantii za zuio.

9.3.2 Kipengele cha Manunuzi

a) Manunuzi Hafifu ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri

Nilibaini mapungufu yafuatayo kuhusu manunuzi ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri:

(i) Kutokuwepo kwa Kumbukumbu za Manunuzi ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri

Kanuni Na. 15 ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inataka Taasisi Nunuzi kutunza kumbukumbu za manunuzi zikiwa na taarifa zifuatazo: maelezo kwa ufupi ya bidhaa, kazi au huduma inayotakiwa kununuliwa, majina na anuani za wazabuni waliopitishwa katika hatua ya awali, waliobakia baada ya kupunguzwa au waliochaguliwa na walioalikwa kuwasilisha zabuni (ikiwa ni pamoja na taratibu zilizotumika kuwachagua), majina na anwani za wazabuni waliowasilisha zabuni, majina na anwani za wazabuni ambao mkataba wa manunuzi au wa kuondoa bidhaa umeingizwa katika bei ya mkataba, bei, namna ambavyo uthaminishaji umelenga ili kupata bei, pamoja na taarifa kwa ufupi za tathmini na ulinganishaji ikijumuisha maombi kwa kufuata mlengo unaozingatia kanuni hizi.

Ilibainika kuwa, utunzaji wa kumbukumbu za jinsi ambavyo manunuzi yalifanyika Wizara ya Maji haukufanyika kiasi cha kuridhisha. Nyaraka muhimu za manunuzi hazikupatikana na hazikuwasilishwa kwa wakaguzi. Nyaraka ambazo hazikupatikana ni pamoja na: makisio ya mhandisi ya gharama; nyaraka za zabuni zilizogawiwa kwa wazabuni na zilizowasilishwa na wazabuni, taarifa ya tathmini iliyokamilika pamoja na barua za mawasiliano kati ya pande tofauti. Faili la Bodi ya Zabuni pia halikuwasilishwa kwa wakaguzi. Hii ni kinyume na matakwa ya kanuni ya 239(8) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

Mbali na mafaili ambayo hayakupatikana, baadhi ya mafaili yenye mawasiliano ya ujumla ama hayakupatikana au hayakuwa na ukamilifu. Kwa mfano, mafaili yanayoanzia mwaka wa fedha 2013 hadi 2017 hayakupatikana na hayakuwasilishwa.

Naishauri Menejimenti ikabidhi kumbukumbu za ununuzi zilizokosekana kwa ajili ya mapitio ya ukaguzi.

(ii) Manunuzi Kutumia Nyaraka za Zabuni Ambazo Hazijatimia

Nilibaini kuwa Mwajiri alianzisha mchakato wa manunuzi ya kazi ya ujenzi na mkataba wa kusimamiwa kazi bila kuwa na nyaraka zote zinazohitajika kwa ajili ya mchakato huo (rejea muhtasari wa kikao cha kuanza kilichofanyika 17 Novemba, 2013, ajenda kipengele Na. 7). Hii ilitokea kwa sababu mapitio ya usanifu hayakufanyika kama ambavyo ilitarajiwa au ulikuwa wa kiwango ambacho hakikutarajiwa. Huu ni uvunjaji wa kanuni 184 ya sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 na Kanuni 239(8) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

Naishauri Menejimenti iwe inatumia makabrasha ya zabuni yaliyotimia kama inavyoainishwa kwenye Ibara ya 184 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni ya 239 (8) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

(iii) Kutokuwepo kwa Matakwa ya Kiufundi na Michoro

Mkataba ulisainiwa bila kuwepo kwa matakwa ya kiufundi na michoro kwa sababu vilikuwa bado vinakusanywa; na mkandarasi alianza kazi bila ya kuwa na nyaraka hizi muhimu. Msimamizi wa kazi (Mhandisi Mshauri) M/S Don Consult alitaarifu kuwa, mkandarasi alikuwa ameanza kazi kwa kutumia nakala vivuli za nyaraka zake za zabuni zilizowasilishwa pamoja na zabuni yake. Hii ilishuhudiwa kutoka katika muhtasari wa makubaliano ya mkataba kipengele Na. 18 kinachoongelea umuhimu wa kuufanyia tathmini mradi ndani ya mwezi mmoja baada ya tarehe ya kuanza kazi. Ijapokuwa tathmini hiyo ilitarajiwa kuwa tayari ndani ya mwezi mmoja, matakwa ya kiufundi yalisainiwa na kuwasilishwa kwa mkandarasi na Mhandisi Mshauri mwaka mmoja baadaye. Zaidi, ilichukua muda wa takribani miaka mitatu kufanya tathmini hiyo. Tarehe ya kuidhinisha michoro ya njia ya bomba ya kugawa maji iliyopitiwa ni 2 Machi, 2018 na kuthibitishwa mahali penye njia ya bomba za kusafirisha maji ilikuwa 26 Machi, 2019. Mpaka mwezi Desemba 2020 kulikuwa hakuna seti kamili ya michoro iliyokuwa imeidhinishwa.

Upungufu huu ulichangia kuwapo kwa ubora hafifu wa kazi. Hii ni kwa sababu, kazi ya usanifu isiyokuwa kamili iliyofanywa na M/s. ECG na kazi ya kupitia iliyofanywa na M/S Don Consult ndizo zilizotumika kutengeneza nyaraka za kujazia zabuni zenye marudio zinazojumuisha michoro kwa ajili ya mkataba Na. III na IV kama inavyoshuhudiwa katika barua Na. DCL/MOW/PH2/2015/06 na DCL/MOW/PH2/2015/07 ya tarehe 13 Octoba, 2015 na 11 Novemba, 2015, mtawalia.

Zaidi ya hayo, ukosefu wa nyaraka za mkataba zilizotimia ulichangia kuwapo kwa athari hasi zifuatazo: migogoro, mabadiliko na uchelewaji katika utendaji kazi kutokana na mabadiliko ya upangaji wa bomba, maboresho katika tenki la kuhifadhia maji, nyongeza ya kazi ya uchimbaji katika eneo lenye mawe, mabadiliko ya nyongeza ya gharama kutokana na kukosekana kwa kipengele cha utoboaji wa chini ya reli na chini ya barabara. Haya yako wazi katika barua za mkandarasi Na. BDR/S539/0218/2019, BDR/S543/0218/2019, BDR/S537/0218/2019 ya tarehe 18 Februari, 2019, pamoja na muhtasari wa mkutano uliofanyika tarehe 17 Novemba, 2013, Ajenda kipengele cha saba.

(iv)Ulegezaji wa Masharti ya Mkataba

Nilibaini kuwa, katika nyaraka ya zabuni jumla ya malipo ya fedha ya awali yalikuwa 10% ya jumla ya bei ya mkataba, wakati marejesho ya fedha hiyo ya awali yalikuwa kiwango cha 10% ya kila Hati ya Malipo iliyokuwa inaidhinishwa. Katika makubaliano ilikubaliwa kuiongeza kiasi cha malipo ya fedha ya awali ifikie 20%; pia fedha ya marejesho ya fedha ya awali 18%. Hii ni kinyume cha kanuni 225(2) ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 ambayo inapiga marufuku makubaliano kubadili masharti na matakwa ya mkataba yaliyotajwa katika nyaraka za zabuni.

Naishauri Menejimenti itekeleze kikamilifu matakwa ya mikataba kama yalivyoanishwa katika mapungufu yaliyoainishwa hapo juu kuhusiana na vipengele vya mikataba na michoro.

(v) Kukosekana Uthibitisho wa Uhalali wa Ongezeko la Bei

Nilibaini kuwa tathmini ya mkandarasi ilikuwa na marekebisho ya makosa ambayo yalisababisha ongezeko la Dola za Marekani 202,367 (sawa na Sh. milioni 445) bila ya kuwapo kwa waraka wowote unaoweka wazi hilo ongezeko. Nilishindwa kuthibitisha endapo marekebisho yalikuwa halali, na kama yalikuwa yanakubaliana na kanuni[21] Na. 5(1) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013. Kutokana na tathmini ya wakaguzi, yafuatayo ni vipengele ambavyo vilionekana kuwa vimejazwa bei ya juu kama inavyoonyeshwa katika **Kiambatisho 9-1.**

Kiambatisho 9-1 kinaonesha kuwa vipengele vilijazwa bei ya juu sana. Hii ilisababisha ongezeko la bei kwa kiasi cha Dola za Marekani 1,486,041 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 3.2. Endapo uchambuzi mzuri ungefanyika, Wizara ingeweza kuokoa kiasi hicho cha fedha.

Naishauri Wizara ya Maji ihakikishe kwamba makadirio ya kiasi na gharama za vifaa yanapitiwa kwa umakini ili kuepuka uwezekano wa kuzidishwa kwa bei za vifaa.

(vi) Kufanya kazi Pasipokuwa na Mkataba Kulikotokana na Mwajiri Kuchelewa Kuidhinisha Mabadiliko

Kumekuwa na kuchelewa kuidhinisha mabadiliko ya nyongeza ya muda. Nilibaini matukio mawili, ambapo Mhandisi Mshauri alikuwa anafanya kazi pasipokuwa na mkataba uliohuishwa baada ya ule wa awali muda wake kuisha kabla kazi haijakamilika. Mara ya kwanza ni miezi 7 iliyokuwa kati ya Juni 2018 na Januari 2019 alipokuwa akisubiria kupitishwa kwa mabadiliko namba 1; na miezi 10 kati ya Desemba 2019 na Septemba 2020 alipokuwa akisubiria kupitishwa kwa Mabadiliko namba 2.

Naishauri Menejimenti iharakishe kufuatilia kibali cha mabadiliko ya mkataba (adenda) ili mkataba usajiliwe bila ya kuchelewa zaidi.

[21] PPA

(vii) Kutofuata Mwongozo wa Mfadhili

Sehemu 4.7 ya Mwongozo wa Manunuzi wa Mfadhili Mwenza[22] wa Mradi inataka Mwajiri kuwasilisha taarifa ya tathmini ya kiufundi kwa mfadhili ili ipitishwe kabla ya kuendelea na hatua ya ufunguaji wa taarifa za zabuni zinazotaja kiasi cha fedha. Ilibainika kuwa Mwajiri alikiuka sharti hili na mfadhili akamtumia Nukushi[23] akiilalamikia Wizara ya Maji ambayo ilifanya tathmini ya kiufundi na ya kutaja kiasi cha fedha kwa pamoja na kuiwasilisha kwa mfadhili. Taarifa hiyo ilikuwa imeunganishwa na akamtafuta mkandarasi wa mshindi wa mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe, kinyume na matakwa ya Mwongozo wa mfadhili. Kupitia nukushi ya mfadhili, ilibainika kuwa haikuwa mara ya kwanza kwa Wizara ya Maji kutofuata utaratibu na mwongozo kama mfadhili, kwani suala hilo lilitokea kwa Mradi wa Maji Mugango – Kiabakari-Butiama mkoani Mara.

Naishauri menejimenti iandae taarifa ya upembuzi wa kiufundi kama inavyoagizwa na Ibara 4.7 ya Mfadhili Mwenza wa Kifedha wa Mradi (Mfuko wa Maendeleo wa Saudia) na Ibara ya 4.7 ya Muongozo wa Manunuzi.

(viii) Majibu Yasiyoeleweka Wakati wa Ufafanuzi wa Zabuni

Majibu kwa hoja za wazabuni hayakufanyika vizuri kwa vile majibu yaliyotolewa hayakuwa na maelezo ya kutosha kuifunga hoja. Hii ni kinyume na matakwa ya Kanuni 239(8) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

Kwa mfano, maelezo Na. 1 yanayohusu ufafanuzi wa matakwa ya kiufundi juu ya aina ya mabomba ya DI yalikuwa hivi:

Jedwali 9- 7: Hoja za mzabuni na majibu ya mwajiri

Hoja ya mzabuni:	Majibu ya Mwajiri:
Kipengele Na. 02620, ukurasa wa 5 kati ya kurasa 10 sehemu 2.1.3-Unene wa kuta ni za daraja la ubora la K pamoja na viungio vyake vilivyotakiwa kwa mujibu wa kipengele ISO2531-1998 ambayo	Hii aina mpya ya viwango vya ubora[24] inaweza ikafuatwa baadaye katika hatua ya ununuzi wa vifaa. Hata hivyo,

[22] Saudi Fund for Development-SFD
[23] Fax Na. SFD REF. NO: TD-2013/18364 ya tarehe 12 Aprili 2013
[24] ISO classification

imepitwa na wakati, pamoja na hayo siku hizi tangu mwaka 2009 wazalishaji wa bomba za DI na viunganishi vyake wanazalisha daraja la ubora la daraja la C (C-Class) kama inavyotakiwa kwa mujibu wa kipengele ISO 2531-2009	inatarajiwa kuwa matakwa ya kiufundi kwa ujumla yatabaki vilevile.

Chanzo: *Nyaraka za zabuni*

Badala ya kutoa matakwa ya kiufundi ambayo yangesaidiwa na uchambuzi[25] wa kitaalamu, mwajiri alijibu kwa kusema "Hii aina mpya ya viwango vya ubora[26] inaweza ikafuatwa baadaye katika hatua ya ununuzi wa vifaa; na hata hivyo, inatarajiwa kwamba matakwa ya kiufundi kwa ujumla yatabaki vilevile". Matokeo yake, jibu hili ambalo halikuifunga hoja lilisababisha kutokea kwa mgogoro mkubwa wakati wa utekelezaji wa mradi ambao pia ulisababisha kuchelewa kukamilika kwa mradi na kuongezeka kwa gharama za bomba za chuma (DI).

Mapitio yaliyofanywa kwenye Uchambuzi wa Mhandisi Mshauri aliouwasilisha kwa barua Na. DCL/SMK/CONTRACT IV/BADR/516 ya tarehe 12 Octoba 2018 yameonesha kuwa, bei mpya za mabomba ya DI yamechangia kuongezeka kwa gharama kwa kiasi cha Dola za Marekani 1,504,435.92 kwa kutumia viwango vipya. Viwango vilivyotumika ni vile vilivyotumika kuleta mabomba ya DI kwa ajili ya mkataba Na. IV. **Jedwali Na. 9-8** linatoa ufafanuzi zaidi kuhusu tathmini niliyofanya kuhusiana na ongezeko la gharama.

Jedwali 9- 8: Gharama ya nyongeza kutokana na mabadiliko ya bei mabomba ya DI

Aina ya Bomba & saizi	Idadi iliyo rejewa (mpya) Kiasi (m)	Bei ya Zamani Dola za Marekani	Jumla katika Dola za Marekani	Bei Mpya Dola za Marekani	Jumla katika Dola za Marekani
Bomba la Chuma (DI) daraja la ubora C30 ukubwa DN900	1,202	554	665,908.00	609.56	732,691.12

[25] hydraulic analysis
[26] ISO classification

Bomba la Chuma (DI) daraja la ubora wa C30 ukubwa DN800	24,000	462	11,088,000.00	517.44	12,418,560.00
Bomba la Chuma (DI) daraja la ubora wa C30 ukubwa wa DN500	2,220	380	843,600.00	428.24	950,692.80
Jumla			12,597,508.00		14,101,943.92
Gharama iliyoongezeka					**1,504,435.92**

Source*: Uchambuzi wa Msimamizi wa Mradi (Consultant) Uliowasilishwa kwa barua yenye kumbukumbu namba: DCL/SMK/CONTRACT IV/BADR/516 ya tarehe 12 Octoba 2018*

Jedwali Na. 9-8 linaonesha ongezeko la kiasi cha jumla ya Dola za Marekani 1,504,435.92 ambacho ni sawa na ongezeko la Sh. bilioni 3.3. Ongezeko hili la gharama lilichangiwa na Wizara kushindwa kutoa maelezo ya kutosheleza kwa hoja zilizowasilishwa na wakandarasi wakati wa zabuni.

(ix)Mapungufu katika Uwasilishaji wa Zabuni na Uandaji wa Mikataba

Kuna madai kuwa, Mkandarasi M/S BADRI East Africa aliingiza barua za zabuni baada ya tarehe ya kuwasilisha zabuni kinyume cha sheria (rejea barua ya mshauri wa mradi yenye kumbukumbu namba DCL/SMK/CONTRACT IV/Client/1120 na 1126 za tarehe 26 Agusti, 2020 na 9 Septemba, 2020). Hata hivyo, barua hizi hazikuwasilishwa kwa bahasha tofauti; badala yake, ziliingizwa kwenye zabuni iliyowasilishwa. Aidha, Mzabuni hakuonesha rejea ya barua hiyo kwenye fomu yake ya zabuni. Mbaya zaidi, mwajiri alikubali barua zote kutoka kwa mzabuni/mkandarasi hata zile ambazo zilibadilisha masharti na matakwa muhimu ya zabuni. Hii ni kinyume na Kanuni 83 (1), 5 (1), 78 (1), 79 (3) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2013 na masharti ya jumla ya mkataba kifungu cha 15.6.3.

Barua za zabuni za Mkandarasi zinabadilisha matakwa muhimu ya kiufundi na matakwa yaliyoainishwa kwenye nukuu za makadirio ya ukubwa wa kazi na makadirio ya gharama za ujenzi na matakwa ya mkataba kwa ajili ya kumpendelea Mkandarasi. Hii ni kinyume na matakwa ya kanuni ya 83 (1), 5 (1), 78 (1) na 79

(3) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 na masharti ya jumla ya mkataba kifungu cha 15.6.3; ambapo, kwa pamoja vinazuia udanganyifu na ushawishi usiofaa.

Naishauri menejimenti ihakikishe mikataba inaandaliwa kwa ufasaha na kuwaelekeza wazabuni (wakandarasi) watekeleze matakwa ya ukabidhishaji wa zabuni kama inavyoelekezwa na Sheria na Kanuni za Manunuzi.

9.3.3 Kipengele cha Afya, Usalama na Mazingira

a) Kutokidhi Vigezo vya Alama za Usalama na Vifaa Kinga

(i) Kufanya Ujenzi bila Vifaa vya Kiusalama

Kulingana na ukaguzi uliofanyika, ilibainika kuwa hakukuwa na alama za kutosha za usalama kazini na vifaa kinga katika maeneo ya Mradi.

Mkandarasi wa Mkataba wa Kwanza alionekana kutofuata masharti ya afya na usalama kazini kama ilivyobainishwa katika Masharti ya Jumla Na. 4.8 ya Mkataba wa Mradi pamoja na Sheria ya Afya na Usalama kazini namba 5 ya mwaka 2003. Wafanyakazi katika mradi huu walifanya kazi bila kuwa na vifaa kinga, na hapakuwa na alama za maonyo katika mazingira hatarishi ya Mradi. Mazingira hatarishi, kama vile kiingilio cha maji ya mradi, hayakuwa na alama yoyote ya maonyo juu ya mazingira yaliyo karibu na mto ambao unasemekana kuwa na maji yenye kina kirefu. Picha namba 2 hapo chini inaonesha wafanyakazi katika eneo la mradi wakiendelea na kazi bila ya kuwa na vifaa kinga kamili vya kiusalama. Hali hii husababisha kuwa katika hatari ya kupata madhara.

Picha namba 9-2: *Wafanyakazi wakifanya kazi ya Kufunga nondo bila kuwa na Vifaa Kinga kamili (**Chanzo**: Taarifa ya Maendeleo ya Ujenzi wa Mradi)*

Vilevile, taarifa ya Afya na Usalama iliyoandaliwa na Afisa Afya na Usalama wa Mkandarasi ilionesha kuwapo kwa ajali iliyopelekea kifo cha mfanya kazi mmoja. Kifo hiki kilitokea kwenye Mtambo wa Kutibu Maji kutokana na kuanguka kutoka urefu wa mita saba alikokuwa akifanya kazi bila kuwa na vifaa kinga.

(ii) Ukosefu wa Udhibiti wa Uchafuzi wa Kisauti

Mkandarasi alikadiria kiasi cha Dola za Marekani 15,015.50 katika Kifungu cha 6.1 cha Kazi za Awali kipengele cha 8.7 cha Makadirio ya Gharama za Mradi. Kiasi hicho cha pesa kilitengwa kwa ajili ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira, hususani uchafuzi wa kisauti. Wakati wa ukaguzi, ilibainika kwamba hakukuwa na mikakati ya kutosha ya kupunguza uchafuzi huo wa mazingira kutokana na kutokuwapo kwa vigezo mahususi vilivyowekwa na Mkandrasi kwa kazi hiyo.

Vilevile, wakaguzi waliangalia kumbukumbu za malipo na kubaini kwamba kiasi cha Dola za Marekani 15,015.50 kililipwa kwa Mkandarasi kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 6.1 cha Kazi za Awali kipengele cha 8.7 cha makadirio ya gharama za mradi. Wakaguzi hawakuona umuhimu wa kuidhinisha malipo hayo kwa kuwa hakukuwa na uthibiti yakinifu wa Uchafuzi wa Kisauti katika Mradi husika.

(iii)Utekelezaji Usioridhisha Katika Masuala ya Kijamii na Kimazingira

Nilibaini kutokuwapo kwa tathmini ya Madhara ya Kijamii na Kimanzingira kama inavyohitajika kwa mujibu wa Kanuni za Usimamizi wa Mazingira Kifungu cha 81. Vilevile, Kifungu cha 63(8) cha Sheria ya Usajili wa Wahandisi ya Mwaka 2010 kinasisitiza kufanyika kwa tathmini ya madhara ya kijamii na kimanzingira kabla ya kuendelea na utekelezaji wa mradi wowote.

Wakati wa Ukaguzi, ilibainika kwamba mwajiri aliandaa tathmini ya msingi ya madhara ya kijamii na kimanzingira wakati mradi ulipoanza. Hata hivyo taarifa ya tahimini hiyo haikupelekwa si kwa Mkanadrasi wala Mshauri wa Mradi kwa ajili ya kutekeleza.

Kutohusishwa kwa tathmini ya masuala ya kijamii na kimazingira katika Mradi huu kumesabisha madhara makubwa katika usanifu. Mathalani, usanifu wa kiingilio cha maji ya mradi ulifanyika bila kuhusisha uwezekano wa kutokea mafuriko. Hii ilithibitishwa na kutokea kwa mafuriko mwezi Aprili 2020. Mafuriko haya yalizamisha miundo mbinu yote ya Kiingilio cha maji ya mradi hivyo kupelekea vifaa ghali kama pampu za maji kuwa katika hatari kubwa ya kuharibika kwa kuwa vilitakiwa kusimikwa chini ya uso wa ardhi. Kama suala la mafuriko lingehusishwa katika usanifu, aina mbadala wa pampu zinazosimikwa juu ya uso wa ardhi (pampu za wima) zingetumika badala ya kutumia zilizopo (za chini/za ulalo) ili kuepusha uwezekano wa kuzama kwenye maji kama ilivyoelekezwa kwenye picha namba 9.3 na 9.4 hapa chini:

Picha namba. 9-3 Aina na Muundo wa Pampu na mota zilizotumika kwenye Mradi.	Picha namba. 9-4 Aina na Muundo wa Pampu na mota ambazo zingetumika ili kuepusha madhara ya mafuriko.

Picha namba. 9.3 na 9.4: Ulinganisho wa aina na muundo wa pampu na mota zilizotumika kwenye mradi dhidi ya aina na muundo wa pampu na mota ambazo zingetumika ili kuepusha madhara ya mafuriko

(iv) Ukosefu wa Usalama wa Kutosha Katika Maeneo Ujenzi wa Mradi

Ilibainika kuwa suala la usalama wakati ujenzi wa mradi unaoendelea halikutiliwa maanani na wahusika. Hii ni kinyume na Masharti ya Jumla ya Mkataba Na. 4.8 pamoja na Kifungu cha 60, 62 na 93-0 cha Sheria ya Afya na Usalama Kazini namba 5 ya mwaka 2003 inayeelezea juu ya tathmini ya vihatarishi, vifaa kinga na usalama wa mfanyakazi.

Wakati wa ukaguzi hapakuwa na usalama wa kutosha wa kialama katika maeneo hatarishi. Mathalani, eneo la pampu za tenki la Kisangara hapakuwa na alama yoyote ya kiusalama ili kupunguza uwezekano wa kuanguka kutoka juu kama ilivyobainishwa katika picha namba 5. Vilevile, mitaro ya mabomba iliachwa wazi kwa muda mrefu bila kuwa na alama yoyote ya tahadhari kama ilivyoelelezwa na picha namba 9-5 na 9-6 hapo chini.

Picha namba 9-5: Eneo la Pampu ya Maji-Kisangara linaonesha eneo la wazi ambalo halijawekewa alama za zuio la kiusalama.	Picha namba 9-6: Mtaro wa Bomba la Maji ulioachwa wazi bila kuwa na alama za zuio la kiusalama.

Naishauri Menejimenti izingatie yafuatayo: kuwapitia wafanyakazi wake vifaa vya usalama maeneo ya ujenzi; kuandaa taratibu za kudhibiti uchafuzi wa mazingira kwa sauti; kufanya upembuzi wa athari za mazingira kwa jamii, na kuhakikisha tahadhari za udhibiti zinachukuliwa ili kupunguza uwezekano wa kutokea ajali za mapungufu ya kiusalama.

(v) Ukosefu wa Mpango wa Usimamzi wa Masuala ya Kijamii na Kimazingira

Kifungu cha 81(1, 2 na 3) na 99(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 na kifungu cha 63(8) cha Sheria ya Usajili wa Wahandisi ya Mwaka 2010 vinahitaji kuwapo kwa tathmini ya madhara ya manzingira kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi.

Katika kupitia taarifa mabalimbali za mafaili ya Mradi ilibainika kwamba tathmini ya Madhara ya Kimanzingira haikufanyika katika hatua za uandaaji wa mpango kazi wa mradi. Hali hii ilipelekea kutokuwapo kwa mikakati thabiti ya kuzuia uharibifu wa mazingira wakati wa utekekelezaji wa Mradi.

Wakati wa kutembelea eneo la Mradi ilibainika kuwepo kwa mitaro iliyo wazi kwa zaidi ya miezi sita. Mitaro iliyo wazi ni hatari kwa usalama wa jamii na wanyama wanaozunguka maeneo ya mradi.

Maeneo yaliyochimbuliwa kuzunguka tenki la maji la Kiverenge na Same Kuu hayakufukiwa vizuri. Hii inapelekea uwezekekano wa kuwapo kwa mmomonyoko wa udongo; hivyo kulegeza uimara wa matenki hayo kama ilivyoanishwa kwenye picha namba 8 hapo chini. Usanifu wa Mkataba namba IV wa Mradi huu wa Maji haukuzingatia madhara ya mmomonyoko wa udongo katika uimara wa majengo kwenye manteki ya Kiverenge na Same Kuu ambayo yamejengwa mlimani.

Kama inavyoonekana kwenye picha namba 9-7, 9-8 na 9-9, mitaro ya mabomba ya maji imeachwa wazi kwa mda mrefu. Katika kipindi cha ukaguzi kulikuwa na urefu wa takribani kilometa 23 za mitaro ya maji iliyokuwa haijafukiwa.

Picha namba 9-7: Mtaro ulio wazi katika bomba la maji la kuanzia Tenki la Kiverenge mpaka Tenki la Same Kuu.	Picha namba 9-8: Mmomonyoko wa Udongo kuzunguka Tenki la Maji la Kiverenge Tenki.	Picha namba 9-9: Mtaro ulioachwa wazi kusubiri uthibitisho wa gharama za uchimbuaji mawe katika bomba la maji la Kiverenge mpaka Same Kuu.

Naishauri Menejimenti itekeleze matakwa ya Sheria ya Menejimenti ya Mazingira ya mwaka 2004; na kuhakikisha kitengo husika kwenye Wizara ya Maji kinafanya kazi za menejimenti na usimamizi wa mazingira kwa ufanisi.

9.3.4 Usimamizi wa Mikataba Usiojitosheleza

Matokeo ya masuala yanayohusiana na kufuata vigezo na masharti ya mkataba, hususani katika usimamizi wa mradi unaolenga muda, gharama, ubora pamoja na malipo ya vyeti na adhabu (kama vile tozo kwa kuchelewesha kazi) yameelezewa katika sehemu hii.

a) Udhibiti wa Muda wa Mkataba Usiojitosheleza

Kanuni ya 114 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 zinaitaka taasisi nunuzi kuhakikisha kuwapo kwa usimamizi yanikinifu wa kazi yoyote inayofanyika na pia kuhakikisha kazi inakamilika kwa muda na gharama zinazokubalika.

Nilibainisha kuwa, mikataba yote mitatu ya Mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe ilishindwa kukamilisha utekelezaji wake kwa muda ulioainishwa katika mikataba hiyo. Taarifa juu ya kuisha kwa muda na asilimia ya ukamilishaji ya mikataba yote mitatu imeainishwa katika Jedwali Na. 9-9 hapo chini.

Jedwali 9- 9: Asilimia za ukamilifu wa miradi yote mitatu kama ilivyochukuliwa mnamo mwezi Desemba 2020

Mradi Na.	Muda wa Awali wa Ukamilifu	Muda wa Ukamilifu baada ya Marejeo	Asilimia za ukamilifu
I	16 Julai 2017	28 Oktoba 2019	64.00
III	4 Aprili 2021	HAUPO	60.35
IV	30 Julai 2019	31 Julai 2020	87.00

Chanzo: *Nyaraka za Mradi pamoja na Taarifa za Maendeleo ya Mradi*

Jedwali Na. 9-9 hapo juu linabainisha kuwa, asilimia za ukamilishaji wa mikataba yote si za kuridhisha. Mwishoni mwa mwezi Aprili 2021 huduma ya maji ilitakiwa iwe imepatikana katika wilaya za Same na Mwanga. Kinyume chake Mkataba Na.1 uliokuwa unatekeleza ujenzi wa miundo mbinu ya vyanzo vya maji ulikuwa umekamilika kwa 64% wakati miaka minne imeshakwisha. Hali hii inadhihirisha kuwa hakuna matarajio ya kupata huduma iliyokusudiwa kwa watumiaji wa maji.

b) Ongezeko la Muda kwa Sababu Ambazo Zinaweza Kuepukika

Ilibainika kuwa Wizara ya Maji iliidhinisha ongezeko la muda kwa sababu ambazo zinaweza kuepukika, na hakukuwa na ulazima wa kuongeza muda. Kumbukumbu za kuidhinisha ongezeko la muda zimeainishwa katika **Jedwali Na. 9-10** hapa chini.

Jedwali 9- 10: Ongezeko la muda wa kukamilisha mradi na sababu zake

Badiliko la Mkataba Na.	Tarehe Kuanza Ongezeko la Muda	Tarehe ya Kikomo cha Ongezeko la Muda	Sababu za kuongeza Muda
1	16 Julai, 2017	01 Mei, 2018	• Ucheleweshwaji wa Malipo ya Awali • Ucheleweshwaji wa Usanifu wa Mapungufu ya kazi za Umeme kati ya Michoro na Makadirio ya Gharama za Mradi • Ucheleweshwaji wa idhini ya kuendelea na manunuzi ya mabomba ya maji • Ukosefu wa hati ya kumiliki eneo na mabadiliko ya eneo la kujenga tenki la Kisangara • Ucheleweshwaji wa idhinisho la michoro ya nondo ya mkandarasi

Badiliko la Mkataba Na.	Tarehe Kuanza Ongezeko la Muda	Tarehe ya Kikomo cha Ongezeko la Muda	Sababu za kuongeza Muda
2	02 Mei, 2018	30 Novemba, 2018	• Ucheleweshwaji wa marekebisho ya usanifu wa umeme kutokana mapendekezo ya TANESCO • Ucheleweshwaji wa Usanifu wa Mapungufu ya kazi za Umeme kati ya Michoro na Makadirio ya Gharama za Mradi • Ucheleweshwaji wa idhinisho la michoro ya nondo ya mkandarasi
3	01 Desemba, 2018	19 Aprili, 2019	• Ucheleweshwaji wa Malipo ya Awali • Ucheleweshwaji unaotokana na shughuli za Umeme • Ucheleweshwaji wa idhini ya kuendelea na manunuzi ya mabomba ya maji • Ukosefu wa hati ya kumiliki eneo na mabadiliko ya eneo la kujenga tenki la Kisangara • Ucheleweshwaji wa kazi za pambu za maji • Mafuriko katika kiingilio cha maji y mradi • Ucheleweshwaji wa idhinisho la mfumo wa kuchanganya kemikali.

Chanzo: ***Mabadiliko ya Mkataba***

Jedwali Na. 9-10 linaainisha sababu zilizopelekea kuongezeka kwa muda wa kukamilisha mradi. Uchambuzi unaonesha kuwa sehemu kubwa ya sababu hizo ilitokana na ucheleweshaji wa malipo kwa mkandarasi, mapungufu katika usanifu, na ucheleweshaji katika kuidhinisha usanifu uliofanywa na Mshauri Mwelekezi wa Mradi. Hata hivyo, sababu tajwa hapo juu zingeepukika kama Wizara ingehakikisha kuwa kuna usimamizi wa kutosha wa mikataba.

Ongezeko la muda limepelekea kuongezeka kwa gharama za awali za Mradi kiasi cha Dola za Marekani 2,584,257.17 sawa na 43.45% ya gharama za awali. Pia, gharama za jumla za usimamizi wa mradi ziliongezeka kwa Dola za Marekani 906,947.44 sawa na ongezeko la 210% na Sh. 1,175,019,439.70 sawa na 931% ya gharama za mkataba.

Makadirio ya Chini ya Muda wa Usimamizi wa Mkataba

Wakati wa ukaguzi ilibainika kwamba Wizara haikuweka mipango thabiti ya Mkataba wa Usimamizi wa Mradi. Mkataba ulitakiwa uwe wa miezi 30 pamoja na miezi 12 ya taarifa za uharibifu/madhara, lakini Wizara ya Maji ilipitisha Mkataba wa miezi 30 tu ambao ni Mkataba wa Usimamizi wa Mradi tu. Hali hii ilipelekea badiliko la mkataba la kwanza ili kuongeza miezi 12 kufanya muda wa mkataba wa usimamizi uwe sawa na muda wa Mkataba wa Mkandarasi. Vilevile, kumekuwa na badiliko la mkataba la pili kuongeza wafanyakazi kutokana na ucheleweshwaji ulioainishwa katika mabadiliko ya mkataba wa mkandarasi na sababu za mabadiliko hayo. Hadi kufikia Desemba 2020, kulikuwa na ongezeko la muda wa mradi la miezi 30, sambamba na ongezeko gharama za Mradi la Sh. 1,770,750,000 sawa na 106% ya gharama za awali za mradi.

Naishauri Menejimenti iongeze usimamizi wakati wa kutekeleza mikataba ili kuhakikisha kazi zinazotekelezwa kwenye mkataba zinamalizika ndani ya wakati uliokubalika.

c) Kutojitosheleza Katika Usimamizi wa Gharama

Katika kupitia kumbukumbu za malipo, mapungufu yafuatayo yalibainika:

(i) Kutokujitosheleza Katika Mazungumzo ya Kupitisha Mikataba ya Nyongeza

Katika kupitia na kufanya uchambuzi wa gharama za awali za mradi, ilibainika kuwapo kwa gharama zilizoongezeka kutokana na ongezeko la muda lililobainishwa katika hati za malipo (IPC), ambapo kuna vipengele ambavyo gharama zake hazikupaswa kuongezeka kutokana na kutoathiriwa na ongezeko la muda. Hata hivyo, Wizara ya Maji ilipitisha vipengele hivyo na kusababisha ongezeko la gharama lisilo la lazima. Uchambuzi wa vipengele hivyo ni kama ulivyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-11** hapa chini.

Jedwali 9- 11: Vipengele ambavyo havikuathiriwa na muda lakini gharama zake ziliongezeka

Kipengele katika nukuu ya makadirio	Kipengele katika	kipengele	Gharama za mwanzo za mkataba	Jumla ya gharama zilizopitishwa mpaka sasa	Gharama zilizoongezeka (Dola za Marekani)

	hati za malipo		(Dola za Marekani)	(Dola za Marekani)	
ukurasa wa 1 kati ya 6 kipengele cha 10	4.4	Mengineyo (Ainisha)	756,297.4	1,199,069.03	442,771.63
Ukurasa wa 1 kati ya 6 kipengele 14	6.1	Kutengeneza picha za ujenzi	118	187.09	69.09
Kurasa ya 2 kati ya 6 kipengele cha 1	7.1	Mpangilio wa ukaguzi wa kiwanda	25,960	41,159.16	15,199.16
Ukurasa wa 2 kati ya 6 kipengele cha 2	7.2	Ukaguzi usiotegemea na huduma za vipimo	29,500	46,771.77	17,271.77
Ukurasa wa 2 kati ya 6 kipengele cha 10	8.7	Kuzuia kelele wakati wa ujenzi	15,016.50	22,048.57	7,032.07
Ukurasa wa 3 kati ya 6 kipengele 7	10.5	Mengineyo (Ainisha)	464,849.20	736,993.51	272,144.31
Ukurasa wa 3 kati ya 6 kipengele cha 11	14.1	Kamera ya kidigitali (pikseli kubwa 8)	472	1,498.91	1,026.91
Jumla kuu				**2,047,728.04**	**755,514.94**

Chanzo: *Nukuu za makadirio ya nyongeza ya kwanza ya mkataba na hati ya malipo namba 21*

Jedwali Na. 9-11 linaonesha kwamba Dola za Marekani 755,514.94 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 1.6 malipo yake yaliidhinishwa kwa vipengele ambavyo havikuathiriwa na ongezeko la muda. Kiasi hiki cha fedha kilicholipwa zaidi kwa Mkandarasi kimesababisha hasara kwa Serikali. Hali hii imesababishwa na: Wizara ya Maji kutopitia nyaraka; kutojitosheleza kwa maombi ya malipo yaliyofanywa na mkandarasi; na Mshauri Mwelekezi kutokufanya uchambuzi unaojitosheleza wa madai ya Mkandarasi.

(ii) Ucheleweshwaji wa Malipo kwa Wakandarasi

Nyaraka za mkataba (kiambatisho kwa zabuni namba 29 ya kanuni za jumla za mkataba namba 14.7(b)) kinataka malipo yafanyike ndani ya siku 90 kwa sarafu ya kigeni na ndani ya siku 60 kwa sarafu ya ndani baada ya kupokelewa na mhandisi mshauri.

Mapitio ya nyaraka za malipo ya mkataba namba 1 yanaonesha kuwapo kwa ucheleweshwaji wa malipo; ambapo malipo kwa wakandarasi wazawa ni kati ya siku 3 hadi 906 katika hati zote 19, na malipo kwa wakandarasi wa kigeni yanachelewa kati ya siku tano hadi 794.

Kuchelewa kwa malipo yaliyofanywa mpaka Julai 2019 kumesababisha riba ya kucheleweshwa kwa malipo kufikia dola 475,149.69 kama ilivyo katika barua ya mhandisi mshauri kwa Wizara ya Maji yenye Namba ya Kumb.ECGHH/SMK/MOW#128/2018 ya tarehe 6 Novemba 2019.

Zaidi, ilibainika kuwa malipo yote kwa mkandarasi ya mkataba namba tatu na nne yalichelewa. Kwa fedha za mfuko wa KUWAIT, muda mfupi uliocheleweshwa ulionekana kuwa siku 56 na siku nyingi za ucheleweshaji zilikuwa 161. Pia, kwa kuzingatia mfuko wa serikali ya Tanzania, muda mfupi uliocheleweshwa ni siku 66 wakati muda mrefu uliocheleweshwa ni siku 342.

Malipo yaliyocheleweshwa kwa mkandarasi yalisababisha gharama za madai ya kucheleshwa malipo kwa kufuata kanuni husika za mkataba (PCC) sehemu ya 43 inayotaka asilimia tatu ya kiwango cha riba kwa ucheleweshwaji wa malipo. Mpaka kufikia Novemba 2020, kuchelewa kwa malipo kulionekana katika hati za malipo nane, na ilipelekea gharama za madai ya Dola za Marekani 441,686.

Zaidi ya hayo, kuchelewa kwa malipo kwa mkandarasi kumepunguza maendeleo ya kazi za mradi na kupelekea usimamizi hafifu. Hii ilipelekea taratibu ndefu za uhakiki wa malipo kutoka Wizara ya Maji kwenda kwa wafadhili.

(iii)Malipo Yasiyo Sahihi ya Vipengele vya Awali

Nilibaini kuwa 95.8% ya jumla ya vipengele vya awali ililipwa, ambayo ni sawa na Dola za Marekani 4,437,700, kama ilivyoonekana katika hati namba 2 na 3 wakati maendeleo ya mradi yakifikia 54%. Hiyo ndiyo asilimia ya vipengele ya awali na ilizidi kwa asilimia 41.8 ambayo ni sawa na Dola za Marekani 1,215,110 kama ilivyotajwa katika jedwali Na. **9-12** hapa chini. Hivyo, malipo ya vipengele vya awali yaliyozidi yalisababisha

mradi kuwa katika hatari ya kutorejesha kiasi kilicholipwa ikitokea mkataba umevunjwa.

Jedwali 9- 12: Hali ya malipo ya vipengele vya awali

Jumla ya vipengele vya awali kulingana na hatua ya mradi	Kiasi (Dola za Marekani)	Asilimia
Kiasi cha Mkataba	2,911,000	100.0
Jumla ya kiasi kilicholipwa	2,791,000	95.8
Kiasi kilichotakiwa kulipwa kulingwana na hatua ya mradi	1,575,890	54.0
Jumla ya vipengele vya awali vilivyozidishiwa malipo	1,215,110	41.8

Chanzo: *Marejeo ya nyaraka za mkataba na ripoti za maendeleo ya mradi*

Nashauri kuwa, aidha Wizara ya Maji itoe maelezo ya fedha zilizolipwa zaidi ya kiwango kilichopangwa na malipo yasiyothibitshwa ambayo yalilipwa kwa wakandarasi, au Menejimenti irudishe fedha hizo kutoka kwa wakandarasi.

d) Masuala ya Usimamizi wa Ubora

Uhakiki wa ubora katika mradi wa maji Same-Mwanga-Korogwe umelezewa katika sehemu namba 01400 (mahitaji ya ubora wa vipimo) na katika Mwongozo wa usanifu wa Wizara ya Maji ya mwaka 2009. Kutokana na kuzuru maeneo ya ujenzi mapungufu yafuatayo yalibainika kuhusiana na ubora wa kazi:

(i) Kunyimwa Ubora wa Miundo Iliyojengwa

Mara baada ya kuzuru maeneo ya ujenzi ilibainika kuwa baadhi ya miundo iliyojengwa haikuwa katika ubora mzuri. Miundo ambayo haikuwa katika ubora mzuri imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 9-13.**

Jedwali 9- 13: Kasoro zilizoonekana wakati wa ukaguzi wa ujenzi

Eneo la muundo	Jina la muundo	Kasoro zilizoonekana	madhara	sababu
Kiingizo cha maji	Zege la tenki la maji ghafi	nyufa	Inaweza kupunguza uimara wa zege	Utendajikazi hafifu
	Chumba cha mita ya mtiririko	makovu katika zege	Nondo inaweza kutokeza na kusababisha kutu	Utendajikazi hafifu
Kituo cha Umeme	Nyumba ya Kudhibiti Umeme	Kutu katika nondo za nguzo	Inaweza kupunguza nguvu ya nondo	Utendajikazi hafifu

		Mkunjo wa nondo za nguzo kutokana na ukosefu wa kianzilishi cha ngazi.	Inaweza kupunguza nguvu ya nondo	Utendajikazi hafifu
Mtambo wa kutibu maji	Zege la njia ya kutembelea	Nyufa za kutoka juu kwenda chini	Inaweza kupunguza uimara wa zege	Utendajikazi hafifu
	Ukuta wa nyumba ya kusukuma maji	Nyufa ya ukuta	Inaweza kupunguza uimara wa zege	Utendajikazi hafifu
Kisangara	Tenki la maji la Kisangara	makovu katika ukuta wa tenki	Kufichua Nondo kupata kutu	Utendajikazi hafifu

Chanzo: *Uchambuzi wa kikaguzi juu ya kasoro zilizoonekana wakati wa kuzuru eneo la ujenzi*

Jedwali Na. 9-13 linaonesha kasoro nyingi zilizoonekana zilisababishwa na utendaji kazi usioridhisha wakati wa ujenzi.

Kulikuwa na masuala ya utendajikazi katika zege la miundo ya kutibu maji, hasa makovu katika zege kuonesha udhaifu katika kudhibiti ubora wakati wa kazi za zege kama ilivyooneshwa katika picha iliyochukuliwa katika mkataba namba 1.

Picha namba 9-10: ubora hafifu wa zege na utendajikazi katika mtambo wa kutibu maji katika Nyumba ya Mungu – mkataba namba 1.

(ii) Matokeo ya Vipimo vya Ubora wa Zege na Ushindiliaji wa Udongo

Majaribio ya nasibu yalifanyika kupitia maabara ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ya mkoani Kilimanjaro kuangalia ubora wa zege katika ujenzi wa miundo na kufukia udongo katika mifereji ya bomba. Muhtasari wa matokeo kwa mkataba namba 1,3 na 4 yamewasilishwa katika **Jedwali Na. 9-14.**

Jedwali 9- 14: Matokeo ya miundo ya zege na udongo kwa mkataba Namba 1

Kipengele	Kipimo	Matokeo	Mahitaji ya kiufundi	Maoni
A. Nguvu ya zege katika Nyumba ya Mungu - mkataba namba 1	N/mm^2			
Shimo katika kituo cha kusukuma maji (Tenki la maji la Kisangara)	N/mm^2	35.6	35	Imefaulu
Shimo katika kituo cha kusukuma maji (tenki la Kisangara)-ukuta	N/mm^2	40.4	35	Imefaulu
Kituo cha kusukuma maji ghafi- zege la Dari	N/mm^2	37.5	35	Imefaulu
Kituo cha kusukuma maji ghafi- zege la dari	N/mm^2	44.3	35	Imefaulu
Nyumba ya kusukuma maji yalio tibiwa-ukuta	N/mm^2	41.5	35	Imefaulu
Nyumba ya kusukuma maji yaliyotibiwa-zege la kitako	N/mm^2	39.1	35	Imefaulu
Nyumba ya kusukuma maji yaliyotibiwa - zege la dari	N/mm^2	38.0	35	Imefaulu
B. Vipimo vya Ushindiliaji wa udongo - mkataba namba 1				
Wastani wa nyuzi ya ushindiliaji katika mfereji wa bomba -mkataba namba 1				
i) Eneo la 1		87.9	80-90%	Imefaulu
ii) Eneo la 2		56.5	80-90%	Imefeli
iii) Eneo la 3		80.4	80-90%	Imefaulu
C. Vipimo vya Nguvu ya zege kisangara - Mwanga - mkataba namba 3				
Tenki la Mwanga (ukuta)	N/mm^2	39.7	35	Imefaulu
Tenki la Mwanga - zege la Mfuniko	N/mm^2	31.7	35	Imefeli
Tenki la Mwanga (ukuta namba 2)	N/mm^2	39.4	35	Imefeli
D. Vipimo vya ushindiliaji wa udongo mkataba namba 3				
Wastani wa nyuzi ya ushindiliaji katika mfereji wa bomba - mkataba namba 3				
i) Eneo la 1		69.0	80-90%	Imefeli
ii) Eneo la 2		75.3	80-90%	Imefeli
iii) Eneo la 3		64.4	80-90%	Imefeli

Kipengele	Kipimo	Matokeo	Mahitaji ya kiufundi	Maoni
E. Vipimo vya nguvu ya zege katika tenki la Kiverenge same-mkataba namba 4				
Tenki la Kiverenge				
i) Kuta	N/mm^2	41.8	35	Imefaulu
ii) Mfuniko	N/mm^2	36.2	35	Imefaulu
iii) Sakafu	N/mm^2	37.5	35	Imefaulu
Tenki la Same kuu				
i) Kuta	N/mm^2	42.3	35	Imefaulu
ii) Mfuniko	N/mm^2	33.3	35	Imefeli
iii) Sakafu	N/mm^2	36.4	35	Imefaulu
F. Vipimo vya ushindiliaji wa udongo-mkataba namba 4				
Wastani wa nyuzi za ushindiliaji katika mfereji wa bomba – mkataba namba 4				
Kipengele		**Matokeo**	**mahitaji**	**Maoni**
G. Vipimo vya nguvu ya zege katika Nyumba ya Mungu - mkataba namba 1				
i) Eneo la 1		65.8	80-90%	Imefeli
ii) Eneo la 2		61.9	80-90%	Imefeli

Chanzo: *Taarifa ya matokeo ya vipimo yaliyofanyika na maabara ya TANROADS Kilimanjaro, 2020*

Jedwali Na. 9-14 inaonesha kuwa kuna miundo ambayo imefeli katika vipimo vya ubora. Eneo lililoathirika kwa kiwango cha juu lilikuwa katika ushindiliaji wa udongo ambalo limeonekana kuwa na tatizo katika mikataba yote mitatu. Baadhi ya miundo ilifeli katika vipimo vya nguvu ya zege. Hali ni mbaya zaidi katika mkataba namba 1.

Hivyo ushauri wangu ni kuwa, Menejimenti iandae haraka mpango kazi kwa ajili ya viporo vya kazi, na ihakikishe kuna bajeti ya kutosha kufadhili kazi hizo. Aidha nashauri iwekwe juhudi ya kukamilisha mtambo mkuu wa kutibu na kusukuma maji kutoka Nyumba ya Mungu kwenda Kisangara. Pia, ifuatie kazi ya kuweka mabomba ya kusafirisha maji kwenda sehemu

za kuhifadhia maji. Kisha ifuatiwe na kazi ya kuweka mtandao wa maji na kuunganisha majumbani.

(iii)Ubora Mzuri wa Miundombinu Iliyojengwa kwa Zege

Vipimo nasibu visivyo haribifu vilifanyika ili kuangalia ubora wa zege katika miundo ya ujenzi. Vipimo hivyo vya zege vilikuwa katika kuta na dari la tenki la Kisangara, dari na kuta nyumba ya kusukuma maji ghafi, kuta katika nyumba ya kusukuma maji yaliyotibiwa, kitako na dari. Muhtasari wa matokeo umeoneshwa katika **Jedwali Na. 9-15.**

Jedwali 9- 15: Matokeo ya vipimo visivyoharibifu katika miundombinu ya mradi

Kipengele	Matokeo	Mahitaji ya kiufundi	Kipimo	Maoni
Kitako cha kituo cha kusukuma maji (tenki la Kisangara) - zege	35.6	35	N/mm^2	Imefaulu
Kitako cha kituo cha kusukuma maji (tenki la kisangara) - ukuta	40.4	35	N/mm^2	Imefaulu
Kituo cha kusukuma maji ghafi-zege	37.5	35	N/mm^2	Imefaulu
Kituo cha kusukuma maji ghafi - ukuta	44.3	35	N/mm^2	Imefaulu
Nyumba ya kusukuma maji ghafi-ukuta	41.5	35	N/mm^2	Imefaulu
Nyumba ya kusukuma maji ghafi (kitako)	39.1	35	N/mm^2	Imefaulu
Nyumba ya kusukuma maji yaliyotibiwa	38.0	35	N/mm^2	Imefaulu

Chanzo: *Taarifa ya vipimo vya maabala vilivyofanyika na TANROADS*

Jedwali Na. 9-15 linaonesha kuwa kupitia vipimo vilivyofanyika kwa ajili ya kuangalia nguvu ya zege, miundo yote ilifaulu kutokana na vipimo vyote kufuzu mahitaji ya kiufundi ambayo kiwango cha chini kilitakiwa kuwa mgandamizo wa 35 N/mm^2.

(iv) Ubora wa Ushindiliaji wa Udongo

Vipimo haribifu vilifanyika katika udongo wa kujaza katika mifereji ya kulaza bomba ili kutathmini kiwango cha ushindiliaji na bomba la chuma kama ifuatavyo.

Matokeo ya Vipimo vya Ushindiliaji

Matokeo ya vipimo vya ushindiliaji yamewasilishwa katika **Jedwali Na. 9-16** hapo chini.

Jedwali 9- 16: Matokeo ya vipimo vya ushindiliaji katika maeneo ya mradi

Kipengele	Kizio	Mahitaji ya kiufundi	Kipimo	Maoni
Vipimo vya ushindiliaji wa udongo mkataba namba 1				
Wastani wa viwango vya ushindiliaji katika njia za bomba – mkataba namba 1				
Eneo la 1	N/mm^2	87.9	80-90%	Imefaulu
Eneo la 2	N/mm^2	56.5	80-90%	Imefeli
Eneo la 3	N/mm^2	80.4	80-90%	Imefaulu
Wastani wa viwango vya ushindiliaji katika njia za bomba – mkataba namba III				
Eneo la 1	N/mm^2	80-90%	69.0%	Imefeli
Eneo la 2	N/mm^2	80-90%	75.3%	Imefeli
Eneo la 2	N/mm^2	80-90%	64.4%	Imefeli

Chanzo: *Taarifa ya Vipimo vya Matokeo Kutoka TANROADS 2020*

Jedwali Na. 9-16 linaonesha vipimo vya uhakiki wa ubora kwa udongo uliotumika kufukia mabomba. Imebainika kuwa maeneo mawili kati ya sita yaliyochaguliwa yalifaulu. Maeneo manne yaliyobaki hayakufikia hitaji la kiwango cha chini kama ilivyo katika mahitaji ya ufundi sehemu ya 01400. Hii huonesha kuwa ubora wa ushindiliaji haukufikia viwango vilivyowekwa.

Vipimo Visivyo Haribifu

Vipimo visivyo haribifu vilifanyika katika miundo ya zege katika kuta na dari za tenki la Mwanga. Matokeo ya vipimo yamewasilishwa katika **Jedwali Na. 9-17** hapo chini.

Jedwali 9- 17: Matokeo ya vipimo vya nguvu ya zege Kwa mkataba Namba III

Kipengele	Mahitaji ya kiufundi	Matokeo	Maoni
Vipimo vya nguvu ya zege - mkataba namba 3			
Tenki la Mwanga (ukuta)	35 N/mm^2	38.7N/mm^2	Imefaulu
Tenki la Mwanga (dari ya juu)	35 N/mm^2	31.7N/mm^2	imefaulu

Chanzo: *matokeo ya vipimo vya maabara vilivyofanyika na TANROADS 2020*

(v) Kufanya Kazi Bila ya Viwango na Miongozo Muhimu

Mahitaji ya kiufundi sehemu ya 014000 sehemu ndogo ya 1.6.5: Alama na viwango - inataja kwamba mkandarasi anatakiwa kukabidhi kwa mhandisi mshauri nakala mbili za viwango vya sasa, maelezo ya kiufundi, taratibu na alama za utendaji, mitambo na vifaa vilivyokabidhiwa. Tofauti ya alama na viwango ikitokea, kanuni kali zitatumika.

Imeonekana kuwa si Mkandarasi pekee bali hata Mhandisi Mshauri hawakuwa na nakala ya viwango husika vilivyotajwa katika maelezo ya kiufundi ya mkataba kama nukuu ya nyaraka kwa kufuata pamoja na kuthibitisha.

Vihatarishi vinavyohusiana na ukosefu wa nakala ni kuwapo kwa ubora usiojitosheleza na udhaifu katika utekelezaji wa kazi kama ilivyoshuhudiwa katika usakinishaji wa mabomba. Usakinishaji wa mabomba ulitumia malighafi isiyoidhinishwa ya kufukia bila ushindiliaji sahihi. Katika hali hiyo, mabomba yana uwezekano wa kuharibika mapema.

(vi)Ubora Usioridhisha wa Kazi ya Usakinishaji

Ukaguzi katika eneo la ujenzi ulionesha kuwa ubora wa usakinishaji wa mabomba haukuwa wa kuridhisha, na haukufuata mahitaji ya mwongozo wa usanifu wa Wizara ya Maji ya mwaka 2009 sura ya 4 pamoja na mahitaji ya kiufundi sehemu ya 02300 kulingana na usakinishaji wa mabomba, ufukiaji na ushindiliaji, hii ilishuhudiwa katika picha namba 11 na 12.

Vilevile, imeonekana katika picha namba 11 na 12 kuwa ufukiaji wa mabomba ulifanyika kwa kutumia udongo usiofaa ambao umechimbwa katika mifereji ya kulaza bomba bila ya kushindiliwa. Hii ni kinyume na mwongozo wa usanifu wa Wizara ya Maji ya mwaka 2009 sehemu ya 4.1.1.3 na mahitaji ya kiufundi sehemu ya 02300. Mkandarasi hakufuata taratibu stahiki na mahitaji ya kiufundi. Pia, Mhandisi Mshauri hakukagua na kuhakiki kazi zake. Hii ni kinyume na kanuni za jumla za mkataba wa Mhandisi Mshauri ambayo inashauri kulinda manufaa halali na kanuni za jumla za mkataba sehemu ya 7.1 vinataka Mhandisi Mshauri kutekeleza kazi zake kwa uaminifu.

Picha namba 9-11: Kufukia kwa kutumia udongo dhaifu mweusi, kutoshindiliwa kwa mabomba magumu ya plastiki ya milimita 500 - mtandao wa usambazaji Same-Mwanga.	**Picha namba 9-12**: Kufukia kwa kutumia udongo dhaifu mweusi, kutoshindiliwa kwa mabomba magumu ya plastiki kwa mtandao wa usambazaji wa Same-Mwanga
	

Picha namba 9-13: Ufukiaji kwa kutumia malighafi zenye mawe zilizochimbwa kwa bomba la chuma la usambazaji mkuu yenye kipenyo cha milimita 900 karibu na Kiverenge-Same kuu.

Naishauri Menejimenti iandae miongozo ya utekelezaji wa kazi za maji na kuanza kutumia kama inavyoelekezwa na Ibara ya 014000 na Ibara ndogo ya 1.6.5 ya taratibu na viwango.

(vii) Ubora wa Zege Usioridhisha na Ushindiliaji Usioridhisha wa Malighafi ya Ufukiaji Mabomba

Wakati wa kuzuru eneo la ujenzi, vipimo wa ubora wa zege vilifanyika. Nilibaini kwamba, vipimo vya dari ya juu vilivyopimwa katika Same Kuu vilifeli, lakini Mhandisi Mshauri alikagua na kupitisha kazi zake. Hii ni kinyume na kanuni za jumla za Mhandisi Mshauri namba 3.1.1 na 7.1 ambavyo vinamtaka kusimamia shughuli za ujenzi kwa uaminifu.

Zaidi, vipimo vya kinasibu vya kuangalia ubora wa kazi kwenye ushindiliaji wa udongo wa kufukia mabomba vilifanyika. Matokeo ya vipimo vya malighafi hizo yameoneshwa katika **Jedwali Na. 9-18** hapa chini.

Jedwali 9- 18: Matokeo ya vipimo vya udongo na zege kwa mkataba Namba 1

kipengele	Matokeo	Mahitaji ya kiufundi	Kipimo	Maoni
Vipimo vya nguvu ya zege kwa Kiverenge Same - mkataba namba 4				
Tenki la Kiverenge				
i) kuta	41.8	35	N/mm^2	Imefaulu
ii) Dari ya paa	36.2	35	N/mm^2	Imefaulu
iii) Dari ya sakafu	37.5	35	N/mm^2	Imefaulu
Tenki Same kuu				

kipengele	Matokeo	Mahitaji ya kiufundi	Kipimo	Maoni
i) kuta	42.3	35	N/mm^2	Imefaulu
ii) Dari ya paa	33.3	35	N/mm^2	Imefeli
iii) Dari ya sakafu	36.4	35	N/mm^2	Imefaulu
Vipimo vya ushindiliaji vya udongo-mkataba namba 4				
Wastani ya viwango vya ushindiliaji kwa mkataba namba 4 katika mabomba				
i) Eneo la 1	65.8	80-90%		imefeli
ii) Eneo la 2	61.9	80-90%		imefeli

Chanzo: *Taarifa vipimo vya maabara vilivyofanyika TANROADS*

Nashauri Wizara ya Maji itathmini: (a) Njia zote za mabomba ya maji yalipopitishwa na kubainisha maeneo yote yenye kasoro katika ushindiliaji na kurekebisha kasoro hizo; na (b) Uimara wa tabaka la zege lililowekwa na kubainisha kasoro zote na kuzirekebisha ipasavyo.

9.3.5 Masuala ya Usimamizi wa Mikataba

a) Kuidhinishwa kwa Ongezeko la Muda Baada ya Mkataba Kuisha Muda Wake

Katika kupitia mabadiliko ya Mkataba, ilionekana kuwa mabadiliko ya mkataba yaliidhinishwa baada ya muda wa mkataba kukamilika. **Jedwali Na. 9-19** hapa chini linafafanua hali halisi.

Jedwali 9- 19: Kuchelewa kuidhinisha mabadiliko ya mkataba kwa ajili ya kuongeza muda wa mkataba

Kipengele	Muda wa Mkataba Kumalizika	Tarehe ya Uthibitisho wa Ongezeko la Muda.	Muda Uliocheleweshwa (Siku)
Badiliko la Mkataba Namba 1	16 Julai, 2017	17 Julai, 2017	1
Badiliko la Mkataba Namba 2	02 Mei, 2018	27 Mei, 2018	25
Badiliko la Mkataba Namba 3	01 Desemba, 2018	18 Februari, 2019	79

Chanzo: *Mabadiliko ya mkataba*

Jedwali Na. 9-19 linaonesha muda wa ucheleweshaji katika kuidhinisha ongezeko la muda wa kazi katika mkataba kati ya siku ya 1 hadi 79. Hii inamaanisha kwamba, baadhi ya kazi zilifanyika

bila ya kuwapo kwa mkataba, ambapo ni kinyume na matakwa ya Kanuni ya 111(1) (4), 5(1) 5(2) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

b) Ongezeko la Muda Nje ya Utaratibu

Ukaguzi wa nyaraka za kikao cha ngazi ya juu kilichoitishwa tarehe 18 Machi, 2020 pamoja na barua ya mwajiri yenye Kumbukumbu Na. BC 226/303/05A/05 ya tarehe 2 Aprili, 2020, nilibaini kuwa, Mwajiri aliongeza tena siku 338 kama muda wa matazamio kwa mkandarasi kuendelea na kazi ambao ulikwisha mwezi wa tisa, 2020. Hii ni baada ya kuisha kwa ongezeko la muda wa mradi. Hakuna kifungu kwenye mkataba kinachoonesha mwajiri kutoa muda wa matazamio kwa mkandarasi; na ni kinyume na Kanuni 5(1) na 111(1) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 pia ni kinyume cha Masharti ya Jumla ya Mkataba 1.1.3.3, 8.2 & 8.7. Ijapokuwa Mkandarasi alipewa muda wa matazamio kuendelea na kazi bila ongezeko la fedha, lakini muda huo wa huruma ulisababisha ongezeko la fedha kwa mkataba wa Mhandisi Mshauri wa mradi ECG. Kwa kufuata kiambatisho cha kipengele cha 16 kwenye Masharti ya Jumla ya Mkataba 8.7 na 14.15 (b) ya zabuni, mwajiri alitakiwa kufidia ongezeko la fedha la Mhandisi Mshauri wa mradi kutoka kwenye malipo ya Mkandarasi.

c) Mkandarasi Kufanya Kazi Bila Dhamana Kuanzia Mwezi Desemba 2019 Mpaka Mwezi Desemba 2020

Wakati wa Ukaguzi, nilibaini kuwa mkandarasi hakupeleka dhamana ya utendaji, dhamana ya malipo ya awali na bima ya mradi licha ya kukumbushwa mara nyingi na Mhandisi mshauri, kinyume na Masharti ya Jumla ya Mkataba 4.2 na 18. Mkandarasi alipeleka maoni kwa mwajiri ya kumaliza kazi badala ya kutumia hizo gharama kulipia hizo dhamana hii ni kupitia barua ya mkandarasi yenye kumbukumbu namba REF/MAK/SMK//4.2#0204/20 ya tarehe 11 Octoba, 2020 na REF/MAK/SMK//4.2#0205/20 ya tarehe 26 Octoba, 2020, wakati huo mkandarasi aliomba malipo ambayo hayajalipwa yafidie gharama za dhamana anazotakiwa kuwa nazo, mwajiri hakuchukua hatua yeyote katika hilo.

Wakati wa kutembelea maeneo ya mradi, niligundua kuwa Wizara ya Maji hawakujibu mapendekezo ya Mkandarasi; na Mkandarasi alisimamisha kazi nyingi kutokana na kutojibiwa na Wizara ya Maji. Mhadisi Mshauri alimuomba mwajiri kumjibu Mkandarasi ili kupata mwafaka wa mapendekezo ya Mkandarasi kupitia barua yenye kumbukumbu: ECGHH/SMK/MOW#189/2020 ya tarehe 14 Octoba, 2020.

d) Kuchelewa Kuundwa kwa Bodi ya Usuluhishi

Wakati Masharti Maalum ya Mkataba 20.2.1 imeeleza kuwa pande mbili za mkataba zitateua bodi ya usuluhishi baada ya kuanza mradi. Mwezi Septemba, 2019 Mkandarasi alifanya juhudi kwa kuanzisha mchakato wa kupata bodi ya usuluhishi (REF/MAK/SMK/4.2#0159/19 kwa msisitizo wa ushauri wa mhadisi mshauri kwa mwajiri kwa barua yenye kumbukumbu namb: ECGHH/SMK/MOW#126 ya tarehe 30 Septemba, 2019. Hapakuwa na mrejesho wala ushirikiano chanya toka kwa mwajiri. Kwa hiyo, migogoro mingi kati ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri haikupatiwa ufumbuzi. Hivyo basi, kuchelewa kuundwa kwa bodi ya usuluhishi wa migogoro hakukupatiwa ufumbuzi; hivyo kupelekea ongezeko la muda na gharama ya mradi.

Naishauri Menejimenti ishughulikie mapungufu ya Menejimenti ya mikataba kama yalivyojadiliwa hapo juu kwenye maeneo ya ununuzi, ukaguzi wa ndani na Menejimenti ya mikataba. Aidha, naishauri Menejimenti ifanyie mapitio ya haraka na kuhuisha makabrasha yote ya mikataba (kama vile maelekezo ya zabuni, taratibu za mikataba, gharama za makadirio ya vifaa, na michoro na majedwali ya mkataba mmoja mmoja).

9.3.6 Usimamizi wa Rasilimali Watu Usiojitosheleza

Matokeo ya ukaguzi katika usimamizi wa rasilimali watu yaliyojumuishwa katika sehemu hii yameelezewa kwa kuzingatia watekelezaji muhimu wa mradi kama ilivyoainishwa hapa chini:

a) Idadi ya Wafanyakazi Isiyojitosheleza

Upungufu wa Wataalamu wa Kiufundi Wenye Sifa

Nilifanya tathmini ya maeneo matatu ya Wizara ya Maji ambayo ilikuwa inahusika kwa ukaribu zaidi na utekelezaji wa mradi. Iligundulika kuwa vitengo hivyo vina upungufu wa wafanyakazi 56 kati ya wafanyakazi 68 wanaohitajika, sawa na 76%. **Jedwali Na. 9-20** hapo chini linaonesha uchambuzi zaidi juu ya upungufu wa wafanyakazi.

Jedwali 9- 20: Idadi ya wataalamu wa kiufundi kwenye vitengo vya maji vilivyohitajika Wizara ya Maji

Kitengo	Taarifa za wafanyakazi			Upungufu katika asilimia (%)
	Mahitaji 'A'	Waliopo 'B'	Upungufu 'C=A-B'	(A-B/A)*100%
Idara ya inayoshughulikia vyanzo vya Maji (DWR)	17	8	9	53
Idara inayohusika na Usambazaji maji safi na ukusanyaji maji taka (DWSS)	39	7	32	82
Idara ya ubora wa Maji (DWQ)	12	1	11	92

Chanzo: *Orodha ya Watumishi wa Wizara ya maji kwa mwaka 2020/21*

Upungufu wa wafanyakazi uliopo katika Wizara ya Maji umechangia kuwapo kwa ushiriki usiojitosheleza wa wataalamu wa kiufundi katika mradi wa Same-Mwanga–Korogwe. Hii ilithibishwa kwa kuwapo kwa msimamizi wa Wizara ya Maji ya Maji katika mradi, ambaye ni Mhandisi wa Magari (Automobile Engineer), badala ya Mhandisi Ujenzi. Hii ni kinyume na kifungu 64(1) cha Sheria ya Usajili wa Wahandisi ya Mwaka 2010 Sura ya 63 ambacho kinaainisha kuwa kila kazi za uhandisi lazima isimamiwe na Mhandisi wa kada husika ambaye lazima awe kwenye eneo la mradi wakati kazi za ujenzi zikiwazinaendelea.

b) Upungufu wa Watumishi Katika Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi

Kifungu cha 37(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kinabainisha kwamba, katika kila Taasisi nunuzi lazima kuanzishwe kitengo cha manunuzi chenye wataalamu wanaotosheleza. Kitengo cha manunuzi lazima kiwe na

wataalamu wa manunuzi, wataalamu wa kiufundi, pamoja na wataalamu wa utawala kadiri watakavyohitajika.

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa, Kitengo cha manunuzi kilichopo katika Wizara ya Maji kina ukosefu wa wataalamu wa kiufundi na wa manunuzi. Maelezo ya muundo wa kitengo cha manunuzi katika Wizara ya Maji yameainishwa katika **Jedwali Na. 9-21** hapo chini.

Jedwali 9- 21: Idadi ya wataalamu wa Kitengo cha Manunuzi katika Wizara ya Maji

Kada	Idadi ya wataalamu waliyopo			Asilimia
	wanaohitajika	Awaliopo	Upungufu	Upungufu (%)
	'A'	'B'	'C' = A-B	=A-B/A*100
Mkurugenzi	1	1	0	-
Afisa ugavi mkuu daraja la I	1	1	0	-
Afisa ugavi mwandamizi	2	2	0	-
Afisa ugavi daraja I	4	4	0	-
Afisa ugavi daraja II	10	7	3	30
Jumla	**18**	**15**	**3**	**17**

Chanzo: *Makadirio ya Mahitaji ya watumishi katika Wizara ya Maji kwa mwaka 2020/21*

Hali hii imesababisha utendaji hafifu katika Wizara ya Maji. Kwa mfano, mapungufu katika uandaaji wa nukuu za makadirio ya ukubwa wa kazi na bei yalipelekea mkataba namba tatu kuwa na makosa ya gharama kwa jumla ya Dola za Marekani 4,332,326.57.

c) Idadi ndogo ya Wafanyakazi Katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Kifungu 86(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kinaainisha kwamba Mkuu wa kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa kila taasisi ya umma anatakiwa kuandaa na kuwasilisha kwa afisa uhasibu mkuu taarifa ya ukaguzi ya robo muhula.

Wakati wa mahojiano na mkaguzi mkuu wa ndani wa Wizara ya Maji ilibainika kuwa, kitengo cha ukaguzi wa ndani kina wafanyakazi wachache na kina upungufu wa wakaguzi wa ndani wanne. Kitengo kimeshindwa kufanya ukaguzi katika miradi yote ya Wizara ya Maji kutokana na uhaba wa rasilimali watu.

Upungufu wa wafanyakazi katika kitengo cha ukaguzi wa ndani umesababisha mapungufu katika kupanga, kuanzisha, kutekeleza na kukamilisha ukaguzi wa miradi. Moja ya miradi ambayo haikukaguliwa ipasavyo na Mkaguzi wa Ndani wa Wizara ni mradi wa maji wa Same-Mwanga–Korogwe. Hii ilithibitishwa kwa kutokuwapo kwa taarifa ya ukaguzi wa mradi wa Same-Mwanga–Korogwe kwa takribani miaka sita ya fedha.

d) Mafunzo Yasiyojitosheleza kwa Ajili ya Kuendeleza Wafanyakazi

Kanuni 103(1) (6) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya Mwaka 2003 kinamwelekeza kila mwajiri kuwajibika katika kutoa mafunzo na kuendeleza wafanyakazi wake. Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa mafunzo ya mwisho kutolewa na Wizara ya Maji kwa wafanyakazi wake yalifanyika mwaka 2018, ambayo idadi kubwa na wafanyakazi waliohusika walikwisha kustaafu na wengine walikwishahamishwa kutoka wizara ya maji kwenda taasisi nyingine.

Ukosefu wa mafunzo kwa wafanyakazi umesababisha Wizara ya Maji kutoweza kufikia malengo iliyojiwekea kama vile kuwa na wafanyakazi wenye ujuzi unaojitosheleza katika usimamizi wa miradi.

e) Ukosefu wa Mipango Endelevu kwa Ajili ya Wataalam wa Kiufundi

Kifungu cha 7(1) (b) cha Sheria ya Watu Wasio Raia wa Tanzania (Kanuni ya Ajira) Na. 1 ya mwaka 2015 kinabainisha kwamba mtu yeyote anayekusudia kuajiri mfanyakazi asiyekuwa raia anapaswa kuandaa mpango endelevu utakaowezesha wafanyakazi wazawa kupata utaalamu na ujuzi kutoka kwa mwajiriwa huyo ili wakati mwingine waweze kufanya kazi hiyo iliyokuwa inafanywa na raia wa kigeni. Pia kifungu namba 5.3 cha viambatisho vya kwenye mkataba wa mshauri wa mradi kinaelekeza watendaji wa Wizara ya Maji kuwepo eneo la mradi kwa ajili ya kupata ujuzi.

Ilibainika kuwa, Wizara ya Maji haina mpango endelevu ulioandaaliwa kwa ajili ya kuwaendeleza na kuwapa mafunzo wataalamu wa ndani ya Wizara ili waweze kufanya kazi zinazofanywa na wataalamu kutoka nje ya nchi kama ilivyoelezewa kwenye mkataba.

Kwa hiyo, kutokana na kutokuwapo kwa mipango iliyoandaliwa ili kuwawezesha wataalamu wa ndani Wizara ya Maji imeendelea kuingia gharama kubwa kwa ajili ya kuajiri wataalamu wa nje ya nchi.

f) Kutokuwapo kwa Meneja wa Mradi na Msaidizi Wake Walioteuliwa na Wizara ya Maji

Sehemu ya 3.02 cha makubaliano ya mkopo baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mfadhili (BADEA) yaliyofanyika tarehe 11 Oktoba, 2014 inaainisha kwamba, mkopaji atalazimika kuteua Meneja wa mradi (ambaye atatakiwa kuwa ni Mhandisi ujenzi au mhandisi wa maji) mwenye uzoefu usiopungua miaka mitano katika utekelezaji wa miradi yenye kufanana na mradi atakaokwenda kusimamia.

Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa hakuna Meneja wa Mradi wala msaidizi wa Meneja wa Mradi aliyeteuliwa na Wizara ya Maji kwa ajili ya kushiriki kama mtaalamu wa ndani wa Wizara katika utekelezaji wa mradi wa Same –Mwanga-Korogwe. Pia, ilibainika kuwapo kwa wasimamizi wawili wa mradi waliokuwepo katika eneo la mradi, ambao mmoja alikuwa ni mhandisi magari na mwingine ni Mhandisi ujenzi mhitimu.

g) Ucheleweshwaji wa Madai ya Malipo kwa Wafanyakazi

Mwongozo wa Utumishi Na. L.2(1) kwa Utumishi wa Umma wa mwaka 2009 unamtaka mtumishi wa umma kupewa malipo ya kujikimu kwa kila siku pindi atakapokuwa nje ya kituo chake cha kazi.

Katika kupitia majalada ya wafanyakazi yanayohusu malalamiko ya wafanyakazi nilibaini kuwa, msimamizi wa mradi wa Same-Mwanga-Korogwe alilalamika juu ya ucheleweshwaji wa malipo ya jumla ya Sh. 38,400,000 ambayo ni malipo ya kujikimu kwa kipindi cha kuanzia Aprili 2018 hadi Agosti 2019 kupitia barua yenye namba ya kumbukumbu MW/PF.14738 ya tarehe 21 Mei 2020 na barua namba MW/PF.14738 ya tarehe 30 Machi 2020 licha ya ukweli kwamba alikuwa tayari yuko kwenye eneo la mradi akiendelea na utekelezaji wa mradi. Ucheleweshaji wa malipo umebainishwa katika **Jedwali Na. 9-22** hapa chini.

Jedwali 9- 22: Ucheleweshwaji wa malipo ya kujikimu kwa msimamizi wa mradi

Na	Mwezi	siku	Kiwango kwa siku	Kiasi
1	Aprili hadi Desemba, 2018	247	80,000	19,760,000
2	Januari hadi wa Agosti, 2019	233	80,000	18,640,000
Jumla				**38,400,000**

Chanzo: *Majalada binafsi ya wafanyakazi wa Wizara ya maji*

Mapitio ya taarifa ya mradi wa Same–Mwanga-Korogwe ya mwaka 2019 iliyoandaliwa na mkaguzi wa ndani ilionesha kuwa kumekuwa na ucheleweshaji wa malipo yaliyoainishwa kisheria kwa wawakilishi wa mshitiri waliyopo katika eneo la mradi. Kutokulipwa kwa malipo hayo kulitokana na kutokutilia mkazo suala la malipo ya wasimamizi waliopo kwenye miradi ya Wizara. Pia, ucheleweshaji wa malipo uliathiri uhuru wa utendaji wa wawakilishi wa mshitiri katika utekelezaji wa mradi.

h) Wataalamu Kutoka Nje ya Nchi Kufanya Kazi Bila ya Kuwa na Vibali vya Kazi

Kufungu namba 9 (1) cha kanuni namba 1 ya kumwajiri mtu asiye raia wa Tanzania ya mwaka 2015 kinabainisha kuwa, mtu asiye raia wa Tanzania haruhusiwi kujihusisha na shughuli yoyote katika kada yoyote hadi pale atakapokuwa na kibali halali ambacho kitamruhusu mtu huyo kuajiriwa au kufanya kazi katika kada iliyobainishwa kwenye kibali hicho cha kazi.

Mapitio niliyofanya katika taarifa ya robo mwaka ya mradi juu ya waajiriwa wasio raia wa Tanzania nilibaini kuwa wataalamu saba wa kigeni kutoka kwa Mkandarasi M.A. Kharaf & Sons waliokuwa wanatekeleza mkataba namba moja na wataalamu 10 wa kigeni kutoka kwa Mkandarasi BADR EAST AFRICA waliokuwa wanatekeleza mkataba namba tatu (3) na nne (4) hawakuwa na vibali halali vya kufanya kazi hapa nchini.

Mapungufu yaliyobainika yalichangia hatari ya kuchelewa kwa mradi na kuathiri ajira kwa wazawa na kupunguza uhamishaji wa teknolojia. Zaidi, kwa kiasi fulani ilisababisha Serikali kupoteza mapato ambayo yangetokana na malipo ya ada ya vibali vya kazi. Pia yalipunguza kiwango cha ajira kwa wataalamu wazawa.

i) Watendaji Muhimu wa Mradi kwa Upande wa Mkandarasi Walioainishwa Kwenye Mkataba Na. III Wamebainishwa Tena Kwenye Mkataba Na. IV

Agenda Na. 8 (iii) ya kikao cha maridhiano kilichofanyika terehe 27 Oktoba, 2017 (Mkataba namba III - Zabuni Na. ME/011/2013-2017/W/49) kinaainisha kwamba, utekelezaji wa mkataba namba III kutoingiliana na utekelezaji wa mkataba namba IV katika wafanyakazi, vifaa vya utekelezaji, pamoja na ofisi za mradi.

Pia vigezo vya zabuni na masharti ya jumla ya mkataba vinamwelekeza kila Mkandarasi kuwasilisha orodha tofauti ya watendaji muhimu ambao watafanya kazi katika mkataba husika tuu.

Ilibainika kwamba, watendaji muhimu tisa waliokuwa wanafanya kazi katika mkataba namba III walikuwa pia wanatumika katika utekelezaji wa mkataba namba IV kama ilivyothibitika kutoka kwenye taarifa Na. 25 na 45 ya maendeleo ya kazi (orodha ya wafanyakazi waliopo kwenye eneo la mradi).

Mkandarasi alikuwa na kipengele cha malipo kwa ajili ya watendaji muhimu wa mradi kwa kila mkataba, lakini yeye alijinufaisha kwa kutumia wataalamu wa mradi mmoja kutekeleza miradi miwili. **Jedwali Na. 9-23** hapa chini linaonesha watendaji ambao walikuwa wanatumika katika mikataba miwili kwa wakati mmoja.

Jedwali 9- 23: Orodha ya watendaji muhimu waliojitokeza katika mkataba Namba III & IV

Cheo	Mkataba III	Mkataba IV	Malipo yaliyoainishwa katika mkataba (Dola za Marekani)	
			Mkataba III	Mkataba IV
Msimamizi wa Ujumla	√	√	470,000	491,300
Msanifu/Mchumi	√	√		
Msimamizi wa mradi	√	√		
Mwakilishi wa mkandarasi	√	√		
Mipango na usanifu	√	√		
Mpimaji Mkuu	√	√		
Afisa rasilimali watu	√	√		
Afisa manunuzi na usafirishaji	√	√		

Msimamizi wa vibarua eneo la kazi	√	√		

Chanzo: *Taarifa ya maendeleo ya kazi namba 25 na 42 ya mkataba III and IV, ya mwaka 2020.*

Hali hii ilisababisha kuwa na utendaji mbovu wa kazi za mradi kutokana na mkandarasi kutokuwa na wataalamu wa kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi, ambao ulichangia ujenzi wa miundombinu iliyo chini ya kiwango.

j) Wafanyakazi wa Mkandarasi Kufanya Kazi Bila ya Kuwa na Vyeti vya Usajili

Kifungu namba 19 na 20 cha Sheria ya Usajili wa Wahandisi ya Mwaka 2010, sura ya 63 na Kanuni zake za mwaka 2010 kinabainisha kwamba wahandisi kutoka nje ya nchi lazima wasajiliwe na Bodi ya Usajili wa Wahandisi kabla ya kuanza kazi katika mradi wowote ndani ya nchi. Pia nafasi za kazi za uhandisi lazima zitumikiwe na wahandisi waliosajiliwa na bodi husika. Pia, kifungu namba 34 (1)(a) cha Sheria ya Usajili wa Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya Mwaka 2010 kinaainisha kuwa mtu yeyote ambaye anafanya kazi kama msanifu majengo au mkadiriaji majenzi bila kusajiliwa na bodi ya usajili wa wasanifu majengo na wakadiriaji majenzi anavunja sheria.

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa wafanyakazi 13 wa mkandarasi BADR katika mkataba namba III na IV, na wafanyakazi 23 wa mkandarasi M.A. Kharafi & Sons katika mkataba namba moja walikuwa wanafanya kazi katika mradi wa Same-Mwanga-Korogwe bila ya kuwa wamesajiliwa na Bodi husika.

Hali hii ilihatarisha ubora wa kazi na ufanisi katika utekelezaji wa mradi kutokana na kuwapo kwa wataalamu wasiokidhi vigezo katika mradi.

Hivyo, naishauri Wizara ya Maji izingatie yafuatayo:- (a) kutatua tatizo la upungufu wa wafanyakazi kwenye maeneo ya wataalamu, kitengo cha ukaguzi wa ndani, na kitengo cha menejimenti ya manunuzi; (b) kuboresha programu za mafunzo na kuendeleza wafanyakazi; (c) kuandaa mpango endelevu wa wafanyakazi wataalamu; (d) kuteua meneja mkuu na meneja msaidizi wa mradi; (e) kuhakikisha kwamba madai

ya watumishi yanalipwa kwa wakati; (f) kuhakikisha wataalamu kutoka nje wanakabidhi vibali vyao vya kazi bila ya kuchelewa zaidi; (g) kuhakikisha kwamba mtendaji mkuu mwingine anaajiriwa ili wawe wawili, badala ya mmoja wa sasa, kwa ajili ya mikataba namba III na IV; na (h) kuhakikisha wakandarasi wanawasajili wafanyakazi wao katika bodi husika za kitaalamu.

9.3.7 Usimamizi Usiojitosheleza wa Fedha za Mradi wa Same, Mwanga na Korogwe

a) Utoaji Fedha Chini ya Bajeti

Mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe unafadhiliwa kwa mkopo kutoka OFID, BADEA, KUWAIT Fund, SAUDI Fund pamoja na serikali ya Tanzania. **Jedwali Na. 9-24** hapo chini linaonesha mchanganuo wa mkopo (bajeti) na kiasi kilichotolewa mpaka sasa kwa kila mfadhili.

Jedwali 9- 24: Kiasi cha mkopo kilichobajetiwa na kiasi kilichotolewa na kila mfadhili

Mfadhili	Bajeti(kwa Dola za Marekani)	Bajeti(Sh.)	Kiasi kilichotolewa(kwa Dola)	Kiasi kilichotolewa (Sh.)
OFID	15,000,000		7,897,453	
BADEA	12,000,000		3,566,728	
Mfuko wa KUWAIT	34,000,000		13,061,451.53	
Mfuko wa SAUD	25,000,000		8,335,909.41	
Serikali ya Tanzania	24,340,000	40,684,310,000		41,641,595,281.73

Chanzo: *Bajeti ya mradi toka Wizara ya Maji*

b) Asilimia 51% tu ya Kiasi Kilichobajetiwa kwa Ajili ya Mradi Kilitolewa

Serikali ilibajeti Sh. 70,783,803,000 kwa ajili ya mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe kwa mwaka wa fedha 2014/15 mpaka 2019/20 lakini iliweza kupeleka Sh. 40,225,721,374.36 sawa na 57% ya bajeti nzima. **Jedwali Na. 9-25** inaonesha mchanganuo wa bajeti na utoaji wa fedha kwa kila mwaka.

Jedwali 9- 25: Kiasi kilichobajetiwa na kiasi kilichotolewa

Mwaka wa fedha	Bajeti(kwa shilingi za Tanzania)	Kiasi kilochotolewa(kwa shilingi za Tanzania)	Asilimia za fedha zilizotolewa (%)
2014/15	10,278,803,000	0	0
2015/16	Taarifa hazikutolewa	2,996,072,183.29	N/A
2013/17	19,224,000,000	3,111,374,456.64	16
2017/18	12,000,000,000	10,164,613,571.95	85
2018/19	18,000,000,000	15,151,178,047.20	84
2019/20	11,281,000,000	8,802,483,115.27	78
Jumla	**70,783,803,000**	**40,225,721,374.36**	**57**

Chanzo: *Randama na hati za malipo.*

Mchanganuo wa **Jedwali Na. 9-25** unaonesha kwamba kwa miaka sita iliyopita Serikali iliweza kupeleka fedha sawa na 57% ya bajeti yote. Hii inamaanisha kwamba, serikali ilipeleka fedha pungufu kwenye mradi huu kwa Sh. 30,558,081625.64, sawa na 43%. Pia ilionekana kuwa utolewaji fedha chini ya bajeti ulichangia kuchelewa kulipwa kwa wakandarasi, hatimaye kusababisha mrundikano wa kazi zilizofanyika lakini hazijalipwa.

Naishauri Menejimenti ya Wizara ya Maji (a) kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuhakikisha wanafanya mapitio ya taratibu za kutoa vibali vya matumizi ya fedha ili kuepuka uwezekano wa kuchelewesha kuruhusu utoaji wa fedha; hivyo kuchelewesha malipo kwa wakandarasi na kusababisha tozo ya riba ya ucheleweshaji (b) iwasiliane na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba fedha zinapelekwa kwa watekeleza miradi kwa wakati (c) itafute njia ya kupata mikopo yenye masharti nafuu itakayowezesha miradi kutekelezwa kwa uhakika (d) ifanyie mabadiliko vipengele vyenye mapungufu kwenye makubaliano ya mkataba ili kuboresha utekelezaji wa shughuli za mradi.

c) Kutokufunguliwa Akaunti ya Mradi na Kutokuandaliwa Vitabu vya Fedha

Kifungu cha 4.01 cha makubaliano ya mkopo kutoka BADEA kinahitaji mkopaji kufungua akaunti ya mradi pamoja na kuandaa vitabu vya fedha ya mradi. Wakati wa ukaguzi, nilibaini kwamba

hakukuwa na akaunti ya mradi wala vitabu vya fedha vilivyoandaliwa.

Nilibaini kuwa uongozi wa Wizara ya Maji ulishindwa kuzingatia kifungu tajwa cha makubaliano ya mkopo kinachowataka kufungua akaunti ya benki ya mradi pamoja na kuandaa vitabu vya fedha. Kutokana na kutokuwapo kwa akaunti ya mradi, imekuwa vigumu kuzithibitisha fedha zilizotolewa kwa ajili ya mradi.

Naishauri Menejimenti ifungue akaunti ya benki kwa ajili ya shughuli za mradi. Pia, iandae vitabu vya hesabu na kuhakikisha vinakaguliwa kama ilivyobainishwa kwenye makubaliano ya mkataba.

d) Malipo ya Afya, Usalama na Mazingira Yaliyokosa Uthibitisho Dola za Marekani 49,148

Kifungu Na. 4.18.1 cha Mkataba wa Jumla kinamtaka Mkandarasi kuchukua hatua zote za kutunza mazingira (ndani na nje ya kambi) kuzuia uharibifu na usumbufu kwa watu na mali unaotokana na uchafuzi, kelele na mambo mengine yatokanayo na shughuli za mradi.

Katika kupitia vyeti vya malipo kwa Wakandarasi, nilibaini kiasi cha Dola za Marekani 49,148 zililipwa kwa mkandarasi mwenye namba za mlipa kodi 100-202-646 kwa mkataba Na. I na mwenye namba za mlipa kodi 10-006179-w kwenye mkataba namba III na IV kwa ajili ya gharama za kuzuia kelele bila ya kuambatisha uthibitisho na mbinu zilizotumika kuzuia kelele mpaka kufikia hiyo gharama. Jedwali 9-26 hapo chini inaonesha kwa kina malipo yaliyofanyika kwa wakandarasi.

Jedwali 9- 26: Mchanganuo wa malipo yaliyofanyika kwa wakandarasi

Na.ya mkataba	Na. ya vyeti vya malipo	Kiasi kwa Dola za Marekani
IV	2 & 3	17,100
III	2	10,000
I	21	22,048
Jumla		**49,148**

Chanzo: *Nukuu za Makadirio ya Ukubwa wa Kazi na Bei na vyeti vya malipo*

Mchanganuo kutoka **Jedwali Na. 9-26** unaonesha kwamba malipo ya fedha za afya, usalama na mazingira yalilipwa kwa vyeti 4 vya malipo.

Hii ilionekana kusababishwa na udhibiti usio imara wa mifumo ya udhibiti wa ndani wakati wa kushughulikia malipo ya wakandarasi ambapo viambatisho vya madai ya kodi havikupitiwa.

Naishauri menejimenti ikabidhi viambatisho husika kwa ajili ya uhakiki wa malipo yaliyofanyika.

e) Fedha za Matazamio Zilizokatwa Kwenye Malipo Bila ya Kubakizwa na Mwajiri Dola za Marekani 2,762,995.34

Kifungu Na. 4.3.2 (b) cha Mkataba wa Jumla kinamtaka Mwajiri kukata fedha za matazamio kwa asilimia ya malipo mpaka kifikie kiwango cha mwisho kilichokubalika kwenye mkataba.

Katika kupitia vyeti vya malipo ilibainika kwamba fedha za matazamio kiasi cha Dola za Marekani 2,762,995.34 zilikatwa kwenye mkataba Na. I kutoka kwa mkandarasi mwenye namba za mlipa kodi 100-202-646 lakini fedha hizo hazitunzwi na mwajiri. Kwa mujibu wa mkataba Na. III na IV, fedha za matazamio hazikukatwa kwa sababu zilikatiwa bima kulingana na kifungu maalum cha mkataba 41. **Jedwali Na. 9-27** linaonesha mchanganuo wa fedha za matazamio zilizokatwa.

Jedwali 9- 27: Makato ya Fedha za Matazamio Zilizokatwa Lakini Hazitunzwi na Mwajiri

Na.ya mkataba	Kiasi kwa dola za marekani
I	2,762,995.34
III& IV	0

Chanzo: *Vyeti vya malipo*

Hii kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na mkandarasi kulipwa moja kwa moja na wafadhili kwa sababu hakukuwa na akaunti ya benki ya mradi. Hivyo inamaanisha haitakuwa na fedha za haraka za kufanya marekebisho wakati wa kipindi cha matazamio.

Naishauri Menejimenti ichukue fidia za fedha za matazamio na kuzihifadhi kwa ajili ya kutumika wakati wa kipindi cha matazamio ya mkandarasi.

f) Marekebisho ya Bei ya Mkataba Juu ya Kikomo Kinachokubalika kisheria Bila Idhini

Kanuni ya 61 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inasema kwamba marekebisho ya mkataba hayapaswi kuongeza jumla ya bei ya mkataba kwa zaidi ya 15% ya bei halisi ya mkataba bila idhini ya Mamlaka inayoidhinisha bajeti.

Mikutano ya Mazungumzo juu ya Nyongeza za Mkataba Namba 1 hadi 5 kati ya Wizara ya Maji na Washauri M/S Engineering Consultants Group na M/S Howard Humphreys (T) Ltd ambao walikuwa wakitekeleza Mkataba namba moja ilijadili na kukubali kuongeza malipo kwa washauri kwa kiwango cha 10% kutoka zile zilizooneshwa kwenye mkataba wa Mshauri hivyo kusababisha kuongezeka kwa bei ya mkataba kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 9-28.**

Jedwali 9- 28: Kiasi cha Mkataba Kilichorekebishwa Juu ya 15%

Tarehe	Nyongeza ya Mkataba	Fedha za Nje (Kiasi kwa Dola za Marekani)	Fedha za Ndani (Sh.)
Julai 2013	Mkataba wa mwanzo(a)	432,320	126,149,375
Desemba 2014	1	511,700	381,718,496
Desemba 2017	2	716,005	668,447,942.6
Novemba 2018	3	854,428.4	850,273,563.5
Agosti 2019	4	1,142,014.81	1,163,721,455
Mei 2020	5(b)	1,339,248.44	1,301,138,815
	b-a	906,928.44	1,174,989,440
Ongezeko la Asilimia		209%	931%

Chanzo: *Mkataba na Nyongeza ya Mkataba*

Uchambuzi wa nyongeza hapo juu unaonesha kuwa kulikuwa na ongezeko la Dola za Marekani 906,928.44 juu ya viwango vilivyopitishwa vya fedha za nje na Sh. 1,174,989 kwa viwango vya juu vya fedha za ndani vilivyopitishwa ambayo ni sawa na ongezeko la 209% na 931%, mtawalia.

Pia ilibainika tofauti ya bei ya mkataba kwa mshauri aliyeitwa Don Consult LTD ambaye alisimamia mkataba namba tatu na nne. Mkataba wa awali ulikuwa kiasi cha Sh. 1,666,600,000. Mshauri huyo alipendekeza marekebisho ya bei ya mkataba kupitia nyongeza namba 1 na 2 ya mkataba iliyotiwa saini tarehe 31 Januari, 2019 na 22 Septemba, 2020, mtawalia, ambacho baadae

kilisababisha kupanda kwa bei ya mkataba hadi Sh. 3,437,350,000, sawa na ongezeko la 106%. Hii pia ilikuwa kinyume na mahitaji ya Kanuni ya 61 (4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2013.

Sababu kuu za kuongezeka kwa gharama ni pamoja na: (i) Kasi ndogo katika utekelezaji wa mkataba ulioleta kuongeza muda; na (ii) Tofauti ya kipindi cha Mkataba kati ya Washauri wa Makandarasi ambapo kila mmoja wao alikuwa na kipindi tofauti cha mkataba. Hii ilipelekea mkataba kugharimu zaidi ya ilivyotarajiwa.

Naishauri Menejimenti ihakikishe inapata kibali kutoka mamlaka za bajeti inapotokea kumefanyika mabadiliko ya mkataba ambayo yanazidi kiwango kinachoruhusiwa.

g) Malimbikizo ya Riba kutokana na Ucheleweshaji wa Kuwalipa Wakandarasi Dola za Marekeni 966,240.96 na Sh. 892,271,045

Kifungu namba 14.8.1 cha masharti ya jumla ya mkataba kinasema kuwa kama mkandarasi hatalipwa kwa wakati kulingana na kifungu namba 14.7 cha masharti ya jumla ya mkataba, mkandarasi atastahili kupokea riba ya malimbikizo kwa kila mwezi kutokana na kiasi ambacho hakikulipwa kwa kipindi chote cha ucheleweshaji malipo na mkandarasi atastahili malipo hayo bila masharti yoyote.

Ilibainika kuwa, ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi wenye Namba za Utambulisho wa Mlipa Kodi Na. 10-006179-W na 100-202-646 kwa mkataba namba I, III na IV kama inavyoonekana hapa chini:

Mkataba namba Tatu

Ilibainika kuwapo kwa ucheleweshaji wa malipo kwa mzabuni mwenye namba ya utambulisho wa mlipa kodi Na. 10-00-6179 kama ilivyodhihirishwa na barua zenye namba ya Kumb. DCL/SMK/CONTRIII/CLIENT/IPC/01A ya tarehe 11 Machi, 2019 na namba ya Kumb DCL/SMK/CONTRIII/CLIENT/IPC.03A ya tarehe 23 Mei, 2019 zilizoandikwa na mshauri wa ujenzi mwenye namba ya utambulisho wa mlipa kodi Na.100-178 akiwasilisha madai ya

limbikizo la riba kiasi cha Dola za Marekani 354,969.63 kwa mkandarasi aliyetekeleza mkataba namba tatu.

Mkataba namba Moja

Kulikuwa na malimbikizo ya riba kiasi cha Sh. 892,271,045 na Dola za Marekani 475,149.69 kutokana na ucheleweshaji wa malipo kwa mkandarasi mwenye namba ya utambulisho wa mlipa kodi Na. 100-202-646 alikua akitekeleza mkataba namba moja. Hii imedhihirishwa na barua yenye Namba ya Kumb. ECGHH/SMK/KF500/2019 ya tarehe 8 Agosti 2019 iliyoandikwa na Mhandisi Mshauri wa ujenzi, akiwasilisha stahiki za riba kutokana na ucheleweshaji wa malipo tangu kuanza kwa mkataba tarehe 25 Julai 2019. Hii ilikuwa kinyume na kifungu namba 14.8 cha masharti ya jumla ya mkataba

Mkataba namba Nne

Kifungu namba 14.2.1 cha masharti ya jumla ya mkataba kinamtaka mwajiri kumlipa mkandarasi malipo ya awali kama mkopo usio na riba kwa ajili ya kumwezesha kifedha baada ya mkandarasi kuwasilisha dhamana kulingana na masharti ya jumla ya mkataba. Pia, kifungu namba 14.8.1 cha masharti ya jumla ya mkataba kinasema kuwa kama mkandarasi hatalipwa kwa wakati atastahili kupokea riba ya malimbikizo kwa kila mwezi kutokana na kiasi ambacho hakikulipwa.

Kinyume na masharti hayo, Wizara ya Maji ilipaswa kumlipa mkandarasi mwenye namba ya utambulisho wa mlipa kodi Na. 10-00-6179-W malipo ya awali sawa na 15% ya malipo ya mkataba kiasi cha Dola za Marekani 35,249,096.76 sawa na Sh. 77,548,004,072 mara atakapowasilisha dhamana ya benki inayokubalika (Kifungu namba 14.1.1 ya masharti maalum ya mkataba kama yalivyorekebishwa kwenye kikao cha mazungumzo kilichofanyika tarehe 13 Mei 2013). Hata hivyo, lakini kiasi hicho hakikulipwa ambapo ilipelekea malimbikizo ya riba kiasi cha Dola za Marekani 136,121.64 ambazo zililipwa kupitia hati ya malipo namba mbili.

Sababu zilizopelekea ucheleweshwaji wa malipo hayo ya awali ni pamoja na: Mlolongo mrefu wa taratibu za malipo kuanzia ngazi ya Wizara ya Maji, wafadhili wa mradi, pamoja na ucheleweshaji wa fedha kutoka Hazina.

Hayo yote yalichangia gharama za utekelezaji wa mradi kuongezeka na kusababisha matumizi ya fedha ambazo zingeweza kutumika katika shuhuli nyingine za kiuchumi.

Naishauri Menejimenti ihakikishe kwamba madai ya wakandarasi yanalipwa kwa wakati ili kuepuka tozo za riba kutokana na adhabu ya kuchelewesha kufanya malipo kwa wakandarasi.

h) Kodi ya zuio Iliyokatwa Pasipo Uthibitisho wa Kuwasilishwa kwa Kamishna wa Mapato ya Ndani, Sh. 96,921,534.37

Kifungu cha 83 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (iliyorekebishwa mwaka 2008) kinawataka mawakala wa kodi ya zuio kukata kodi ya asilimia 2 au 5 ya malipo ghafi kutokana na manunuzi ya bidhaa au huduma na kuwasilisha kwa Kamishna wa Mapato ya ndani Tanzania siku saba baada ya kukamilika kwa kila mwezi.

Uchambuzi uliofanywa kwenye nyaraka za malipo ulibaini kuwa kodi ya zuio Sh. 96,921,534.37 ilikatwa kutoka hati za malipo zenye thamani ya Dola za Marekani 1,274,708.11 sawa na Sh. 2,931,876,415.38 lakini hapakuwa na uthibitisho kuwa ziliwasilishwa kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato ya Ndani.

Naishauri Menejimenti ihakikishe inapeleka kwa wakati kodi ya zuio iliyokatwa kutoka kwa wazabuni kama inavyoelekezwa na Ibara ya 83 ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2008. Aidha, inatakiwa kuwasilisha viambatisho vya malipo hayo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya uhakiki.

i) Dhamana ya Utendaji na Malipo ya Awali kwa Wakandarasi Yaliyogharamiwa na Mwajiri, Dola za Marekani 1,737,120

Kifungu cha jumla cha mkataba 4.2.1 kinamtaka mkandarasi kujigharamia dhamana ya utendaji pamoja na malipo ya awali. Katika kupitia vyeti vya malipo kwa mkataba namba,1,3 na 4 imebainika kuwa wakandarasi walilipwa na mwajiri kiasi cha Dola za Marekani 1,737,120 kwa ajili ya kugharamia dhamana ya utendaji na malipo ya awali kinyume na matakwa ya mkataba.

Jedwali Na. 9-29 inaonesha mchanganuo wa malipo ya dhamana ya utendaji na malipo ya awali

Jedwali 9- 29: Dhamana ya utendaji na malipo ya awali yaliyogharamiwa na mwajiri

Mkataba namba	Aina ya dhamana	Namba ya Cheti cha malipo	Kiasi kwa (Dola za Marekani
III	Dhamana ya malipo ya awali	2	150,000
	Dhamana ya utendaji	2	200,000
IV	Dhamana ya malipo ya awali	2	250,000
	Dhamana ya utendaji	2	330,000
I	Dhamana ya malipo ya awali	2	10,620
	Dhamana ya utendaji	2	796,500
Jumla			**1,737,120**

Chanzo: *vyeti vya malipo*

Hii ilionekana kusababishwa na udhibiti usio imara wa mifumo ya udhibiti wa ndani wakati wa kushughulikia malipo ya wakandarasi, ambapo ilipelekea kuongezeka kwa gharama za mkataba kwa Dola za Marekani 1,737,120 bila ongezeko la kazi yenye thamani hiyo.

j) Makato ya fedha za Zuio kwa Mkandarasi Ambazo Hazikukatiwa bima Lakini Zikalipwa Mkandarasi, Sh. 822,112,678

Kifungu maalum cha mkataba 41 kinataka fedha za zuio kukatiwa bima kwa 5% ya cheti cha malipo kwa muda wa miezi 42. Kifungu maalum cha mkataba Na. 41 pia inataka kiwango cha makato ya fedha ya zuio kuwa ni 10%.

Katika kupitia vyeti vya malipo pamoja na hati za malipo, ilibainika kwamba mkandarasi alilipwa fedha za zuio Sh. 822,112,678 ambazo zilitakiwa kukatwa au kulipiwa bima baada ya kulipia bima 5% pekee badala ya 10% katika malipo ya jumla ya Sh. 16,442,253,740. Hii ilionekana kusababishwa na uongozi wa Wizara kupitiwa katika tafsiri ya kifungu tajwa. Hatimaye, ilisababisha kukosekana fedha za karibu za ukarabati wakati wa kipindi cha matazamio.

Naishauri Menejimenti ya Wizara ya Maji ihakikishe inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia mapungufu yatakayojitokeza

kwenye miradi ya maji wakati wa kipindi cha matazamio kama mkataba unavyoagiza.

k) Malipo ya Awali yenye Thamani ya Dola za Marekani 5,287,363.9 Yaliyolipwa kwa Dhamana ya Benki Zinazokinzana

Katika kupitia vyeti vya malipo pamoja na hati za malipo ilibainika kuwa mkandarasi aliyekuwa anafanya shughuli za mkataba namba III aliwasilisha dhamana ya benki yenye namba CRDB16-IGT815 yenye thamani ya Dola za Marekani 5,287,363.9. Uthibitisho wa moja kwa moja kutoka kwa mdhamini kwa barua yenye namba ya kumbukumbu EA.35/390/02/13 ilibainisha kuwa, dhamana iliyowasilishwa na mkandarasi kutoka benki haikuwa halali, lakini uthibitisho uliofanywa na uongozi wa Wizara ya Maji kwa mdhamini ulibaini kuwa dhamana hiyo ilikuwa halali.

Hii ilionekana na kusababishwa na mdhamini kutoa majibu yanayokinzana kwenye suala la dhamana iliyoonekana kutoka kwake. Hii inamaanisha kwamba, kuna uwezekano wa mkandarasi kulipwa fedha za awali bila dhamana na kupelekea kutokuwa na uhakika wa marejesho ya fedha hizo pindi mkandarasi akishindwa kutekeleza mkataba.

Naishauri Menejimenti itilie mkazo kwenye usimamizi wa mikataba na kuhakikisha kwamba wanatekeleza vipengele vya mkataba kwa ukamilifu.

l) Ushahidi wa Malipo ya Bima Ambazo Hazikuwasilishwa Dola za Marekani 1,112,049

Kifungu cha jumla cha mkataba 18.1.7 kinamhitaji mlipa bima baada ya kulipa bima kuwasilisha ushahidi wa kulipa bima kwa mbia mwingine wa mkataba.

Katika kupitia vyeti vya malipo kwa mkandarasi ilibainika kuwa, wakandarasi walilipwa kiasi cha Dola za Marekani 1,112,049 kama fidia ya malipo ya bima bila kuwasilisha ushahidi wa malipo hayo. **Jedwali Na.9-30** linaonesha mchanganuo wa malipo hayo ya bima.

Jedwali 9- 30: Malipo ya bima yaliyolipwa bila ushahidi wa kukatwa kwa bima

Mkataba namba	Mchanganuo wa bima	Cheti cha malipo	Kiasi kwa Dola za Marekani
III	Bima ya kazi	3	180,000
	Bima ya mtu wa tatu	3	120,000
IV	Bima ya kazi	2	250,000
	Bima ya mtu wa tatu	2	150,000
I	Bima ya kazi	21	210,000
	Bima ya mtu wa tatu	21	202,049
Jumla			**1,112,049**

Chanzo: *Vyeti vya Malipo*

Hii ilionekana kusababishwa na kutokuhakikiwa kwa nyaraka za bima alizowasilisha mkandarasi. Hii inaweza kupelekea mkandarasi kulipwa fedha nyingi kuliko kiasi alicholipa bima au kutolipa bima kabisa.

Hivyo, naishauri Menejimenti iwasiliane na mkandarasi ili awasilishe kadi za bima zilizolipiwa ikiwa ni sehemu ya kutekeleza matakwa ya mkataba.

SURA YA KUMI

UTEKELEZAJI WA MRADI WA UZALISHAJI WA SUKARI MBIGIRI

10.1 Utangulizi

Kampuni Hodhi ya Mkulazi ni kampuni iliyoundwa kwa ushirikiano baina ya Mfuko wa pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) tarehe 6 Septemba 2016. Lengo kuu la kampuni ni kuzalisha na kuingiza sukari nchini. Kwa sasa, Kampuni Hodhi ya Mkulazi inamilikiwa kwa pamoja na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Jeshi na Jeshi la Magereza. Muundo wa hisa za Ubia utakuwa asilimia 96 itakayomilikiwa na NSSF na asilimia nne itamilikiwa na Magereza.

Lengo kuu la kampuni ni kuzalisha sukari yenye ubora pamoja na bidhaa zinazotokana na miwa. Ili kufikia lengo hili kampuni ina mpango wa kutekeleza miradi miwili ya sukari ambayo italenga kuzalisha tani 250,000 za sukari kwa mwaka. Mojawapo ya miradi hiyo ni mradi wa uzalishaji sukari wa Mbigiri ambao utatekelezwa katika shamba namba namba 217 lililopo Mkulazi, Wilaya ya Morogoro Vijijini. Lengo la uzalishaji kwa shamba la Mkulazi ni kuzalisha tani 200,000 za sukari kwa mwaka. Mradi mwingine upo katika eneo la Mbigiri lililopo katika wilaya ya Kilosa katika mkoa wa Morogoro. Mradi huu unalenga kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka.

10.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini kama usimamizi wa shamba na kiwanda cha uzalishaji sukari vilifuata viwango vilivyowekwa vya utekelezaji na kama thamani ya fedha ilizingatiwa.

Ukaguzi ulilenga kupima kama kampuni Hodhi ya Mkulazi ilizingatia yafuatayo: usimamizi wa shamba ulifanyika kwa kuzingatia mpango na miongozo iliyowekwa, taratibu za ugavi zilifanyika kwa kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi, usimamizi wa fedha kama ulifanywa kwa kufuata miongozo ya fedha na shughuli za ujenzi zilikamilishwa kwa wakati na zinakidhi ubora uliokusudiwa na kwa gharama stahiki.

Mkaguliwa mkuu alikuwa Kampuni Hodhi ya Mkulazi yenye jukumu la utekelezaji wa mradi katika shamba la Mbigiri. Ukaguzi ulijumuisha shamba lote la Mbigiri, ambapo ulikagua kazi zote za usimamizi wa

shamba na kiwanda cha uzalishaji sukari kwa kuzingatia shughuli za kilimo cha miwa, ugavi, usimamizi wa fedha na ujenzi. Shamba la Mkulazi halikukaguliwa kwa sababu hadi kipindi cha utekelezaji wa Ukaguzi huu hakukuwa na uendelezaji wowote ambao ulikuwa umefanyika.

Ukaguzi wangu ulijikita katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 hadi Januari 2020/21. Muda huu uliniwezesha kupima jinsi mradi ulivyotekelezwa toka mradi ulipoanza mwaka 2016/17 na kutarajia kufika tamati mwaka 2022/23.

10.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inatoa muhtasari wa hoja kuu za ukaguzi zinazohusiana na usimamizi wa shamba, ugavi, usimamizi wa fedha na shughuli za ujenzi kama zilivyoainishwa hapo chini:

10.3.1 Mapungufu katika Usimamizi wa Shughuli za Shamba

a) Visima vyenye Thamani ya Sh. Milioni 81.5 Vilichimbwa Lakini Havikutumika

Kampuni Hodhi ya Mkulazi iliingia mkataba wa kuchimba visima na wakala wa kuchimba visima (DDCA) na kusaini mkataba wenye namba MKL/W/03/2017) tarehe 7 Novemba 2017 kwa gharama ya Sh. 815,000,000 kwa ajili ya kufanya utafiti, kuchimba visima vinane, pamoja na kuweka pampu za maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika mashamba ya Mkulazi na Mbigiri mkoani Morogoro. Muda wa mkataba ulikuwa miezi sita kuanzia mwezi Novemba 2017 hadi mwezi Mei 2018.

Hata hivyo, kwa mujibu wa uhakiki niliofanya tarehe 20 Novemba 2020 nilibaini kuwa visima vinne vilivyopo katika shamba la Mbigiri kitalu E3, D2, E4 na F4 vilichimbwa lakini vilikuwa havitumiki. Pia, nilibaini kuwa Mkandarasi aliondoka eneo la kazi licha ya kuwa alikuwa tayari ameshalipwa asilimia kumi 10 ya gharama zilizoainishwa kwenye mkataba kiasi ambacho ni sawa na Sh. 81,500,000.

Kwa mujibu wa Menejimenti ya Kampuni ya Mkulazi, kutokutumika kwa visima vilivyochimbwa kulitokana na visima hivyo kutokutoa maji ya kutosha kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji kama ilivyokuwa imepangwa. Pia ukosefu wa maarifa ya kufanya shughuli za kijiolojia

ambazo zilipelekea kubadilika kwa mara kwa mara kwa mbinu za uchimbaji uliosababisha kuwa na visima zisivyo na matokeo kusudiwa.

b) Matumizi ya Mbolea na Dawa za Kuulia Wadudu Bila Kuwa na Nyaraka za Uthibitisho

Katika mwaka wa fedha 2019/20 Kampuni ya Mkulazi ilianzisha vitabu vya kurekodi taarifa za utoaji wa mbolea na dawa za kuua wadudu kwa Idara ya Kilimo. Lengo la kuwa na vitabu hivi ni kunakili kiasi cha mbolea na dawa za kuulia wadudu zinazotumika, kitalu kilichowekwa mbolea na dawa, tarehe na jina la mhudumu aliyeweka mbolea na dawa za kuulia wadudu. Katika mwezi wa Agosti 2020 vitabu hivyo vilitumika ipasavyo.

Mapitio ya kitabu cha fedha cha mwaka 2018/19 na leja ya vifaa vya stoo kwa mwaka 2018/19 na 2019/20 yalibaini kuwa, kabla ya kuanza kutumia vitabu hivyo mbolea na dawa za kuulia wadudu zenye thamani ya Sh. 155,290,000 zilitolewa ghalani ila hapakuwa na uthibitisho wa namna zilivyotumika. Kwa mujibu wa mahojiano na Menejimenti ya Mkulazi, mbolea na dawa za kuulia wadudu zote zilinunuliwa na kutumika. Hata hivyo, menejimenti ilishindwa kutoa uthibitisho wa matumizi hayo.

Kadhalika, baada ya kuanzishwa kwa vitabu vya kutolea mbolea na dawa za kuua wadudu zinazotumika kila siku kama njia ya kudhibiti matumizi, bado mapungufu yaliyobainishwa hapo juu yalionekana. Mapitio ya nyaraka zinazotumika kutolea mbolea ya AMIDAS (SN.51-100) na kitabu cha ghalani cha mwaka 2019/20 yalibaini kwamba, mbolea na dawa za kuulia wadudu zenye thamani ya Sh. 86,599,000 zilitolewa ghalani bila kuwa na uthibitisho kama zilitumika shambani au la.

Hali hii inasababishwa na udhaifu katika kudhibiti matumizi ya mbolea na dawa za kuulia wadudu. Mapitio ya vitabu vinavyotumika kutoa mbolea na dawa za wadudu yalionesha kwamba vitabu hivyo vilirekodiwa na wafanyakazi wa shambani na kutiwa saini na mtaalamu wa Kilimo ambaye sio mfanyakazi wa shambani. Msimamizi wa shamba na viongozi wa makundi ambao ni wafanyakazi wa shambani ambao wanapaswa kuhakikisha kwamba mbolea ama dawa za wadudu zimetumika kama ilivyopaswa shambani hawakuwa

wamesaini popote katika vitabu hivyo vya kudhibiti matumizi ya mbolea na dawa za wadudu.

c) Hasara ya Sh. Milioni 379.34 kwa Ajili ya Kuteketeza Miwa Iliyopitiliza Muda wa Kuvunwa

Katika kikao cha bodi ya wadhamini kilichofanyika tarehe 22 Juni 2020 kilichofanyika katika Ofisi za Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), bodi ya wakurugenzi iliamua kuvuna na kuuza kwa miwa yote iliyopitiliza muda wake ili kuzuia kuharibika zaidi kwa miwa hiyo. Bodi ya wadhamini iliazimia kuwa, uvunaji na mchakato wa ugavi lazima vifuate sheria na miongozo ya nchi.

Mapitio ya mawasilisho ya nyaraka zilizojadiliwa na bodi ya wadhamini yalionesha kwamba, kiasi cha hekta 740.43 kilikuwa na miwa iliyopitiliza muda wake wa kuvunwa.

Mapitio ya taarifa za shamba za tarehe 30 Septemba na Desemba 2020 pamoja na uchambuzi wa wakaguzi uliotokana na kutembelea shamba tarehe 20 Novemba 2020 yaligundua kwamba, miwa iliyozidi muda wake ilionekana katika vitalu mbalimbali ikiwa imeharibiwa sababu ilipoteza thamani yake ya kiuchumi. Kwa hiyo, makisio ya gharama za uzalishaji kiasi cha Sh. 379,338,245 ilitumika kuhudumia miwa hiyo iliyoharibiwa. Hivyo gharama halisi za uzalishaji miwa katika vitalu hivyo ilikuwa hasara kwa Kampuni.

Menejimenti ya Mkulazi ilieleza kuwa maamuzi ya kuharibu miwa iliyopitiliza muda wake ilitokana na ukweli kwamba, Kampuni haikuwa imesimika Kiwanda cha kuchakata sukari. Mapitio ya Mpango kazi wa kampuni ya Mkulazi wa mwaka 2019/20 hadi 2023/24 yalionesha kuwa mitambo ya kuchakata sukari ilitakiwa kusimikwa na kuanza kufanya kazi ifikapo mwezi Desemba mwaka 2020.

Pia, kuharibu miwa iliyozidi muda wake wa kukaa shambani kunaashiria kutokuwepo kwa umakini katika kuandaa mazingira rafiki ya kuzalisha sukari kabla ya kusimikwa kwa mtambo wa kuchakata sukari.

d) Uwezakano wa Kupata Hasara ya Sh. Milioni 499.93 kwa Miwa Iliyopitiliza Muda Wake wa Kuvunwa

Kampuni ya Mkulazi na Kiwanda cha sukari cha Mtibwa waliingia makubaliano ya kuuza miwa kwa hiari na kuvuna miwa mnamo tarehe 17 septemba 2020. Mkataba wa kuuza na kuvuna miwa ulianza kutekelezwa katika msimu wa mavuno wa mwaka 2020/21. Mapitio ya taarifa zilizojadiliwa na bodi ya wadhamini ya Kampuni ya Mkulazi yalionesha kuwa Kampuni ilipanga kuvuna hekta 740.43 za miwa uliopitiliza muda wake wa kuvunwa katika msimu uliotajwa hapo awali. Lengo la makubaliano hayo lilikuwa kufidia gharama zilizotokana na kuzalisha miwa hiyo ili kuzuia Kampuni isipate hasara zaidi endapo miwa hiyo isingeuzwa kabla ya kusimikwa kwa kiwanda cha kuchakata sukari cha Mbigiri.

Hta hivyo, iligundulika kuwa hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2020 Kampuni ya Mkulazi ilifanikiwa kuvuna hekta 318 tu ambazo ni sawa na asilimia 43 ya eneo lililopangwa kuvunwa. Hii ilimaanisha kwamba, Kampuni ilikuwa nyuma kwenye zoezi la kuvuna kutokana na makubaliano waliyoyafanya na kiwanda cha Mtibwa. Hivyo, ikapelekea maeneo mengine yaliyopangwa kutokuvunwa katika wakati muafaka. Vitalu hivyo vilivyopandwa miwa vina miwa yenye umri zaidi ya miezi 30. Endapo miwa hiyo haitavunwa ifikapo mwezi Februari 2021, itapoteza thamani yake kiuchumi na kupelekea hasara kwa kampuni.

Sera ya Kilimo cha Miwa ya Kampuni ya Mkulazi na utaratibu wa uendeshaji shamba za mwaka 2020 zinasema kuwa, miwa iliyopandwa inatakiwa kuvunwa inapofikisha umri wa miezi 11 hadi 14. Kwa kuwa miwa mingi iliyopandwa ina umri wa zaidi ya miezi 30, hivyo kuna hatari ya kupoteza thamani yake ya kiuchumi. Kushindwa kuvuna miwa iliyopandwa kwa wakati inaweza kupelekea kampuni kupata hasara ya Sh. 499,934,750.

e) Usimamizi Usioridhisha wa Wakulima wa Nje

Sera ya kilimo ya mwaka 2013 inataka kila uwekezaji mkubwa wa Kilimo kuhakikisha kwamba unawanufaisha wananchi wa eneo linalozunguka uwekezaji. Pia inalenga kuwawezesha wakulima kufikia mahitaji yao. Nilibaini mapungufu yafuatayo katika kuwasimamia wakulima:

(i) Wakulima wa Nje Wamepata Hasara Kutokana na Ucheleweshaji wa Kusimika Kiwanda cha Sukari Katika Shamba la Mbigiri

Mkataba wa pande tatu uliosainiwa kati ya kampuni ya Mkulazi, Benki ya Azania na chama cha ushirika cha kati cha Magole wa mwaka 2018 ulibainisha kwamba, wadau walikubaliana kukuza mnyororo wa thamani wa sukari kwa kuanzisha mahusiano baina ya wakulima, benki na Kampuni; ambapo benki iliridhia kutoa mkopo. Mkopo huo wenye jumla ya Sh. 4,962,800,000 ungetumika kugharamia gharama za kilimo ambazo ni gharama za kuanda mashamba, mbolea, dawa za wadudu, mbegu na kuchimba visima.

Mapitio ya mkataba wa pande tatu na nyaraka nyinginezo yalionesha kwamba Benki ya Azania ilikataa kutoa kiasi cha Sh. 1,797,050,000 kwa wakulima wa nje ambazo zingewawezesha wakulima wa nje kukidhi gharama za kuandaa mashamba, kununua mbolea na dawa za wadudu, mbegu na kuchimba visima. Benki ilikataa kutoa mkopo huo kwa sababu kampuni ya Mkulazi haikuweza kusimika mtambo wa kuchakata sukari hadi wakati ukaguzi huu unakamilika.

Kutokana na changamoto tajwa hapo juu kampuni ya Mkulazi na Chama cha ushirika cha Magole walilazimika kufanya marekebisho ya mkataba wa ugavi wa miwa mwezi Machi 2020. Mapitio ya kipengele Na. 7.4 cha mkataba uliofanyiwa marekebisho yalionesha kuwa katika kipindi ambacho Kampuni ilikuwa haijasimika kiwanda, wakulima wa nje wangeruhusiwa kuuza miwa yao katika Kiwanda kilichopo jirani kulingana na maridhiano yatakayoafikiwa baina ya wakulima na kiwanda hicho. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2020/21 wakulima wa nje walianza kuuza miwa yao katika kiwanda cha Mtibwa.

Matokeo ya kukosekana kwa mkopo na changamoto zilizowakabili wakulima wa nje zitasababisha athari katika kushiriki katika uzalishaji wa miwa[27]. Hivyo, hapo mbele kampuni inaweza kuathirika kwa kushindwa kupata miwa ya kutosha kama mali ghafi kwa ajili ya kuchakata sukari.

(ii) Usimamizi Usioridhisha wa Ufanisi wa Wakulima wa Nje

Mapaitio yangu ya Sera ya wakulima wa nje ya mwaka 2020 yalionesha kwamba, Kampuni ya Mkulazi ilipaswa kusimamia utendaji wa

[27] Barua yenye kumbukumbu namba :ABL/HQ/CR/09-09/VOL.01/VC kutoka benki ya Azania kwenda kampuni ya Mkulazi ya tarehe 9 Octoba 2019

wakulima wa nje kwa kuwapatia ushauri wa kiufundi ili kuhakikisha kuwapo kwa miwa ya kutosha kwa ajili ya kiwanda. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba kampuni ilishindwa kusimamia utendaji wa wakulima wa nje kama ifuatavyo:

Mahojiano yaliyofanywa na afisa wa Kampuni ya Mkulazi anayewasimamia wakulima wa nje yalibaini kwamba, Kampuni ilipaswa kufanya usimamizi wa mara kwa mara angalau mara moja kwa mwezi kwa wakulima wa nje ili kuona maendeleo yao. Hata hivyo, kutokana na uhaba wa rasilimali watu, iliwawia vigumu kusimamia kwa ufanisi utendaji na maendeleo ya wakulima wa nje.

Mapitio ya taarifa za uzalishaji wa wakulima wa nje yalionesha kuwa wakulima wa nje kupitia vyama vyao vya msingi wameshindwa kufikia malengo waliyoyaweka katika uzalishaji wa miwa. Kwa mwaka wa fedha 2017/18 lengo lililowekwa lilikuwa kulima na kupanda ekari 3,200 za miwa lakini walifanikiwa kulima na kupanda ekari 1,044 za miwa. Kwa mwaka wa fedha 2019/20, lengo lilikuwa kupanda ekari 2500 lakini walifanikiwa kulima na kupanda ekari 1035 tu.

Vile vile, wakaguzi walitembelea mashamba ya wakulima wa nje yaliyopo katika vijijji vya Mbigiri na Msowero na kugundua kuwa ekari 202 zilizopo katika chama cha msingi cha Msowero zilikuwa na miwa iliyozidi muda wake wa kuvunwa. Endapo miwa hiyo itaendelea kuwa shambani kwa kipindi kitakachozidi miezi sita bila kuvunwa, itapoteza thamani yake ya kiuchumi. Mapitio ya nyaraka za bajeti ya chama cha kati cha wakulima wa nje wa Magole kwa mwaka wa fedha 2019/20 yalionesha kwamba makisio ya bajeti ya kulima ekari moja ya miwa ilikuwa ni kiasi cha Sh. 907,000. Hivyo, hasara inayotarajiwa kuwapata wakulima wa nje kutokana na ekari 202 za miwa kuzidi muda wake wa kuvunwa kwa chama cha msingi cha Msowero ni sawa na Sh. 183,214,000.

Ninaisihi Menejimenti ya Kampuni Hodhi ya Mkulazi (MHCL):

(a) Kuharakisha ununuzi na uwekaji wa mitambo ya uzalishaji wa sukari katika shamba la Mbigiri;

(b) Kuimarisha udhibiti wa ndani ili kuhakikisha matumizi ya mbolea, dawa za kuulia magugu, na utumiaji mafuta unazingatia matumizi yaliyokusudiwa na viwango vilivyowekwa; na

(c) **Kuanzisha na kudumisha Mfumo wa Usimamizi wa gharama za shamba ili kusaidia Kampuni kusimamia kwa ufanisi gharama za kilimo na kupima utendaji wa shughuli za kilimo kwa muda mrefu.**

10.3.2 Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba

Ukaguzi ulibaini udhaifu katika utekelezaji wa shughuli za manunuzi na ugavi. Udhaifu huo ulionekana katika maamuzi yasiofaa katika kununua greda (Motor grader).

(a) Hasara ya Sh. Milioni 101.53 Iliyotokana na Maamuzi Yasiyofaa ya Ununuzi wa Greda (Motor Grader)

Kifungu cha 75 (b) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma namba 7 ya mwaka 2011 na kufanyiwa marekebisho mwaka 2016 inaruhusu bodi ya zabuni kupitia na kuchambua ripoti. Pia, inaweza kukataa kuidhinisha zabuni zilizochaguliwa na kukitaka au kutoa maelekezo kwa kitengo cha manunuzi kupitia upya mchakato wa tenda au kutangaza upya kwa zabuni hiyo au kuchukua hatua nyingine.

Iligundulika kuwa, wakati wa ufunguzi wa zabuni uliofanyika tarehe 23 Septemba 2019 bei iliyokuwa inasomwa kwa zabuni namba. PA/150/2019-2020/G/02 LOT 2 ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 10-1** hapo chini.

Jedwali 10- 1: Bei Tajwa/iliyosomeka Kwenye Zabuni Namba PA/150/2019-2020/G/02 Lot 2

Na	Mzabuni	Maelezo
1	Mantrac Tanzania Limited	Sh.780,723,636 Kodi ya ongezeko la thamani imejumuishwa
2	Achelis Tanganyika Limited	Sh. 566,783,000 Kodi ya ongezeko la thamani haijajumuishwa
3	General Motors Investment Limited	Sh. 276,120,000 Kodi ya ongezeko la thamani haijajumuishwa
4	Eristic (T) Investment	Sh. 431,617,500 Kodi ya ongezo la ongezo la thamani haijajumuishwa
5	Avic Shantui (T) Limited	Sh. 327,096,000 Kodi ya ongezeko la thamani haijajumuishwa
6	Lonagro Tanzania Limited	Sh. 826,581,600 Kodi ya ongezeko la thamani imejumishwa

Chanzo: *Repoti ya tathmini (Evaluation report) 2019*

Pia mapitio ya ripoti ya tathmini yalionesha kuwa wazabuni watatu ambao ni Mantrac Tanzania Limited, Achelis Tanganyika Limited and Eristic (T) Investment, walifaulu mchakato wa tathmini ya awali.

Katika mchakato wa tathmini ya kina, wazabuni wote watatu walijikuta wakishindwa kutimiza vigezo, hasa vigezo vya kiufundi.

Katika kikao cha dharura cha bodi ya zabuni kilichofanyika tarehe 2 Novemba, 2019, taarifa ya tathmini ilipelekwa kitengo cha manunuzi kwa ajili ya kufanyiwa tathmini upya ambapo walifuta vipimo vifuatavyo: Injini yenye uwezo usiopungua ujazo wa mafuta wa 6.5 – 8 badala ya ujazo wa 9-12 na tenki la mafuta lisilopungua ujazo wa lita 300 badala ya lita 400, kifaa cha kuinulia mizigo kilichopo nyuma ya greda chenye uwezo usiopungua 450 badala ya 600mm, kifaa cha kuchimbia udongo kilichopo mbele ya greda chenye uwezo usiopungua 500 badala ya 800mm kama ilivyoshauriwa na idara ya watumiaji. Mchakato wa kutathmini ulifanyika upya baada ya kufuta vigezo tajwa hapo juu. Hivyo, riporti ya tathmini ya marudio ilihitimisha kwamba hakukuwa na mzabuni aliyekidhi vigezo.

Tarehe 4 Januari 2020 bodi ya zabuni iliamua kupitisha nyaraka za tenda zilizorekebishwa kwa ajili ya manunuzi ya Mota greda 250 HP yenye tenda namba PA/150/2019-2020/G/02 LOT 2. Wazabuni wote waliowasilisha nyaraka zao za zabuni walialikwa kutuma maombi upya, na mwisho wa maombi ilikuwa tarehe 14 Januari 2020. Zabuni mpya ilifuta vigezo vya kifaa cha kuinulia mizigo kilichopo nyuma ya greda chenye upana wa 2200-2400 hadi 1100mm.

Ni wazabuni wawili tu kati ya wazabuni sita walioomba zabuni ambao walikidhi vigezo. Nao ni Mantrac (T) limited kwa bei ya Sh. 770,339,400 na Lanagro Tanzania Limited kwa bei ya Sh. 794,000,000 kodi ya ongezeko la thamani imejumuishwa. Tathmini ya zabuni ilifanyika katika kikao cha tisa cha bodi ya zabuni ambacho kilipitisha ripoti ya tathmini na Zabuni alipewa MS Mantrac kwa thamani Sh. 770,339,400, kodi ya ongezeko la thamani imejumuishwa.

Kufuatia kufutwa kwa vigezo vya ununuzi wa kifaa cha kuinulia mizigo kilichopo nyuma ya greda chenye upana wa 2200-2400 hadi wakati wa mchakato wa kutangaza upya zabuni, inamaanisha kwamba hakukuwa na tofauti kubwa katika bidhaa tajwa. Kifungu namba 28.4 cha maelekezo ya zabuni kilitaja kuwa taasisi ya manunuzi inaweza kufuta vigezo ambavyo havina madhara kwa vifaa tajwa. Hii ni kama vigezo hivyo havitaathiri utendaji wa vifaa tajwa; na kwamba kufuta vigezo hivyo hakutaathiri mchakato wa kuwachagua wazabuni kwa madaraja.

Nimebaini kwamba, Kampuni ya Mkulazi haikufuta vigezo vya ununuzi wa kifaa hicho wakati wa mchakato wa tathmini kwa mara ya pili, bali kampuni ilifuta vigezo wakati wa mchakato wa kutangaza zabuni upya kwa mara ya pili; ambapo ilipelekea wazabuni wachache washiriki. Mchakato wa manunuzi wa kifaa tajwa ulichelewa kwa ajili ya matumizi ya shughuli iliyokusudiwa, pamoja na kuongezeka kwa shughuli za manunuzi, na mwisho zabuni alipewa Mantrac (T) limited kwa gharama ya Sh. 770,339,400, kodi ya ongezeko la thamani imejumuishwa, badala ya Achelis Tanganyika Limited kwa gharama ya Sh. 566,783,000, bila kujumuisha kodi ya ongezeko la thamani.

Kutokana na hali hii, Kampuni ya Mkulazi iliingia gharama za ziada kiasi cha Sh. 101,535,460 kutokana na maamuzi mabovu ya manunuzi; ambapo gharama hizi zingeweza kuepukwa endapo yangefanyika maamuzi makini.

(b) Kujumuishwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani Katika Bidhaa Zenye Msamaha wa Kodi Zenye Jumla ya Sh. bilioni 1.79

Kifungu namba 6(1) na kifungu cha kwanza na cha pili cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kifungu namba 148 R.E cha mwaka 2019 kinaonesha kuwa, bidhaa za kilimo, vikiwemo vifaa vya umwagiliaji na vipuli, ni miongoni mwa bidhaa zilizo na msamaha wa Kodi wa Ongezeko la Thamani.

Ukaguzi ulichambua kama mchakato wa manunuzi wa kutoa zabuni kwa wazabuni haukujumuisha kodi ya ongezeko la thamani katika bidhaa za kilimo ambazo zina msamaha wa kodi. Mapitio ya nyaraka za manunuzi kwa wazabuni waliopewa zabuni kutoka mwaka 2018/19 hadi 2020/21 yalibaini kuwa, Kampuni ya Mkulazi ilitoza kodi ya ongezeko la thamani ya Sh. 1,797,043,446 wakati wanawapatia mikataba wazabuni walioshinda zabuni katika bidhaa ambazo zina msamaha wa kodi kama ilivyobainishwa katika **Jedwali Na. namba 10-2** hapo chini.

Pia, iligundulika kwamba Kampuni ya Mkulazi haikudai marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani. Mahojiano yaliyofanywa na maafisa wa Kampuni yalibainisha kuwa kampuni ilishindwa kudai marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani kwa sababu kampuni haikuwa imesajiliwa kwa ajili ya tozo la ongezeko la thamani.

Jedwali 10- 2: Kujumuisha kodi ya Ongezeko la Thamani katika bidhaa zilizona na msamaha wa kodi

Na	Taarifa za ugavi	Kiasi (Sh.)	Kodi ya ongezeko la thamani asilimia 18 (Sh.)
1	Zabuni ya kusambaza mabomba na kuyaunga kwa kiwango cha 400HA (Zabuni namba PA/150/2019-20/G/11 LOT 2)	1,196,460,173	215,362,831
2	Kusambaza mfumo wa umwagiliaji wa kunyunyizia, Vifaa (kwa sehemu ya kwanza)	440,000,000	79,200,000
3	Ujenzi na kusimika kwa miundo mbinu ya mfumo wa umwagiliaji kwa hekari 756 kwenye shamba la Mbigiri	8,347,114,531	1,502,480,615
Jumla		**9,983,574,704**	**1,797,043,446**

Chanzo: *Mapitio ya nyaraka za zabuni za kampuni ya Mkulazi (2020)*

Hivyo basi, madai ya marejesho ya ongezeko la kodi ya thamani yangeweza kutumika kugharamia shughuli nyingine muhimu.

Ninaisihi Kampuni Hodhi ya Mkaluzi (MHCL) kuharakisha mchakato wa usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ili kuzuia Kampuni kuingia gharama zaidi wakati wa kupata huduma na au bidhaa. Pia, kuhakikisha uamuzi sahihi unafanywa ili gharama za ziada ziepukwe.

10.3.3 Usimamizi Usioridhisha wa Masuala ya Kifedha

Mapungufu yafuatayo yalibainika kuhusiana na usimamizi wa masuala ya kifedha:

(a) Kodi ya Zuio Haikutozwa

Mkataba wa makubaliano ya kutoa huduma za shamba kati ya Kampuni ya Mkulazi na Jeshi la Magereza ulihusisha vibarua kwa ajili ya kazi za shamba na kazi zisizo za shamba. Kifungu namba 26.3 cha mkataba huo kilitaka baada ya kutoa huduma, mtoa huduma anatakiwa kuwasilisha maombi ya malipo; na mmiliki wa shamba (kampuni ya Mkulazi) itapaswa kujibu kwa kuwalipa mtoa huduma (jeshi la Magereza) na kama nyaraka zote zitakuwepo, Kampuni inapaswa kukata kodi ya zuio kutoka kwenye malipo yaliyolipwa.

Hata hivyo, mapitio ya hati za malipo yamebaini kwamba Kampuni ya Mkulazi imekuwa ikilipa malipo moja kwa moja kwa vibarua wa shamba ambao Kampuni ya Mkulazi haikuingia nao makubaliano.

Hivyo katika suala hili kampuni ililipa jumla ya Sh. 688,203,339.05 moja kwa moja kwa vibarua badala ya Jeshi la Magereza kwa muda wa miaka 2018/2019 na 2019/20 mfululizo. Mahojiano yaliyofanywa na maafisa wa kampuni ya Mkulazi yalibainisha kuwa Kampuni haikuzingatia jambo hili ijapokuwa ilifanya hivyo baada ya Jeshi la Magereza kuomba kampuni ya Mkulazi iwalipe vibarua moja kwa moja. Kampuni ya Mkulazi ilitekeleza hilo bila kurejea kwenye masharti na vigezo vya mkataba wa makubaliano. Kiasi kilicholipwa kila mwaka kimeainishwa katika **Jedwali Na. 10-3** hapo chini.

Jedwali 10- 3: Jumla ya kiasi kilicholipwa na kampuni moja kwa moja kwa vibarua

Mwaka wa Fedha	Kiasi (Sh.)	Kiasi ambacho kodi ya zuio haikutozwa (Sh.)
2018/19	292,509,000.00	14,625,450
2019/20	395,694,339.05	19,784,717
Jumla	**688,203,339.05**	**34,410,167**

Chanzo: *Vitabu vya Fedha*

Jedwali Na. 10-3 linaonesha kiasi cha Sh. 292,509,000 na Sh. 395,694,339.05 kwa mwaka wa fedha 2018/19 na 2019/20 kililipwa moja kwa moja kwa vibarua. Pia, Kampuni haikutoza asilimia tano ya kodi ya zuio ambayo ni kiasi cha Sh. 34,410,167 kama matakwa yaliyoainishwa katika masharti ya mkataba.

(b) Kutokuwepo kwa Hati ya Bima kwa Mali za Kampuni

Kipengele namba 29 cha sera ya menejimenti mali ya Kampuni ya Mkulazi kinataka mali zote zisizohamishika kukatiwa bima, na zifanyiwe mapitio mara kwa mara. Pia meneja wa rasilimali watu anapaswa kuhakikisha kuwa mali zote zinazohamishika zinakatiwa bima ili kuzikinga na majanga kama vile moto, wizi na kuhakikisha majengo yote ya kampuni yanakatiwa bima pia.

Hata hivyo, mapitio ya rejesta ya mali zisizohamishika na sera ya bima yalibaini kuwa mashine za Kampuni, magari na majengo hayakukatiwa bima kama inavyopaswa kulingana na sera tajwa hapo juu.

Mahojiano yaliyofanywa na maafisa wa kampuni ya Mkulazi yalionesha kwamba uongozi wa Kampuni utahakikisha kuwa mali zote zisizohamishika zinakatiwa bima. Jumla ya magari 13 na

mashine zenye thamani ya Sh. 2,874,668,225.90 hazikuwa zimekatiwa bima. Ilibainika kuwa, uzembe kwa maafisa wanaohusika ilikuwa ni moja ya sababu ya kutokatia bima mali hizo.

Kutokukatia bima mali za kampuni kunaweza kupelekea hasara endapo ajali na majanga yatatokea na kuathiri utendaji wa kampuni.

(c) Kampuni ya Mkulazi Haijasajiliwa kwa Ajili ya Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani

Kifungu namba 29 (2) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani inazitaka Taasisi za Serikali ambazo zinafanya shughuli za kiuchumi kusajiliwa kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani. Pia, kifungu namba 3 cha sheria hiyo hiyo kinataja kwamba kamishna mkuu anaweza kumsajili mlipakodi kama mfanyabiashara endapo atakidhi vigezo na masharti yafuatavyo: (a) Endapo atatoa vielelezo vya kumhakikishia kamishna kuhusu nia yake ya kuanzisha shughuli ya kiuchumi, ikijumuisha: mikataba, zabuni, mipango ya majengo, mipango ya biashara, taarifa za kibenki; (b) Mtu huyo atafanya manunuzi, na manunuzi hayo yatatozwa kodi ikiwa amesajiliwa; na (c) Kuainisha muda ambao shughuli za kiuchumi zitaanza kuzalisha bidhaa zitakazotozwa kodi.

Kampuni ya Mkulazi kama Taasisi ya Serikali inayotarajia kufanya shughuli za kiuchumi inapaswa isajiliwe kwa ajili ya kodi ya tozo la ongezeko la thamani.

Ukaguzi ulibaini kuwa, tangu kuanzishwa kwake, Kampuni ya Mkulazi haisajiliwa kwa ajili ya tozo la ongezeko la thamani. Pia mahojiano yaliyofanyika na maafisa wa Mkulazi yalidhihirisha kuwa hadi kipindi cha ukaguzi kinamalizika, Kampuni bado ilikuwa kwenye mahojiano na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhusiana na kusajiliwa kwa kodi ya ongezeko la thamani. Ucheleweshaji huo ulitokana na kwamba watendaji wa kampuni walizembea kufuatilia kwa karibu suala la usajili.

Kutokana na kampuni ya Mkulazi kutokusajiliwa kwa kodi ya ongezeko la thamani, inapoteza kiasi kikubwa cha fedha sababu kodi ya ongezeko la thamani imekuwa ikitozwa wakati wa manunuzi ya bidhaa bila kuzidai. Hivyo, kusababaisha kuongezeka kwa gharama za bidhaa hizo. Ukaguzi ulibaini kwamba Kampuni iliingia mikataba 52; ambapo

miongoni mwayo ilikuwa na thamani ya Sh. 50,279,515,851.70. Mikataba hiyo imejumuisha kodi ya ongezeko la thamani yenye kiasi cha Sh. 7,669,756,655.34 katika miaka ya fedha 2017/18 hadi 2019/20.

Kama kiwango hicho kingelipiwa kodi ya ongezeko la thamani wakati wa manunuzi ya bidhaa za kampuni, kingeokoa fedha ambazo zingetumika kwa ajili ya manufaa ya kampuni.

(d) Mgawanyo wa Ubia Wenye Mashaka Baina ya NSSF na Jeshi la Magereza

Marejeo andiko Na. 6 ya ubia na andiko la ushirika yanaonesha kuwa hisa za mtaji za kampuni ni Sh. bilioni 30. Fedha hizo zimegawanyika kwa hisa za shilinngi bilioni kumi. Tarehe 8 Agosti 2018 hisa zilizopitishwa na kampuni ziliongezeka hadi Sh. bilioni 250 kwa mgawanyo wa hisa za kawaida 25,000,000 za Sh. 10,000 kwa kila hisa.

Ukaguzi ulibaini kuwa, mgawanyo wa hisa uliowasilishwa katika taarifa za fedha za kampuni ni 96% kwa NSSF na asilimia nne kwa Jeshi la Magereza. Mapitio ya makubaliano ya ubia ya tarehe 17 Oktoba 2020 kati ya bodi ya wadhamini wa NSSF na jeshi la Magereza yalibainisha kuwa wawili hao walikubaliana kwenye mali alizochangia Magereza zenye thamani ya Sh. 19,380,164,500 ambayo ni sawa na asilimia 7.6 ya hisa za mtaji wa kampuni. Hivyo, Jeshi la Magereza linastahili kuongezewa mgawanyo wa hisa zaidi kulingana na kiasi cha mali alizochangia.

(e) Malipo ya Kiasi cha Sh. 202,020,000 Yalilipwa kwa Mkandarasi Bila Kuwapo kwa Nyaraka za Uthibitisho

Mnamo tarehe 15 Septemba 2020 Kampuni ya Mkulazi iliingia mkataba wenye nambari PA/150/2019-2020/W/04 Lot 1 na mkandarasi anayejulikana kama M/S China Schuan International Corporation Co. Ltd (SIETCO) kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa matatu ya kuhifadhia maji kwa ajili ya umwagiliaji katika eneo la Mbigiri lililopo wilaya ya Kilosa Mkoa wa Morogoro. Gharama ya mkataba ilikuwa Sh. 4,448,502,230.41, zikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani.

Mapitio ya jalada la mkataba, nyaraka za malipo, na taarifa ya ukaguzi wa eneo la kazi yalibainisha kuwa Kampuni Hodhi ya Mkulazi ilimlipa

mkandarasi kiasi cha Sh. 202,020,000 kama malipo ya awali bila kuwa na vielelezo vya malipo ya vipengele vilivyolipwa.

Malipo hayo yalisababisha kupotea kwa thamani ya fedha yenye kiasi cha Sh. 202,020,000 kwa kuwa matumizi ya fedha hizi hayakuwa na vielelezo vya kuthibitisha matumizi yake. **Kiambatisho 10-1** kinaonesha maelezo ya vipengele vilivyolipwa lakini uhalali wa malipo haukuthibitika.

Menejimenti ya MHCL inapaswa:-

(a) Kuhakikisha kodi ya zuio inakatwa katika malipo ya wakandarasi yanayofuata. Kwa kuongezea, MHCL kuhakikisha kuwa katika siku zijazo makato ya kodi ya zuio yanafanyika.

(b) Kuhakikisha mchakato wa usajili wa VAT unakamilika ili kuzuia Kampuni kuingia gharama zaidi wakati wa kupata huduma na au bidhaa;

(c) Kufikiria tena kuifanya kisasa zaidi michakato ya biashara na kupata mifumo thabiti ili kufikia malengo yaliyotarajiwa;

(d) Kuhakikisha kuwa mali zote, hususani mali zinazohamishika kama mashine na magari, zinasajiliwa na nambari za usajili wa umma;

(e) Kuhakikisha kuwa, mali zote ikiwa ni pamoja na mashine, magari na majengo zinakatiwa bima ili kuepusha upotevu wa siku zijazo;

(f) Kurudia uwiano wa hisa katika mchango wa kila mbia na inashauriwa kuharakisha mchakato wa usajili wa wanahisa wapya; na

(g) Kuhakikisha kuwa hati za malipo yanakuwa na viambatisho vya kutosha.

SURA YA KUMI NA MOJA

UPIMAJI WA UTENDAJI HALISI KATIKA MIRADI SABA

11.1 Utangulizi

Sura hii inatoa maelezo na uchambuzi wa utendaji halisi wa miradi saba iliyokaguliwa katika mwaka wa fedha 2019/20.

11.2 Tathmini ya Mwaka ya Utendaji wa Miradi Saba Inayotekelezwa

Sehemu hii inatoa maelezo na uchambuzi wa matokeo yanayohusiana na tathmini ya utendaji ya kila mwaka katika miradi saba inayotekelezwa na Wizara, Idara na Wakala wa Serikali (MDAs) kutoka sekta tatu: Uchukuzi, Nishati na Maji. Miradi hii ni pamoja na miradi minne chini ya sekta ya nishati, miwili chini ya sekta ya usafirishaji na mmoja chini ya Sekta ya Maji kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 11-1.**

Uchambuzi wa matokeo umewasilishwa kwa kuzingatia vipengele muhimu vinne: navyo ni upangaji, usanifu na uhifadhi wa nyaraka za zabuni; michakato ya ununuzi; afya, usalama na mazingira (HSE); na usimamizi wa mikataba ambao hujumuisha usimamizi wa rasilimali watu, usimamizi wa muda wa mikataba, usimamizi wa fedha na usimamizi wa ubora. Kaguzi sita six[28] zilizobaki zimeelezewa katika sura zinazofuata.

Jedwali 11- 1: Miradi inayoshughulikiwa na ukaguzi wa kiufundi

Na	Jina la Mradi	Mtekelezaji	Sekta
1	Kimataifa: Rumonge - Gitaza (45k) na Kabingo-Kasulu-Manyovu (km 260) Mradi wa Kuboresha Barabara	Wakala wa Barabara Tanzania	Uchukuzi
2	Programu ya Usaidizi wa Sekta ya Uchukuzi (TSSP) Kuboresha Barabara ya Tabora-Koga-Mpanda (km 347) na Barabara ya Mbinga-Mbamba Bay (km 67)	Wakala wa Barabara Tanzania	Uchukuzi

[28] (i) Mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (ii) Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) (iii) Mradi wa Upanuzi wa Barabara ya (Kimara-Kibaha) (iv) Mradi wa Umeme wa Maji wa Bwawa la Mwalimu Nyerere (v) Mradi wa Uboreshaji wa Maji wa Same - Mwanga (vi) Mradi waUzalishaji wa Sukari wa Mbigiri.

3	Mradi wa Kuunganisha Umeme Kenya na Tanzania	Shirika la Umeme Tanzania	Nishati
4	Upembuzi Yakinifu wa Mradi wa Bwawa la Kikonge	Shirika la Umeme Tanzania	Nishati
5	Mradi wa Umeme wa Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo	Shirika la Umeme Tanzania	Nishati
6	Uwekezaji wa Miundombinu ya Msingi ya Kusafirisha Umeme (BTIP)	Shirika la Umeme Tanzania	Nishati
7	Mradi Endelevu wa Utoaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Arusha	AUWSA	Maji

Chanzo: *Barua Inaonyesha Mapungufu ya Manejimenti kwa Mwaka Fedha 2019/2020*

11.2.1 Mapitio ya Usanifu Usiotosheleza - Kipande cha Mbinga-Mbamba Bay na Kipande cha Usasula-Komanga Chini ya Programu ya Usaidizi wa Sekta ya Tanzania (TSSP)

Ili kuhakikisha kuwa nyaraka na taarifa ni sahihi, kamili na inafuata viwango vinavyokubalika kimataifa, aya 5.1 ya mkataba Na. TRD/HQ/1032/2016/17 kati ya Wakala wa Barabara Tanzania na M/S LEA International Ltd (Mbinga-Mbamba Bay km 67) na mkataba Na. TRD/HQ/1033/2016/17 kati ya Wakala wa Barabara Tanzania na M/S SMEC International (Usesula - Komanga umbali wa km 108) zinahitaji mshauri kufanya maboresho yote yanayohitajika kutoka katika usanifu uliokamilishwa pamoja na kuboresha gharama (makadirio ya wahandisi). Hata hivyo, ukaguzi wangu juu ya mapitio ya usanifu ulibaini mapungufu yafuatayo:

- Kukosekana kwa ithibati ya ongezeko la asilimia 69 kwa kuzingatia uwakilishi kwa sababu ya kuboreshwa kwa matabaka (G3) kutoka mita za ujazo 870,000 hadi mita za ujazo 1,400,000 kutoka kwenye usanifu wa awali uliofanywa na M/S COWI (eneo la Usesula-Komanga).

- Ukaguzi wa haidroliki na haidrolojia uliofanywa haukuainisha namna ya kukabiliana na upungufu uliokuwa umeonekana wakati wa awamu ya ujenzi wa mradi (sehemu ya Usesula-Komanga)

- Muhtasari wa ripoti ya ukaguzi wa usanifu wa M/S LEA International Ltd ulianisha mahitaji ya ziada kulingana na mabadiliko (pamoja na mahitaji ya ziada) kwa maelezo ya michoro

na Makadirio ya Gharama za Ujenzi. Hata hivyo, hakukuwa na mpango na wasifu wa michoro ya sehemu nzima juu ya mabadiliko yaliyotambuliwa ambayo yalipelekwa kwa mwajiri na pia wakati wa ujenzi (eneo la Usesula-Komanga).

- Uchimbaji wa kawaida uliongezeka kutoka mita za ujazo 800,000 hadi 1,100,000. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 38 ya ilivyopangwa awali na Kampuni iitwayo "UWP South Africa/Tanzania". Hata hivyo, uthibitisho wa ongezeko hilo haukuwa na viambatisho wala haukuwekwa kimaandishi (katika eneo la Usesula-Komanga)

- Wakati wa ukaguzi uliofanyika mwezi Oktoba 2020, kiasi cha uchimbaji wa kawaida kilikuwa na mita za ujazo 2,517,278 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 129 ya kiasi kilichokaguliwa. Inakadiriwa kuwa idadi ya mwisho inaweza kuongezeka hadi takriban mita za ujazo 2,800,000 sawa na asilimia 154.54. Pia ilibainika kuwa, ongezeko hilo halina ushahidi wa kutosha (Mbinga-Mbamba Bay).

- Nilibaini zaidi kuwa, wakati wa ukaguzi Oktoba 2020, madaraja mawili yaliyojengwa (km 131 + km540 na km 127 + km 534) hayakuwa katika eneo la awali lililobuniwa (Mbinga-Mbamba Bay).

Ninamshauri Wakala wa Barabara kuanzisha:

(a) Adhabu na vikwazo kwa uzingatiaji duni wa Hadidu za Rejea na mapungufu yaliyobainika katika ripoti za mapitio ya muundo; na

(b) Taratibu za ufuatiliaji wa udhibiti wa ubora na uhakikisho wa washauri wa ukaguzi wa muundo ili mabadiliko kama hayo yasiyofaa katika wigo wa kazi yasitokee wakati wa utekelezaji wa mkataba.

11.2.2 Kutokuwa na Mpango Unaofaa wa Manunuzi ya Shughuli ya Ujenzi na Huduma - Kimataifa: Rumonge - Gitaza (45km) and Kabingo - Kasulu - Manyovu (260km) Road Upgrading Project.

Nilikagua mpango wa ununuzi wa kila mwaka wa TANROADS unaohusiana na mwaka wa fedha 2018/19 ambao ulihusisha mawanda ya kimataifa: Rumonge - Gitaza (km 45) na Kabingo -

Kasulu - Manyovu (260 km) Mradi wa Kuboresha Barabara ulikuwa miongoni mwa shughuli zilizopangwa.

Nilibaini kuwa kazi ya mradi wa Kabingo - Kasulu - Manyovu (km 260.6) chini ya mkataba Na. TRD/HQ/1035/2019/20 ya fungu 1-4 ilipangwa kutiwa saini tarehe 10 Januari 2019. Pia, washauri walipaswa kutia saini kandarasi zao tarehe 15 Agosti 2019 kwa ajili ya usimamizi wa wakandarasi. Hii inamaanisha kwamba, wakandarasi walitakiwa kutia saini na kusubiri kwa miezi saba ili washauri watie saini kandarasi zao za usimamizi. Kipindi hiki kimezidi muda wa kujipanga wa makandarasi, ambayo ni miezi mitatu baada ya kutiwa saini kwa kandarasi. Kulingana na mikataba, makandarasi hawawezi kuanza kazi zao kabla ya idhini ya washauri. Mpango wa ununuzi wa mwaka haukuandaliwa vema kwa maana mkandarasi hawezi kuanza kazi kabla ya wahandisi washauri kusaini mikataba yao.

Hii siyo tu kinyume na Kanuni ya 69 (3) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016), lakini pia inaongeza hatari ya kuchelewesha kukamilika kwa kazi.

Ninamshauri mtekelezaji wa mradi kuhakikisha kuwa kuna mipango sahihi ya manunuzi ya mkandarasi wa ushauri wa kazi na huduma.

11.2.3 Mapungufu Katika Kuongeza Muda wa Uhalali wa Zabuni na Kutolewa kwa Malipo ya Awali - Kabingo - Kasulu - Manyovu (km 260.6)

Ili kudhibitisha utoshelevu wa mchakato wa zabuni inayohusiana na mkataba Na. TRD/HQ/1035/2019/20 ya mradi wa uboreshaji wa barabara (Kabingo-Kasulu-Manyovu), nilikagua mafaili ya kandarasi, ripoti za hali halisi ya mradi na kufanya ziara ya eneo la mradi. Nilibaini yafuatayo:

a) Ongezeko la Muda wa Uhalali wa zabuni Zaidi ya Muda Uliohitajika

Tathmini iliyofanywa juu ya mchakato wa kumpata mkandarasi ambao ni pamoja na uchambuzi wa kipindi cha uhalali wa zabuni kupitia hati za zabuni, mafaili ya mkataba, na ripoti ya upimaji wa mradi wa kumpata mkandarasi wa kazi kwenye vifungu (1-4)

vinavyohusiana na mkataba Na. TRD /HQ /1035/2019/20 ya mradi wa uboreshaji wa barabara (Kabingo - Kasulu - Manyovu) imebaini kuongezwa kwa kipindi cha uhalali wa zabuni. Hii ni kwa sababu ilichukua siku 224 badala ya siku 40 kama ilivyoainishwa katika mpango wa ununuzi wa kila mwaka (APP) na hati ya zabuni. Ilibainika kuwa, Wakala wa barabara Tanzania ilichukua siku 349 kwa kipindi chote cha mchakato wa zabuni kutoka matangazo hadi kutia saini kwa mkataba badala ya siku 89 kama ilivyoainishwa katika mpango wa ununuzi wa kila mwaka.

b) Ucheleweshaji Mkubwa wa Ununuzi wa Washauri Wasimamizi

Kifungu 8.1.1 cha masharti ya jumla ya mkataba (GCC) ya mkataba Na. TRD /HQ /1035/2019/20 ya mradi wa uboreshaji wa barabara (Kabingo - Kasulu - Manyovu) uliainisha kuwa mkandarasi alipaswa kuanza kazi baada ya kupokea maagizo ya mhandisi na mshauri akikabidhiwa eneo la mradi.

Kinyume na GCC, ukaguzi wa mafaili ya kandarasi na ripoti za maendeleo zinazohusiana na fungu 3 (makutano ya Mvuge-Nduta) uligundua kucheleweshwa kwa zaidi ya siku 200 katika kutoa kandarasi kwa mshauri (M/S Conseil Ingeniere) kama ilivyotolewa tarehe 15 Septemba 2020, wakati mkandarasi (M/S STECOL Corporation) alipewa kandarasi tarehe 12 Februari 2020. Ucheleweshaji wa kupata mkandarasi ulipelekea kuharibu ratiba za mkandarasi na mpango wa kazi ambao pia unaathiri tarehe ya kukamilika kwa mradi na manufaa yaliyokusudiwa pia.

c) Kuchelewesha Kutolewa kwa Malipo ya Mapema (malipo ya awali) Sh. 48,845,899,638.47

Kifungu cha 14.7.1 cha GCC kwa mkataba Na. TRD/HQ/1035/2019/20 ya mradi wa uboreshaji wa barabara (Kabingo - Kasulu - Manyovu) unataja kuwa "malipo ya mapema yanapaswa kutolewa ndani ya siku 42 baada ya kutoa barua ya kukubalika au ndani ya siku 21 baada ya kupokea hati zinazohusiana na malipo ya awali yaliyolipwa"

Kinyume na kifungu hicho, uhakiki ulibaini kuwa wakati wa ukaguzi Oktoba 2020, malipo ya awali kwa awamu mbili yaliyofikia kiasi cha Sh. 24,140,302,482.31 yalicheleweshwa kulipwa kwa kipindi cha hadi siku 80 wakati ankara nyingine mbili

za malipo ya awali zilitolewa tarehe 23 Juni 2020 na 15 Juni 2020 jumla ya Sh. 24,705,597,156.16 zilikuwa bado hazijalipwa ikiwa ni ucheleweshaji wa zaidi ya siku 123. Ulipaji usio kwa wakati wa malipo ya awali unazuia mkandarasi kufanya maandalizi ya awali, hatimaye kuathiri kipindi cha kukamilika kwa mradi pia kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 11-2**.

Jedwali 11- 2: Maelezo ya kucheleweshwa kwa malipo ya awali

Jina la Mkandarasi	Kiasi cha Ankra (Sh.)	Maelezo
M/S Zhejiang Communications Construction	11,426,940,692.19	Imecheleweshwa kwa siku 80, ikilinganishwa na tarehe 18 Mei 2020 ankra ilipotolewa na kulipwa tarehe 19 Agosti 2020, kazi zinahusiana na awamu ya 1.
M/S Sinohydro Corporation	12,561,125,156.99	Ankra ilitolewa tarehe 23 Juni 2020 lakini mpaka wakati wa Ukaguzi uliofanyika Oktoba 2020 malipo yalikuwa hayafanyika. Huu ni ucheleweshaji zaidi ya siku 123, kazi inahusiana na fungu la 2.
M/S STECOL	12,713,361,790.12	Imecheleweshwa kwa siku 53, kama ilivyopewa ankara tarehe 3 Juni 2020 na kulipwa tarehe 19 Agosti 2020, kazi zinahusiana na kifungu Na. 3.
M/S CHICO	12,144,471,999.17	Ankra ilitolewa tarehe 15th June, 2020 lakini mpaka wakati wa Ukaguzi uliofanyika Octoba 2020 malipo yalikuwa hayafanyika,ikiwa ni ucheleweshaji wa siku 123, kazi ilikuwa ya kifungu Na. 4
Jumla	**48,845,899,638.47**	

Chanzo: *Hati za Malipo*

Ninawahimiza watekelezaji wa mradi kuhakikisha kuwa malipo ya awali yanatolewa kwa wakati kwa wakandarasi ili kuwezesha shughuli za uandaaji wa eneo la mradi. Hii itasaidia kuharakisha ukamilishaji wa mradi. Kwa kuongezea, kuhakikisha hakuna nyongeza yoyote ya muda inayotolewa zaidi ya muda uliohitajika.

11.2.4 Nyaraka za Ununuzi Zilizokosekana - Mradi wa Uwekezaji wa Miundombinu ya Msingi ya Kusafirisha Umeme (BTIP)

Kanuni ya 10 (1) na 88 (4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016) inataka taasisi inayonunua kuhifadhi kumbukumbu za kutosha za maandishi ya shughuli zote za ununuzi kwa uwazi na kupatikana kwa urahisi habari za ununuzi. Kila tendo la manunuzi ni lazima liratibiwe na taarifa

zake zihifadhiwe kikamilifu. Hii itasaidia ukaguzi kuanzia mwanzo wa kupokea mahitaji ya manunuzi hadi mwisho wa mkataba.

Mapitio ya nyaraka za zabuni na taarifa ya tathmini kwa mkataba Na. PA/001/2015/HQ/W/49 (Lot 2 –T6) na mahojiano na Kitengo cha Manunuzi cha Shirima la Umeme Tanzania, niligundua kuwa kuna nyaraka zinakosekana zinazohusiana na zabuni na tathmini kama vile nakala ya tangazo, barua za kuteuliwa wajumbe wa kamati na tathmini. Nyaraka hizi hazikuweza kutolewa zilipotakiwa wakati wa ukaguzi.

Ninahimiza menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania kuimarisha utunzaji wa nyaraka za michakato ya ununuzi ili kuongeza uwajibikaji na uwazi ili ziweze kutumika kwa kumbukumbu ya baadaye.

11.2.5 Kazi kubwa bado Hazijaanza Kutokana na Kusubiri Kukamilika kwa Makubaliano ya Fedha kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) - BTIP (vituo vya Iringa na Shinyanga)

Shirika la Umeme Tanzania liliingia mkataba Na. PA/001/2015/HQ/W/49 tarehe 28 Machi 2018 (ambayo pia ni tarehe ya kuanza kwa kazi) na Kampuni ya Umeme ya M/S Sieyuan kwa ujenzi wa vituo vya umeme 400/220kV huko Iringa na Shinyanga (T6-fungu 1) kwa jumla ya mkataba wa Dola za Marekani 41,905,593 na Sh. 348,800,000 chini ya " Uwekezaji wa Miundombinu ya Msingi ya Kusafirisha Umeme (BTIP)" na tarehe iliyotarajiwa kukamilika ni Januari 2020.

Mapitio yangu ya mafaili ya kandarasi, ripoti za maendeleo, na uhakiki halisi katika maeneo ya mradi huko Iringa na Shinyanga mwaka Novemba 2020 yalibaini kuwa, mkandarasi bado hajafanya kazi kubwa za ujenzi kwa kuchelewa kwa zaidi ya miezi 10. Nilibaini zaidi kuwa, mkataba wa kazi hizo ulisainiwa kabla ya kumalizika kwa mkataba wa makubaliano ya mkopo (marekebisho ya makubaliano ya fedha nambari 4) kati ya Serikali ya Tanzania na EIB ambayo ilikuwa ikizuia mkandarasi kuanza kazi kuu.

Ninamsisitiza mtekelezaji wa mradi husika kufanya ufuatiliaji kwa Wizara ya Fedha na Mipango ili kuhakikisha kuwa,

Marekebisho Namba 4 ya makubaliano ya fedha yametiwa saini ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa mradi.

11.2.6 Kuchelewesha Kukamilika kwa Kazi na Mapungufu Yaliyoonekana katika Utekelezaji - BTIP (Vituo vya Dodoma na Singida)

Sambamba na nambari ya mkataba PA/001/2015/HQ/W/49 ya ujenzi wa vituo vidogo vya Dodoma na Singida (T6 fungu Na. 2), ukaguzi wangu wa mafaili ya kandarasi, ripoti za maendeleo na hali halisi ya utekelezaji ulibaini maendeleo duni ya kazi zinazokadiriwa kuwa asilimia 87.8 mpaka wakati wa ukaguzi Oktoba 2020. Hata hivyo, kazi zilitegemea kuanza tarehe 28 Machi 2018 na zilitarajiwa kukamilika Januari 2020, huku muda wa nyongeza ukitolewa hadi tarehe 31 Desemba 2020 ili kukamilisha kazi zilizobaki.

Ukaguzi zaidi wa maendeleo halisi ya mradi ulibaini vizuizi vinavyohusiana na udhibiti wa ubora na mapungufu katika kazi ya ujenzi wa vipande vya alumini na shughuli za zege. Wakati vipande vya alumini vilikuwa vimepindwa baada ya kujichomoza, ubora wa zege ulikuwa hauridhishi ikilinganishwa na mpango wa udhibiti ubora.

Kwa kuongezea, nilibaini vitu vinne kwenye makadirio ya gharama za ujenzi (laini ya 33kV, chaja mbili za betri na transfoma 220kV) vyenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani 383,301.67 zinazohusiana na njia ya kV ya Dodoma na Singida haikujumuishwa kwenye BoQ ya awali. Mkandarasi aliwasilisha makadirio yake kama mbadala wa vitu vya BoQ vilivyoachwa kwa kupendekeza 440kV kwa njia ya kuchepuka ya Singida kwa gharama ya jumla ya Dola za Marekani 975,396. Ninaona kuwa, tofauti zinaweza kuleta gharama za ziada za kandarasi ambazo mshauri anapaswa kukagua kabisa mahitaji ya ziada yaliyowasilishwa kwa uwezekano wa kupunguza gharama. Kwa mfano, kuhusiana na mahitaji ya ziada ya mkandarasi wa laini ya 440kV, naomba Shirika la Umeme Tanzania liagize mkandarasi kupendekeza suluhisho mbadala la uwekaji wa mirija ya bafa ya mirija ya aluminiamu kwa transfoma ya 220kV badala ya 440kV. Pia, lifuate maelezo ya kiufundi yaliyotolewa na muuzaji ili kupunguza gharama na kiwango cha kudondoka baada ya

kufungwa kwa kuzingatia vigezo vya kiufundi vilivyopo kwenye mkataba.

Ninamshauri mtekelezaji wa mradi husika kumwamuru mkandarasi kuandaa mpango mpya wa kazi ulioboreshwa akionesha juhudi za kukamilisha kazi ndani ya muda wa ziada ulioidhinishwa.

11.2.7 Kasi Ndogo Katika Utekelezaji wa Shughuli za Mradi Ambazo Zinarudisha Nyuma Ratiba ya Ukamilishaji - Mradi wa Umeme wa Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo (Sehemu ya Njia ya Kusafirisha Umeme - Tanzania)

Shirika la Umeme Tanzania liliingia mkataba Na. PA/001/2017-8/HQ/W/22 na Kampuni ya Sterlin na Wilson kwa bei ya kandarasi ya Dola za Marekani 13,979,307.90 na Sh. 2,681,953,030.79 kwa ununuzi wa mkandarasi wa EPC. Hii ilikuwa kwa ajili ya usanifu, usambazaji, usanikishaji, upimaji na uwekaji wa laini ya 220kV Rusumo - Nyakanazi chini ya Mradi wa Umeme wa Maji wa Maporomoko ya Rusumo (sehemu ya njia ya kusafirisha umeme - Tanzania) kwa kipindi cha miezi 18. Mkataba ulisainiwa tarehe 29 Mei 2019 (ambayo pia ni tarehe ya kuanza) na tarehe inayotarajiwa kukamilika ni Novemba 2020.

Kinyume na tarehe iliyotajwa hapo juu ya kukamilika, ukaguzi wangu wa mafaili ya kandarasi, ripoti za maendeleo, na uhakiki wa maeneo ya mradi Novemba 2020 uligundua kucheleweshwa kwa utekelezaji wa shughuli za mradi na makadirio ya maendeleo halisi ni 6.48%. Nilibaini kwamba, kazi zilikuwa katika hatua za mwanzo wakati mkandarasi alikuwa amelipwa jumla ya Dola za Marekani 1,397,930.79 na Sh. 268,195,303. Maelezo zaidi yameoneshwa katika **Kiambatisho Na. 11-1.**

Ninafahamu kuwa kasi ndogo ilitokana na ucheleweshaji wa kupata misamaha ya ushuru na kuzuka kwa janga la COVID-19. Hata hivyo, ninaisihi menejimenti kufuatilia haraka misamaha ya ushuru inayosubiriwa na kuzingatia ushauri na kuchukua tahadhari ili angalau shughuli nyingine za mradi ziweze kuendelea licha ya kuwapo kwa janga la COVID-19. Ni maoni yangu kuwa, kasi ndogo ya utekelezaji inaongeza hatari ya kucheleweshwa kukamilika na uwezekano wa gharama za ziada

za mradi katika siku zijazo kwa sababu ya kupanda kwa bei ya vifaa na fahirisi nyingine za uchumi.

Ninamhimiza mtekelezaji wa mradi husika kuwasiliana na mkandarasi na mshauri elekezi ili kuhakikisha mpango kazi wa mwaka unatekelezwa bila kucheleweshwa zaidi. Pia, Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe kuwa malipo ya hati za kazi zilizowasilishwa yanalipwa kwa wakati na misamaha ya ushuru iliyoombwa kwa mradi inatolewa mara moja.

11.2.8 Kuchelewesha kuwekwa kwa Minara Miwili ya Umeme Nchini Rwanda kwa Sababu ya Vizuizi vya Idhini ya Kuingia Nchini Rwanda - Mradi wa Umeme wa Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo (sehemu ya njia ya kusafirisha umeme - Rwanda)

Mkataba Na. PA/001/2017-18/HQ/W/22 ya Mradi wa Umeme wa Rusumo-Nyakanazi (njia ya kupitishia Rwanda 220kV) ilihitaji kukamilika kwa ufungaji wa minara miwili ya umeme kwa upande wa Rwanda ifikapo Agosti 2020.

Wakati wa ukaguzi Novemba 2020, nilibaini kuwepo kwa kazi zinazosubiri uwekaji wa minara miwili kwa upande wa Rwanda kwa sababu ya vizuizi vya idhini ya kuingia iliyotokana na janga la COVID-19. Kazi zinazosubiri ni pamoja na uchunguzi wa mchanga na uchimbaji wa msingi. Hivyo, ningependa kusisitiza kwamba Shirika la Umeme Tanzania kupitia Serikali ya Tanzania liimarishe mawasiliano na Serikali ya Rwanda ili kutatua suala la idhini ya kuingia; na kwamba, kazi za ufungaji wa minara hiyo miwili ianze bila kucheleweshwa zaidi.

Ninamshauri mtekelezaji wa mradi husika kwa kushauriana na Wizara ya Nishati waanzishe haraka mazungumzo na mamlaka zinazohusika za Rwanda juu ya kuachia vizuizi vya kuingia ili shughuli zilizopendekezwa katika maeneo mawili ya mnara zifanyike.

11.2.9 Mkandarasi Mshauri Kunyimwa Ufikiaji Kamili wa Maeneo ya Mradi - Mradi wa Kuunganisha Umeme Kenya na Tanzania

Kifungu cha 33.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba Na. KETRACO/PT/017/2014-PA/001/2015/HQ/W/49 fungu T1 (Singida-Babati), fungu T2 (Babati-Arusha), fungu T3 (Arusha-

Namanga) kati ya Shirika la Umeme Tanzania na M/S Consortium Energoinvest (EMC) Limited (mshauri) wa tarehe 6 Aprili 2017, kinamtaka mwajiri kumpa mshauri uwezo wa kuyafikia maeneo ya mradi wakati wa utoaji wa huduma zake.

Kinyume na kifungu hicho, uhakiki wangu ulibaini kuwa hadi wakati wa ukaguzi uliofanyika Novemba 2020 mshauri bado alikuwa hajayafikia maeneo matano kati ya maeneo 387 ya mradi yaliyotambuliwa chini ya fungu T1 kutokana na kunyimwa haki ya kupita. Huu ni ucheleweshwaji wa zaidi ya miezi 44 tangu tarehe ya kuanza kwa mkataba ambayo ni 6 Aprili 2017.

Kwa kuongezea, nilibaini ucheleweshaji wa kutoa kibali cha kufika kwenye mradi ndani ya siku 21 kuanzia tarehe za mkataba (tarehe ya makabidhiano) kwa fungu T2 na T3 ambayo ulicheleweshwa kutolewa kwa kipindi cha miezi 11 na 14 dhidi ya tarehe halisi ambazo ni 23 Juni 2017 na 31 Machi 2017, mtawalia. Ni maoni yangu kwamba, kuchelewesha kuyafikia maeneo hayo kunazuia mkandarasi mshauri kutekeleza majukumu yake vya kutosha na kuathiri kukamilika kwa shughuli za mradi.

Ninaisihi menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania kuharakisha fidia ya mwisho kwa watu walioathirika na mradi ili kupunguza ucheleweshaji zaidi na madai ya ziada yanayotokana na muda kupita na matumizi duni ya rasilimali na wakandarasi. Kwa kuongezea, kuhakikisha kuwa, katika kazi zote zijazo wakandarasi wanapewa ufikiaji kamili wa eneo la mradi kwa wakati

11.2.10 Kuchelewesha Kutoa Notisi ya Serikali (GN) ya Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) - Upembuzi Yakinifu wa Mradi wa Bwawa la Kikonge

Shirika la Umeme Tanzania liliingia mkataba Na. PA/001/2016-17/HQ/ /020 na Kampuni ya Studio ING. G. Pietrangeli (SP) kwa upembuzi yakinifu wa Mradi wa Umeme wa Rusumo - Nyakanazi. Sambamba na utekelezaji wa shughuli za mkataba, aya ya 4.5 na 4.6.1 ya Waraka wa Hazina nambari ya 6 wa 2017 unahitaji msamaha wa kodi kutolewa kwa bidhaa, vifaa na vyombo kupitia utoaji wa Ilani ya Serikali (GN).

Kinyume na Waraka huo wa Hazina, nilibaini kuwa Shirika la Umeme Tanzania kupitia Wizara ya Nishati iliwasilisha ombi la msamaha wa ushuru kwa Wizara ya Fedha na Mipango tarehe 3 Julai 2018. Hata hivyo, mpaka wakati wa ukaguzi Novemba 2020 hawakupewa msamaha wala ufafanuzi na Wizara ya Fedha na Mipango. Ni maoni yangu kuwa, ucheleweshaji zaidi unaongeza hatari ya kuzidi kwa gharama ya mradi ambapo ninahimiza Shirika la Umeme Tanzania ifuatilie haraka msamaha wa ushuru kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa utekelezaji wa kutosha wa shughuli za mshauri.

Ninalisihi Shirika la Umeme Tanzania lifuatilie haraka msamaha wa ushuru kutoka kwa Wizara ya Fedha na Mipango ili kutekeleza vyema shughuli za mshauri.

11.2.11 Mshauri Akiendelea na Kazi Kupitia Mkataba Uliomalizika - Upembuzi Yakinifu wa Mradi wa Bwawa la Kikonge

Tarehe 11 Desemba 2018 TANESCO iliingia mkataba Na. PA/001/2016-17/HQ/C/019 na Multiconsult (mshauri) kwa ajili utoaji wa huduma ya kandarasi ya ushauri kwa Mkakati wa Utafiti wa Mazingira na Tathmini ya Jamii wa miezi mitano na tarehe inayotarajiwa kukamilika ni Februari 2020.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, mkataba ulimalizika mnamo Februari 2020 lakini wakati wa ukaguzi Novemba 2020 mshauri alikuwa akiendelea na kazi bila kuhuishwa kwa mkataba uliomalizika. Kuendelea kufanya kazi na mkataba uliokwisha muda wake ni batili na huongeza hatari ya kupoteza kinga ya kisheria ikiwa kutakuwa na mgogoro/mzozo hapo baadaye.

Ninashauri uongozi uimarishe udhibiti wa usimamizi wa mikataba kama vile marekebisho ya kuongeza kipindi cha mkataba yanapaswa kukamilika kwa wakati.

11.2.12 Kuongezeka kwa Viwango vya Malipo ya Ziada Kutagharimu Shirika la Umeme la Tanzania Dola za Marekani 4,412,556 - Mradi wa Kiunganishi cha Umeme cha Kenya Tanzania (KTPIP)

Shirika la Umeme Tanzania liliingia mkataba Na. PA/001/2015/HQ/W/49 na Kampuni ya Consortium Energoinvest (EMC) Limited (mshauri) wa uwekaji (usanikishaji) wa kituo kipya

jijini Arusha na upanuzi wa kituo kidogo huko Singida kwa makadirio la malipo maalum ya kibali cha mzigo yanayofikia Dola za Marekani 5,883,408. Hii ni ada inayokadiriwa kwa magari yaliyopakia zaidi kulipishwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kama inavyotakiwa na Sehemu ya 4 (2) ya Sheria ya Udhibiti wa Mizigo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2016 na Kanuni ya 11 (1) ya Udhibiti wa Mizigo ya Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Hatua za Utekelezaji) Kanuni ya 2017.

Hata hivyo, mnamo tarehe 28 Mei 2019 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano iliongeza viwango vya malipo ya ziada kuwa Dola za Marekani 1,470,852 ambazo zinatokana na gharama za ziada zinazotarajiwa kwa kiasi cha Dola za Marekani 4,412,556 ambazo TANESCO italazimika kulipa na kuongeza gharama za mradi.

Ninasihi Shirika la Umeme Tanzania kuwasiliana haraka na wafadhili husika kwa uwezekano wa ufadhili wa ziada ili kuepusha ucheleweshaji wa utekelezaji wa shughuli za mradi katika siku zijazo. Pia, kuhakikisha kuwa kuna mpango wa ufadhili wa kulipia gharama za malipo wakati malipo yanapotakiwa kufanyika. Zaidi, mawasiliano yafanyike na Wizara inayohusika juu ya jinsi mabadiliko ya ushuru yatavyoshughulikiwa kwenye mkataba uliopo kabla ya kuanza mabadiliko hayo ya ushuru ili kuepusha upotoshaji wa mipangilio ya fedha iliyopo na mikataba iliyopo.

11.2.13 Kutoanzishwa kwa Bodi ya Usuluhishi wa Migogoro - Mradi wa Umeme wa Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo

Shirika la Umeme la Tanzania liliingia mkataba Na. PA/001/2017-18/HQ/W/22 na Kampuni ya Sterlin na Wilson wa Mradi wa Umeme wa Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo. Kifungu cha 8.2.1 cha GCC kinaainisha kuanzishwa kwa "Bodi ya Usuluhishi wa Migogoro" ndani ya siku 28 baada ya tarehe ya kuanza kwa mkataba. Bodi hiyo itawajibika kwa upatanishi au utatuzi wa mabishano yanayotokea kati ya wahusika wakati wa utekelezaji wa kandarasi na makubaliano yanasainiwa baada ya kuanza kwa utekelezaji wa makataba wa kati au wa muda mrefu.

Kinyume na mahitaji, wakati wa ukaguzi Novemba 2020 nilibaini kuwa Bodi ya Usuluhishi wa Migogoro ilikuwa bado haijaanzishwa. Hali hii inaongeza hatari ya kuwa na migogoro ya muda mrefu na isiyotatuliwa wakati wa utekelezaji wa mkataba.

Kwa hivyo, ninawahimiza washirika wa kandarasi kuanzisha Bodi ya Mizozo bila kuchelewesha zaidi ili kuepusha hatari ya kutokubaliana ikiwa kutakuwa na mzozo na mkandarasi.

11.2.14 Gharama ya Nyongeza kwa Sababu ya Kucheleweshwa Malipo ya Madai ya Makandarasi Sh.132,499,311.04

Kiambatisho Na. 1 cha mkataba Na. KETRACO/PT/017/2014-PA/001/201/HQ/W/49 fungu T1 (Singida-Babati), fungu T2 (Babati-Arusha) na fungu T3 (Arusha-Namanga) chini ya Mradi wa Kuunganisha Umeme Kenya na Tanzania kinamtaka mwajiri kuidhinisha malipo ya wakandarasi ndani ya siku 90 baada ya kupokea ankara. Ikiwa atachelewesha malipo kiwango cha riba cha 0.5% kitatozwa kwa mwaka hadi malipo yatakapokamilika.

Kinyume na usimamizi wa mkataba, hakiki yangu ilibaini kuwa, kati ya jumla ya madai 31 ya mkandarasi yaliyowasilishwa kwa fungu T1, 29 sawa na 97% yalilipwa baada ya siku 90. Jumla ya madai 23 ya wakandarasi yaliwasilishwa kwa fungu T2. Madai 22 sawa na 96% walilipwa baada ya siku 90. Jumla ya madai 11 ya mkandarasi yaliwasilishwa kwa fungu T3. Madai saba sawa na 64% yalilipwa baada ya siku 90.

Kuchelewa kwa malipo ya madai ya mkandarasi kunatokana na gharama za ziada kwa mradi kutoka kwenye riba inayotozwa. Kwa mfano, nilibaini adhabu kutoka kwa ada ya riba inayopatikana ya Dola za Marekani 9,214.25 sawa na Sh. 21,054,561 na Sh. 9,689,523.99 kwa fungu T1, T3 na T4 ambazo zinaweza kuongeza gharama za jumla za mradi.

Kwa hivyo, nashauri Shirika la Umeme Tanzania kuhakikisha kuwa madai ya wakandarasi yanalipwa kwa muda uliokubaliwa ili kuepuka adhabu kutoka kwa ada ya riba inayoongeza gharama za mradi.

Nilikagua zaidi mafaili ya kandarasi, hati za malipo na ripoti za maendeleo zinazohusiana na ujenzi wa mifumo ya maji na ofisi za AUWSA. Nilibaini kuwa wakati wa ukaguzi 15 Oktoba 2020 AUWSA ilikuwa bado haijalipa madai ya wakandarasi yanayohusiana na mikataba mitatu ambayo ilipelekea malipo ya riba hadi kiasi cha Sh. 101,755,225.80. Kuchelewesha kufanya malipo haya ni kinyume na kifungu cha 4.6.1 cha GCC ya mikataba. Kwa hiyo, ninasihi AUWSA ilipe madai ya wakandarasi waliosalia ili kuepusha mkusanyiko zaidi wa ada ya riba ambayo itaongeza gharama za mradi kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 11-3** hapa chini.

Jedwali 11- 3: Gharama za Riba Kutokana na Malipo Yaliyocheleweshwa

Mkataba Na.	Kiasi cha riba kilichotozwa (Sh.)
Mkataba.Na AUWSA/AfDB/W/002/2017 wa Ujenzi wa Mabwawa ya Udhibiti wa Taka	38,000,004.95
Mkataba Na. AUWSA/AfDB/W/009/2017 wa Ujenzi wa ofisi za kanda za AUWSA	4,497,156.34
Mkataba Na. AUWSA/AfDB/W/010/2017 wa Ujenzi wa Mfumo Mpya wa Maji	59,258,064.51
Jumla	**101,755,225.80**

Chanzo: *Hati za malipo na mafaili ya miradi*

Kwa hivyo, ninahimiza Shirika la Umeme Tanzania na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha kuhakikisha kuwa madai ya wakandarasi yanalipwa kwa muda uliokubaliwa ili kuepuka tozo inayotokana na ada ya riba inayoongeza gharama za mradi.

11.2.15 Kushindwa Kupata Kiasi cha Sh. 344,320,647.56 Kutoka kwa Mhandisi Mshauri Aliyesitishiwa Mkataba - Mamlaka ya Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA)

Mamlaka ya Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA) ilisitisha mkataba namba AUWSA/AfDB/W/005/2017 na M/S Tanchi Brothers Construction Ltd kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi kuu (AUWSA).

Mapitio yangu yaligundua kuwa, mkataba ulisitishwa tarehe 11 Desemba 2019 kwa sababu ya utendaji mbovu wa mshauri. Sambamba na kifungu cha 7.7 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba,

AUWSA inatakiwa kurejeshewa jumla ya Sh. 344,320,647.56. tofauti kati ya adhabu inayostahili ya Sh. 1,073,127,835.76 na thamani ya kazi iliyotekelezwa na vifaa vilivyokuwepo kwenye mradi Sh. 728,807,188.20. Wakati wa ukaguzi tahehe 15 Oktoba 2020 AUWSA bado ilikuwa haijarejeshewa kiasi cha Sh. 344,320,647.56 kutoka kwa mshauri licha ya kusitisha mkataba.

Niligundua kuwa, kucheleweshwa kurejeshwa kiasi cha fedha kulitokana na ufuatiliaji duni wa usimamizi wa AUWSA. Ucheleweshwaji huo, huongeza uwezekano wa kupoteza fedha za umma ikiwa kiasi hicho hakitarejeshwa.

Nilibaini zaidi kuwa mkataba ulikatishwa bila kupelekwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG). Hii ni kinyume na Kanuni ya 113 (1) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 (iliyorekebishwa mwaka 2016) ambayo inahitaji mikataba au makubaliano iliyokatishwa ipelekwe PPRA na AG kwa taarifa na/au hatua inayofaa.

Ninamshauri mtekelezaji wa mradi kufanya ufuatiliaji ili kiasi cha Sh. 344,320,647.56 kiweze kurejeshwa kutoka kwa Kampuni ya Tanchi Brothers Construction Co Ltd bila ucheleweshaji zaidi.

SURA YA KUMI NA MBILI

MASUALA MENGINE YA UTENDAJI WA MIRADI YALIYOBAINIKA WAKATI WA UKAGUZI WA FEDHA

12.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha mapungufu yanayohusiana na utendaji wa uhalisia yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa kifedha kwa mwaka wa fedha 2019/20. Inawasilisha miradi mingine mbali na matokeo ya ukaguzi wa kaguzi za kiufundi kumi na tatu zilizowasilishwa katika Sura ya tano hadi kumi na moja.

12.2 Muhtasari wa Matokeo ya Ukaguzi

Uchambuzi wangu unaonyesha kuwa changamoto kubwa zilizobainika wakati wa Ukaguzi zinazohusiana na kazi za ujenzi ni kuchelewesha kuanza kwa kazi za ujenzi, miradi ya ujenzi iliyotelekezwa, kutorekebishwa kwa mapungufu ya ujenzi pamoja na utekelezaji usioridhisha wa Programu ya Kusaidia Elimu ya Ufundi, Mafunzo na Elimu kwa Walimu (STVET-TE). Uchambuzi wa mapungufu haya umewasilishwa katika aya ifuatayo:

12.2.1 Miradi Miwili ya Maji Iliyotelekezwa yenye Kiasi cha Sh. Bilioni 2.71

Katika kutembelea eneo la mradi uliofanyika mwezi Novemba 2020 nilibaini kuwa, miradi miwili inayotekelezwa chini ya sekta ya maji yenye thamani ya Sh. 2,711,354,794 imetelekezwa licha ya ukweli kwamba kulikuwa na shughuli ambazo hazijatekelezwa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 12-1**.

Miradi iliyotelekezwa kama ilivyotajwa hapo juu ilitokana na kucheleweshwa kwa malipo kwa wakandarasi na eneo la mradi kutofikika kulikotokana na kunyesha kwa mvua kubwa. Kuwapo kwa miradi iliyotelekezwa kumesababisha kuchelewesha kukamilika kwa miradi na hivyo kuchelewesha kupatikana kwa faida zilzokusudiwa kwa jamii.

Jedwali 12- 1: Kazi ambazo hazijakamilika kutokana na miradi iliyotelekezwa

Na	Wahusika wa Mkataba	Mkataba No	Lengo	Kiasi(Sh)	Maelezo

1	Kashwasa na Kampuni Exact line Engineering (Group) Ltd	AE/063/2017-2018/W/2	Upanuzi wa Ujenzi wa Mabomba ya Kusambaza Maji kutoka Mpango wa Ugavi wa Maji ya Ziwa Victoria kwenda Vijiji vya Izuga, Mwakuzuka na Kabondo	1,383,691,128	Tarehe ya kukamilika ilirekebishwa hadi 23 Juni 2020, hata hivyo ziara ya eneo la mradi iliyofanyika mwaka Julai 14, 2020 ilibaini kuwa Mkandarasi aliutelekeza mradi tangu 23 Desemba 2019 wakati kuna shughuli zilikuwa hazijakamilika
2	Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Mwanza (MWAUWASA) na Kampuni Halem Construction CO.Limited	AE/042/2018-2019/W/43 LOT 2	Ujenzi wa Mifumo ya Ugavi wa Maji eneo la Nyampande	1,327,663,666	Mkataba ulianza tarehe 9 Juni 2019 na ulipangwa kukamilika tarehe 9 Juni 2020, hata hivyo ziara ya eneo la mradi ilibainisha kuwa, mradi huo ulikuwa bado haujakamilika na mkandarasi alitelekeza mradi kwa miezi miwili tangu Juni 2020 wakati kuna bora shughuli

Chanzo: *Kutembelea miradi, taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa miradi na nyaraka za mikataba*

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Maji kuhakikisha kuwa madai ya wakandarasi yanalipwa kwa wakati unaofaa ili kuwawezesha kumalizia utekelezaji shughuli za miradi na pia usimamizi wa wakandarasi uimarishwe ili kuhakikisha ubora wa kazi iliyofanywa na thamani ya Fedha inapatikana.

12.2.2 Kucheleweshwa Kuanza kwa Ujenzi - Kiasi cha Sh. Bilioni 1.47

Nimebaini kuwa kazi tatu za ujenzi zilizopangwa zenye thamani ya Sh.1,470,370,951 zinazotekelezwa chini ya Matokeo Makubwa Sasa katika Mradi wa Elimu ya Malipo kwa Matokeo (BRN EPforR) na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zilikuwa bado hazijaanza kutekelezwa licha ya kupatikana kwa fedha na kukamilisha taratibu za manunuzi. Kazi hizi zilikuwa ujenzi wa maabara ya Kemia na kupanua maabara ya biolojia iliyopo Chuo Kikuu cha Elimu cha Mkwawa (MUCE), ukarabati wa nyumba katika Ukumbi wa bwalo namba 2 na bwalo namba 5 huko Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (UDSM) na ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Msingi Madudu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kwa bei ya mkataba ya kiasi cha Sh. 912,816,346, Sh. 508,754,605 na Sh. 48,800,000, kwa mfuatano.

Hii ilitokana na usimamizi usioridhisha katika kutekeleza mradi wa ujenzi uliopangwa licha ya kuwapo kwa fedha zilizotengwa. Wakati kwa Chuo Kikuu cha Elimu cha Mkwawa (MUCE) kulikuwa na kutokubaliana juu ya matokeo ya vipimo vya malighafi kulingana na utaratibu uliofanywa na mshauri kuhusu ubora wa muundo wa zege na Uharibifu wa Mazingira unaosababishwa na shughuli za kibinadamu zilizoathiri utekelezaji wa shughuli za ujenzi katika Shule ya Msingi Madudu.

Ni maoni yangu kuwa, kucheleweshwa kuanza kwa kazi za ujenzi kunaweza kusababisha ongezeko la gharama kutokana na thamani ya fedha ya wakati sasa kupitia kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma kwenye soko.

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolojia kuhakikisha kuwa, masuala yanayosubiri kutatuliwa yanashughulikiwa na shughuli za ukarabati na ujenzi zinaanza pasipo kucheleweshwa zaidi. Kwa kuongezea, menejimenti iharakishe utekelezaji wa miradi kwa wakati uliopangwa.

12.2.3 Utekelezaji Usioridhisha wa Mradi wa STVET-TE

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilikuwa ikitekeleza Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi na Mafunzo ya Ualimu (STVET-TE)

kwa kipindi cha miaka mitano (3 Julai 2014 hadi 31 Desemba 2019). Hata hivyo, hali ya mradi wakati wa kufungwa haikuwa inaridhisha kwani kiasi cha Sh. 12,937,752,197.13 kilitolewa. Hii ni sawa na takriban asilimia kumi ya kiasi cha mkopo kilichokubaliwa cha Sh. 128,641,649,100.

Nilibaini zaidi kuwa, wakati wa utekelezaji wa mradi kwa miaka mitano, kulikuwa na jumla ya wakandarasi sita wenye kandarasi ya jumla ya kiasi cha Sh. 41,292,740,527.90 zinazohusika na ujenzi wa Vituo vya Ufundi vya Mikoa vitatu[29], upanuzi na uboreshaji wa Vyuo vya Ualimu vitatu[30] pamoja na ujenzi wa maabara na semina katika Chuo cha Ufundi cha Arusha. Wakandarasi walilipwa jumla ya kiasi cha Sh. 7,012,709,183.99 kufikia 31 Desemba 2019

Kwa kuongezea, nilibaini kuwa kati ya wakandarasi sita ambao walikuwa wakifanya kazi za ujenzi, wawili walisitishwa kwa sababu ya udanganyifu. Barua ya kusudio la kuvunja mikataba mingine miwili ilitolewa na Makao Makuu ya VETA. Ongezeko la muda halikuweza kufanyika kwa kandarasi moja; na ile iliyobaki, ujenzi bado unaendelea. Hata hivyo, kwa mikataba iliyovunjwa au ambayo ombi la kuvunjwa lilifanyika, kazi zimesimama tangu kufungwa kwa mradi na mipango ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kukamilisha shughuli za ujenzi kupitia miradi mingine kama Elimu na Ujuzi wa Ajira za Uzalishaji (ESPJ).

Hii ilisababishwa sana na kuchelewa kupata idhini kutoka AfDB, kucheleweshwa idhini ya taratibu za ununuzi katika viwango tofauti na kutofaulu kupata msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa bidhaa na huduma zilizonunuliwa chini ya mradi kama ilivyodhaniwa hapo awali.

Maoni yangu ni kuwa, malengo yaliyokusudiwa ya STEVET-TE hayakufikiwa; kwa hivyo, Serikali inaweza kulipa mkopo pamoja

[29] Geita, Njombe na Rukwa.
[30] Mpwapwa na Kleruu chini ya MoEST na Chuo cha Ufundi Morogoro chini ya VETA
Mikataba ya ujenzi ilisainiwa baina ya Mkao Makuu ya VETA na wakandarasi, isipokuwa mkataba wa Chuo cha Ufundi Arusha ambapo mkataba wake ulikuwa baina ya Mkandarasi na MoEST.

na riba kwa wafadhili bila kutoa faida kwa walengwa. Kwa upande mwingine, Serikali itaingia gharama ya kulipa tozo za ahadi (commitment charge) ambayo haina faida kama inavyotakiwa na kipengele Na. 3.03 cha makubaliano ya fedha kinachonasema kwamba, "Mkopaji atalipa malipo ya dhamana ya 0.5% kwa mwaka ya sehemu ambayo haijalipwa ya mkopo".

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Elimu,Sayansi na Tekinolojia kuhakikisha kuwa masuala yote yanayohusu utekelezaji wa miradi yanashughulikiwa kwa wakati ikiwemo kuidhinisha manunuzi katika ngazi tofauti za utekelezaji na kuomba msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa huduma na bidhaa zinazonunuliwa.

12.2.4 Kazi Ndogo Ndogo za Ujenzi Ambazo Hazikukamilika Wakati wa Makabidhiano Mradi

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Wizara ya Madini kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) ilikabidhi maeneo ya miradi ya Vituo vya Nishati kwa Bariadi, Musoma na Bukoba na kupitia SKY Architects kama matokeo ya kutokamilika kwa kazi za ujenzi za mkataba wenye kumbukumbu Na. ME/008/SMMRP/W/12 na SUMA JKT.

Katika kupitia zaidi muhtasari wa mabidhiano kwa miradi husika (tarehe 16 Juni 2019 kwa Bariadi na Musoma na 17 Septemba 2019 kwa Bukoba) nilibaini kuwa, katika makabidhiano ya eneo la mradi "kulikuwa na makabidhiano yasiyo kamili" wakati wakisubiria marekebisho madogomadogo ambayo yalikuwa hayajafanywa na mkandarasi kama vile kasoro kwenye uzio uliojengwa, umaliziaji usioridhisha wa “crushing shades”, usafi wa jumla na kutoa AC na kupaka rangi kuta katika ofisi nyingine. Ilikubaliwa katika kikao kwamba kasoro zote zifanyiwe kazi mpaka ifikapo tarehe 15 Oktoba 2019. Hata hivyo, hakuna kasoro zozote ambazo zimeshafanyiwa kazi na mkandarasi kwa majengo ya Bariadi na Musoma ingawa kwa jengo la Bukoba baadhi ya mapungufu yalifanyika.

Hii ilitokana na juhudi zisizojitosheleza za ufuatiliaji wa Wizara ya Madini juu ya urekebishaji wa kasoro ndogondogo kama ilivyokubaliwa katika kikao. Hii inaweza kusababisha uchakavu

wa majengo ambayo yanaweza kuwa na athari za gharama katika siku za usoni.

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Madini kuhakikisha kwamba mkandarasi anafanya marekebisho ya mapungufu ya kazi za ujenzi kabla ya kumalizika kwa kipindi cha matazamio pamoja na kulipa tozo ya ucheleweshaji wa kazi (liquidated damages).

12.2.5 Kutokuwa na Uhakika wa Kukamilika kwa Ujenzi wa Vituo Vitatu vya Ubora vilivyotelekezwa

Mapitio yangu yaligundua kuwa kufuatia kufungwa kwa fedha za mradi na Benki ya Dunia, Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) ilihamisha Dola za Marekani 1,250,809.32 sawa na kiasi cha Sh. 2,839,151,286.14 kwenda katika Akaunti ya Amana ya Madini ili kukidhi majukumu yanayotokana na mkataba Na.ME/008/SMMRP/W/13 na Na. ME/008/SMMRP/C/61 na SUMA JKT ya ujenzi wa kituo cha ubora huko Mpanda, Chunya na Songea ambayo ilikuwa ikiendelea hadi 30 Juni 2019.

Mapitio yangu zaidi yalibaini kuwa fedha zilizohamishwa zilitumika kwa shughuli nyingine za Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) na Dola za Marekani 54,376.84, sawa na kiasi cha Sh. 125,119,477.54 zilirudishwa kwa Benki ya Dunia licha ya ukweli kwamba, kulikuwa na kazi zilizotelekezwa. Pia, nilibaini kuwa, Wizara ilikuwa tayari imeshalipa jumla ya Sh. 1,661,012,747.06 ikiacha majukumu ambayo hayajalipwa kiasi cha Sh. 1,991,516,949.94 ambayo yatalipwa na Wizara wakati wa kupewa hati ya kukamilisha kazi.

Uhakiki uliofanyika zaidi katika maeneo ya mradi mnamo tarehe 12 Agosti 2020 na 14 Agosti 2020 huko Mpanda, Chunya na Songea ulibaini kuwa miradi hiyo ilitelekezwa tangu 2019; na hakukuwa na ushahidi wa kuanza tena kazi za ujenzi kwa siku za usoni.

Hii ilitokana na ucheleweshaji wa kuongeza muda wa mikataba kwa sababu ya kumalizika kwa mikataba hii wakati Wizara ya Madini ilikuwa haina uhakika juu ya upatikanaji wa fedha. Nina maoni kwamba, ujenzi uliotelekezwa unamaanisha kwamba

thamani ya fedha kwa mradi huo haikuweza kufikiwa vyema; hivyo, manufaa yaliyotarajiwa ya Vituo vya Ubora yatacheleweshwa au kutopatikana kabisa.

Ninashauri uongozi wa Wizara ya Madini kutoa maelezo na ushahidi juu ya jinsi majukumu yatalipwa kwa wakandarasi na washauri wanapostahili na ni chanzo gani cha fedha kitatumika. Kwa kuongezea, katika usimamizi wa baadaye wa Wizara ya Madini inahimizwa kuhakikisha uamuzi sahihi juu ya miradi iliyojitolea inafanywa vizuri na kuhakikisha ufadhili wa kutosha upo kabla ya kurudisha fedha kwa Mshirika wa Maendeleo.

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Madini kutoa maelezo yenye ushahidi dhidi ya jinsi madeni yatakavyolipwa kwa wakandarasi na washauri elekezi ikiwemo na vyanzo vya fedha vitakavyotumika kwa malipo hayo.Kwa kuongezea,katika siku zijazo menejimenti ya Wizara ya Madini ihakikishe inafanya maamuzi sahihi katika utekelezaji wa shughuli za miradi na kuhakikisha upatikanaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya miradi isiyokamilika zinabakizwa kabla ya kuzirudisha kwa Washirika wa Maendeleo.

SEHEMU YA NNE

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Sehemu ya nne inahusu sura mbili ambazo ni sura ya 13 na 14 zinazohusu hitimisho na mapendekezo, mtawalia.

Sura ya 13 inatoa hitimisho la matokeo yaliyowasilishwa katika sura zilizotangulia. Sura hii imegawanywa katika maeneo manne ambayo ni: hitimisho la jumla na hitimisho mahususi juu ya utendaji wa fedha, manunuzi, utendaji wa mradi, pamoja na matokeo ya utekelezaji ya kaguzi za kiufundi.

Sura ya 14 inatoa mapendekezo ambayo yanashughulikia kasoro kubwa zilizobainika katika uchambuzi uliofanywa kuhusu ripoti za ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/20. Mbali na mapendekezo yaliyotolewa katika suala lililowasilishwa katika kila sura, sura hii inahusu mapendekezo ambayo yameelekezwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu.

SURA YA KUMI NA TATU

HITIMISHO

13.1 Utangulizi

Sura hii inatoa hitimisho la matokeo ya ukaguzi yaliyowasilishwa katika sura zilizotangulia. Nimegawanya hitimisho langu katika maeneo manne ambayo ni: hitimisho la jumla na hitimisho maalum juu ya utendaji wa fedha, ununuzi na utendaji halisi wa miradi ya maendeleo na matokeo ya utekelezaji wa ukaguzi wa kiufundi.

13.2 Hitimisho la Jumla

Hitimisho langu linaonesha kuwa Serikali imefanya juhudi kubwa katika kuhakikisha miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Taasisi za Serikali ikishirikiana na Wadau wa Maendeleo (DPs) inafikia makisio ya mwaka wa fedha 2019/20 pamoja na kufanikisha malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Awamu ya Pili (FYDP II), 2016/17-2020/21 ambayo utekelezwaji wake unategemea kukamilika mwaka wa fedha 2020/21. Kwa kuzingatia hilo, nilibaini mipango ya Serikali katika kukuza sekta mbalimbali, hususani zile zinazoambatana na kusaidia katika kuwekeza kwenye miundombinu inayosaidia kubadilisha Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati kupitia viwanda na maendeleo ya watu kwa ujumla. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mikubwa, hasa katika sekta za nishati, maji na usafirishaji, ukiachilia mbali miradi mingine inayohusu elimu, kilimo, jamii na sekta mbalimbali.

Ninatambua mipango ya Serikali katika kushughulikia changamoto zilizojitokeza katika miradi ya maendeleo, hasa katika sekta ya maji, kwa kuanzisha Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) chini ya Wizara ya Maji ambayo ilizinduliwa Julai 2019. Ni matarajio yangu kwamba, Wakala utashughulikia changamoto ambazo Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa zinakabiliwa katika kushughulikia miradi ya maji katika mamlaka yao, kwani ina jukumu la kuhakikisha maendeleo na usimamizi endelevu wa miradi ya usambazaji maji na usafi wa mazingira vijijini. Pia, nimebaini juhudi zilizofanywa na Serikali

katika utekelezaji wa Waraka wa Hazina Namba 2 (sambamba na Fedha za Miradi) iliyotolewa tarehe 4 Septemba 2019 ikilenga kuboresha uwajibikaji na uwazi, hasa katika kushughulikia changamoto za bajeti ya fedha zilizopokelewa na Watekelezaji wa Miradi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia mikopo na misaada.

Kwa kuongezea, ninatambua juhudi zinazoendelea kufanywa na Watekelezaji wa Miradi katika kuandaa taarifa za kifedha ambazo zinaendana na viwango vya uandaaji wa hesabu na zinaonesha usahihi wa taarifa za kiutendaji wa kifedha za miradi ya maendeleo inayokaguliwa. Mafanikio haya huleta imani kati ya wadau, hasa washirika wa maendeleo na wananchi kwa ujumla.

Mbali na juhudi zilizochukuliwa na Serikali, uchambuzi wangu wa jumla pia unaonesha kujirudia kwa mapungufu yaliyobainika katika taarifa zangu zilizopita kulingana na usimamizi wa Miradi ya Maendeleo nchini. Changamoto kuu zilizobainika zinatokana na: udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa kifedha, manunuzi, na utendaji halisi wa miradi ya maendeleo. Nimebaini pia mapungufu mbalimbali kupitia taarifa za kiufundi zinazohusiana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya ujenzi, uchukuzi, maji, nishati na kilimo na changamoto kubwa zilitokea katika usimamizi wa mikataba. Ni matumaini yangu kwamba, taarifa hii itatumika kama kielelezo cha kuendeleza na kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) - 2021/22-2025/26.

13.3 Hitimisho Mahsusi

13.3.1 Utendaji wa Kifedha

Hitimisho langu katika usimamizi wa kifedha linahusu hati za ukaguzi zilizotolewa, utekelezaji wa mapendekezo yangu ya miaka iliyopita pamoja na masuala yanayohusiana na usimamizi wa fedha.

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa, zaidi ya asilimia 90 ya miradi ilipata hati za ukaguzi zinazoridhisha kwa miaka mitano mfululizo kutoka mwaka 2015/16 hadi 2019/20. Ni maoni yangu kuwa, mwenendo huu utazidi kuboresha mchakato wa kufanya uamuzi kati ya watumiaji wa taarifa za kifedha na kuweka uaminifu kwa

Watekelezaji wa Miradi mbele ya Wadau kwamba fedha walizokabidhiwa kwa ajili ya miradi zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.
Nina Mashaka na utekelezaji wa mapendekezo ya miaka ya awali, kwani kiwango cha utekelezaji bado kipo chini kwa asilimia 50 kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2019/20. Ni maoni yangu kwamba, Maafisa Masuuli wanapaswa kuweka mikakati yenye ufumbuzi katika eneo hili, kwani kumekuwa na kujirudia kwa hoja hususani zile zinazohusiana na usimamizi wa matumizi ya fedha na ukiukaji wa matakwa ya makubaliano ya miradi.

Kwa muktadha huu, eneo la usimamizi wa miradi linatakiwa lipewe kipaumbele na Maafisa Masuuli, kwani ni muhimu katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo unakuwa na matokeo yenye tija na endelevu nchini. Kwa mfano, nimebaini kuwa kuna hatari kwa Serikali kulipa tozo ya riba inayofikia Sh. 8,178,283,863.58 kutokana na kuchelewa kulipwa kwa madai ya wakandarasi, kinyume na makubaliano ya mkataba; hivyo kuhatarisha kukamilika kwa shughuli zilizopangwa za miradi hii. Kwa kuongezea, nilibaini jumla ya Sh. 1,360,377,044 zilizokopwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia akaunti za Programu ya Elimu na Ujuzi kwa Ajili ya Kazi za Uzalishaji (ESPJ) hazikurejeshwa kwenye miradi, hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa ajili ya mradi huo.

13.3.2 Usimamizi wa Manunuzi na Utawala

Kwa maoni yangu, kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa chini ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016), kulikuwa na uthibitisho kwamba Watekelezaji wa Mradi kwa ujumla walizingatia matakwa ya Sheria ya manunuzi na kanuni zake katika kutekeleza shughuli za mradi katika mwaka wa fedha 2019/20, isipokuwa mapungufu machache yaliyoonyeshwa katika ukaguzi wangu.

Miongoni mwa mapungufu yanayobainika kila mara katika ukaguzi wangu yanayohusiana na manunuzi ni pamoja na manunuzi ya bidhaa na huduma bila zabuni ya ushindani, manunuzi ya bidhaa na huduma bila idhini ya Bodi ya Zabuni, pamoja na manunuzi yaliyo kwenye mpango wa manunuzi lakini hayakutekelezwa. Kwa mfano, nilibaini

shughuli za manunuzi wa Mradi wa Maendeleo ya Jiji Kuu la Dar es Salaam (DMDP) zenye thamani ya Sh. 16,088,893,656.40 hazikujumuishwa katika Mpango wa Manunuzi wa Mwaka.

Uchambuzi wangu unahitimisha kwamba mapungufu yanayohusiana na kutofuata Sheria na Manunuzi ya Kanuni kwenye utekelezaji wa shughuli za miradi yalichangiwa zaidi na utaratibu usioridhisha unaotumiwa na Bodi za Zabuni za Taasisi husika katika kufuatilia shughuli za Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi. Kitengo hiki ni muhimu sana katika kuhakikisha shughuli za manunuzi zinazohusiana na miradi ya maendeleo zinafuata matakwa ya Sheria ya Manunuzi na Kanuni zake. Pia, husaidia kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya manunuzi kwa Bodi ya Zabuni na Maafisa Masuuli. Zaidi, huongoza ipasavyo idara za watumiaji katika mchakato wa kuanzisha mahitaji yao.

Ni maoni yangu kwamba, kutozingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi, hasa juu ya misingi muhimu ya manunuzi ya umma ambayo inazuia uwazi na uwajibikaji, sio tu huleta hatari ya kutopata thamani ya fedha kutokana na manunuzi lakini pia hupunguza uwezo wa Serikali kupata bidhaa na huduma kwa haki kutoka kwa wazabuni na wadau wengine.

13.3.3 Usimamizi wa Mkataba na Utendaji Halisi wa Miradi

Nimelinganisha utekelezaji wa miradi na usimamizi wa mikataba kwa kuwa ni shughuli muhimu katika usimamizi wa miradi, hasa ile inayohusiana na ujenzi. Niligundua mapungufu katika usimamizi wa mikataba kwa wakandarasi na watekelezaji wa miradi ya maendeleo inayohusiana na sekta za nishati, maji, uchukuzi na kilimo. Pia nilibaini mapungufu mengine yanayohusiana na usimamizi wa mkataba wa bidhaa na huduma.

Uchambuzi wangu kuhusu manunuzi ya ujenzi, bidhaa na huduma katika mwaka wa fedha 2019/20 ulibaini masuala yanayojirudia kila mara katika eneo hili. Masuala hayo yanahusu bidhaa kupokelewa pasipo kuthibitishwa na Kamati ya Ukaguzi na mapokezi ya bidhaa na malipo kufanywa kwa Wazabuni kwa bidhaa na huduma ambazo hazijapokelewa.

Kwa upande mwingine, mapungufu ya kawaida katika kusimamia mikataba ya ujenzi ni pamoja na vidhibiti vinavyohusiana na uthibitishaji wa hati za Wakandarasi kama dhamana halali za utendaji, dhamana ya malipo ya mapema na kutokuwapo kwa idhini ya kuongeza muda wa kukamilisha mkataba. Masuala haya yalitokana na utaratibu usiofaa wa ufuatiliaji wa nyaraka za mkataba kwa watendaji wanaohusika. Nilibaini kuwa Watekelezaji wa miradi wengi husimamia miradi ya ujenzi bila mpangilio maalum. Hii huleta changamoto katika kufuatilia miradi ya ujenzi, hususani maswala ya kiutawala kama dhamana kumalizika muda wake kabla ya mradi husika kumalizika, ongezeko la muda wa kukamilisha miradi ya maendeleo, malipo ya wakandarasi na yanayohusiana na hayo. Kwa maoni yangu, ni jambo la muhimu kwa Watekelezaji wa Miradi kutumia njia za kielekroniki katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

Mbali na masuala ya kawaida, pia kulikuwa na masuala maalum ambayo yalitokea katika kusimamia utekelezaji wa miradi inayoweza kuhusishwa na utaratibu usio wa makini wa kusimamia mikataba. Kwa mfano, kiasi cha fedha Sh. 704,155,443.20 kililipwa mara mbili kwa mkandarasi SUMA JKT kutoka fedha za Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP). Vivyo hivyo, kulikuwa na malipo yaliyozidishwa kwa ajili ya malipo ya awali Sh. 492,135,303.14 na Sh. 2,566,436,434.80 yalilipwa bila kuwasilisha dhamana ya malipo ya mapema iliyofanywa na watekelezaji wa miradi mbalimbali.

Kuhusiana na utekelezaji halisi wa miradi, nina wasiwasi na utendaji usioridhisha wa mradi wa programu ya kusaidia elimu ya ufundi, mafunzo na elimu kwa walimu (STVET-TE) uliotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ilikuwa na kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji uliomalizika 31 Desemba 2019 lakini ni asilimia 10 tu ya kiwango cha mkopo kilichokubaliwa na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) kilitolewa kwa wakati wote wa utekelezaji wa mradi. Kuhusiana na hili, malengo yaliyokusudiwa ya mradi hayakufikiwa kama inavyotarajiwa, wakati Serikali inapaswa kulipa sehemu ya mkopo uliopokelewa pamoja na tozo ya hiyari kwa Benki ya Maendeleo Africa (AfDB).

Pia, nilibaini miradi miwili ya maji iliyotelekezwa yenye jumla ya Sh. 2,711,354,794 kutokana na kucheleweshwa kwa malipo kwa wakandarasi na kutofikiwa kwa eneo la mradi kutokana na mvua kubwa.

Kwa kuongezea, kufuatia kumalizika kwa muda wa ufadhili wa mradi kutoka kwa Benki ya Dunia kwa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP), nilibaini kutokuwapo kwa uhakika wa kukamilika kwa ujenzi wa vituo vitatu vya ubora huko Mpanda, Chunya na Songea uliokuwa unatekelezwa na Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) uliotekelezwa na Wizara ya Madini. Kuhusiana na suala hili, kuwapo kwa miradi iliyotelekezwa kumesababisha kuchelewa kufikia malengo yaliyopangwa; hivyo kuchelewesha kupeleka faida inayotarajiwa kwa jamii.

13.3.4 Hitimisho Mahsusi juu ya Matokeo ya Ukaguzi wa Kiufundi

Hitimisho maalum la kaguzi sita za kiufundi linawasilishwa kama ifuatavyo:

- **Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR)**

Shirika la Reli Tanzania limeonesha juhudi katika utekelezaji wa ujenzi wa Reli ya Kisasa katika awamu ya kwanza na ya pili. Kwa ujumla, kazi za ujenzi ambazo ni pamoja na ujenzi wa kalavati, njia za kupita chini, vivuko vya juu, madaraja, madaraja maalum, kingo za kuzuia mmomonyoko wa barabara , matabaka ya lami, sehemu za kushushia mzigo, pamoja na uwekaji wa majengo ya vituo yalizingatia vipimo vilivyohitajika.

Hata hivyo, maendeleo ya kazi hayapelekei kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hii ni kwa sababu, ukubwa wa kazi ya ujenzi wa awamu ya kwanza (Dar es Salaam hadi Morogoro) umeongezwa mara nne zaidi ya awali; na kuna uwezekano mdogo kuwa awamu hii itamalizika Aprili 2021. Kulingana na ukomo wa nyongeza ya muda, hali inatia shaka kwani hadi kufikia Desemba 2020 hali ya utekelezaji ilikuwa imefikia asilimia 88.39 dhidi ya asilimia 95.96 iliyopangwa kutekelezwa hadi kufikia Desemba 2020.

Vivyo hivyo, hali ni mbaya kwa awamu ya pili ya ujenzi (Morogoro hadi Makutopora) kwa sababu mpaka kufikia Desemba 2020 hali

halisi ilikuwa 52.2% dhidi ya matarajio ya 98.7% yaliyopangwa tangu mradi huo kuanza. Mradi ulitarajiwa kukamilika ifikapo Februari 2021. Hii ilisababishwa na ucheleweshaji wa maandalizi ya mwanzo ya ujenzi, ucheleweshaji wa ujenzi wa mwanzo, uchelewaji wa manunuzi ya ardhi pamoja na kucheleweshwa kuanza kwa usanifu na ujenzi wa kiungo cha bandari (port link) chenye urefu wa kilomita tatu.

- **Utekelezaji wa Mradi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere**

Ninahitimisha kuwa kwa kadiri maendeleo yanayohusiana na utekelezaji wa mradi huu, Shirika la umeme Tanzania linafanya maendeleo mazuri katika kusimamia ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere kwa kuzingatia muda, gharama na ubora ili kuhakikisha kufikiwa kwa malengo ya mradi. Hata hivyo, TANESCO inahitaji kuweka juhudi zaidi kuhakikisha kunakuwa na uzingatiaji wa matakwa ya mkataba yanayohusiana na ushiriki wa wafanyakazi kwenye mradi, udhibiti wa ubora na mazingira, kijamii, usalama wa kazini na masuala ya afya wakati wa utekelezaji wa mradi.

- **Mradi wa Miundombinu ya Usafiri wa Mabasi ya Yaendayo Haraka (BRT)**

Ripoti hiyo inahitimisha kuwa, thamani ya fedha kwenye utekelezaji wa mradi huu haikufikiwa. Hii ni kwa sababu, utekelezaji wa awamu zote mbili (awamu ya kwanza – kazi za barabara na awamu ya pili - kazi za ujenzi) haukuridhisha katika vipengele vya utekelezaji wa mradi kwa wakati, gharama na ubora kulingana na sheria na masharti ya mkataba. Sababu kuu ni usimamizi usioridhisha wa mwajiri na kuchelewesha kuchukua hatua za haraka kwenye mapungufu.

- **Mradi wa Upanuzi wa Barabara ya Morogoro**

Thamani ya fedha kwa utekelezaji wa mradi huo inaweza ikapatikana kwa sababu mradi unatarajiwa kukamilika kwa wakati unaokubalika, gharama inayokubalika na kwa kufuata maagizo na Mahitaji ya Mwajiri. Hata hivyo, maboresho makubwa yanahitajika kwa wakati wa malipo ya Mkandarasi, kufuatana na taratibu za Afya, Usalama na Mazingira, na idhini sahihi ya matokeo ya mradi.

Kwa kuongezea, Serikali inaweza ishindwe kutatua shida ya msongamano wa magari na ucheleweshaji magari kupita katika

barabara ya Morogoro. Hii inatokana na ukosefu wa juhudi za pamoja na ukosefu wa ujumuishaji na mipango mikuu ya Taasisi ndani ya Serikali. Hii ni kwa sababu kuanzishwa kwa kituo cha kisasa cha Mabasi huko Mbezi-Mwisho na mamlaka ya Manispaa jijini Dar es Salaam, ambayo inakadiriwa kuhudumia mabasi 700, kunatarajiwa kusababisha msongamano zaidi wa magari na kusababisha usumbufu zaidi kwenye makutano yanayoingia barabara ya Morogoro.

- **Hitimisho la Ukaguzi wa Jumla juu ya Utekelezaji wa Mradi wa Uzalishaji Sukari wa Mbigiri**

Kwa jumla, kulingana na hoja za ukaguzi zilizowasilishwa katika sura ya tatu ya ripoti hii, ukaguzi wangu unahitimisha kuwa Kampuni Hodhi ya Mkulazi (MHCL) imeonesha juhudi wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Uzalishaji wa Sukari wa Mbigiri. Hata hivyo, uboreshaji unahitajika ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi unafikia lengo lililokusudiwa. Hii ni kwa sababu Kampuni Hodhi ya Mkulazi haikutii viwango vya kutosha vinavyoathiri utekelezaji wa Mradi wa Uzalishaji Sukari wa Mbigiri. Pia, kutokana na kucheleweshwa kwa ufungaji wa mitambo ya kiwanda, Kampuni Hodhi ya Mkulazi na wakulima wa nje walipata hasara.

Kwa maana hiyo, Kampuni Hodhi ya Mkulazi haikusimamia ipasavyo shughuli za shamba, kwani kulikuwa na udhibiti dhaifu juu ya mafuta, mbolea na matumizi ya dawa za kuulia wadudu ambayo husababisha matumizi mabaya ya vitu vilivyotajwa. Pia, utaratibu usiofaa wa kudhibiti gharama kwa shughuli za shamba ulibainika. Matokeo yake, kampuni ilishindwa kuweka gharama halisi za uzalishaji wa miwa.

Mchakato wa zabuni na manunuzi haukusimamiwa vya kutosha na Kampuni Hodhi ya Mkulazi (MHCL), ikimaanisha kuwa, kuna manunuzi yaliyofanywa zaidi ya bajeti na kusababisha hasara kwa sababu ya maamuzi mabaya yaliyofanywa. Pia, kuna ucheleweshaji wa zabuni na ununuzi ambao ulisababisha Kampuni kutotimiza malengo yake ipasavyo. Kwa kuongezea, kutokujenga jengo la kiwanda kwa wakati na kusimika mitambo ya uzalishaji ulisababisha hasara kwa kampuni na wakulima wa nje.

Kushindwa kwa Kampuni kutekeleza vya kutosha shughuli za kilimo, ununuzi na udhibiti wa kifedha, kumepunguza uhakikisho wa kufikia lengo la mradi uliokusudiwa wa kuzalisha tani 250,000 za sukari kwa mwaka.

SURA YA KUMI NA NNE

MAPENDEKEZO

14.1 Utangulizi

Sura hii inatoa mapendekezo ya jinsi ya kushughulikia kasoro zinazojitokeza katika taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Sehemu hii inatoa mapendekezo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kulingana na hitimisho na nini kinachopaswa kufanyika ili kuzipatia ufumbuzi kasoro zilizobainika na kuboresha ufanisi katika utekelezaji wa miradi nchini.

Kwa hiyo, mapendekezo ya jumla yametolewa ili kushughulikia kasoro zote mtambuka zinazoathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali na mapendekezo maalumu yametolewa ili kushughulikia mapungufu katika utekelezaji wa miradi ambayo yamejitokeza kwenye sekta husika.

14.2 Mapendekezo ya Jumla

Ofisi ya Waziri Mkuu inashauriwa kuhakikisha kuwa Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara, Idara, na Wakala wa Serikali zinazotekeleza miradi zinazingatia yafuatayo:

1. Kuanzisha Ofisi ya Uratibu wa Miradi ya Maendeleo Serikalini ambayo itasaidia taasisi zinazotekeleza miradi na kutathmini utekelezaji wa miradi hii katika sekta zote nchini.
2. Kuanzisha viashiria muhimu vitakavyotumika kupima utendaji katika kutekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo muhimu, ikiwemo eneo la usimamizi wa fedha na kuchukua hatua kwa watekeleza wa miradi ambao wameshindwa kufikia malengo ya utendaji yaliyowekwa.
3. Kutengeneza mfumo wa kielektroniki ambao utasaidia watekeleza miradi kuongeza ufanisi kwenye usimamizi na uendeshaji wa miradi ya ujenzi.
4. Kutengeneza na kusimamia mpango kazi maalumu utakaosaidia kushughulikia mapungufu niliyoyabaini kwenye utekelezaji wa miradi sita mikubwa ya kimkakati ambayo ni: Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), Mradi wa Bwawa la Nguvu za

Umeme la Mwalimu Nyerere, Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, Mradi wa Upanuzi wa Barabara ya Morogoro, Mradi wa Maji wa Same-Mwanga, na Mradi wa Uzalishaji Sukari Mbigiri.

14.3 Mapendekezo Mahsusi

Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na menejimenti za Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazotekeleza miradi kuhakikisha kwamba:

1. Wizara ya Fedha na Mipango iupitie na kuuboresha mpango wake na utaratibu wa kupeleka fedha kwa watekeleza miradi kama unavyooneshwa kwenye Waraka wa Hazina Na. 2 uliotolewa tarehe 2 Septemba 2019. Hii itasaidia kuboresha upelekeji wa fedha kwa wakati kwenda kwa watekeleza miradi na kuendana na bajeti.
2. Maofisa Masuuli kuhakikisha wanaongezea nguvu mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye malipo, utunzaji wa nyaraka za fedha, marejesho ya masurufu na makato ya kodi ya zuio.
3. Wizara ya Madini kutafuta chanzo cha uhakika cha ufadhili wa kifedha kutoka Benki ya Dunia na Serikali kwa ajili ya kulipa madeni ya wakandarasi wanaotekeleza mradi wa SMMRP II. Hii itasaidia kupunguza uwezekano wa migogoro ya madai kwa siku za baadaye.
4. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ifanye upembuzi ili kubaini sababu zilizochangia utendaji usioridhisha wa mradi wa STEVET na kuchukua hatua stahiki.

Kiambatisho 3- 1: Watekelezaji wa Miradi Wenye Hati Zisizoridhisha - Mfuko wa Afya

Na	Halmashauri	Msingi wa kutoa hati Isiyoridhisha
1	Halmashauri ya Monduli	**Matumizi ambayo hayana viambatisho yaliyotumika kwa shughuli za HBF kiasi cha Sh. milioni 5.53** Halmashauri ilishindwa kuleta maelezo ya malipo pamoja na viambatisho vya matumizi ya kiasi cha Sh. 5,531,070 zilizotumika kwa shughuli za Mfuko wa Uchangiaji wa Afya (HBF) katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, kinyume na Kifungu cha 104 (1) na (2) cha Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya 2009; na hivyo, kupunguza mawanda ya ukaguzi wangu unaohusiana na bakaa za fedha zilizohamishiwa mwaka wa kutoka mwaka wa fedha 2018/19 ambayo ilihamishiwa kwa Akaunti ya Maendeleo ya Halmashauri mwishoni mwa mwaka.
2	Halmashauri ya Mji wa Mafinga	**Nyaraka zisizojitosheleza juu ya malipo ya jumla ya kiasi cha Sh. Milioni 26.19** Mapitio ya shughuli za Halmashauri yalibainisha kuwa malipo ya jumla ya kiasi cha Sh. 26,190,600 yanayohusiana na HBF hayakuwa yamewekewa viambatisho vinavyotakiwa. Hii inamaanisha kuwa kuna mfumo duni wa udhibiti wa ndani juu ya utunzaji na uwekaji wa nyaraka ndani ya Halmashauri, kinyume na aya ya 6.7.2 ya LAAM 2019
3	Halmashauri ya Missenyi	Nilibaini kuwa Halmashauri ililipa kiasi cha Sh. 13,645,441 kwa kwa ajili ya wadai wa mwaka jana ambao hawakuwekwa katika taarifa za fedha za 2018/19. Kwa maana hii, matumizi ya mwaka huu yenye kiasi cha Sh. 13,645,441 yamezidishwa yakilinganishwa na malipo ya mwaka uliotangulia (ambayo yamepunguzwa kwa kiwango sawa na hicho).
4	Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe	Nilibaini kuwa, Menejimenti ya Halmashauri iliwasilisha taarifa za Fedha za HBF bila kujumuisha usuluhishi wa faida/hasara kilichotokana na shughuli za kawaida na mtiririko wa fedha kutoka kwa shughuli za uendeshaji zinazofikia kiasi cha Sh. 9,504,000 kama sehemu ya taarifa ya mtiririko wa fedha au kwenye taarifa za kifedha kulingana na mahitaji ya Aya ya 29 ya Viwango vya Kimataifa vya uandaaji Hesabu katika Sekta nambari 2 (IPSAS) na Aya ya 3.6 ya Muongozo Namba. 6 ya Mei, 2020 iliyotolewa na Mhasibu Mkuu.

Na	Halmashauri	Msingi wa kutoa hati Isiyoridhisha
5	Halmashauri ya Wilaya ya Itigi	**Faida iliyolimbikizwa kuonyeshwa kwa kiasi kikubwa zaidi ya kinachotakiwa kwa thamani ya Sh. Milioni 53.36** Katika mwaka 2019/20 Halmashauri ilibadilisha salio anzia la misaada ya kawaida kwa mwaka 2018/19 ili kurekebisha makosa ya kipindi cha kilichopita. Hata hivyo, marekebisho yaliyofanyika kuhusu ziada iliyokusanywa yalirekodiwa vibaya. Halmashauri ilifanya marekebisho kwa kupunguza salio la faida iliyolimbikizwa badala ya kuongeza salio kwa faida iliyolimbikizwa. Katika mantinki hii, salio la faida iliyolimbikizwa iliyoripotiwa katika taarifa ya hali ya kifedha na taarifa ya mabadiliko ya mali halisi imepunguzwa kwa kiasi cha Sh. 53,362,000.
6	Halmashauri ya Wilaya ya Urambo	**(i) Malipo Yenye Viambatisho Hafifu Sh. Milioni 17.20** Ukaguzi wangu umebaini malipo kiasi cha Sh. 17,204,504 yamelipwa, ilhali yakiwa na viambatisho hafifu, kinyume na Agizo No. 8(2)(c) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009. **(ii) Kukosekana kwa Hati za Malipo Sh. Milioni 6.53** Nimebaini malipo ya kiasi cha Sh. 6,530,996 ambayo yameripotiwa kwenye taarifa ya hesabu hayakuwa na hati za malipo; hivyo nimeshindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Aidha, kukosekana kwa hati za malipo ni kinyume na Agizo No. 8(2)(c) na 104(2) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.
7	Halmashauri ya Wilaya ya Nzega	**(i) Malipo Yenye Viambatisho Hafifu Sh. Milioni 35.99** Ukaguzi wangu umebaini malipo kiasi cha Sh. 35,994,000 yamelipwa, ilhali yakiwa na viambatisho hafifu, kinyume na Agizo No. 8(2)(c) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009. **(ii) Mali Zisizohamishika Zimeripotiwa Zikiwa na Thamani Hasi Sh. milioni 5.05** Nimebaini mali zisizohamishika kiasi cha Sh. 5,055,000 ambazo zimeripotiwa kwenye kwenye hesabu zikiwa na thamani. Hii ni kinyume na kifungu cha 67 na 77 cha taratibu za Viwango vya Hesabu vya Kimataifa katika Sekta ya Umma. **(iii) Madeni ya Muda mrefu yasiyolipwa Sh. Milioni 68.5** Aya ya 3.2.1 (c) ya waraka ya Uhasibu Na.6 wa mwaka 2019/20 juu ya uandaaji wa taarifa za kifedha kwa

Na	Halmashauri	Msingi wa kutoa hati Isiyoridhisha
		mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2020 inawataka Maafisa Masuuli kuepuka kulimbikiza madeni kwa muda mrefu. Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ililiripoti madeni yenye thamani ya Sh. 67,642,494 ambayo yalikuwa hayajalipwa tangu tarehe 20 Agosti 2013 hadi 18 Aprili 2015. Pia, iliripoti madai ya wafanyakazi jumla ya Sh. 860,000 ambayo yalikuwa hayajalipwa tangu tarehe 30 Juni 2017. Hali hii inaleta mashaka ya kulipikia kwa madeni haya.
8	Halmashauri ya Wilaya ya Bunda	**Kukosekana kwa Hati za Malipo Sh. 30.88 Milioni** Nimebaini malipo ya kiasi cha Sh. 30,884,701 ambayo yameripotiwa kwenye taarifa ya hesabu hayakuwa na hati za malipo. Hivyo, nimeshindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Aidha, kukosekana kwa hati za malipo ni kinyume na Agizo Na. 8(2)(c) na 104(2) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.
9	Halmashauri ya Wilaya ya Butiama	**(i) Kutofautiana kwa taarifa za fedha kwenye kitabu cha ulinganifu wa fedha kwa Sh. milioni 61.84** Uhakiki wa kitabu cha ulinganifu wa fedha (trial balance) ulibaini kutokukubaliana kwa Sh. 61,845,679 kati ya upande wa upokeaji na upande wa utoaji. Hii ni kwa sababu, salio lililoripotiwa kwa upande wa upokeaji ni Sh. 596,731,650 wakati upande wa utoaji ni Sh. 658,577,329. **(ii)Mabadiliko ya takwimu za mwaka wa nyuma pasipo kuwa na maelezo Sh. Milioni 99.13** Uhakiki wa taarifa ya kifedha kwa kulinganisha takwimu za mwaka wa nyuma umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Butiama ilirekebisha baadhi ya takwimu za mwaka wa nyuma pasipo kutolea maelezo, kinyume na Aya 54 ya Viwango vya kimataifa vya uhasibu kwa sekta ya umma na matakwa ya Mwongozo wa kihasibu namba 2 ya 2018/19 juu ya mtaji unaotokana na fedha za walipakodi (Taxpayers fund) na utambuzi wa mapato yanayotokana na matumizi ya ununuzi wa mali za kudumu. **(iii) Kutofanyika kwa usuluhishi wa fedha za mapato na matumizi ya shughuli za kila siku** Aya 3.6 ya Waraka wa kihasibu Namba 6 ya tarehe 08 Juni 2020 inazitaka Taasisi zinazotoa taarifa za kifedha

Na	Halmashauri	Msingi wa kutoa hati Isiyoridhisha
		kuandaa usuluhishi wa faida/hasara inayotokana na shughuli za kila siku za Taasisi. Zaidi ya hayo, viwango vya kimataifa vya uhasibu kwa sekta ya umma vinatoa machaguo; ambapo, usuluhishi huo unaweza ukaripotiwa kama sehemu ya taarifa ya mtiririko wa fedha (cash flow statement) au ukaripotiwa kwenye maelezo ya ziada za taarifa za kifedha. Kinyume na matakwa ya aya hapo, nimebaini kuwa usuluhisho wa taarifa ya mtiririko wa fedha zinazotokana na shughuli za kila siku haukufanywa.
10	Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu	**(i) Hati za malipo zilizokosekana wakati wa Ukaguzi Sh. Milioni 14.32** Mapitio ya taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/20 na kitabu cha fedha cha mradi yalibaini kuwa, Halmashauri ililipa jumla ya Sh. 744,145,417 chini ya idara ya afya. Hata hivyo, malipo ya Sh. 14,320,000 hayakuweza kuthibitishwa kutokana na kukosekana kwa hati za malipo. Kwa hivyo, sikuweza kubaini usahihi na uhalisi wa malipo hayo kwa shughuli ambazo zilifanywa. **(ii) Malipo yaliyofanywa bila kuwa na Viambatisho Sh. Milioni 40.80** Ukaguzi wa matumizi kwa mapitio ya hati za malipo na viambatisho vyake umebaini kuwa, hati za malipo zilizolipwa chini ya mfuko wa afya wa pamoja (HBF) zenye thamani ya Sh. 40,802,290 zilikuwa na viambatisho pungufu. Upungufu huo ulibainika katika vipengele vya: orodha ya malipo iliyosainiwa, ripoti za ukaguzi wa Wakala wa ufundi na umeme Tanzania (TEMESA), leja za vifaa vya store, idhini ya malipo ya muda baada ya masaa ya kazi, risiti za kukiri mapokezi, na risiti za kielektoniki (EFD). **(iii) Matumizi ya mafuta yasiyothibitishwa Sh. Milioni 28.72** Ukaguzi wangu ulishindwa kuthibitisha matumizi ya mafuta yenye thamani ya Sh. 28,717,039 yaliyonunuliwa katika mwaka wa fedha 2019/20. Hii ilitokana na kukosekana kwa hati za mapokezi ya mafuta kwenye hati za malipo husika kwa ajili ya kurahisisha utambuzi wa namba ya leja ya stoo iliyotumika kurekodia mafuta na hata kusaidia kufuatilia mgawanyo wa mafuta kwenye magari husika ya Halmashauri. Kwa nyongeza, hakukuwa na hati za mapokezi ya mafuta, leja ya vifyaa vya stoo,

Na	Halmashauri	Msingi wa kutoa hati Isiyoridhisha
		hati za kutoa mafuta stoo, kitabu cha kurekodi matumizi ya mafuta kwa kila gari, vibali na karatasi za matumizi ya mafuta.
11	Halmashauri ya Wilaya ya Magu	**(i)** Kuripotiwa kwa ruzuku ya kawaida pungufu kwa Sh. 98,638,312 **(ii)** Kuripotiwa kwa takwimu ya vifaa vinavyotumika pungufu kwa Sh. 68,661,974
12	Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga	**(i) Kuripotiwa thamani pungufu ya bidhaa za matumizi ya kawaida kwenye hesabu za mwisho Sh. milioni 11.88** Taarifa linganishi za taarifa za kifedha na Taarifa ya Mapato na Matumizi ziliripoti matumizi ya kawaida yenye thamani ya Sh. 401,042,485 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2020, badala ya Sh. 412,919,954 iliyohakikiwa na Ukaguzi, hivyo kupelekea kuripotiwa thamani pungufu kwa Sh. 11,877,469. **(ii) Malipo yaliyofanywa bila kuwa na Viambatisho Sh. Milioni 9.23** Ukaguzi wangu kwenye hati za malipo umebaini kuwa, hati zilizolipwa chini ya mfuko wa afya wa pamoja (HBF) zenye thamani ya Sh. 9,230,000 zilikuwa na viambatisho pungufu kama vile orodha ya malipo iliyosainiwa, sajili za mahudhurio ya vikao, na dakika za mikutano, kinyume na agizo la ununuzi wa ndani (LPO). Hii imezuia Ukaguzi wangu katika kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanywa. **(iii) Matumizi ya mafuta yasiyothibitishwa Sh. Milioni 5.78** Ukaguzi wangu wa leja za mafuta, hati za mapokezi ya vifaa, hati za kutolea vifaa na nyaraka zingine umebaini kuwa, katika mwaka huu wa Ukaguzi Idara ya Afya ilinunua lita 2,817 za mafuta yenye thamani ya Sh. 5,784,741 ambayo yaligawanywa kwenye magari. Hata hivyo, sikuweza kuthibitisha kuthibitisha matumizi yake kwa sababu Halmashauri haikutunza vitabu vya kumbukumbu za utumiaji wa mafuta ya magari (log books).
13	Halmahsuri ya Wilaya ya Kakonko	**Kuripotiwa kiasi kidogo cha matumizi ya Ruzuku ya kawaida kwa Shs. Milioni 5.88** Kinyume na matakwa ya aya ya 44 na 45 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma(IPSAS) 23, Halmashauri iliahirisha matumizi ya ruzuku ya kawaida ya Sh. 2,019,000 (iliyoripotiwa katika muhtasari Na. 1)

Na	Halmashauri	Msingi wa kutoa hati Isiyoridhisha
		badala ya Sh. 7,895,000 (iliyoripotiwa katika muhtasari Na. 6), kiasi ambacho hakijatumika katika mwaka husika **Ruzuku iliyoahirishwa iliripotiwa pungufu kwa kiasi cha Sh. 5,876,000** Halmashauri ilipaswa kuahirisha kiwango ambacho hakikutumika katika mwaka husika kwa sababu masharti ya kutumia yalikuwa bado hayatimizwa. Kwa hiyo, ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyoahirishwa imeripotiwa pungufu kwa Sh. 5,876,900.
14	Halmashauri ya Wilaya ya Longido	**(i) Malipo yaliyofanyika bila ya kuwa na nyaraka zinazojitosheleza Sh. Milioni 47.31** Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilibaini matumizi ya Sh. 47,317,534.90 ambayo yalifanyika bila ya kuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Agizo la 8 (2) (c) la Randama ya fedha ya Serikali za Mitaa, 2009. Uthibitisho wa malipo hayo haukuweza kupatikana. **(ii) Malipo ya posho kufanyika zaidi Sh. Milioni 1.20** Katika kupitia vocha za malipo pamoja na nyaraka zinazohusiana na malipo haya nilibaini kuwa posho ya jumla ya Sh. 1,195,000 zililipwa zaidi kinyume na miongozo ya Serikali ya ulipaji posho iliyosababishwa na udhibiti duni wa usimamizi wa fedha taslimu. Hii inamaanisha kuwa fedha za umma zilitumiwa vibaya.
15	Halmashauri ya Wilaya ya Musoma	**(i) Matumizi ya ruzuku ya kawaida kuripotiwa zaidi Sh. 900,000** Katika kupitia taarifa ya utendaji wa kifedha na Muhtasari Na. 11 wa taarifa za kifedha nilibaini kuwa matumizi ya ruzuku yaliripotiwa zaidi kwa Sh. 900,000. Hii ni kwa sababu iliripotiwa Sh. 297,445,200 katika taarifa ya utendaji wa kifedha badala ya Sh. 296,545,200 ambayo ni takwimu sahihi iliyosababisha taarifa ya fedha mtiririko isiwe sawa kwa Sh.900,000. **(ii) Majengo ambayo hayakutolewa katika taarifa ya kifedha Sh. Milioni 6.74** Katika kupitia Muhatsari Na. 29 wa mali za kudumu (PPE) wa taarifa za Kifedha nilibaini kuwa majengo ambayo yana thamani halisi katika vitabu ya Sh. 6,738,097 bado yapo katika taarifa ya msimamo wa

Na	Halmashauri	Msingi wa kutoa hati Isiyoridhisha
		kifedha badala ya kutoyatambua katika Muhatsari Na. 29 wa mali za kudumu (PPE). Jengo hilo lilipaswa kuingizwa katika Taarifa kuu za Fedha za Halmashauri na sio katika taarifa za Fedha za Mfuko wa Afya wa Pamoja (HBF).

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi mwaka 2019/20*

Kiambatisho 9- 1: Vipengele Kwenye Nukuu ya Gharama za Vifaa na Huduma Vyenye Bei Kubwa Ikilinganishwa na Bei za Soko

Maelezo	Kipimo	Idadi	Bei iliyojazwa		Bei ya Soko		Jumla ya Tofauti
			kiasi (Dola za Marekani)	Jumla (Dola za Marekan) 'A'	kiasi (Dola za Marekan)	Jumla (Dola za Marekan) 'B'	A-B (Dola za Marekan)
95- Mwanga Sehemu ya Karakana 8: Milango & Madirisha sehemu 081400: Mlango wa Mbao wenye Fremu: Aina ya mlango wa mbao wenye fremu utakuwa kama ulivyofafanuliwa ikijumuisha na ukamilishaji wake, pamoja na viunganishi vyake, kuufunga mahali pake, uwazi wake umetolewa vipimo vyake Kipengele Na.5: Mlango wenye shata moja Aina yenye namba (4) vipimo 800 x 2200 milimita, HW seti (10).	Na	3	230,000	690,000	260	780	689,220
Kazi za nje Ukarabati wa matenki (4) ya maji. Matenki matatu (3) yenye ukubwa wa mita za ujazo 225 na tenki moja (1) lenye ukubwa wa mita za ujazo ($75m^3$) pamoja na barabara za kuwezesha kufika eneo la mradi	Kwa ujumla	1	580,000	580,000	25,000	25,000	555,000
Magari kwa ajili ya Mhandisi na Mwajiri: "Brand new 4 x 4".	Na	3	160,000	480,000	79,393	238,179	241,821
Jumla ya Hasara							**1,486,041**

Chanzo: *Nukuu ya gharama ya vifaa na huduma, Nyaraka za zabuni na Taarifa za Maendeleo ya Mradi*

Kiambatisho 10- 1: Vipengele Vilivyolipwa kwa Mkandarasi Bila Uthibitisho

Item	Maelezo	Unit	idadi	kiwango- Shilingi	Amount paid - Shilingi	Maoni ya ukaguzi
B.13	Kuangalia gharama za ubora na kufanya majaribio ya sehemu ya kazi kama yanakidhi vigezo vilivyowekwa	LS	1	34,000,000.00	45,220,000.00	Malipo yanapaswa kuthibitishwa kwa maombi ya mwajiri kufanyiwa majaribio, hati za malipo, nyaraka za maabara. Nyaraka hizi hazikuonekana
B.21	Ofisi ya mhandisi	LS	1	28,000,000.00	36,400,000.00	Hakuna nyaraka za kuthibitisha malipo kama mkataba, risiti za malipo
B.22	Eneo la makazi la mhandisi	LS	1	9,000,000.00	12,000,000.00	Hakuna nyaraka za kuthibitisha malipo kama mkataba, risiti za malipo
B.31	Ununuzi wa gari 1 Nos. four-wheel drive station wagon 1	Gari - Mwezi	3	4,500,000.00	18,000,000.00	Hakuna nyaraka za kuthibitisha malipo kama mkataba, risiti za malipo
B.32	1 Na. space cab pick – up	gari - Mwezi	3	3,600,000.00	14,400,000.00	Hakuna nyaraka za kuthibitisha malipo kama mkataba, risiti za malipo
B.41	Kuruhusu kununua vifaa vya utafiti vya mhandisi	Miezi	3	16,000,000.00	64,000,000.00	Hakuna kifaa kilichonunuliwa
B.61	Kufanya program ya afya na usalama katika eneo la kazi	LS	1	12,000,000.00	12,000,000.00	Malipo haya yalipaswa ya kuthibitishwa na nyaraka za matumizi kama vocha za malipo na risiti kama manunuzi ya mipira ya kiume, daftari la mahudhurio. Lakini kampuni haikuwa na vithibitisho vyovyote na mkandarasi alilipwa.
	Jumla				**202,020,000**	

Chanzo: *cheti cha malipo Namba nne*

Kiambatisho 11- 1: Maendeleo ya Utekelezaji wa Kazi za Ujenzi hadi Kufikia Novemba 2020

S/N	Maelezo ya kazi	Asilimia inayochangia katika Utekelezaji Wa Mkataba	Asilimia ya Maendenle ya kazi kwa Ujumla
1	Maandalizi ya vifaa na eneo la ujenzi (Mobilization)	1.75	0.68
2	Usanifu wa nguzo na uhadisi	0.9	0.41
3	Usanifu wa Msingi na uhandisi (Foundation design and engineering)	0.4	0.34
4	Usanifu wa Nyaya na Miundombinu ya msingi ya umeme na uhandisiya umeme	0.1	0.1
5	Utafiti wa Kina	0.45	0.32
6	Uchunguzi wa Udongo	0.85	0.43
7	Usafishaji na utengenezaji wa njia za kuingia na kutoka eneo la ujenzi	1.35	1.15
8	Kuwewa Alama za Mchoro wa Jengo Aridhini	0.05	0.00
9	Kufanya majaribio ya aina za nguzo	1.65	0.41
10	Mchakato wa manunuzi	68.4	0.53
11	Kusimika Msingi	14.5	1.86
12	Ujenzi wa nguzo	4.5	0.00
13	Kusimika Miundo mbinu ya msingi wa umeme	3.75	0.00
14	Mafunzo	0.5	0.25
15	Kazi za kumalizia Kukamilisha Ujenzi	0.55	0.00
16	Kukabidhi mradi	0.15	0.00
17	Kuondoka na kuondoa vifaa eneo la ujenzi	0.15	0.00
Jumla		**100**	**6.48**